

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA NNE

---

Kikao cha Tisa – Tarehe 7 Februari, 2019

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

#### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Nne, Kikao cha leo ni cha Tisa. Katibu.

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

#### HATI ZA KWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:

**MHE. JUMA S. NKAMIA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2018.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA):**

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2018.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI):-**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2018.

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu.

**NDG.STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu sana. Muulizaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Lucy Simon Magereli, swali liwe fupi.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Siku ya Jumatatu tarehe 4 Februari, 2019, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wakati wa majamuisho ya Taarifa za Kamati ya Kudumu ya Miundombinu na Kamati ya Viwanda na Biashara alitoa kauli ndani ya Bunge lako iliyomaanisha kusema Serikali imejidhatiti kukuza mitaji yake yenyewe ili kuacha kutegemea mitaji ya uwekezaji na misaada kutoka nje na alitamka akisema wawekezaji wengi ni wezi na wana mikataba ya kinyonyaji. Je, huo ndiyo msimamo wa Serikali kuhusu wafadhili na wawekezaji wa nchi hii?

**SPIKA:** Najaribu kulipima hilo swali kwa sababu sina uhakika kama Naibu Waziri wa Mambo ya Nje alisema hivyo maana ni swali ambalo linahitaji *reference*. Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba sina uhakika kama Naibu Waziri wetu aliwahi kutoa kauli hiyo kwa sababu huo siyo msimamo wa Serikali. Msimamo wa Serikali ni kukaribisha wawekezaji kuwekeza kwenye sekta zote za kibashara na tunatoa fursa hiyo kwa mwekezaji ye yote wa ndani mwenye uwezo na wale wa nje wanakaribishwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali tumefanya kazi kubwa ya kujenga mazingira ya uwekezaji mzuri hapa nchini. Tuna ardhi ya kutosha na tumetoa maelekezo katika Halmashauri zote kutenga ardhi kwa ajili ya kufungua milango ya wawekezaji wanaotaka kuwekeza kwenye sekta ya ardhi lakini pia tuna madini na sekta nydingi ambazo kila moja anayetaka kuwekeza anao uhuru wa kufanya hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jukumu letu Serikali ni kuhakikisha kwamba tunatengeneza mifumo rahisi ya kumwezesha mwekezaji kuwekeza biashara yake na kufanya biashara yake katika mazingira rahisi. Pia Serikali inajitahidi kukutana na wawekezaji wakati wowote kuzungumza nao ili kusikia changamoto ambazo zinawakabili kwenye uwekezaji wao. Ndiyo sababu Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli ameendelea kutoa wito wa ujenzi wa uchumi wa Tanzania kupitia viwanda na sehemu kubwa ya viwanda vinawakaribisha wawekezaji ili waweze kuwekeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nitumie nafasi hii kutoa wito kwa wawekezaji wote nchini na wale wa nje kuja Tanzania kuwekeza; sekta za uwekezaji ziko nydingi, Serikali inajenga miundombinu, tumejenga barabara nzuri za kufanya biashara zao, tunaendelea kuboresha reli, Shirika la Ndege na usafiri wa majini, malengo yetu ni kumwezesha mwekezaji na mfanyabiashara huyu kufanya biashara yake katika mazingira rahisi. Kwa hiyo, huo ndiyo msimamo wa Serikali wa kuhamasisha uwekezaji na kwamba tutawalinda wawekezaji wale wanaojenga viwanda vya ndani na tutalinda viwanda vya ndani ili viweze kufanya biashara yake vizuri zaidi. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Edwin Sannda.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii. Mheshimiwa Waziri Mkuu natamani sana kujuu mpaka sasa Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha kwamba tunaboresha na kurahisisha mazingira ya kufanya biashara nchini?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhalii.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sannda, Mbunge wa Kondoa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake haliko mbali sana na swali la Mheshimiwa Lucy ambalo alitaka Serikali itoe msimamo wa namna ambavyo inaboresha biashara na kutoa fursa ya uwekezaji kuwekeza hapa nchini. Swali hili la mpango au mkakati wa Serikali wa kuboresha biashara, kama ambavyo nimesema kwenye swali la awali kwamba Serikali imejenga mazingira mazuri ya kuwezesha kufanya biashara.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba wafanyabiashara ndiyo wanaochangia pato la Serikali hapa nchini. Katika kuchangia pato la Serikali lazima tuhakikisha wafanyabiashara wote; wafanyabiashara wakubwa, wa kati, wadogo wakiwemo wamachinga, mamalishe tuwape fursa ya wazi, pana ya kuweza kufanya biashara hiyo kwa sababu wao wanachangia pato hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika uchangiaji wa pato hilo maana yake lazima Serikali sasa tuendelee kuwashamasisha wafanyabiashara, tunaendelea kuhakikisha tunajenga mazingira mazuri ya kufanya biashara maeneo yote. Watanzania wote ni mashahidi, Mheshimiwa Rais wetu pia kama ambavyo nimesema awali mmeona juzi jitihada za kutoa vitambulisho kwa ajili ya kuwatambua wafanyabiashara wadogo ili waweze kuratibiwa maeneo yao na wafanye biashara vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia wafanyabaishara wa kati nao uko mpango unaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara kuhakkisha kwamba wanakutana na Waziri kujua mwenendo wa biashara kwenye maeneo yao na hivyo hivyo kwa wafanyabiashara wakubwa. Wote mnajua kwamba tunalo Baraza la Wafanyabiashara ambalo pia Mwenyekiti ni Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli amekutana na wafanyabiashara mara kadhaa ili kusikiliza matatizo wanayokutana nayo katika uendeshaji wa biashara zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mkakati wa kujenga mazingira mazuri ya kibiashara unaendelea ikiwemo pia na upanuaji wa sekta zinazowasaidia wafanyabiashara kufanya vizuri wka maana ya kujenga miundombinu, barabara zote nchini kama nilivyosema awali zimepanuliwa na zinaunganisha mikoa. Kwa hiyo, mfanyabiashara ana uwezo wa kufanya biashara kutoka Katavi mpaka Dar es Salaam akipita kwenye barabara nzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tumenunua ndege, wale wote ambaao wanataka kufanya biashara za ndege za ndani na mpango wetu kwenda nje wanayo fursa ya kufanya hilo. Pia usafiri majini, Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria tunajenga meli mpya ili ziweze kusafirisha abiria na wafanyabiashara kutoka eneo moja mpaka lingine. Kwa hiyo, jitihada zote hizi lengo letu ni kuhakkisha kwamba wafanyabiashara wanafanya biashara katika mazingira mazuri na huo ndiyo mpango wa Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie wafanyabiashara kuendelea kupanga mipango mizuri kwenye mpango wa biashara zao, Serikali inaandelea kuwaunga mkono na pale ambapo wanapata matatizo yoyote kwenye biashara tutaendelea kukutana pamoja na Waziri yupo lakini pia Ofisi yangu iko wazi tunawakaribisha kuja kuzungumzia changamoto ambazo zipo. Muhimu ni tufuate kanuni na sheria na taratibu ambazo zinakuruhusu kufanya biashara. Ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi kuuliza swali kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na songombingo ilioipelekeza zao la korosho kwa msimu uliopita ambaa sasa hivi tunaendelea nao kukosa soko jambo lililopelekeza Serikali kuingilia kati na kutangaza kwamba inakwenda kununua korosho za wakulima. Hata hivyo, hadi leo wakulima walio wengi hawajapata fedha zao wakati korosho tayari zimeshachukuliwa na Serikali. Siyo hivyo tu, kuna baadhi ya wakulima wameanza kulipwa kidogo kidogo lakini kinachoshangaza wakulima wengi wanalipwa Sh. 2,600 kwa kilo kinyume na Mheshimiwa Rais alivyotangaza kwamba korosho anakwenda kuzinunua kwa Sh. 3,300 kwa kilo.

Mheshimiwa Spika, nini kauli ya Serikali kulingana na hii sarakasi inayoendelea sasa hivi kwenye zao hili la korosho? Kwa sababu sasa hivi msimu wenyewe unakwenda kuisha lakini wakulima malalamiko ni makubwa sana? Nini kauli ya Serikali? Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha Bunge cha wiki mbili hizi suala la korosho limezungumzwa sana na Wizara kwa maana Serikali imetoe ufanuzi sana namna ambavyo tunaendelea kufanya malipo ya zao la korosho kwa wakulima wanaolima zao hili walioko kwenye mikoa hii mitano ya Ruvuma, Mtwara, Lindi, Pwani na Tanga ambako sasa wako kwenye masoko. Tunachosema zao la korosho siyo kwamba lilikosa soko bali lilikosa bei nzuri, wanunuzi wapo lakini lilikosa bei nzuri. Pale ambapo wanunuzi walikuwa wanana kwa bei ya chini sana kuliko hata ile bei ya kwenye soko la dunia na ilikuwa haimletei

faida mkulima. Kwa nia nzuri ya Mheshimiwa Rais akaamua korosho hizi sasa tutanunua kwa Sh.3,300 bila makato yoyote yale. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alipotoa kauli sasa Bodi ya Mazao Mchanganyiko yenye dhamana kisheria ya kununua mazao na kutafuta masoko popote pale na hasa kwa mazao ambayo yanaonekana yanasuasua kupata masoko ilianza kazi yake. Imetafuta fedha, baada ya kufanya tathmini ilishajua kiwango cha korosho kitakachozalishwa na gharama zake, wana uwezo nalo, wameanza kazi hiyo na sasa wanaendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tamko la Mheshimiwa Rais kununua kwa Sh.3,300 kwa kilo maana yake anazungumzia *standard grade* ile bei kwa korosho ya daraja la kwanza. Zao la korosho lina *grade I, II*, iko sheria inayoongoza Bodi ya Korosho kwamba korosho za daraja la II zitauzwa asilimia 80 ya bei ya daraja la I. Kwa hiyo, bei iliyyotamkwa ni ya daraja la I, unapokuwa na korosho daraja la II maana yake sasa unarudi kwenye sheria yetu mkulima huyu atalipwa kwa bei ya daraja la II ile asilimia 80 ya bei ya daraja la I. Kwa hiyo, ndicho ambacho kinafanyika, hiyo Sh.2,600 ni *calculation* ya asilimia 80 ya bei ya daraja la I. (*Makof*)

Mheshimiwa Spoika, lakini malipo haya yanaendelea vizuri na kama vile tulijua swali litakuja tena na wakati wote kwa kuwa timu iliyoko kule Mtwara inaendelea kutoa taarifa mpaka jana tumewaongezea tena shilingi bilioni 100 na sasa inafanya zaidi ya shilingi bilioni 500 kulipa na mahitaji yetu sisi ni shilingi bilioni 700. Kwa hiyo, wakishamaliza tunaongeza na kuhakikisha tunamaliza na kama ambavyo unajua niliingilia kati mchakato mzima na kuwapa tarehe ya mwisho ya kulipa wakulima ambayo ni tarehe 15, tuna uhakika kufikia siku hiyo tutakuwa tumefikia kiasi kikubwa cha malipo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niwahakikishie wakulima kwamba malipo yanaendelea na sehemu kubwa ya wakulima tumeendelea kuwalipa na hasa wale walioko

chini ya kilo 1,500 lakini sehemu kubwa ya malipo ambayo yanakuja sasa ni wale wa zaidi ya kilo 1,500, uhakiki umeshafanyika na wanatambulika na sasa utaratibu wa kulipa ambao unaendelea ndiyo ambao utawafanya wakulima sasa kila mmoja aweze kupata fedha yake. Nataka niwahakikishie wanunuzi wa korosho na wakulima wa korosho kwamba korosho zote kama ambavyo tumetamka mara zote kwamba tutazinunua kama ambavyo imekubalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini taratibu zinazoendelea ni ili tujue kwa uhakika zaidi mkulima anayelipwa kuwa ndiye mwenye mali na ndiyo anayelipwa, huo ndiyo mkakati ambao unaendelea kwa sasa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wenzangu na hasa mnaotoka kwenye maeneo ya korosho muwe na amani kabisa, Serikali inaendelea na utaratibu wa kulipa na tutawalipa wakulima wote kwenye maeneo yote. Wakulima wenyewe wawe na imani na Serikali yao na mpango ambao unaendelea kwamba kila mkulima aliyepima korosho zake atafikiwa na atapata malipo yake. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali, Mbunge wa CUF.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba kumuuliza swali moja Mheshimiwa Waziri Mkuu linalofanana kidogo na swali alilouliza Mheshimiwa Kuchauka.

Mheshimiwa Spika, wiki mbili zilizopita Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa Mkoani Mtwara na akatoa maagizo kwa timu zote zinazofanya uhakiki wa kupitia mashamba ya wakulima ziwe zimekamilisha zoezi lile ifikapo tarahe 5 Februari, 2019. Leo tunapongea tarahe 7 Februari, 2019 wakulima wengi wenye korosho zinazoanzia tani moja na nusu na kuendelea bado hawajafikiwa na zoezi hili la uhakiki.

Mheshimiwa Spika, nataka kupata majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba kwa kuwa mpaka leo

bado watu hawajafikiwa na uhakiki, nini kauli ya Serikali kwamba inaongeza siku za uhakiki au kwamba zoezi ndiyo limefikia mwisho ili wakulima waweze kujua kwa sababu hawaoni hizo timu za uhakiki zikiwaendea kwenda kuwashakiki? Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Bobali, Mbunge wa Mchingga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mchakato wa uuzaaji wa zao hili la korosho kulikuwa na eneo ilikuwa ni lazima tufanye uhakiki hasa wale wenye korosho zaldi ya kilo 1,500 na ili kuwatambua ilikuwa ni lazima tujiridhishe kama korosho ni zake kwa kufanya uhakiki? Awali utaratibu huu ulikuwa unafanywa na Bodi ya Mazao Mchanganyiko pekee jambo ambalo lilihusisha watumishi wengi lakini bado walikuwa hawakidhi mahitaji ya ukubwa wa maeneo ya wakulima wa korosho.

Mheshimiwa Spika, baada ya kugundua kwamba kulikuwa na tatizo hilo, nilipokuwa Mkoani Mtwara nilitoa maelekezo mapya na nilikuwa na tarehe 27 na ndipo nilitoa maagizo kwamba utaratibu wa uhakiki ushuke chini uhusishe Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa maana ya Halmashauri ambako pia tunajua tuna Mkuu wa Wilaya mwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama lakini tuna Mkurugenzi ana Afisa Ushirika na Maafisa Kilimo waunde timu zifanye kazi ya uhakiki baada ya kuwa wamepewa majina ya watu wao wenye kilo zaidi ya 1,500 kwenye maeneo yao. Hizi wilaya zina utofauti wa ukubwa na idadi ya wakulima, kwa hiyo kuanzia tarehe 28 kama walikuwa wameshaanza kujipanga mpaka tarehe 5, inaweza kuwa baadhi ya wilaya ambazo ni kubwa sana kama ambavyo unasema Mheshimiwa hawajakamilisha lakini zoezi hilo halikomi na kuwaacha ambao hawajahakikiwa kuwa wasihakikiwe. Tarehe ile ilikuwa ni ya

kimkakati wahakikishe wanafanya kwa haraka, wanawafikia wakulima ili kila mmoja awe ameshahakikiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini uzuri ni kwamba wilaya kadhaa ambazo zina idadi ndogo ya wakulima waliolima korosho na kufikia kilo 1,500 zoezi limekamilika na sasa wanasubiri ulipwaji. Wilaya zile kubwa kama Tandahimba, Nanyamba, Newala, Masasi, Nanyumbu, Liwale, Nachingwea karibu wilaya nydingi, kama vile Rufiji, ni wilaya kubwa na kama Bodi ile ilikuwa na idadi ndogo ya watu wa uhakiki kuna uwezekano wakaongeza. Sisi tunasema muhimu zaidi wakulima wahakikiwe kila mmoja aweze kupata haki yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kupitia kwako nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kila mkulima atahakikiwa lakini naamini mpaka tarehe 5 idadi kubwa kwa sababu ya msisitizo watakuwa wameshafikiwa na wote watalipwa. Kwa hiyo, wale wote ambao hawajafikiwa watafikiwa na watafanyiwa uhakiki kwa haraka zaidi kwa sababu tumeshusha kazi hii ifanywe sasa na Halmashauri za Wilaya, Mkuu wa Wilaya na Kamati yake ya Ulinzi na Usalama anaweza kuhusisha mpaka Watendaji wa Kata ili kuwatambua wakulima waliolima kiwango kikubwa cha korosho. Kwa hiyo, kazi hiyo inaendelea vizuri. Ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi Mbunge wa Viti Maalum.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa shukrani ya dhati kwa kunipatia fursa hii ili niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swalii.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na hali ya kusuasua katika utekelezaji wa Miradi ya REA kufikisha umeme vijijini. Hivi Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba miradi hii sasa inakwenda kwa kasi ili wananchi wa vijijini waweze kupata umeme, kwani umeme ni maendeleo? Naomba jinsi

Serikali ilivyojipanga na kuhakikisha kwamba sasa Miradi hii ya *REA* itakwenda vizuri katika nchi yetu. (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tuna Miradi ya *REA* na inatekelezwa nchi nzima. Wizara ya Nishati kupitia *TANESCO* ilishapata wakandarasi na imewasambaza wanafanya kazi hizo maeneo yote. Malengo ya Serikali ni kuhakikisha kwamba miradi hii inatekelezwa kila eneo kadri tulivyokubaliana na mikataba na wale wakandarasi wanaofanya kazi hiyo. Pia sisi na Mheshimiwa Waziri tunapopita huko tunafuatlia mwenendo wa utekelezaji wa miradi hiyo ili tujiridhishe vijiji vyote viliivyoingia kwenye orodha viweze kupata umeme kadri tulivyokubaliana na wakandarasi wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini tutambue kwamba hapa katikati kulikuwa na migogoro kidogo kati ya wazalishaji nguzo na wamiliki wa mashamba yanayozalisha nguzo ambapo walikuwa wanatofautiana kuhusu kodi. Jambo hili nilipolipata mezani kwangu nililifanyia kazi kwa kuita mamlaka zote ili kupata maelezo ya msingi ili kuhakikisha kwamba kazi hii inaendelea. Nashukuru sana Mikoa ya Iringa na Njombe pamoja na na Wilaya zote kwamba tatizo walilokuwa wanabishana nalo la ulipaji kodi ambalo hasa lilikuwa linagusa kwenye tafsiri ya sheria lilikwisha na kazi inaendelea vizuri, wazalishaji nguzo wanaendelea kuzalisha nguzo na wale wakandarasi wanaendelea kupelekewa nguzo kwenye maeneo yao na kazi inaendelea vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wenzangu na hasa Mheshimiwa Mbunge uliyetaka majibu na Watanzania wote kwenye vijiji ambavyo vimewekwa kwenye mpango kwa ajili ya kupelekewa umeme, tutahakikisha unakwenda kwenye maeneo yote. Serikali inayo fedha kuwalipa wakandarasi,

wakandarasi nao wanawajibika kutekeleza kwa mujibu wa mikataba na wale wote ambao tumesaini mikataba ya kuzalisha nguzo waendelee na kazi hiyo, pale ambako wanatakiwa kutekeleza masharti maeneo wanayozalisha nguzo wafanye hivyo kwa sababu uzalishaji huo na malipo yote ni ya kisheria. Kwa kuwa wameendelea kutekeleza jambo hili tumemuachia kazi Mkuu wa Mkoa wa Iringa kuhakikisha kuwa wazalishaji wanaendelea vizuri na kazi yao na wakandarasi wanaoingia kwenye Wilaya hizo wanapewa mizigo yao na wanasafiri kwenda kwenye maeneo yote ili kazi iweze kuendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, zoezi la usambazaji umeme linaendelea na kama kuna tatizo la kususua huko Waheshimiwa Wabunge mtupe taarifa ili Mheshimiwa Waziri na yejote mwenye dhamana anaweza kwenda kuona tatizo liko wapi ili tutatue tatizo hilo. Malengo ya Serikali ni kuhakikisha kwamba tunapata umeme maeneo yote ili Watanzania mpaka kwenye ngazi ya vijiji, kama ambavyo mmsesikia sasa uwekaji wa umeme tunaweka kwenye nyumba zote ya bati, isiyokuwa ya bati ili Watanzania wapate mwanga. Malengo yetu tunaamini yatakamilika na pale ambako kutakuwa na tatizo tutashughulikia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge uwe na amani. Ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante. Tunakwenda CHADEMA sasa, Mheshimiwa Pascal Yohana Haonga, Mbunge wa Mbozi, uliza swali lako.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Suala la kuongeza mishahara kwa watumishi wa umma siyo suala la utashi wa mtu bali ni suala la kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Na.8 ya mwaka 2002 pamoja na Kanuni zake za 2003. Ni lini sasa Serikali itaacha kukiuka sheria hii kwa kutopandisha mishahara kwa watumishi wa umma na ituambie rasmi ni lini itapandisha mishahara kwa watumishi wa umma?

**SPIKA:** Hiyo sheria inasomekaje?

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, ni Sheria ya Utumishi wa Na.8 ya mwaka 2002 ambayo inaeleza kupandisha mishahara pamoja na stahiki mbalimbali za watumishi wa umma.

**SPIKA:** Si ungetusomea basi hiyo sheria inavyosema. Siyo kila mtu ana nakala hata Mheshimiwa Waziri Mkuu hana nakala, hawezi kukariri sheria zote. (*Makofi*)

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, swali kwa ufupi linahusu kupandisha mishahara watumishi wa umma, ndiyo *logic* sasa ya swali hili. (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Siyo swali hilo.

**WABUNGE FULANI:** Tulieni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Haonga, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali hajakiuka sheria unayoitaja, kama inasema hivyo, kwa kutolipa nyongeza ya mishahara. Serikali lazima iwe na mipango na mipango ile iliyonayo Serikali lazima imnufaishe mtumishi au yejote ambaye anapata stahiki hiyo. Nia ya Serikali kwa watumishi ni njema bado ya kuhakikisha kwamba wanapata mishahara na stahiki zao na wanalipwa madeni yanayozalishwa kutokana na utendaji kazi wao. Hiyo ndiyo nia njema ya Serikali na tunatekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia kwenye eneo la mishahara hili Watanzania wote na wafanyakazi mnajua kwamba nchi hii tulikuwa na idadi kubwa ya wafanyakazi na wengine hawakuwa wafanyakazi kwa mujibu wa orodha na wote walikuwa wanalipwa mishahara na posho mbalimbali. Kwa hiyo, ili kutambua nani anastahili kupata mshahara kiasi gani na kwa wakati gani Serikali ilianza na mazoezi makubwa mawili. Moja, tulianza kwanza kuwatambua watumishi halali

na hewa. Baada ya kuwa tumekamilisha zoezi hili baadaye tulikuja kutambua watumishi wenye vyeti stahiki vya kufanya kazi hiyo kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa mazoezi yote yamekamilika huku pia tukiendelea kulipa na madeni ya watumishi ambao tumewatambua pia Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli ameunda Tume ya Mishahara Mishahara na Motisha. Baada ya kuwa tumemaliza kutambua watumishi stahiki sasa Tume ile inafanya mapitio ya kada zote za utumishi wa umma na viwango vya mishahara yao ili kutambua stahiki ya mshahara huo na kada hiyo baada ya kugundua kwamba ziko tofauti kubwa za watu wenye weledi wa aina moja, wamesoma chuo kikuu kimoja, lakini wanapata ajira kwenye sekta mbili mmoja anapata millioni 20 mwingine millioni 5, jambo hili kwenye utumishi halina tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nia ya Mheshimiwa Rais kuunda ile Tume ni kufanya tathimini nzuri ya kutambua weledi wa kazi lakini pia itahusisha na uwajibikaji mahali pa kazi na tija inayopatikana mahali pa kazi ili alipwe mshahara unaostahilli. Kwa hiyo, jambo hili inawezekana limechukua muda katika kuhakikisha kwamba tunafikia hatua hiyo, inawezekana Mheshimiwa Mbunge ukasema kwamba Serikali hajijatimiza Jukumu lake lakini nataka nikuhakikishie kwamba kwa taratibu hizi tunalenga kuhakikisha kila matumishi anapata mshahara kulingana na weledi wa kazi yake au daraja lake ili kuondoa tofauti ambazo zipo za kiwango cha mishahara ambazo zinapatikana kwenye maeneo haya watu wakiwa na weledi wa aina moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutakapokamilisha kazi hii, kwa bahati nzuri ile Tume tayari imeshawasilisha taarifa Serikali na Serikali kuititia Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma inaendelea kuititia, wakati wowote tunaweza kupata taarifa za matokeo ya Tume ile. Kwa hiyo, niwahakikishie watumishi wote nchini kwanza muendelee kuwa watulivu, mbili

muendelee kuiamini Serikali yetu na tatu Serikali inayo nia njema ya dhati kabisa kuhakikisha kwamba watumishi wote wanapata haki zao stahiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri sana Mheshimiwa Rais wetu amekutana na viongozi wa vyama vya wafanyakazi, ameeleza vizuri haya na viongozi wamepata nafasi ya kueleza changamoto zilizopo kwenye sekta ya umma na Serikali tumechukua hizo changamoto zote na tunazifanyia kazi. Kwa bahati nzuri mjadala wetu na vyama vya wafanyakazi unaendelea vizuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge ambaye pia umewazungumzia wafanyakazi uendelee kuwa na imani na Serikali, utaratibu wetu ni mzuri na unalenga hasa kuleta tija kwa mfanyakazi ili aweze kufanya kazi yake vizuri. Kwa hiyo, wakati wowote kazi itakapokamilika tutatoa taarifa kwa wafanyakazi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Venance Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize swalii moja. Nchi yetu imepata bahati ya kuandaa Mashindano ya Vijana ya Afrika (AFCON). Kwa sababu kutakuwa na wageni wengi akiwemo Rais wa Mpira wa Dunia na wageni tofauti ambao wanakuja kuangalia wachezaji wa nchi mbalimbali, kwa hiyo, tutakuwa na ugeni wa kutosha, nilitaka kujua tumehusishaje mashindano haya na utalii wa nchi yetu ili kuutangaza na kuwafanya wageni hao wawe mabalozi watakaporudi kwao? Pia mmehusishaje na Wizara ya Mambo ya Ndani kuhakikisha kwamba...

**SPIKA:** Swalii moja tu.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Kuhakikisha kwamba usalama unakuwepo? Naomba nijibiwe swalii hilo.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mwamoto, majibu ya swalii hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwamoto, Kocha wa Timu yetu ya Bunge, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nataka nitumie nafsi hii kuipongeza Wizara ya Habari, Utamaduni, Michezo na Sanaa, kwa kazi nzuri waliyofanya ya ushawishi kwa Shirikisho la Mpira wa Miguu Duniani ili kuleta mashindano haya kwetu nchini Tanzania. Pongezi hizi pia zifiki chombo chetu au Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania kwa jitihada zake za kuratibu vizuri jambo hili kutoka tulipopata dhamana hiyo mpaka hatua tulioifiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania kupitia Serikali hii ya Awamu ya Tano imeridhia mashindano hayo kufanyika hapa Tanzania na yanafanyika mwaka huu wa 2019. Katika mashindano hayo vijana wetu wanapata fursa ya kushiriki kutoka ngazi ya awali mpaka fainali kama timu zetu zitafika fainali na ndiyo tunaomba taimu yetu ifike fainali ili sisi kama mwenyeji tuweze kufika kwenye fainali na ikiwezekana pia tuchukue kombe la dunia. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali imejiandaa kupokea wageni wote wanaokuja kushiriki mashindano haya hapa nchini na inaendelea na maandalizi hayo kwa kushawishi sekta zote zitakazonufalka na uwepo wa wageni hao kuja hapa nchini kujiandaa. Vikao mbalimbali vinafanywa na Wizara pamoja na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania na wadau mbalimbali wanashirikishwa na Serikali tunajua kazi kubwa inayoendelea kufanywa na tunatambua kwamba tutapokea wageni wengi akiwemo Rais wa FIA hapa nchini na tunaendelea kujenga mazingira kuwapokea wageni wengi zaidi kadri watakavyopatikana. Huduma tunazo, tunazo hoteli, maeneo ya kutoa vyakula lakini pia usafiri wa ndani tunao, kwa hiyo, ni maeneo ambayo tumeendelea kuimarisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia kupitia mashindano haya tumehamasisha mikoa ya jirani na maeneo ambako viwanja

vitatumika na tunaambiwa viwanja vitatu vitatumika wakati wote wa mashindano Dar es Salaam na maeneo mengine, Shirikisho la Mpira litatupa taarifa baada ya kuwa wamekamilisha maandalizi, kwa hiyo, pia na mikoa hiyo nayo itaweza kunufaika. Kwa hiyo, maandalizi ya maeneo yote hayo yanaendelea kufanywa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kupitia swali la Mheshimiwa Mbunge niwahakikishie Watanzania kwamba ujio huu kwetu ni muhimu sana. Kwa hiyo, sote tunatakiwa tushirikiane kuhakikisha kwamba tunapata mafanikio kwa wageni hawa kuingia, kuishi hapa na kurudi makwao wakiwa salama. Kwa hiyo, ni jukumu letu kuhakikisha kwamba tuko salama. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia Shirikisho la Soka Tanzania liendelee kuimarisha maandalizi ya timu yetu ambayo itashiriki kwenye mashindano haya ili hatimaye tuweze kuibuka kidedea. Sisi Watanzania wote tunawajibika sasa kuonesha uzalendo kwa timu yetu itakayofanikiwa kuingia ili kuipa moyo. Kwa hiyo, mchango wa kila mmoja wa namna yoyote ile unahitajika katika suala hili. Kwa hiyo, niwahakikishie Watanzania kwamba mashindano tunayapokea, tuko tayari kuwapokea wageni wake na tutaendelea kushindana kwa sababu na sisi tuna timu ambayo itashindana na naamini tutafanikiwa. Ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tunakushukuru sana kwa muda wako, sasa unaweza ukarudi kwenye kitikitizo. (*Makof*)

Tunashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, nafikiri tumejitahidi angalau tukapata Wabunge wengi zaidi kuuliza maswali, tungeweka nyongeza tusingewapata wale wangine.

Tunaendelea, Katibu.

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI YA KAWAIDA**

**SPIKA:** Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, swali linaulizwa na Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, tafadhali uliza swali lako.

Na. 101

**Ukarabati wa Shule za Serikali – Kilindi**

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza:-

Serikali imekuwa na utaratibu wa kukarabati shule zake za sekondari na za msingi nchini:-

Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati Shule za Sekondari Masagulu, Lwande, Mkuyu na Shule za Msingi Songe na Masagulu zilizopo Wilayani Kilindi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Mwita Waitara, Naibu Waziri, TAMISEMI, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA C. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omary Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi ina jumla ya Shule za Msingi za Serikali 111 na Sekondari 22. Kuanzia mwaka 2015/2016 hadi 2017/2018 kuitia Mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo (*EP4R*), Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi imepatiwa kiasi cha Sh.122,823,097 kwa ajili ya ujenzi

na umaliziaji wa miundombinu ya shule za msingi na sekondari ambapo shule tatu za sekondari na 14 za msingi zimenufaika.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza programu mbalimbali za kuboresha miundombinu mashulen ikiwemo ukarabati wa shule kongwe 89 nchini. Serikali kwa kushirikisha nguvu za wananchi na wadau wengine wa maendeleo itaendelea kuweka kipaumbele cha ukarabati wa miundombinu ya shule ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunza. Aidha, natumia fursa hii kuzielekeza Halmashauri zote kutenga bajeti kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya shule.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza nampongeza na niwapongeze TAMISEMI kwa kutupatia kiasi kilichotajwa kwa ajili ya shule zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba Halmashauri zetu nyingi hazina uwezo wa mapato, lakini natambua dhamira ya Serikali ya kutoa elimu bure. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kukarabati shule kongwe ambazo ni za muda mrefu? Kwa mfano, Shule ya Msingi Masagali ya mwaka 1940 na Shule ya Msingi Songwe 1952? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kutembelea hizi ili ajione hali halisi? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Waitara, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA C. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Kigua kwa kazi nzuri ambayo anaifanya kutetea wananchi wake na hasa kuboresha miundombinu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunavyozungumza hapa kwenye mgawo ambaao umeishia awamu ya saba ya EP4Ramepata mgawo wa shule mbili; Shule ya Kikunde mabweni mawili, matundu sita ya vyoo, vile vile na Shule ya Mafisa ambayo imepata madarasa manne na bweni moja na matundu sita ya vyoo.

Mheshimiwa Spika, vilevile swalii lake la kwanza ni kwamba Serikali ya Awamu ya Tano imejitahidi sana, tumekarabati shule 45 kwa zile shilingi bilioni 60, lakini sasa tunaenda awamu ya pili, tunakarabati shule 17 kwa zaidi ya shilingi bilioni 17. Sasa shule aliyoitaja, tutaangalia kwenye orodha yetu, lakini tutaendelea kadiri itakavyowezekana. Ni nia ya Serikali kukarabati shule zote 89 hizi kongwe, zikamilike, lakini tumeanza zile ambazo tulizirithi kutoka kwa Wakoloni, ili tumalize twende na nydingine zote pamoja na hizi za kisasa ambazo wananchi wanachangia pia.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, naomba nimwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba Mkutano huu ukimalizika tarehe 11 nitakuwa Tanga na Kilindi ni mojawapo. Tanga, Arusha na kuendelea. Kwa hiyo, niko tayari kutembelea shule hizi na kupata maelezo ya ziada. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Tunaendelea. Tuko Wizara hiyo hiyo, swalii la Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa.

Na. 102

**Serikali Kutenga Pesa za Ujenzi wa  
Hospitali ya Wilaya ya Kyerwa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Wilaya ya Kyerwa ina Vituo vitatu vya Afya, lakini kituo kimoja ndicho kina uhakika wa kutoa huduma, vilevile kuna uhaba wa watumishi ambao wanafanya kazi kwenye mazingira magumu pamoja na ukosefu wa nyumba za watumishi:-

Je, Serikali ipo tayari kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na nyumba za watumishi ili kutekeleza llani ya CCM na kuondoa adha wanayoipata akina mama, watoto na wananchi wengine kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA  
NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa ina jumla ya Vituo vya Huduma za Afya 32 vinavyohudumua watu takribani 394,375. Kati ya vituo hivyo, kuna Vituo vya Afya vitatu, vyote vikiwa vya Serikali, Zahanati ziko 28; 23 za Serikali na tano ni za watu binafsi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa ni mionganini mwa Halmashauri 67 nchini zilizopatiwa shilingi bilioni 1.5 kila moja kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Mpaka sasa hatua za awali za ujenzi zinaendelea na ujenzi wa awamu ya kwanza unatarajiwa kukamilika Juni 30, 2019. Vilevile Serikali imipeleka kiasi cha shilingi milioni 800 kwa ajili ya ujenzi na upanuzi wa Vituo vya Afya Murongo na

Kamuli katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa ambapo mpaka sasa ujenzi umekamilika kwa asilimia 98.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Bilakwate, tafadhali.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kututengea hizi pesa kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya, lakini kipekee nachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Jafo kwa jinsi ambavyo nimekuwa nikimsumbuu kuhusiana na Vituo vya Afya na Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, kulingana na jiografia ya Wilaya yangu, ninaomba kuuliza swali. Kwa kuwa tuna vituo vitatu kwenye Tarafa nne na kwenye Kata 24: Serikali iko tayari kututengea kituo kingine kimoja? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kyerwa tuna upungufu mkubwa wa watumishi. Kwenye kituo kingine unakuta kuna watumishi wawili kwenye Zahanati moja: Je, Serikali iko tayari kututengea watumishi wa kutosha ili wananchi waweze kupata huduma? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kwa niaba ya Serikali nipokee pongezi kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge. Katika hali ya kawaida, mtu anayeshukuru tafsiri yake ni kwamba anaomba kingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba tunaendelea kujenga Vituo vya Afya kwa kadiri nafasi ya kibajeti itakavyoruhusu. Jiografia ya Kyerwa hakika ni jiografia ambayo ina utata mkubwa, Jimbo ni kubwa. Naomba aendelee kuiamini Serikali, kwa kadiri bajeti itakavyoruhusu na tutakavyokuwa tunaendelea kujenga Vituo vya Afya, naye tutamkumbuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia kuna swali lake la pili; anaomba kuongeza idadi ya watumishi ili waweze kutoa huduma ambayo inastahili kwa wananchi wake. Sasa hivi Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumeomba kibali cha kuweza kupata nafasi za kuajiri. Kwa kadiri nafasi zitakavyokuwa zimepatikana, hakika katika usambazaji tutahakikisha maeneo ambayo yana uhitaji mkubwa yanazingatiwa. Naamini na eneo lake ni mionganoni mwa maeneo hayo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Bado tuko TAMISEMI, swali linaulizwa na Mheshimiwa; ooh, majibu ya nyongeza Mheshimiwa Mkuchika, tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, ninaomba kutoa maelezo ya nyongeza kuhusu uhaba wa watumishi, hasa afya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Serikali inafanya jitihada za kujenga Vituo vya Afya na Zahanati nchi nzima. Tunakirii kwamba watumishi hawatoshi, ndiyo maana kwa kushirikiana na TAMISEMI tunafanya utaratibu wa kuongeza. Nimesimama hapa kueleza kwamba, sisi upande wa Wizara ya Utumishi na Utawala Bora tutaweka kwanza kipaumbele katika Zahanati na Vituo vya Afya vipyta ambavyo havijaanza kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Viongozi wa Mikoa, Waheshimiwa Wabunge mkiwasimamia, kuhakikisha wanapoleta maombi watuletee kwamba Zahanati mpya

inahitaji watumishi kadhaa, Kituo cha Afya kipyä kinahitaji watumishi kadhaa. Pamoja na uhaba uliopo, lengo ni kwamba Vituo vyote vya Afya na Zahanati zote mpya zifunguliwe mara moja, ndiyo tutawapa kipaumbele, kwa sababu sehemu nyingine huduma bado zitaendelea kutolewa japo kwa upungufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda kwa ruhusa yako pia, nijibu suala la uhaba wa Walimu. Sasa hivi baada ya kufungua mwaka mpya huu wa masomo, Walimu wengi wamestaafu mwaka 2018, wengine wamefariki. Sisi upande wa Utumishi tutaanza kwanza kujaza idadi ya Walimu waliostaafu mwaka 2018, ili tuwe na kiwango cha Walimu kama waliokuwepo mwaka 2018, baada ya hapo tutaendelea na zoezi la kuajiri Walimu wapya.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Bado tuko TAMISEMI, sasa namwita Mheshimiwa Lathifa Chande Kigwalilo. Uliza swali lako tafadhali.

Na. 103

### **Hali Duni ya Huduma za Afya Lindi**

**MHE. LATHIFA H. CHANDE** aliuliza:-

Wananchi wa Mkoa wa Lindi wanakabiliwa na changamoto kubwa ya hali duni ya huduma za afya kwa kuwa na uchache wa Wauguzi, Madaktari wa kawaida na wa akina mama na uhaba wa vifaa na dawa, lakini pia Vituo vya Afya na Zahanati hazitoshi:-

(a) Je, ni lini Serikali itaongeza Wauguzi, vifaa tiba na dawa katika Hospitali ya Wilaya ya Liwale?

(b) Hospitali ya Ruangwa kwa kipindi kirefu imekuwa haina huduma ya X-Ray hali inayowalazimu

wananchi wa Wilaya ya Ruangwa kufuata huduma hiyo Lindi: Je, ni lini Serikali itatatua tatizo hilo?

(c) Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi wa nyumba za Wauguzi na Mganga Mkuu katika Zahanati ya Mtawango katika Kata ya Mtawango, Liwale?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri, TAMISEMI, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali ya Mheshimiwa Lathifa Hasan Chande, Mbunge wa Viti Maalum, Lenye Sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali iliajiri watumishi wa kada mbalimbali za Afya 6,180. Kati ya hao, 89 walipangwa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale. Mwaka wa fedha 2017/2018 na 2018/2019 Halmashauri ya Wilaya ya Liwale imepokea jumla ya shilingi milioni 345.5 kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi. Aidha, upatikanaji wa dawa muhimu katika vituo vyote 242 vya kutolea huduma za afya Mkoani Lindi kuanzia Januari hadi Desemba, 2018 ikiwemo Hospitali ya Wilaya ya Liwale ulikuwa ni kwa zaidi ya asilimia 91.9.

(b) Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Wilaya ya Ruangwa ilifungiwa mashine ya X-Ray mwaka 2015 ambapo mpaka Desemba, 2018 Wagonjwa 7,250 wamehudumiwa. Ni kweli kuna wakati mashine hii ilipata hitilafu na ikashindwa kufanya kazi, lakini hitilafu hiyo ilirekebishwa na mashine ya X-Ray inaendelea kutoa huduma. Mpango wa Serikali ni kuipatia hospitali hii X-Ray ya kisasa.

(c) Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ujenzi wa Zahanati pamoja na nyumba za Watumishi Mtawango ulikuwa ni mradi unaofadhiliwa na TASAF katika mwaka wa fedha 2015/

2016 kujenga nyumba mbili kwa moja (*two in one*), ambapo fedha zilizopangwa na kutumika ni shilingi milioni 27. Hata hivyo, fedha hizo hazikutosheleza kumalizia ujenzi wa nyumba. Hivyo, Halmashauri imepanga kutenga shilingi milioni 10 katika bajeti ya mapato ya ndani ya mwaka 2019/2020 ili kukamilisha ujenzi wa nyumba ya Muuguzi na Mganga katika Zahanati ya Mtawango.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lathifa, umeuliza maswali matatu katika swali moja kwa hiyo, limesababisha majibu yawe marefu sana.

**MHE. LATHIFA H. CHANDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Hapana, sasa kwa sababu umetumia muda mwingi, maswali yako ni matatu, nakunyima la nyongeza.

Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria. Swali litaulizwa na Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa.

Na. 104

**Kuondolewa kwa Mwanasheria Mkuu  
wa Serikali Kushtaki Makosa ya Jinai Nchini**

**MHE. MOHAMED O. MCCHENGERWA** aliuliza:-

Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 ya Mwaka 2018 yamemwondoa Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kushitaki kesi zote za jinai nchini, lakini Katiba ya Jamhuri ya Muungano inamtambua Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika mambo ya Muungano:-

Je, kumwondo moja kwa moja Mwanasheria Mkuu wa Serikali hakuwezi kuathiri makosa ya jinai ya uhaini yanayoweza kutokea Zanzibar kukwama kwa kuwa Mkurugenzi wa Mashitaka hana mamlaka kwa mujibu wa Katiba na mambo ya Muungano kushitaki Zanzibar?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Mavunde, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 59(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Sheria ya Ofisi ya Mashitaka, Sura ya 430, masuala ya ufunguaji, uendeshaji na usimamizi wa mashitaka ya jinai nchini yako chini ya Mkurugenzi wa Mashitaka na siyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kwa upande wa Zanzibar, masuala hayo yanaongozwa na Ibara ya 56(a) ya Katiba ya Zanzibar na Sheria ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka Na. 2 ya Mwaka 2010. Katika Katiba zote mbili na sheria zake, mamlaka ya mwisho ya kufungua, kuendesha na kusimamia mashitaka ya jinai ni ya Mkurugenzi wa Mashitaka. Hivyo, masuala ya jinai siyo suala la Muungano.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa tarehe 13 Februari, 2018 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alifanya mabadiliko ya muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambapo pamoja na mambo mengine alianzisha Ofisi Huru ya Taifa ya Mashitaka. Ili kuendana na mabadiliko hayo ya muundo, yalifanyika kurekebisha kwenye Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Utekelezaji wa Majukumu) Sura ya 268 kwa kukifuta Kifungu cha 8 na kukibadilisha kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 ya Mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, marekebisho hayo yamemwondoa Mkurugenzi wa Mashitaka na iliyokuwa *Division* ya Mashitaka kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa

Serikali. Hivyo, mabadiliko hayo hayajaathiri kwa namna yoyote ufunguaji, uendeshaji na usimamizi wa mashauri ya jinai nchini. Bado kwa mujibu wa lbara ya 59(d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 Mkurugenzi wa Mashitaka anaendelea kuwa na mamlaka ya juu ya mashauri yote ya jinai nchini.

Mheshimiwa Spika, makosa yote ya jinai yanayotokea katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yanaendelea kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria zilizopo na hayawezi kukwama kwa kuwa kuna mifumo mizuri ya kikatiba, kisheria na kitaasisi ya kuyashughulikia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Spika, naona bado kuna tatizo kubwa kwenye eneo hili na nitatumia fursa ya kufanya *dialogue* na Wizara ya Katiba na Sheria ili kuweza kuweka sawa eneo hili. Naona kuna tatizo kubwa, sina swali la nyongeza Mheshimiwa. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa, siku hizi anauliza maswali ya kuhusu Zanzibar, sijui inakuwaje hii? (*Kicheko/Makofii*)

Sasa Waheshimiwa Wabunge mnacheka nini? Rais Mwinyi alisema, Zanzibar ni njema, atakaye na aje. (*Kicheko/Makofii*)

Tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; swali la Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde.

Na. 105

***TFF Kuipatia ZFA Fedha za FIA***

**MHE. KHATIB SAID HAJI** aliuliza:-

*FIA* inatoa misaada ya fedha kwa Tanzania kuitia  
*TFF*:

Je, ni kiasi gani cha fedha *TFF* imekuwa ikiipatia Zanzibar kupitia *ZFA*?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khatib Said Haji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli *FIFA* inatoa msaada wa fedha kwa mashirikisho ya mpira wa miguu ikiwepo *TFF* kwa ajili ya miradi na programu mbalimbali. Fedha hizo huwa ni maelekezo maalum kwa lengo la kusaidia na kuendeleza maeneo mahususi yafuatayo: Ligi ya Wanawake, ligi ya vijana, masuala ya kiutawala, kuinua vipaji kwa (*Grassroot Program*), *Women's Football Promotion*, pamoja na Maendeleo ya Waamuzi.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka huu *FIFA* itakuwa inatoa jumla ya Dola za Kimarekani milioni 1.25 kila mwaka kwa wanachama wake wote ikiwepo *ZFA*, ambayo ni sehemu ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania kwa mchanganuo ufuatao: fedha za miradi ya maendeleo kiasi cha Dola za Kimarekani 750,000, fedha kwa ajili ya kuendesha ofisi, Dola za Kimarekani 500,000.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa muda wa miaka mitatu sasa kutohana na kutokuwepo kwa uwazi katika matumizi ya fedha na kutokidhi vigezo vyta utawala bora, *TFF* wamekuwa hawapati fedha hizo. Kazi kubwa imeshafanyika kurekebisha dosari zilizokuwepo za kiuhasibu na kiutawala bora. Hivyo, uwezekano ni mkubwa kwa *TFF* na *ZFA* kupokea fedha za msaada huo wa fedha mapema mwaka huu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Konde nimekuona, swali la nyongeza.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Swali langu nililomwuliza, ni kiasi gani cha mgawo wa fedha hizi za *FIFA* wamewahi kuipatia Zanzibar? Jibu lake, anakuja kusema kwamba kuanzia mwaka huu tutapata 1.25. Kwa hiyo, amekwepa kabisa kunijibu swali langu nililomwuliza. Nataka kujua: Je, mmewahi kuipatia mgawo wowote Zanzibar kutokana na misaada hii inayotoka *FIFA*?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Nataka nijue, kwa kuwa *TFF* siyo chombo cha Muungano, Mheshimiwa Waziri wa Michezo sio Waziri wa Muungano na Wizara ya Michezo siyo Wizara ya Muungano; kwa hiyo, anaposema sasa kwamba kuanzia msaada huu unaokuja, mgawo utaenda kwa *ZFA* na *TFF*, nataka nijue, mtatumia *formula* ipi wakati mkijua kwamba masuala ya michezo Zanzibar wana Wizara yao na Tanzania Bara wana Wizara yao: Je, hamwon hapa kwamba kuna mkorogano ambao kwa miaka yote na ndio maana Zanzibar tunakosa msaada huu wa *FIFA*?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri, Habari, Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nikianza na swali lake la kwanza, ametaka kujua kwamba, ni kiasi gani? *TFF* imekuwa ikitoa misaada mbalimbali kwa Chama cha *ZFA* ambacho ni cha Zanzibar. Moja ya miradi ambayo tayari imeshapelekwa *ZFA* ni ujenzi na ukarabati wa Uwanja wa Gombani ambao uko Pemba. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba *TFF* imekuwa haipeleki msaada Zanzibar, hapana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili ambapo ameelezea kwamba suala la michezo siyo la Muungano, nadhani Mheshimiwa Mbunge alikuwa hajaelewa jibu langu la msingi ambalo nimelitoa. Ni kwamba, *ZFA* ni sehemu ya *TFF*. Kwa tafsiri hiyo basi, maana yake fedha ambazo zinaletwa *TFF* zinagawiwa kwa mashirikisho yote ikiwepo *ZFA*

ya Zanzibar, lakini si kwamba, ZFA inaletewa fungu lake peke yake, hapana, kwa sababu, ZFA siyo mwanachama wa CAF, lakini ZFA vilevile siyo mwanachama wa FIFA. ZFA iko chini ya TFF.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Khatibu umeelewa hapo, ZFA ipo chini ya TFF huelewi nini? Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Pudenciana Wilfred Kikwembe uliza swalii lako tafadhali.

Na. 106

### **Barabara ya Kibaoni – Inyonga**

**MHE. Dkt. PUDENCIANA W. KIKWEMBE** aliuliza:-

Je, Serikali itakamilisha lini ujenzi wa barabara ya kutoka Kibaoni kupitia Majimoto mpaka Inyonga kwa kiwango cha lami ukizingatia kuwa daraja la Kavuu limekwishakamilika ili barabara hiyo ianze kutumika?

**SPIKA:** Majibu ya swalii hilo, Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Kwandikwa.

**NAIBU WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Kavuu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kibaoni-Majimoto-Inyonga ni barabara ya mkoa yenye urefu wa kilometra 152 inayohudumiwa na Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Katavi. Barabara hii ni ya changarawe na inapitika majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa barabara hii, Serikali kuititia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) imetangaza zabuni kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni pamoja na kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Zabuni kwa ajili ya kazi hiyo zinatarajiwa kufunguliwa taehe 11 Februari, 2019.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hizo, Serikali imeanza kujenga sehemu ya barabara hii kwa awamu kwa kiwango cha lami kuanzia Mji wa Inyonga ambapo katika mwaka wa fedha 2017/2018, jumla ya kilometra 1.7 zilijengwa. Aidha, katika mwaka wa fedha 2018/2019 mkandarasi wa kujenga kilometra 2.5 amepatikana na yupo katika hatua za maandalizi ya kuleta vifaa na wataalam katika eneo la mradi ili kuanza kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kikwembe, tafadhalii swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PUDENCIA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake yenye matumaini kwa sababu barabara ya kutoka majimoto Inyonga zabuni imeshatangazwa. Swali langu ni kwamba kwa kuwa barabara hii iko chini ya *TANROADS*na *TANROADS*wamesema kwamba wanatangaza zabuni ya kumpata mpembuzi na msanifu ili waweze kuianza barabara hiyo na kwa kuwa zoezi la kutangaza zabuni na mpaka kumpata mkandarasi ni la muda mrefu. Je, ni lini sasa katika maombi yangu maalum ya kilomita 2.0 katika Mji wa Usevya yatapatiwa majibu na barabara hiyo ianze kutengenezwa kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa mkandarasi alipatikana ambaye ameweza kujenga kilomita 1.7 katika Mji wa Inyonga, lakini katika mwaka wa fedha 2018/2019 mkandarasi wa kujenga kilomita 2.5 amepatikana na yupo katika eneo la mradi. Je, ni eneo gani la mradi ambapo mkandarasi huyo yupo?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias John Kwandikwa.

**NAIBU WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nazipokea shukurani alizozitoa, nazipokea kwa dhati, lakini pia kwa furaha nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi ya usanifu kama nilivyojibu katika jibu la msingi tarehe 11 ambayo ni Jumatatu ijayo zabuni itafunguliwa na hii hakuna namna kwa sababu, harakati za ujenzi zinazingatia pia Kanuni na Sheria za Manunuzi. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge tupo kwenye hatua nzuri, mzabuni atakapokuwa amepatikana na sisi tutasimamia kwa umahiri ili hii kazi hii iweze kukamilika kwa wakati. Kwa hiyo, nimtoe hofu pamoja na wananchi wa Kavuu kwa ujumla kwamba sasa ujenzi wa barabara hii utakuwa umeanza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu eneo la kilomita 2.0; eneo hili ni mwendelezo katika Mji wa Inyonga, lakini Mheshimiwa Mbunge nafahamu kwamba iko haja ya kuweka msukumo wa kujenga kipande cha barabara kutoka Kibaoni kuja kwenye Mji wa Usevya ambaao ni Makao Makuu ya Halmashauri. Kwa hiyo nimtoe hofu tu kwamba, usanifu utakapokamiliika na sisi tutaweka kipaumbele ili wananchi hawa wanaokwenda makao makuu waweze kuunganika vizuri na barabara ambayo sasa ukitoka Kizi kuja Kibaoni, hatimaye tuunganishe kipande hiki cha kuja Makao Makuu ya Wilaya, lakini pia sehemu ya Majimoto ambayo ina wafanyabiashara wengi na kuna sehemu kubwa ya uchumi. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi, tutazingatia haya maeneo ambayo ni muhimu kuhakikisha wananchi wanaunganishwa vizuri.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaenda Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, swali la Mheshimiwa Emanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini tafadhali.

Na. 107

**Mgogoro wa Mipaka Kati ya  
Wananchi na Jeshi – Tabora Mjini**

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza:-

Kwa muda mrefu kumekuwa na migogoro ya mipaka baina ya wananchi na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) katika maeneo ya Mkonkole Kata ya Tambuka Reli, Usule Kata ya Mbungani na Kata ya Cheyo Tabora Mjini:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kutatua mgogoro huo ambao ni wa muda mrefu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tafadhalii.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mji wa Tabora, JWTZ lina Kambi kwenye maeneo ya *Airport*, Cheyo, Bomani, Mirambo, Usule na Kalunde. Maeneo yote hayo yalipimwa na ramani zake kusajiliwa. Wakati wa upimaji maeneo mawili walikutwa watu wachache. Eneo la *Airport* alikutwa mwananchi mmoja aliyekuwa anaishi hapo. Mwananchi huyo alishafanyiwa uthamini na ameshalipwa fidia yake. Katika eneo la Usale zilikutwa familia tatu. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa limefanya mawasiliano na familia hizi kwa ajili ya kufanyiwa uthamini na hatua ya kulipwa fidia kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, katika juhudii za kuendeleza makazi katika Mji wa Tabora, Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ilianza kupima viwanda ndani ya eneo la Kambi ya

Mirambo ambalo tayari lilikuwa limepimwa. JWTZ ilichukua hatua ya kulifikisha suala hilo katika Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Tabora ambayo ilisimamisha zoezi hilo. Wakati zoezi llnasimamishwa, tayari wananchi wengine wameshagawiwa viwanja. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaendelea kuwasiliana na Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ili kuwaondoa wananchi hao ambao walipimiwa viwanja ndani ya eneo hilo likiwemo eneo la Tambuka Reli. Uondoshaji wa wananchi hawa utawezesha eneo hilo kuwa huu kwa matumizi ya kijeshi pekee.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA.** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Tabora hasa Manispaa imezungukwa na kambi za jeshi kwa eneo kubwa. Kutokana na hali hiyo kumekuwa na migogoro mikubwa ambayo inapelekeea wananchi ambao wamekuwa wakitumia maeneo kwa muda mrefu kufikia hata kupigwa wanapokuwa wanafanya shughuli zao. Kwa mfano, kuna eneo ambalo kuna barabara inapita katika kata nne eneo la Uyui, kuna eneo la Rada, barabara hii ni ya miaka mingi na ni hiyo tu ambayo wananchi wa kata hizo nne wanaitumia, ikifika saa moja na nusu mpaka saa mbili usiku, wananchi wakipita maeneo maeneo yale wamekuwa wakipigwa na wakati mwингine hata kunyanganywa vifaa vyao vya usafiri zikiwemo baskeli. Je, Serikali ina mpango gani kuhusiana na eneo hilo ambalo wananchi wamekuwa wakitumia kama barabara?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa shughuli nydingi zimesimama katika maeneo hayo hasa za wananchi ambao walikuwa wakitumia maeneo hayo kwa kulima ambayo wamekuwa wakilima muda mrefu, lakini wengine na shughuli zao za kiutamaduni kwenye mapori ambayo wamekuwa hata hawayapi athari yoyote. Je, kutokana na hali hiyo ambayo ni ya muda mrefu Mheshimiwa Waziri yupo tayari sasa kuja Tabora ili tuweze mimi na yeche kwenda kukagua maeneo haya na kuyapatia utatuzi ambao ni mgogoro wa muda mrefu? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili, tafadhali Mheshimiwa Waziri kama Wanyamwezi hawataki jeshi, tunawakaribisha Kongwa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara inayopita kuelekea eneo la Rada la jeshi na kwamba wananchi wanapopita hapo wanapigwa, suala hili nitalifuatilia ili niweze kupata taarifa rasmi ya nini hasa kinachoendelea. Hakuna sheria inayoruhusu wananchi kupigwa, lakini kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge nitakuwa tayari kwenda kufanya ziara katika eneo hili la Tabora Mjini ili njionee mimi mwenyewe hali ilivyo pale na tutafute ufumbuzi, suluhu kwa ajili ya maslahi ya pande zote. Ni vema wananchi watambue kwamba, yale mapori yanayoonekana kama hayana kazi, ni maeneo ambayo wanajeshi wanafanya mazoezi, kwa hiyo yana kazi maalum. Tukifanya hii ziara, tutaweza kuambatana na viongozi wa jeshi ili tuone ni ufumbuzi gani ambaa unaweza ukapatikana.

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo linalekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, linaulizwa na Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum - Njombe, Mheshimiwa Neema.

Na. 108

***MSD kukosa Dawa za Kuongeza  
Damu kwa Mama Mjamzito***

**MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

*MSD kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa dawa za kuongeza damu kwa mama mjamzito na dawa za usingizi:-*

Je, ni lini changamoto hiyo itatatuliwa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Afya, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,  
JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto kuititia Bohari ya Dawa (*MSD*) imeboresha upatikanaji wa dawa muhimu hadi kufikia wastani wa asilimia 90 katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Upatikanaji wa dawa hizi kwa kiasi kikubwa umetokana na ongezeko la bajeti ya dawa hadi kufikia bilioni 269 katika mwaka wa fedha 2018/2019 toka bilioni 31 kwa mwaka wa fedha 2015/2016, pia kuimarika kwa mifumo ya usimamizi wa dawa hizo katika mnyoroo wa ugavi.

Mheshimiwa Spika, dawa za kuongeza uwingi wa damu (*Ferous sulphate/fumerate + Folic acid*) na dawa za usingizi (*Anaesthesia drugs*) ni kati ya dawa zilizo katika orodha ya dawa muhimu zaidi ambazo upatikanaji wake umeimarika hadi kufikia asilimia 90. Kwa sasa dawa hizi zote mbili zinapatikana kwa kiasi kikubwa katika Bohari ya Dawa. Kutokana na umuhimu wa dawa hizi kwa mama wajawazito na katika kuhakikisha tunapambana na vifo vya mama wajawazito, Wizara inawaagiza Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuhakikisha dawa hizi zinapatikana katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mgaya, swali la nyongeza, tafadhali.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nikiri kwamba sisi watu wa Mkoa wa Njombe hospitali zetu na vituo vyetu vya afya tunapata pesa za dawa zaidi ya asilimia 90, lakini bado Mheshimiwa Naibu

Waziri kuna changamoto. Tuna changamoto ya dawa za afya ya akili pamoja na chanjo ya kichaa cha mbwa ambazo inatulazimu vifaa vyta afya kwenda kununua kwa wa zabuni kwa bei kubwa sana. Sasa je, ni lini *MSD* itatatua changamoto hii kuhakikisha kwamba, inapeleka dawa za afya ya akili na chanjo ya kichaa cha mbwa katika vituo vyta afya na hospitali za Mkoa wa Njombe?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, pesa za *Basket Fund* zimekuwa zikichelewa sana katika vituo vyetu vyta afya na hospitali zetu za Wilaya ndani ya Mkoa wa Njombe. Hivi sasa ninavyozungumza Hospitali ya Wilaya ya Ludewa, Hospitali ya Wilaya ya Makete, wamepata pesa za *Basket Fund* kwa *quarter* ya kwanza tu ilihali sasa hivi tuko *quarter* ya tatu. Je, ni lini Serikali itapeleka pesa hizi za *Basket Fund* kwa wakati ili hospitali hizi ziweze kununua dawa kwa sababu bila kuwa na pesa hata waki-place order kule *MSD*, *MSD* hawakubali kuwapatia dawa?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri Afya, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mgaya kwa kuwa mfuatiliaji wa masuala mbalimbali katika sekta ya afya na kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya kule Njombe katika kuwashudumia akinamama na watoto. Sasa naomba niseme kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu ambao tunautumia sasa hivi Serikali ni utaratibu unaitwa *pull system*, hapo awali tulikuwa tunapeleka dawa pasipo kuzingatia mahitaji na uhalisia ambao ulikuwepo katika vituo vyetu vyta kutolea huduma za afya. Sasa hivi utaratibu ni kwamba hospitali zinaagiza kulingana na mahitaji yake na nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, chanjo tunazo zote asilimia mia moja na hizi tunazisambaza kulingana na mahitaji ya mikoa.

Mheshimiwa Spika, la pili, chanjo za kichaa cha mbwa na dawa za afya ya akili; dawa hizi tunazo katika bohari yetu ya madawa na katika stoo zetu za kanda pale Iringa. Niombe tu Mheshimiwa Mbunge atusaidie kuwaomba mamlaka kule kuagiza kwa sababu zile dawa zina mahitaji mahususi, huwezi ukazipeleka tu kwa sababu wagonjwa wa afya ya akili pamoja na wagonjwa ambao wameumwa na mbwa si wengi kiasi hicho. Hata hivyo, sisi kama Serikali kuititia bohari ya dawa, tunazo dawa hizo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, ni kweli tunakiri kwamba pesa za *Basket Fund* zinakuwa zinachelewa na hii kwa sababu fedha hizi nazo zina mkono wa wafadhili, wanapochelewa kutufikishia na sisi mchakato mzima unachelewa kuzifikisha kule. Hata hivyo, niseme tu kwamba fedha za *Basket* siyo chanzo pekee cha fedha ambazo zinatumika katika dawa, tuna fedha za ruzuku za dawa ambazo tunazipeleka, tuna fedha papo kwa papo na tuna fedha za bima ya afya ambazo zote kwa kiasi kikubwa nazo zinapelekwa katika manunuzi ya dawa. Kwa hiyo kutokuwepo kwa pesa ya *Basket Fund*, siyo kigezo na wala siyo sababu ya kukosekana dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya. (*Makofii*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuendelee, leo tuna Kamati tatu, kwa hiyo kazi kidogo pevu, bado sijapata maelekezo ya wageni tulionao nikipata tu nitawatambulisha baadaye kidogo. Nianze na matangazo machache niliyonayo:-

Kwanza, tangazo la Mheshimiwa Mbunge wa Mafia, Mheshimiwa Mbaraka Dau, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wabunge Waislam, anawatangazieni Wabunge wote Waislam kwamba kutakuwa na kikao maalum cha mawaiidha na dua leo tarehe 7 Februari, saa saba mchana baada ya kuahirisha shughuli za Bunge katika ukumbi wa Msekwa. Wabunge Waislam kutakuwa na kikao maalum cha mawaiidha na mgeni mualikwa atakuwa ni Shekhe Hashim Mbonde ambaye ndiye atatoa mhadhara na dua.

Katibu wa Bunge anawatangazieni Waheshimiwa Wabunge kwamba Dkt. Festus Limbu ambaye alikuwa Mbunge mwenzetu hapa, akiwa Mbunge wa Magu ni Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na ni Mbunge mstaafu kama nilivyosema, atafanya uzinduzi wa vitabu vyake viwili leo mchana. Cha kwanza kinaitwa Tanzania Kuelekea Uchumi wa Kati; Jukumu la Serikali ya Awamu ya Tano kilichochapishwa mwezi Machi, 2018.

Cha pili ni Mpango Mkakati wa Kuongeza Ajira na Kukuza Uchumi (*LSD 5 Model*) kilichochapishwa mwezi Januari, 2019. Uzinduzi huu utafanyika leo katika moja ya kumbi za ukumbi wetu wa Msekwa, mara baada ya kuahirishwa kwa Bunge tutakuwepo, lakini pia atakuwepo Mheshimiwa Waziri Joseph George Kakunda kwa ajili ya zoezi hilo, tunaombwa sote tuweze kuhudhuria.

Kama nilivyosema nitakapoletewa karatasi ya wageni wote tulionao nitawatambulisha, kwa hiyo wageni endeleeni kukaa hapo mlipo hadi nitakapowatambulisha.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**WABUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Haya kwa kifupi ninyi wa tatu. Tunaanza na Mheshimiwa Lathifah au haikuwa mwongozo ulisimama tu?

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE:** Mheshimiwa Spika, sikusimama kwa mwongozo.

**SPIKA:** *Okay, wamebaki wawili. Ndiyo Mheshimiwa Masoud, kwa kifupi sana.*

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo kuhusu utaratibu mzima tunaoenda nao juu ya mjadala wa taarifa za Kamati na muda tunaoutumia. Utaona kwamba tunakuwa na taarifa za Kamati mbili na muda tunaotumia ni mdogo sana na hizi ni

taarifa za mwaka. Naomba mwongozo wako juu ya kufanyia marekebisho taratibu hizi kwa kuziongezea muda taarifa za Kamati katika kipindi kinachokua.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** La kwako ni ushauri, niseme ushauri huo nimeuchukua na Kamati ya Uongozi wamesikia maana ndiyo tunaopanga kwa pamoja. *Actually* mwazoni mpango ulikuwa kwamba tuwe tunapokea Kamati nne kwa siku moja lakini tukajitahidi tukafanya kazi mpaka *weekend* angalau tukaweza kuzipunguza kuwa Kamati mbili au tatu kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Musukuma, tafadhali.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba mwongozo wako, kwa kuwa leo tunajadili taarifa za Kamati na tutajadili pia taarifa ya Wizara ya Afya; na kwa kuwa ziko sheria zinazoweza kumruhusu mtu kuitwa mgonjwa lakini tunaona Mheshimiwa Tundu Lissu anazunguka kwenye nchi mbalimbali lakini huku anasomeka kama mgonjwa.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako ni lini Bunge litasitisha mshahara wake kwa kuwa ameshapona, anazurura na Bunge linaendelea na ye ye hayupo na mnaendelea kumlipa mshahara. Anazunguka nje anatukana Bunge na viongozi.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, umenishau.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kuhusu maswali kwa Waziri Mkuu maana maswali anayoulizwa Waziri Mkuu ni maswali ya

kujibiwa na Naibu Mawaziri au Waziri. Tunakuwa tunapoteza muda wa maswali yetu muhimu siku ya Alhamisi kwa maswali ambayo yanafaa moja kwa moja kujibiwa na Waziri wa Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Hilo la mwisho la Mheshimiwa Keissy, ni maoni yake kwetu wote kwamba tuulize maswali ambayo yanafaa Ofisi ya Waziri Mkuu badala ya maswali ambayo yako chini ya kiwango hicho. Kwa hiyo, ni ushauri ametoa kwa sisi Waheshimiwa Wabunge wote tu-*improve* aina ya maswali tunayouliza kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makof!*)

Kuhusu Mheshimiwa Musukuma, ni kweli jambo hili la ndugu yetu, rafiki yetu na Mbunge mwezetu Mheshimiwa Tundu Antiphas Lissu linahitaji kuangaliwa kipekee. Kwa maana ya kwamba Mbunge hayupo Jimboni kwake, hayupo hapa Bungeni tunapofanya kazi, hayupo hospitalini, hayupo Tanzania na taarifa zake Spika hana kabisa, wala hajishughulishi hata kumwandikia Spika kumwambia nipo mahali fulani au nafanya hivi na kama ni mgonjwa hakuna taarifa yoyote ya Daktari, halafu unaendelea kumlipa malipo mbalimbali. Nadhani hoja yako ina msingi kwamba iko haja ya kusimamisha malipo ya aina yoyote ile mpaka hapo ambapo tutapata taarifa rasmi za yuko wapi na anafanya nini. Vinginevyo ni *audit query* tu kwa sababu hatuna *reference*, tulikuwa tunajua yupo hospitali sasa tunamwona yuko duniani, kwa maneno ya Mheshimiwa Musukuma anazurura. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Musukuma yale yaliyo ndani ya uwezo wangu nitayafanya. Ahsante kwa ushauri. (*Makof!*)

Sasa nimepata karatasi ya wageni, ninao wageni pale kwenye *gallery* ya Spika, Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kibaigwa kutoka Jimbo la Kongwa, Mheshimiwa Samwel Mganga. Ahsante na karibu sana. Yupo pia Afisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kibaigwa Athman Nzenga, karibu sana. Pia yupo kaka

yangu kutoka Mirongo katika Jiji la Mwanza Ndugu Ramadhan Nyagani, karibu sana sana. (*Makofii*)

Pia wapo viongozi wa *Tanzania Association of Tour Operators*, Ndugu Merywn Nunes – Trustee; Vice Chair – Ndugu Henry Kimambo; *CEO* – Ndugu Sirili Akiko; *Project Coordinator* - Ndugu Jumapili Chenga; *IT and Photographer* - Ndugu Adbdallh Mbelele; na *CEO, Hotel Association of Tanzania* - Ndugu Nuru Lisa Karamagi. Ahsante sana na karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni wengine wa Mheshimiwa Spika ni Wafadhili wa Mradi wa Kulijengea Uwezo Bunge (*LSP II*), wageni wetu sote sisi Wabunge ambao wamekuwa na ziara ya kulitembelea Bunge ni pamoja na *Governance Term Leader* anayeitwa Ndugu Oliver Blake, Oliver stand up please, ahsante sana karibu sana. *Programmes Manager Govenance Team DFID* - Ndugu Lilian Msuya, karibu Lilian. *Senior Governance and Gender Specilist Embassy of Ireland* - Ndugu Aran Corrigan, karibu. *Head of Gevernance and Human right Embassy of Denmark* - Ndugu Madam Jane Warngreen Rosales, karibu. *Democratic Governance Embassay of Sweden* - Ndugu Claire Henneville, karibu sana. *Project Coordinator LSP* – *UNDP* Ndugu Takawira Musavengana, jina la Kizimbwabwe hili. *Monitor and Evaluation Specialist LSP UNDP* - Ndugu Paul Wilson Mlemya. Karibu sana *team nzima ya LSP II*. (*Makofii*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni pamoja na wageni wanne wa Mheshimiwa Kapt. George Mkuchika kutoka Mkoani Morogoro wakiongozwa na Mbunge Mstaafu wa Morogoro Kusini, Mheshimiwa Semindu Pawa. Mheshimiwa Semindu Pawa yupo wapi, ooh yule pale, ahsante sana. Karibu sana Mheshimiwa Semindu Pawa. (*Makofii*)

Kwa wale Waheshimiwa Wabunge wageni hamtamfahamu vizuri Mheshimiwa Semindu Pawa lakini huyu alikuwa ni mmoja wa Wabunge wenye kipawa kikubwa sana cha kuzungumza. Wakati ule Mheshimiwa Msekwa akiwa

Spika akiona ni karibu na saa 6 Wabunge wanatokatoka nje, Wabunge wanazungumza hawasikilizi basi anatamka kwamba baada ya wachangiaji wawili, watatu afatufa Semendu Pawa. Ikishatangazwa hivyo Wabunge walioko kantini wanarudi na walioko nje wanarudi na akiongea hakuna asiyevunja mbavu kwa kucheka. Karibu sana kaka yetu Mheshimiwa Semindu Pawa. (*Makofi*)

Wageni 80 wa Mheshimiwa Joseph Haule ambao ni wanafunzi 75 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari ya Kilosa ya Mkoani Morogoro, wakiongozwa na Mwalimu Elias Luena. Wanafunzi toka Kilosa, karibuni sana sana. (*Makofi*)

Wageni sita wa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, shemeji yetu, ambao ni wanachama wa CCM kutoka Wilaya Same wakiongozwa na Katibu wa UVCCM Wilaya Ndugu Mussa Mweta. Ahsante na karibu sana. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Ally Keissy ambao ni Katibu wa CCM wa Kata ya Isunta, Ndugu Crispin Wikula na Katibu Mbunge wa Nkasi Kusini Ndugu Crisen Kwimba. Karibuni sana pale mlipo. (*Makofi*)

Wageni saba wa Waheshimiwa Wabunge wenye Ulemavu kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu kwa Watu wenye Ulemavu nchini wakiongozwa na Ndugu Peter Sarungi. Wale pale, karibu sana. (*Makofi*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Joseph Shilole. Wako pale, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Omari Kigoda ambao ni wadau wa huduma za maendeleo ya jamii kutoka taasisi ya Usonji iitwayo *Autism Therapy and Behaviors Learning Centre* kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Shaban Gweli na Ndugu Aziz Chonya. Wako kule juu kabisa, karibuni sana. (*Makofi*)

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Wageni watatu wa Mheshimiwa Flatei Massay ambaao ni wapiga kura wake kutoka Mbulu, Mkoani Manyara wakiongozwa na Ndugu John Tua. Karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 75 na walimu 10 kutoka Shule ya Msingi *Assumption* ya Jijini Arusha wakiongozana na Ndugu Michael Mvungi. *Assumption* karibu sana. (*Makofii*)

Wanafunzi 80 na Walimu kutoka Shule ya Sekondari *St. Monica* ya Jijini Arusha wakiongozwa na Ndugu Samwel Laizer. Karibu sana watoto wa *St. Monica* kutoka Arusha. (*Makofii*)

Wanafunzi 18 na walimu 2 kutoka Chuo cha Elimu na Mafunzo ya Ufundil Stadi (VETA) Dodoma wakiongozwa na Mwalimu Gabriel Sikoi. Karibu sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

### **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kufanya Marekebisho katika Sheria mbalimbali zipatazo tano (5) kwa lengo la kuondoa mapangufu ambayo yamejitokeza katika Sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika Sheria hizo (*A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws*)

(*Kusomwa Mara ya Kwanza*)

**SPIKA:** Ahsante Katibu. Muswada huu ndiyo umeingia unasomwa kwa Mara Kwanza, tumeupata katika utaratibu ya Hati ya Dharura. Kamati ya Uongozi ilikaa jana, tumuujadili na kuukubali kwamba tuufanyi kazi siku ya Jumamosi ya wiki hii. Ni jambo muhimu kwetu na mengi yaliyomo mle yanatokana na maoni ya Waheshimiwa Wabunge ambayo tumekuwa tukiyatoa mara kwa mara

yanayoboresha hasa masuala ya kodi ili kuweka nchi yetu mahali pazuri zaidi. Kwa hiyo, nimeupeleka kwenye Kamati ya Bajeti na jana ile ile imeanza kuushughulikia. Kwa kuwa sasa tumeshausoma rasmi mara ya kwanza waendelee kuushughulikia Muswada huo. Siku ya Jumamosi tutaupokea rasmi humu ndani na kuufanya kazi.

Waheshimiwa Wabunge, Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH- KATIBU MEZANI:**

#### **HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na  
Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa  
Mwaka 2018; na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na  
Serikali za Mitaa kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka  
2018; na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya  
UKIMWI kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2018**

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nawaita Wenyeviti, kila Mwenyekiti atazungumza kwa dakika zisizozidi 15. Kwa hiyo, mjiipange vizuri, zaidi tunachokihitaji ni maoni na mapendekezo na kingine chochote muhimu ambacho kama Mwenyekiti unaona kinafaa kuzungumza.

Naomba nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, atafuatiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa. Karibu sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma, Mheshimiwa Juma Nkamia dakika 15.

**MHE. JUMA S. NKAMIA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa mwaka 2018/2019 kwa mujibu wa Kanuni ya 117, Sehemu ya Kumi na Tano ya Kanuni za Kudumu Bunge.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati hii yameelezwa kwenye Nyongeza ya Nane, Sehemu ya Saba. Aidha, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara tatu ambazo ni Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Wizara Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, shughuli zilizotekelizwa na Kamati kwa mwaka 2018/2019, ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka fedha 2017/2018.
- (ii) Kupokea, kuchambua na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa Wizara inazozisimamia.
- (iii) Kupokea, kuchambua na kujadili taarifa za utendaji wa taasisi za Wizara inazozisimamia.
- (iv) Kupokea, kuchambua na kujadili taarifa za utendaji wa Wizara na taasisi kwa kipindi cha nusu mwaka yaani Julai – Desemba 2018
- (v) Kuchambua Miswada ya sheria na kushiriki semina za mafunzo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Baada ya maelezo hayo kuhusu shughuli

zilizotekelawa na Kamati kwa kipindi cha Machi, 2018 hadi Januari, 2019, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa bajeti ya Serikali katika Wizara. Kwa kuwa utekelezaji wa majukumu ya Wizara zote kwa ajili ya kuwalettea Watanzania maendeleo unategemea uwepo wa bajeti ya kutosha ya fedha zilizotengwa na Serikali na kupitishwa na Bunge lako Tukufu, haitoshi uwepo wa bajeti pekee bali na upelekaji wa fedha hizo za bajeti katika Wizara husika kwa wakati ili kuwawezesha watendaji wa Wizara hizo kutekeleza mipango iliyopangwa kwa mwaka wa fedha husika. Na kwa kuwa bado mwenendo wa bajeti siyo wa kuridhisha hali inayoathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo. Kwa hiyo basi, Kamati inazidi kusisitiza Serikali iendelee kupeleka fedha zote zillzoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya maendeleo yake.

Mheshimiwa Spika, miradi ya maendeleo. Kwa kuwa katika bajeti ya mwaka 2017/2018, Serikali iliidhinishiwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Wizara tatu ambazo Kamati inazisimamia. Na kwa kuwa katika miradi yote ambayo Kamati ilifanya ukaguzi mwezi Machi, 2018, hakuna mradi hata mmoja ambao ulikuwa umeperekewa fedha. Baadhi ya miradi iliyokuwa inaendelea kutekelezwa ilikuwa inatumia bakaa za fedha za miaka iliyopita. Kwa hiyo basi Kamati inaendelea kusisitiza kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo zitolewe kwa wakati ili kuepusha kutekelezwa kwa hasara kwa baadhi ya miradi na kupanda kwa thamani ya fedha kulingana na tofauti ya nyakati.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Asasi zisizo za Kiserikali (AZAKI), kanzi data (*database*) ya AZAKI zote. Kwa kuwa kwa mujibu wa taarifa za Wizara kuna zaidi ya AZAKI 8,000 hapa nchini zilizojikita katika nyanja mbalimbali za afya, maendeleo ya jamii kwa maana ya watoto, wazee na hata masuala ya kijinsia hasa kwa wanawake. Na kwa kuwa pamoja na AZAKI hizi kufanya shughuli zake katika maeneo mbalimbali nchini

mijini na vijiji lakini Wizara kama wasimamizi wa AZAKI haina taarifa za uhakika wa wapi zilipo na hata wakati mwininge Wizara haifahamu shughuli maalum zinazotekelezwa na AZAKI hizo na kuifanya Serikali kushindwa kufuatilia utekelezaji wa shughuli zake. Kwa hiyo basi Kamati inashauri Wizara kutengeneza kanzidata ambayo itaonesha jina la AZAKI, mahali inapotekeleza majukumu yake, wafadhili wa fedha wa AZAKI husika na aina ya majukumu yanayotekelawa. Kwa kufanya hivyo, Wizara itakuwa imesaidia kufanya uratibu na usimamizi wa AZAKI zote hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara ianzishe Kitengo cha Udhibiti ubora wa AZAKI. Kwa kuwa uanzishwaji wa AZAKI unafanyika kwa mujibu wa Sheria na miongozo yake lakini pia zinahitaji udhibiti wa ubora wa shughuli inazofanya. Na kwa kuwa zipo asasi ambazo zinafanya vizuri na baadhi zinakwenda kinyume na sheria na miongozo ya Serikali hali ambayo inaleta ukakasi kwenye jamii. Kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza Wizara kuanzisha kitengo cha udhibiti ubora wa AZAKI ili kuweza kuzisimamia na kuhakikisha zinatekeleza majukumu yake ipasavyo na kuzichukulia hatua kali ikiwemo onyo na hata kupelekwa mbele ya vyombo vy'a sheria ikithibitika zimekwenda kinyume na sheria za nchi. Kwa kufanya hivyo zitaongeza uwajibikaji na usimamiaji wa sheria na miongozo ambayo Serikali imewekwa kwa maslahi mapana ya nchi na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto. Kwa kuwa, utekelezaji wa majukumu ya Idara Kuu, Maendeleo ya Jamii, unategemea sana kiasi cha fedha kinachotengwa. Na kwa kuwa, kwa muda mrefu idara hii haijawahi kutengewa zaidi ya shilingi bilioni 50 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake ikiwemo miradi ya maendeleo, Kamati inaona ni kikwazo kikubwa katika utendaji wa majukumu ya idara hiyo na ukizingatia kwamba, Idara hii inabeba kundi kubwa la watoto, wazee na jinsia zote yaani Watanzania wote. Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali ianze kubadili mtazamo wake na kuipa umuhimu idara hii kwa kuitengea bajeti ya kutosha ili iweze kutatua changamoto za sekta mbalimbali

ikiwemo ya kilimo, afya, maji, miundombinu utalii na nyingine kwa kuwa kila jambo linaanza katika jamii kuititia Maafisa Maendeleo ya Jamii walio katika kila kata hapa nchini ili kuweza kuwaletea maendeleo wananchi.

Mheshimiwa Spika, ukatili wa kijinsia na watoto. Kwa kuwa, Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, imeainisha kwamba, nanukuu: "Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake kwa mujibu wa sheria." Na kwa kuwa, hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la ukatili wa kijinsia na watoto hususan katika baadhi ya Mikoa hapa nchini, mfano Mkoa wa Njombe ambapo watoto wanaendelea kuuwawa jambo ambalo ni kinyume na Katiba ya nchi yetu na matakwa ya makubaliano ya kimataifa lakini pia ni kinyume na haki za binadamu. Kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza Serikali ifanye uchunguzi wa haraka na kuwachukulia hatua kali wale wote watakaobainika kuhusika na vitendo hivyo vyaa kinyama.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (*NHIF*). Kwa kuwa afya ni mtaji mkubwa katika kujiletea maendeleo kwa nchi husika na kwa muda mrefu Serikali imekuwa ikishauriwa na kupokea mapendekezo ya Kamati kwamba ni wakati sasa umefika kuwepo na Bima ya Afya kwa Watu Wote (*Universal Health Coverage*) lakini inashindikana kwa kuwa hakuna sheria ambayo itaweza kusimamia aina hiyo ya bima. Na kwa kuwa, Kamati inaona umuhimu mkubwa wa aina hii ya Bima kwa wananchi wote ambayo itaondoa ubaguzi wa aina yoyote wa nani awe na bima na nani asiwe nayo. Hali ilivyo sasa ni wale walio katika ajira rasmi tu ndiyo wanufaika kwa asilimia kubwa na Bima ya Taifa ya afya na watu hawa hawazidi asilimia 27 ya Watanzania wote. Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote (*Universal Health Coverage Bill*) ili *NHIF* iweze kutekeleza jukumu la kutoa bima ya afya kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, tathmini (*Actuarial Valuation*) ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Kwa kuwa Mfuko wa Taifa

wa Bima ya Afya ni mfuko wa wananchi ambao wanahudumiana kwa kuchangiana (*Risk Pooling Strategies*) kila mwezi ili kuweza kupata huduma za afya kwa maana ya kwamba anayeugua anahudumiwa na waliowazima. Fedha hizi zinapaswa kuwepo na ili mteja aone kama zipo anatarajia kupata huduma za afya wakati wote na mahali popote alipo bila kikwazo chochote. Na kwa kuwa, Kamati imekuwa ikishuhudia Mfuko huu ukifanya uwekezaji wa aina mbalimbali na hata kutoa mikopo kwa taasisi za Serikali kwa ajili ya kufanya uwekezaji ambao baadhi hauendani na hata na makusudio ya uanzishwaji wa Mfuko huo. Kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza kuwa Mfuko huo utekeleze majukumu yake ya msingi ambayo ni malengo mahsus ya kuundwa kwake. Aidha, Serikali ifanye tathmini ya mfuko (*Actuarial Valuation*) ili kuweza kufahamu uhai na nguvu ya Mfuko husika.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kuwezesha wawekezaji katika uzalishaji wa dawa hapa nchini. Kwa kuwa nchi yetu ina kauli mbiu ya urchumi wa viwanda na moja ya eneo ambalo Serikali inaweza ikafanya vyema zaidi ni uwekezaji katika mazingira bora ya viwanda vya uzalishaji wa dawa za binadamu hapa nchini. Na kwa kuwa, ili kufanikisha uzalishaji wa dawa hapa nchini ushirikishwaji wa sekta binafsi ni muhimu ili ziweze kuzalisha dawa hizo hapa nchini ili ziuzwe kwa gharama nafuu. Kwa hiyo basi, Kamati inashauri Serikali iharakishe mchakato wa mpango wa kuziwezesha sekta binafsi katika kuzalisha dawa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda unakwenda mbio mno, naomba taarifa yangu hii yote iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Sheria ya Huduma za Habari. Kwa kuwa mwaka 2016 Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya Huduma za Habari (*The Media Service Act 2016*) kwa ajili ya kusimamia masuala yote ya habari ikiwemo weledi wa wanataluma ya uandishi wa habari, wamiliki wa vyombo vya habari ikiwemo magazeti, redio na televisheni. Na kwa kuwa

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Kamati imekuwa ikishuhudia baadhi ya magazeti yakikiuka maadilii, taaluma na weledi wa kupata habari hapa nchini. Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali isimamie kikamilifu Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 kwa kuvichukulia hatua vyombo vyote vya habari na wamiliki wake wanaokiuka sheria kama ambavyo ilikusudiwa ili kuweza kuitunza heshima ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Sanaa Tanzania. Kwa kuwa kuna vipaji vingi ambavyo vipo kwenye jamii lakini Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) halijaweza kuvitambua. Na kwa kuwa, kuibuliwa kwa vipaji hivyo kutaongeza idadi ya wasanii waliopo nchini na hivyo kuongeza mapato ya nchi kutokana na kazi watakazokuwa wanazifanya. Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali kupitia BASATA iandae mkakati maalum wa kuibua vipaji hivyo kuanzia ngazi ya chini ya jamii ili Watanzania wote waweze kunufalka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa moja ya kazi za BASATA ni kutoa ushauri na misaada ya kiufundi kwa wasanii na wadau wa sanaa nchini na hivi karibuni kumekuwa na fungia fungia ya nyimbo za wasanii na matamasha ya wasanii. Na kwa kuwa wasanii hawa wamekuwa wakipata mapato mengi kutokana na *HITS* wanazopata kupitia mitandao ya jamii kama *Youtube* na Serikali imekuwa haipati chochote kutokana na mahusiano yasiyoridhisha kati yao na wasanii hao. Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri BASATA kutekeleza jukumu lake la kuwalea wasanii na kuachana na tabia ya kuwafungiafungia. (*Makofi*)

**SPIKA:** Malizia sasa.

**MHE. JUMA S. NKAMIA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba taarifa yangu hii iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA SHUGHULI ZA  
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA  
MAENDELEO YA JAMII KWA MWAKA 2018/ 2019 – KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0      UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, nashukuru kwa kunipa fursa hii ili kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa mwaka 2018/ 2019.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 123 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu Tatu. Sehemu ya Kwanza ni utangulizi wenyewe kueleza muundo na majukumu ya Kamati. Sehemu ya Pili inaeleza kuhusu namna Kamati ilivyotekeliza majukumu yake na yaliyobainika wakati wa utekelezaji huo. Sehemu ya Tatu inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati na mwisho kabisa ni Hitimsho la Taarifa.

**1.1      Muundo na Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Majukumu ya Kamati hii yameelezwa kwenye Nyongeza ya Nane, 7 (1) (a-d) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Majukumu hayo ni kama ifuatavyo:-

- a)      Kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia;
- b)      Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge ilio chini ya Wizara inazozisimamia;
- c)      Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo pamoja na Taasisi zilizo chini yake; na
- d)      Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

Aidha, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane 5 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara tatu ambazo ni: -

- a) Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;
- b) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na
- c) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

### **1.2 Shughuli zilizotekelizwa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka 2018/2019, Kamati imetekeliza shughuli mbalimbali kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge kama ifuatavyo:

- a) Kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo illyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2017/2018;
- b) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa Wizara inazozisimamia;
- c) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za utendaji wa Taasisi za Wizara inazozisimamia;
- d) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za utendaji wa Wizara na Taasisi kwa kipindi cha nusu Mwaka (Julai – Disemba 2018);
- e) Kuchambua Miswada ya Sheria; na
- f) Kushiriki Semina za mafunzo.

### **SEHEMU YA PILI**

### **2.0 UCHAMBUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoolezwa awali, kwa mwaka 2018/2019 Kamati imetekeliza majukumu yake kwa kufanya uchambuzi na kujadili Taarifa mbalimbali pamoja na kufanya ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo na kuchambua Muswada wa Sheria kama ifuatavyo:

## **2.1 Kupokea Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi mbalimbali**

**Mheshimiwa Spika**, Katika nyakati tofauti kuanzia mwezi Machi, 2018 hadi Januari, 2019, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara inazozisimamia kama ifuatavyo:-

### **2.1.1 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliendelea kutekeleza majukumu mbalimbali uliyoipa yakiwemo kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Taasisi ambazo Kamati ilikutana nazo na kuweza kupokea na kujadili Taarifa zao ni pamoja na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Bohari Kuu ya Dawa (MSD), Hospitali ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto (KDHI). Aidha, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara hii kuhusu utekelezaji wa majukumu katika Hospitali za Mikoa nchini. Utendaji wa Taasisi hizo zilizotajwa ni kama ifuatavyo;

#### **a) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)**

**Mheshimiwa Spika**, Mnamo tarehe 26 Oktoba, 2018 Waziri aliwasilisha Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya yenye kujumuisha chimbuko la Mfuko huo pamoja na majukumu yake na ushirikiano wake na Bohari Kuu ya Dawa (MSD) katika kutatua changamoto za upatikanaji wa huduma za Afya nchini. Mfuko huo ulianzishwa na kundi la watumishi wa Umma kwa kuzingatia dhana ya mshikamano wa kijamii katika kuweza kugharamia huduma za afya mionganoni mwa wanachama wake.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ilieleza pia Mfuko wa Bima ya Afya una vyanzo vitatu vya mapato ambavyo ni pamoja na michango ya wanachama, mapato ya uwekezaji wa fedha katika miradi na vyanzo vingine mbalimbali. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa, Mapato hayo yamekuwa yakiongezeka kila mwaka. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 mapato yalikuwa ni shilingi **Bilioni 488.595** ambapo kwa mwaka 2018/2019 yanatarajiwa kuwa kiasi

cha shilingi **Bilioni 589.283** ikiwa ni ongezeko la **asilimia 17.0** ikilinganishwa na mwaka 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa pia kuwa, Wizara imeendelea kutekeleza maelekezo na ushauri mbalimbali wa Kamati ili kuboresha utendaji wa NHIF ikiwemo kubuni utaratibu wa kuwa na vifurushi vya Bima ya Afya ambavyo vitawawezesha wananchi wengi kupata huduma hiyo, kuyashawishi mashirika mbalimbali kujunga na NHIF, kuhakikisha Bima ya afya kwa wote (*Universal Health Coverage*) inaanza mapema, Mfuko kufanya re - insurance na makampuni mengine ya nje ili kusaidia kupunguza mzigo mkubwa kwa mfuko.

Mapendekezo yote haya yaliyotolewa na Kamati yetu na Serikali imekuwa ikiyafanyia kazi na hivyo kubuni vifurushi vipyta vikiwemo **DUNDULIZA** na **JIPIMIE** ambavyo vinawanufaisha wananchi. **Kamati inapongeza jitihada hizi.**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hayo, Kamati ilielezwa baadhi ya mafanikio ambayo NHIF imepata hadi sasa ni kuongezeka kwa idadi ya wanachama wa Mfuko kutoka wanachama **164,708** mwaka 2001/2002 hadi kufikia wanachama **873,012** sawa na **asilimia 8** ya watanzania wote, Utekelezaji wa mpango wa Tumaini la Mama unaolenga kutoa bima ya afya kwa akina mama wajawazito, watoto na familia zao na kuwekeza katika miundombinu ya kutolea huduma ikiwemo ujenzi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa-Dodoma na Taasisi ya Mifupa MOI awamu ya tatu.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mafanikio hayo ya Mfuko, Kamati ilielezwa kuhusu changamoto zinazoendelea kuukabili Mfuko ikiwemo, kukosekana kwa uhiari wa wananchi kujunga na Mfuko, kukosekana kwa huduma zinazolipiwa katika baadhi ya maeneo, watoa huduma kutotumia fursa ya mikopo itolewayo na Mfuko na kuongezeka kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambayo yanaongeza gharama kubwa kwa mfuko. **Kamati inaona kuwa kuna umuhimu na uharaka wa Serikali kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa wote ili wananchi wengi wawewe**

kujiunga na mfuko huu na kuwepo na uhakika wa upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wote nchini kama zilivyo nchi za Ghana na Rwanda ambapo baadhi ya Wajumbe wa Kamati walipata fursa ya kwenda kujifunza na kuona huduma za afya zilivyoboreshwu kutokana na uwepo wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote.

**b) Bohari Kuu ya Dawa (Medical Stores Department -MSD)**

**Mheshimiwa Spika**, Katika vikao vya Kamati vilivyoofanyika mwezi Oktoba 2018, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Bohari Kuu ya Dawa. Taarifa hiyo ilieleza Sheria inayompa mamlaka MSD kutekeleza majukumu yake (kifungu cha 3(2)). Aidha, kifungu cha 4 (2) cha Sheria ya MSD kinaeleza majukumu makuu ya MSD ambayo ni pamoja na kutengeneza, kusimamia na kuendesha mfumo wa kibashara wenye tija ya manunuvi, utunzaji na usambazaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa, MSD inahudumia jumla ya vituo vya kutolea huduma za afya vipatavyo **5,432** nchi nzima kuititia Bohari za Kanda nane (8) ambazo ni Kanda ya Dar es Salaam, Mtwara, Mbeya, Iringa, Dodoma, Tabora, Mwanza na Moshi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa baadhi ya mafanikio ambayo MSD imepata hadi sasa ambayo ni pamoja na ufikishaji wa dawa katika maeneo mengi ya nchi katika vituo vya kutolea huduma za afya, kuingia mikataba ya ununuvi wa dawa na wazalishaji moja kwa moja bila kuititia kwa mtu wa katika na kufanikisha kushusha bei baadhi ya dawa na kuongeza kiwango cha upatikanaji wa dawa muhimu hadi kufikia **asilimia 93** nchi nzima kwa mwaka 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa kwa sasa MSD inasambaza dawa zenye thamani ya shilingi **Bilioni 600** kwa Mwaka kwa nchi nzima. Aidha, kuhusu kuanzishwa kwa

mradi wa uzalishaji wa dawa kwa ushirikiano na Sekta binafsi, Waziri alieleza mchakato wake unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwaka huu 2019 ambao utawezesha kukuza uchumi wa nchi na kuongeza upatikanaji wa dawa kwa wakati. **Ni Imani ya Kamati kuwa mradi huu utaanza kama ambavyo Waziri alieleza na kutatua changamoto zitokanazo na uagizaji wa dawa nje ya nchi.**

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilielezwa juu ya changamoto kubwa ambayo MSD inakabiliwa nayo ya mtaji mdogo wa kununua dawa kutokana na ucheleweshwaji wa fedha za kununua dawa kutoka katika vituo vya kutolea huduma ya afya na kuongezeka kwa deni la Serikali linalofikia shilingi **Bilioni 200** ambazo linachangiwa na ununuzi wa Dawa na usambazaji wake. **Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha deni hili linalipwa mapema ili MSD iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.**

c) **Idara Kuu Maendeleo ya Jamii kuhusu Asasi zisizo za Kiserikali (AZAKI)**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya utekelezaji wa Asasi zisizo za kiserikali (AZAKI) iliwasilishwa katika kikao kilichofanyika Mwezi Oktoba, 2018. Kamati ilielezwa kuhusu chimbuko la Asasi hizo, Sera inayoongoza AZAKI ya mwaka 2001 na Sheria yake ya mwaka 2002.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa pia utaratibu wa usajili wa AZAKI ambao unafanyika katika Wizara mbalimbali ikiwemo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Viwanda na Biashara jambo ambalo Kamati inaona linaleta mkanganyiko.

**Mheshimiwa Spika**, AZAKI zimekuwa zikitekeleza majukumu mbalimbali katika jamii kama vile kuwezesha shughuli mbalimbali ikiwemo Afya, Kilimo, Maji na Elimu katika ujenzi wa majengo na uhamasishaji wa jamii kubadili tabia, ujenzi wa miundombinu ya maji, miundombinu ya elimu na

kutoa huduma kwa makundi maalumu wakiwemo watoto, wazee na wasiojiweza. Aidha, AZAKI zinatoa fursa za ajira kwa watanzania wapatao **3414** hadi kufikia 2015 na kuongezeka kwa mapato kila mwaka yatokanayo na fedha za ada na faini za Asasi hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mchango wa AZAKI kwa jamii ya Watanzania kumekuwa na changamoto mbalimbali zinazoikabili Wizara katika kuratibu shughuli za AZAKI. Changamoto hizo ni pamoja na kutegemea fedha za wafadhilli zenye masharti magumu, Mashirika mengi kufanya shughuli zake katika maeneo ya mjini, kukosekana kwa uwazi na uwajibikaji katika utendaji wa AZAKI na Wataalamu kutotumika katika upangaji na utekelezaji wa shughuli zao.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na changamoto hizo, Kamati ilielezwa kuwa, Wizara imeweka mikakati mbalimbali ya kukabiliana nazo ikiwa ni pamoja na kuimarisha Sheria ya AZAKI, kufanya mapitio ya Sera ya AZAKI na kuimarisha ushirikiano na vyombo vya dola jambo ambalo ni jema.

**d) Hospitali ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto (KDIH)**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 31 Agosti, 2018, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Hospitali ya Magonjwa ambukizi Kibong'oto ambayo ilianzishwa Mwaka 1926 katika Wilaya ya Siha Mkoa wa Kilimanjaro kwa lengo la kutoa huduma za Kifua Kikuu (TB). Mwaka 2010 Hospitali hiyo ilitangazwa kupitia gazeti la Serikali Namba 828 kuwa ni Hospitali maalumu ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi (*Kibong'oto Infectious Disease Hospital*).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa Majukumu makuu ya Hospitali ni pamoja na kufanya uchunguzi, tiba na ufuatiliaji wa magonjwa ya kuambukiza hasa TB, UKIMWI na Magonjwa ya Mapafu yasiyoambukiza, kutoa Mafunzo na tafiti kwa changamoto mbalimbali za afya hasa magonjwa ambukizi na mapafu yasiyoambukiza pamoja na

kufuatilia mwenendo wa magonjwa ya mlipuko na magonjwa yale ya kuambukiza.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa pamoja na hospitali hiyo kuwa Maalum Kitaifa kwa Magonjwa Ambukizi lakini haifahamiki kwa wananchi wengi. **Kamati inaona hali hii inaweza kufanya mapambano dhidi ya kifua kikuu kutofanikiwa mapema.**

### **2.1.2 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa kupokea na kujadili Taarifa za Utendaji wa Taasisi mbalimbali zikiwemo Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kama ifuatavyo: -

#### **a) Chuo Kikuu Kishiriki cha Mkwawa**

**Mheshimiwa Spika**, Mnamo tarehe 31 Oktoba, 2018 Wizara iliyasilisha Taarifa ya utendaji wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa-Iringa. Chuo hicho ambacho awali ilikuwa ni Shule ya Sekondari Mkwawa kilianzishwa rasmi tarehe 1 Septemba, 2005 kama sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam. Chuo kinatoa Shahada za awali ambazo ni Shahada ya Elimu ya Jamii na Ualimu (B.A. Ed), Shahada ya Elimu katika Elimu ya Jamii (B. A Ed. Arts), Shahada ya Elimu katika Sayansi (B.Ed.-Sc) na Shahada ya Sayansi na Ualimu (B. Sc – Ed). Aidha, Chuo kinatoa Shahada ya Uzamili/ Umahiri ya Elimu (*Postgraduates Diploma in Education*) na Shahada za Umahiri/Uzamili za Sayansi na Elimu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa juu ya Miradi ya Maendeleo ambayo inatekelezwa na Chuo. Miradi hiyo ni pamoja na:-

i) Mradi wa Ujenzi wa Ukumbi wa Mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1009 na ujenzi wake uliana mwaka 2008 kwa sasa umekamilika kwa **asilimia 91** na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Februari, mwaka huu 2019. Gharama za mradi ni shilingi **8,803,763,551.97**;

ii) Mradi wa Ujenzi wa Maabara za Sayansi zenyne uwezo wa kuchukua wanafunzi 270 kwa wakati mmoja kwa gharama ya shilingi **2,153,127,897.14**;

iii) Ujenzi wa Ofisi za Wahadhiri 20 zenyne uwezo wa kuchukua wahadhiri 40 kwa gharama ya shilingi **323,833,786.27** ambao umekamilika tangu tarehe 28 Agosti, 2018;

iv) Mradi wa Uchimbaji wa Kisima cha maji ambao ulianza Septemba 2017 na kukamilika Novemba 2017 kwa gharama ya shilingi **103,990,000**. Kisima kimoja kina uwezo wa kuzalisha lita za ujazo 3000 kwa saa na Chuo Kinaendelea kukamilisha uwekaji wa miundombinu kama mabomba, ujenzi wa matenki na ufungaji wa pampu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi inayoendelea chuoni hapo, Kamati ilielezwa kuhusu changamoto ambazo chuo inakumbana ambazo ni kutowajibika kikamilifu kwa Mkandarasi wa ujenzi wa Jengo la Mihadhara hali inayochewesha ukamilikaji wa mradi na upungufu wa miundombinu (Kumbi za mihadhara, ofisi za wahadhiri, maktaba na mabweni). **Kamati inaona ni vyema sheria ikachukua mkondo wake hasa kwa mkandarasi ambaye ameshindwa kutimiza wajibu wake.**

b) **Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli za Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere mnamo tarehe 1 Novemba, 2018. Taarifa ya Chuo ilieleza kuhusu Chimbuko la chuo ambacho kilianzishwa rasmi tarehe 29 Julai, 1961. Aidha, kuanzia Mwaka 1971 hadi 1992 Chuo hicho kilijulikana kama Chuo cha Chama na kuanzia 1992 hadi 2005 kilikuwa kikijulikana kama Chuo cha Sayansi Jamii Kivukoni na mnamo tarehe 01 Oktoba, 2005 Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu kilianzishwa rasmi chini ya Sheria ya Bunge Na. 6 ya Mwaka 2005.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa, chuo kina majukumu mbalimbali yakiwemo ya utoaji mafunzo katika fani za Sayansi Jamii kwa kiwango cha Cheti, Stashahada na Shahada, kutoa mafunzo ya Uongozi (*Leadership*), kuendesha mafunzo ya Elimu ya kuijendeze na kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa sekta za umma na binafsi.

**Mheshimiwa Spika**, Kuhusu utekelezaji wa malengo kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017 hadi sasa, Kamati ilielezwa kuwa, chuo kimefanya kazi mbalimbali licha ya changamoto ya fedha hususan fedha za Miradi ya Maendeleo. Malengo yaliyotekelzeza na chuo kwa kipindi hicho ni pamoja na;

- i) Kuinua ubora wa Elimu na mafunzo katika taasisi kwa kuboresha mazingira kwa kufunga vifaa vya kisasa vya kufundishia;
- ii) Kugharamia uandaaji wa mitaala na ununuzi wa samani na vifaa mbalimbali; na
- iii) Kumalizia ujenzi wa Jengo la Hosteli Kampasi ya Kivukoni na Ukumbi wa Mihadhara na kuongeza udahili kwa wanafunzi wapya 2900.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na malengo hayo yaliyotekelzeza na Chuo, Kamati ilielezwa juu ya changamoto kuu tatu zinazokikumba Chuo kuwa ni uchakavu wa miundombinu (nyumba za watumishi, majengo na barabara), uhaba wa Ofisi za Watumishi na madarasa ya kufundishia na uhaba wa hosteli za wanafunzi katika Kampasi ya Zanzibar kwani hakuna hosteli katika eneo la chuo jambo ambalo Kamati inaona linaathiri maendeleo na upanuzi wa chuo.

### **2.1.3 Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Taasisi mbili zilizo chini ya usimamizi wa Wizara hii.

a) Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA)

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa kuhusu utendaji wa Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) iliwasilishwa na kujadiliwa na Kamati mnamo tarehe 29 Oktoba, 2018. BAKITA ambayo imeanzishwa mwaka 1967 kwa Sheria ya Bunge Na. 27 ni chombo cha Serikali katika kusimamia maendeleo na matumizi ya Kiswahili kitaifa na Kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, BAKITA ina jukumu la ukuzaji na usambazaji wa misamiati na istilahi, usimamiaji wa matumizi fasaha na sanifu ya Kiswahili, utoaji na uimarishaji huduma ya tafsiri na ukalimanu na uandaaji wa mazingira wezeshi kwa ajili ya kubidhaisha Kiswahili.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na majukumu hayo, Kamati ilielezwu kuhusu masuala mbalimbali kama vile Kanzidata (*Database*) kwa ajili ya kusajili na kutunza kumbukumbu za Wataalamu wa Kiswahili imeanzishwa na hadi kufikia mwezi Oktoba, 2018 tayari wataalamu wa kiswahili 270 wamesajiliwa, Mradi wa kuunda Kongoo ya Kiswahili umeanza kutekelezwa; na Baraza limeanza kuandaa machapisho yatakayosaidia kuendeleza Kiswahili Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwu baadhi ya changamoto ambazo BAKITA inakumbana nazo ikiwa ni pamoja na;

i) Kutokuwa na Mamlaka ya Kisheria ya kutoa adhabu kwa wanaokiuka maelekezo na matamko mbalimbali ya Serikali kuhusu matumizi na Maendeleo ya Kiswahili;

ii) Kutotumika kwa lugha ya kiswahili katika Elimu jambo linalofanya istilahi zilizoundwa na kuratibiwa na Baraza kubaki katika mashubaka;

iii) Baadhi ya nyaraka za Serikali kutopitishwa BAKITA kwa ajilli ya kuthibitisha lugha;

iv) Ufinyu wa Bajeti unaokwamisha utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Taasisi na Uhaba wa Watumishi. Kamati inatambua kuwa bajeti ya Taasisi imekuwa ikitegemea ruzuku ya Serikali pamoja na mapato ya ndani. Hata hivyo, imebainika kuwa kuanzia mwaka 2014 – 2018 hakuna fedha iliyotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo licha ya kuwa Bunge lako Tukufu limekuwa likiidhinisha fedha hizo. **Kamati imesikitishwa sana na hali hii.**

## **2.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, inazipa majukumu Kamati za Kudumu za Kisikta ikiwemo Kamati ya Huduma na Maendeleo ya jamii kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha (2017/2018) iliyo chini ya Wizara zinazozisimamiwa na Kamati.


**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza kanuni hiyo, Kamati ilipata fursa ya kutembelea jumla ya miradi mitano (5) iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2017/2018 iliyokuwa inatekelezwa katika mkoa wa Iringa na Mbeya. Miradi hiyo ni pamoja na;

- a) Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii – Rungembba, Mufindi -Iringa (**Namba ya Mradi 6330**);
- b) Mradi wa Ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii – Uyole (**Namba ya Mradi 6330**);
- c) Mradi wa Hospitali ya Kanda Mbeya (**Namba ya Mradi 5422**);
- d) Mradi wa Upanuzi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkawawa (**Namba ya Mradi – 4314**) ; na
- e) Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (**Namba ya Mradi 6333**).

**Mheshimiwa Spika**, hadi Kamati inatembelea na kukagua Miradi hiyo, hakuna hata mradi mmoja uliokuwa umeperekewa fedha licha ya fedha kuidihinishwa na Bunge

Iako Tukufu kiasi cha shilingi **Bilioni 6.832** kama ilivyoelezwa kwenye Taarifa ambayo Kamati iliwasilisha mwezi Mei, 2018 wakati wa uchambuzi wa Bajeti. Hali ya upatikanaji wa fedha ni kama ambavyo imeoneshwa katika Kielelezo Na.1

**Kielelezo Na.1: Hali ya upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo 2017/2018**



*Chanzo: Taarifa ya Wizara na Usanifu wa Kamati*

**2.3 Kupokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na wa Fedha wa 2017/2018 na mchakato wa Bajeti za Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati ilikutana katika vikao vyake na Wizara inazosimamia kwa ajili ya kujadili taarifa ya utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati katika vikao vya uchambuzi wa Bajeti za Wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2017/2018, pamoja na makadirio ya Mapato na Matumizi

ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Taarifa juu ya utekelezaji huo ziliwasilishwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ambayo Kamati ilikuwa imeyatoa kwa Wizara inazozisimamia ulikuwa unategemea kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa fedha. Kama ambavyo imeelezwa awali, hali ya upatikanaji wa fedha imekuwa ni changamoto inazozikabili Wizara zote na hivyo kuathiri utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo mengi ya Kamati. Baadhi ya Maoni ambayo Kamati inaona ni ya msingi na bado mpaka sasa hayajatekelezwa ipasavyo ni pamoja na:-

· Tuzo ya Udhagini (*Scholarship Award*) hasa kwa wanafunzi wanaofanya vizuri katika masomo ya kidato cha sita ambayo Kamati ilipendekeza iitwe *Magufuli Scholarship Award*:

- Uainishaji wa Vyuo Vikuu (*University Classification*) kulingana na ubora wake kutokana na kuendelea kuibuka kwa vyuo vingi hapa nchini;
- Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote (*Universal Health Coverage Bill*) kuletwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaisisitiza na kuendelea kuishauri Serikali maeneo haya na yale yote iliyoyapendekeza katika Taarifa zake za awali iyafanyie kazi.**

## **2.4 Kupokea na kujadili Taarifa za Wizara na Taasisi zake kuhusu Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba 2018)**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha tarehe 14 hadi 25 Januari, 2019, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa za utekelezaji wa majukumu na Bajeti za Wizara na Taasisi inazozisimamia kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba, 2018) kama ifuatavyo:-

### **2.4.1 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto**

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 14 Januari, 2019, Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto iliwasilisha Taarifa yake ya utekelezaji wa majukumu na


Bajeti za Wizara na Taasisi inazozisimamia kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba,2018) ambayo ilipokelewa, kuchambuliwa na kujadiliwa na Kamati. Katika Taarifa hiyo Wizara ilieleza majukumu mbalimbali yaliyotekelawa, na **Fungu 52 (Idara Kuu Afya)**, baadhi ya majukumu hayo ni pamoja na Mpango wa Taifa wa chanjo umefikia asilimia 97, Afya ya Uzazi na Mtoto imefikiwa kwa **asilimia 59** ikilinganishwa na **asilimia 48** mwaka 2017, upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba hususan dawa muhimu katika vituo vya afya umefikia asilimia 96.7, pamoja na chupa za damu salama zilizokusanywa ni 158,755 kati ya 375,000 zilizopangwa sawa na **asilimia 42.3** ya lengo. **Kamati inapongeza jithada hizi.**

**Mheshimiwa Spika**, ukusanyaji wa maduhuli umetekelezwa kwa **asilimia 52** (153,520,009,883/= kati ya 297,013,657,702/= zilizokadiriwa). Kamati inapongeza Wizara kwa ukusanyaji huu mzuri wa maduhuli na ni matumaini ya Kamati kuwa ukusanyaji utafika asilimia 100 ifikapo mwisho wa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019.

Aidha kuhusu upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini

vani ni **asilimia**  
fikia Disemba,  
Ja. 2.

*/a Fedha kwa*




*Chanzo: Taarifa ya Wizara na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **Fungu 53 (Idara Kuu Maendeleo ya Jamii)**, Wizara ilieleza majukumu yaliyotekelawa kuwa ni pamoja na kusimamia utoaji wa mafunzo ya Taaluma ya Maendeleo ya Jamii ambapo wanafunzi 2,677 wamedahiliwa hadi kufikia Disemba, 2018 vikundi vyat malezi 1,184 kwenye Halmashauri 15 vimeanzishwa ili kuimarisha upatikanaji wa haki na maendeleo ya mtoto, wazee wasiojiweza 247,771 wamepata vitambulisho vyat matibabu na jumla ya mashirika yasiyo ya kiserikali 518 yamesajiliwa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Taarifa hiyo ya utekelezaji wa majukumu, Kamati ilieleza katika **Fungu 53** ukusanyaji wa maduhuli hadi kufikia Disemba 2018 ulikuwa ni shilingi **1,172,961,441/=** kati ya **3,090,796,000/=** sawa na **asilimia 37.9**. Kamati inashauri **Wizara iongeze jitihada za ukusanyaji wa maduhuli**. Aldha, upatikanaji wa fedha hadi kufikia Disemba 2018 ni **asilimia 39.7** kama inavyoonekana katika kielelezo Na.3

#### Kielelezo Na.3 : Hali ya upatikanaji wa Fedha kwa Bajeti ya 2018/2019 (Fungu 53)



*Chanzo: Taarifa ya Wizara na Usanifu wa Kamati*

**a) Hospitali ya Taifa Muhimbili**

**Mheshimiwa Spika**, katika vikao vyake vya mwezi Januari, 2019. Kamati ilipokea na kujadili Tarifa ya Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) ambayo imeanzishwa kwa Sheria Na. 5 ya Bunge ya Mwaka 2000 ikiwa ni Mrithi wa lilitokuwa Shirika la Afya Muhimbili.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa katika nusu ya kwanza ya mwaka 2018/2019 kazi mbalimbali zilipangwa na zimeteklezwa. Baadhi ya kazi hizo ni pamoja na kutoa na kuboresha huduma za kibingwa ambapo wagonjwa 274,776 wameonwa, kutoa huduma za tiba kwa wagonjwa 159,663 wakiwemo 30,189 wa magonjwa ya dharura, upasuaji kwa wagonjwa 8,747 umefanyika, wagonjwa 31,206 wamepata huduma za radiliojia (*CT-Scan, Ultrasound na MRI*), Wagonjwa 19 wamepata huduma ya kupandikizwa figo hali iliyosadia pia kuokoa gharama za kupeleka wagonjwa nje ya nchi pamoja na kukamilisha kazi ya uboreshaji wa jengo la upasuaji kutoka vyumba 13 hadi 19.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi cha nusu mwaka, Hospitali imepata **asilimia 73.3** ya bajeti (**59,038,846,864/=** kati ya **87,141,998,341/=**). Kwa mwenendo huu Kamati ina amini lengo litafikiwa ifikapo mwisho wa mwaka.

**b) Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) katika vikao vyake vya Mwezi Januari, 2019. Taasisi ambayo ni Maalum kwa tiba ya magonjwa ya moyo imeanzishwa Septemba, 2015.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai – Disemba, 2018, JKCI ilipanga na kutekeleza shughuli mbalimbali. Baadhi ya kazi zilizoteklezwa ni pamoja na kuajiri Watumishi 10, wagonjwa 44,250 walihudumiwa, upasuaji wa wagonjwa 211 ulifanyika, upasuaji wa moyo kuititia tundu dogo (*catheterization laboratory*) ulifanyika kwa wagonjwa 521, wodi mpya ya watoto imeanzishwa ikiwa na vitanda 32 pamoja kufanya kambi 20 sehemu

mbalimbali nchini kwa kushirikiana na Taasisi nyingine na Mashirika mbalimbali duniani.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa hali ya bajeti siyo mbaya kwani hadi kufikia Disemba, 2018, JKCI imepata shilingi **11,942,393,915/=** katи ya **22,911,630,045/=** sawa na **asilimia 52.1** ya bajeti. **Kamati inashauri jitihada hizi ziendlee.**

**c) Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) katika vikao vya mwezi Januari, 2019. Katika Taarifa hiyo, Kamati ilielezwa kuwa kwa kipindi cha Nusu Mwaka MOI imefanikiwa kutoa matibabu kwa wagonjwa 102,820 wakiwemo wa wagonjwa wa upasuaji 3,024; kuimardha upasuaji wa mgongo kwa tundu dogo (minimum invasive spine surgery) baada ya kununua darubini ya kisasa na seti maalum ya kufanya upasuaji huo; wagonjwa 55,920 walipatiwa huduma za tiba mazoezi (*physiotherapy*) ikilinganishwa na wagonjwa 44,568 wa Disemba 2017 ongezeko la **asilimia 20**. **Kamati inapongeza jitihada hizi**. Aidha, kuhusu upatikanaji wa damu salama, jumla ya chupa 3911 zilikusanywa katи ya hizo chupa 3698 (94.5%) zilikuwa salama na 213 hazikuwa salama.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu suala la bajeti, kiasi kilichopatikana ni shilingi **9,292,847,124/=** katи **16,923,352,451/=** sawa na **asilimia 54.9**. **Kamati inapongeza Serikali kwa utoaji mzuri wa fedha na inashauri utaratibu huu mzuri uendeleee.**

**d) Mamlaka ya Chakula na Dawa**

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 17 Januari, 2019, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na Bajeti ya Mamlaka hiyo ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura 219 na inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala za Serikali , Sura 245 na Marekebisho yake ya Mwaka 2009.

**Mheshimiwa Spika**, Katika wasilisho hilo, Kamati ilielezwa kuwa kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2018, Mamlaka imetekeleza majukumu mbalimbali. Baadhi ya majukumu hayo ni pamoja na kusajili maeneo na kutoa vibali vya biashara ya chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi ambapo maombi 3281 ya usajili wa maeneo ya biashara ya dawa, vipodozi na vifaa yalipokelewa na kati ya hayo maombi **3203** sawa na **asilimia 98** ya maombi yaliidhinishwa, imeteketeza bidhaa zisizokidhi ubora na usalama wa mlaji ambapo jumla ya tani **453.6** za bidhaa zenye thamani ya shilingi **Bilioni 6.94** zilitketezwa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na utekelezaji wa majukumu, Kamati pia ilielezwa kuhusu utekelezaji wa bajeti ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa maduhuli ulikuwa ni shilingi **22,071,294,712** sawa na **asilimia 41** ya lengo la kukusanya **53,310,168** kwa Mwaka, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mishahara umekuwa ni **asilimia 12 (1,446,740,275/=)** ya kiasi kilichoidhinishwa cha shilingi **6,745,600,534/=**. Kamati imesikitishwa na hali hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuhusu changamoto ambazo Mamlaka inakumbana nazo na mbinu za kukabiliana nazo ikiwemo changamoto ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Sura 219 kuitwa na wakati na hivyo kushindwa kukidhi mahitaji ya sasa ya udhibiti ambapo maandalizi ya mapendekezo ya mapitio ya Sheria kwaajili ya Waraka wa Baraza la Mawaziri kuridhia umekamilika. **Kamati inaitaka Wizara kuharakisha kuleta mapendekezo ya marekebisho hayo ili Bunge liweze kufanya kazi na hatimaye kuwa na sheria yenye tija na inayoendana na wakati.**

e) **Taasisi ya Ustawi wa Jamii**

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Ustawi wa Jamii ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 26 ya Mwaka 1973 kwa lengo la kutoa mafunzo, kufanya tafiti na ushauri weledi katika maeneo ya ustawi wa jamii, maendeleo ya jamii na taaluma zinazoshabihiana na ustawi wa jamii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuhusu majukumu yaliyopangwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha wa 2018/2019 yaklwemo:-

- i) Kutoa mafunzo bora ya kitaaluma ambapo wanafunzi **1,064** walidahiliwa ikilinganishwa na **1,185** ya mwaka 2017/2018;
- ii) Kuimarisha mifumo ya tafiti, ushauri weledi na mafunzo ya muda mfupi ambapo Tafiti mbili zinazohusu masuala ya ustawi wa jamii zimefadhliliwa na chuo; na
- iii) Kuwezesha utawala bora na kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia ambayo yametekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu mwenendo wa Bajeti, Kamati imebaini kuwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Taasisi ilikadiria kukusanya kiasi cha shilingi **10,403,984,423/=**. Hadi kufikia Disemba 2018, makusanyo yalikuwa ni **2,900,920,291/=** sawa na **asilimia 27.8 tu** ya Bajeti. Aidha, kwa upande wa upatikanaji wa fedha za Mishahara kutoka Serikalini, Taasisi ilipokea kiasi cha shilingi **1,476,990,000/=** sawa na asilimia **29.2** ya kiasi cha shilingi **5,054,574,423/=** kilichoidhinishwa na Bunge. **Kamati inaona kwamba kwa mwenendo huu ni vigumu kufikia malengo na hivyo kuitaka Taasisi kuongeza juhud za makusanyo ya maduhuli lakini pia Serikali kuhakikisha inaipatia fedha Taasisi hii kama zilivyoidhinishwa na Bunge.**


#### **2.4.2 Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

**Mheshimiwa Spika**, kikao cha kujadili Taarifa ya Wizara hii kilifanyika tarehe 18 Januari, 2019. Katika kipindi cha Julai – Disemba, 2018 Wizara ilipanga kutekeleza kazi mbalimbali. Hadi kufikia Mwezi Disemba, 2018, Wizara iliratibu vipindi 17 vyenye kuelimisha Umma, Magazeti mapya 7 yalisajiliwa na leseni za magazeti 59 zilihuishwa pamoja na vitambulisho (*press cards*) 54 vilitolewa kwa Waaandishi wa Habari. Aidha, Wizara iliratibu maandalizi ya Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa Vijana wenyewe umri chini ya miaka 17 (AFCON U -17) yatakayofanyika mwezi April, 2019.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na taarifa hiyo ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Kamati ilielezwa ukusanyaji wa maduhuli ambapo ilikadiriwa kiasi cha shilingi **1,077,804,000/=**. Hadi kufikia Disemba, 2018 Wizara ilikuwa imekusanya **516,548,949/=** sawa na **asilimia 47.9** ya lengo. **Kamati inapongeza Wizara na inashauri jithada ziendelee ili kufikilia lengo la mwaka.**

**Mheshimiwa Spika**, hali ya upatikanaji wa fedha ni **asilimia 48** kama inavyoonekana katika Kielelezo Na.4.

#### **Kielelezo Na.4: Hali ya Upatikanaji wa Fedha kwa Bajeti ya 2018/2019 (Fungu 96)**



*Chanzo: Taarifa ya Wizara na Usanifu wa Kamati*

a) **Taasisi ya Sanaa na Utamaduni (TASUBA)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Taasisi ya Sanaa na Utamaduni (TASUBA) katika vikao vya Mwezi Januari, 2019. Taasisi hii ambayo ni Wakala wa Serikali ilianzishwa Mwaka 1997 na ilitokana na kilichokuwa Chuo cha Sanaa Bagamoyo.

**Mheshimiwa Spika**, TASUBA ni moja kati ya Taasisi tatu zilizoteuliwa kuwa kituo chenye ubora uliotukuka (*Centre of Excellence*) ili kuendesha mafunzo ya sanaa na utamaduni kwa Wasanii wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, kukuza Sanaa na utafiti kwenye eneo la utamaduni pamoja na kuratibu na kuendesha Tamasha la Sanaa na Utamaduni.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba 2018) TASUBA ilitekeleza majukumu mbalimbali yakiwemo ya kufundisha wanachuo 249 kwa kozi mbalimbali, kuendesha Tamasha la 37 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo mnamo mwezi Oktoba 2018 lililohudhuriwa na watu wapatao 58,000 na vikundi 89 vikiwemo kutoka Kenya, Finland, Ujerumanu na Zimbabwe.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu Bajeti, Kamati ilielezwa kwa kipindi cha nusu Mwaka imefanikiwa kukusanya maduhuli ya shilingi **249,472,100/=** sawa na **asilimia 58.4** ya kiasi cha shilingi **427,000,000/=** kilichopangwa kukusanya kwa Mwaka. Kwa upande wa mishahara, kiasi kilichopokelewa ni **488,045,000/=** sawa na **asilimia 30.7** ya kiasi cha shilingi **1,589,232,000/=** kilichopangwa. Aidha, kuhusu Fedha za matumizi mengineyo (OC) jumla ya shilingi **9,670,000/=** zilipokelewa kati ya **23,213,000/=** zilizopangwa sawa na **asilimia 41.6**. Hakuna fedha iliyotengwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. **Kamati imesikitishwa kuona pamoja na umuhimu wake bado Taasisi hii haitengewi fedha za kutosha na hata za miaka ya nyuma hususan za miradi ya maendeleo mpaka sasa hazijatolewa licha ya ushauri wa Kamati wa mara kwa mara.**

**b) Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC)**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 21 Januari, 2019 Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na bajeti kwa kipindi cha Nusu Mwaka. TBC ambayo imeanzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 186 la Mwaka 2007 ina jukumu la kutoa habari mbalimbali kwa umma, kuburudisha na kuelimisha.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha nusu ya kwanza ya Mwaka wa Fedha wa 2018/2019, TBC ilipanga kutekeleza majukumu mbalimbali yakiwemo ya Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu Dodoma ambapo Michoro ya Jengo imekamilika na kuidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi wa TBC, ukarabati wa Studio za Redio na Televisheni Makao Makuu – Dodoma ambao unaendelea, kuanzisha chaneli ya Utalii ambayo ilizinduliwa na Waziri Mkuu tarehe 15 Disemba, 2018, ununuzi wa magari 11 na kibali chake kimeshatoka pamoja na kukamilisha miradi ya usikivu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuhusu hali ya upatikanaji wa fedha yenye kuonesha ukusanyaji wa maduhuli umekuwa ni shilingi **3,300,960,057/=** kati ya shilingi **11,940,540,000/=** zilizopangwa sawa na **asilimia 27.6** tu. Aidha, kuhusu Mishahara, TBC ilipokea shilingi **4,478,125,720/=** sawa na asilimia **56.4** ya kiasi cha shilingi **7,928,824,000/=** zilizoidhinishwa na Matumizi mengineyo asilimia **31.6 (1,330,000,000/=)** kilipokelewa kati ya **4,200,000,000/=** kilichoidhinishwa. Kwa upande wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo, shilingi **2,500,000,000/=** sawa na **asilimia 50** ya shilingi **5,000,000,000/=** kilichotengwa kimepokelewa. Kamati inashauri fedha hizi ziendelee kutolewa ili ifikapo mwisho wa mwaka, fedha zote ziwe zimetolewa.

**c) Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) katika vikao vyake vyia mwezi Janauri, 2019. BASATA ilianzishwa kwa Sheria Na. 23 ya Mwaka 1984 ambayo pia ilielezwa kuwa imepitwa na wakati.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai – Disemba, 2018 BASATA imetekeleza shughuli mbalimbali zikiwemo kufanya usajili wa wasanii na wadau 845 nchini, kuendesha mafunzo kwa viongozi wa vyama na vikundi vya wasanii na wadau wa Sanaa wapatao 60, midahalo 29 ya jukwaa la Sanaa katika mikoa 13 ya Tanzania Bara iliendeshwa, jumla ya kazi za muziki zipatazo 256 zilihakikiwa na kupewa idhini ya kutumika katika jamii, vikao na Maafisa Utamaduni 152 katika Halmashauri 51 vimefanyika na kufanya vikao vya kujenga uelewa juu ya Kanuni Na. 43 za Mwaka 2018 kwa wasanii na wadau wa Sanaa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla bajeti iliyopokelewa ni **asilimia 45** ya fedha iliyoidhinishwa (**457,954,250/=** kati ya **1,012,277,000/=**) ikiwa na mchanganuo wa Maduhuli yaliyokusanywa kiasi cha shilingi **190,858,250/=** kati ya shilingi **478,080,000/=** zillizopangwa kukusanywa sawa na **asilimia 39.9**. Fedha za Mishahara zilizopokelewa ni shilingi **255,492,000/=** sawa na **asilimia 50** ya shilingi **510,984,000/=** zilizoidhinishwa. Aidha, kwa upande wa matumizi mengineyo (OC) kiasi cha shilingi **11,604,000/=** sawa na **asilimia 49.9** cha shilingi **23,213,000/=** kilichotengwa kilipokelewa. Kama ilivyokuwa kwa TASUBA, **hakuna fedha iliyotengwa kwaajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo**.

#### **2.4.3 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**


**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa ya Wizara hii pamoja na taasisi zake mnamo tarehe 22 Januari, 2019. Katika Taarifa hiyo, Kamati ilielezwa kuhusu majukumu mbalimbali yaliyotekelezwa na Wizara kwa kipindi cha Nusu Mwaka wa Fedha wa 2018/2019. Baadhi ya majukumu hayo ni pamoja na kusimamia Ithibati na uthibiti shule ambapo jumla ya shule 163 zimesajiliwa zikiwemo shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu na kubaini upungufu wa walimu katika shule za msingi na uhaba wa miundombinu kutokana na kuongezeka kwa wanafunzi (Elimu bila malipo).

Aidha, Asasi 11,327 zimekaguliwa, Vyuo 20 vya Maendeleo ya Wananchi vimewekewa samani, Wizara imeandaa na kuzindua Mwongozo wa kutambua na

kuendeleza ugunduzi, ubunifu na maarifa pamoja na kuanza Ujenzi wa Ofisi ya Wizara Jijini Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa utekelezaji wa Bajeti, ukusanyaji wa maduhuli umefanyika kwa **asilimia 47 (216,582,868,016/=** katи ya **460,011,442,840/=**). Aidha, kuhusu upatikanaji wa fedha, hadi kufikia Disemba 2018 Wizara ilikuwa imepokea **asilimia 43.9** ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 5.

**Kielelezo Na. 5 Hali ya upatikanaji wa fedha kwa Bajeti ya 2018/2019 (Fungu 46)**



*Chanzo: Taarifa ya Wizara na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwenendo huu wa ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa fedha ni imani ya Kamati kuwa hadi kufikia mwisho wa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019 mafanikio yatakuwa zaidi ya asilimia 90.

a) **Chuo Kikuu cha Dodoma;**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) katika vikao vyake vya Mwezi Januari, 2019. Katika Taarifa hiyo, Kamati ilielezwa majukumu mbalimbali yaliyotekerezwa na Chuo ikiwa ni pamoja na kudahili wanafunzi 11,854 sawa na asilimia 96.6 ya lengo la kudahili wanafunzi 12,269, kufanya tafiti 2, kutoa huduma za ushauri elekezi 11, kuboresha mahusiano (*collaborations*) na Taasisi 53 za Kitaifa na Kimataifa, kununua magari 8 kati ya 10 yaliyopangwa kununuliwa na kukarabati majengo ya Chuo.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu bajeti, Kamati ilielezwa kuwa Chuo hakijatengewa fedha za maendeleo hali inayoathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo ukiwemo wa ukamilishaji wa ujenzi wa chuo ili kufikia lengo la kudahili wanafunzi 40,000. Aidha, Kamati ilielezwa changamoto ya uhaba wa watumishi ambapo mahitaji halisi ni watumishi 2066 lakini waliopo ni watumishi 1436 sawa na **asilimia 69.5** tu ya lengo. **Kamati inaona kuna umuhimu wa kuongeza idadi ya watumishi kwa Chuo hiki.**

b) **Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu**

**Mheshimiwa Spika**, katika vikao vyake vya Mwezi Januari, 2019 Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa kipindi cha nusu mwaka. Katika taarifa hiyo, mambo kadhaa yalibainika ikiwemo:- wanafunzi 40,114 walipatiwa mikopo kati ya wanafunzi 57,000 waliokuwa na vigezo kutokana na ufinyu wa bajeti, ukusanyaji wa mikopo umefikia **Bilioni 94**, wanufaika wapya 12,612 wamebainiwa na kuongeza idadi ya wanaolipa mikopo kufikia 207,319. Aidha, kuhusu ukusanyaji wa mikopo, hadi kufikia Disemba, 2018

Bodi ilikusanya **asilimia 63** ya lengo (**492,226,037,371/=** kati ya **784,020,977,577/=**).

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu upatikanaji wa bajeti, Bodi imepokea **240,829,473,494/=** kati ya **427,554,000,000/=** sawa na **asilimia 56.3** ya lengo. **Kamati inapongeza Serikali kwa utoaji huu mzuri wa fedha hali ambayo inasaidia wanafunzi kupata mikopo kwa wakati, ni maoni ya Kamati kwa Serikali kuongeza fedha kwa bodi ya Mikopo ili kuweza kuwalipia wahitaji waliobaki.**

c) **Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kwa kipindi cha nusu mwaka katika vikao vyake vya Mwezi Januari, 2019.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa majukumu ambayo Tume ilipanga kuyatekeleza na namna ilivyoyatekeleza, baadhi ya majukumu hayo ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya utafiti zikiwemo Maabara za utafiti wa Taasisi za Utafiti wa Mifugo Tanga, Uyole na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi wa TAFIRI Musoma, kufadhili miradi 10 ya utafiti katika maeneo ya vipaumbele vya Taifa ikiwemo Viwanda, kusambaza matokeo ya utafiti ambapo vipindi na makala 42 yaliandaliwa na kusambazwa katika Redio na Televisheni.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na utekelezaji huo wa majukumu, Kamati ilichambua hali ya upatikanaji wa fedha ambapo ilibainika kuwa kwa ujumla Tume imepokea **asilimia 53** ya bajeti yake (**15,475,438,936/=** kati ya **29,468,130,633/=**). **Kamati inapongeza jitihada hizi ingawa bado fedha hizi zinazoidhinishwa ni kidogo na haziendani na majukumu makubwa ya Taasisi hii. Aidha, Kamati imesikitishwa na Taasisi hii muhimu kuondolewa chanzo chake kingine cha fedha zitokanazo na Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano ya Simu (Tele-Traffic Monitoring System).**

## **2.5 Kupokea Taarifa Mahsus**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa mahsusini mbili kama ifuatavyo:-

### **2.5.1 Taarifa ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kuhusu uanachama wa baadhi ya Taasisi za Serikali hususan Benki Kuu ya Tanzania (BOT)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kufuatilia suala la uanachama wa baadhi ya Taasisi za Serikali ikiwemo Benki Kuu ya Tanzania. Itakumbukwa kuwa Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Sura ya 395, inataka Watumishi wote wa Umma kuandikishwa na kunufaika na huduma zitolewazo na Mfuko huu kwa mujibu wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Mei 2018, watumishi wengi walikuwa tayari wamejiunga kwa zaidi ya **asilimia 99** kama ilivyo katika Sheria wakiwemo Watumishi kutoka Wizara, Idara, Taasisi na Mashirika ya Umma isipokuwa Benki Kuu ambayo ni Taasisi ya Serikali. Benki Kuu ilikuwa inataka huduma za ziada ambazo zilipaswa kulipiwa kwa malipo ya ziada. Kwa maelezo ya Wizara ni kuwa kama Benki Kuu wangejiunga na NHIF gharama yao ingekuwa kiasi cha shilingi **3,466,768,226/= (Premium)** kwa mwaka kwa huduma za kawaida kama watumishi wa taasisi nyingine. Lakini kwa kuwa Benki Kuu ilikuwa na mahitaji maalum kwa maana ya kuhitaji huduma za ziada jumla ya Shilingi **1,838,439,986/=** zingehitajika kwa ajili ya kupata huduma hizo.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilitoa ushauri mzuri ambao ulifanyiwa kazi na Serikali na suala hili la BOT kujunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) limefanikiwa na kwa sasa BOT ni wanachama wa NHIF.

## **2.5.2 Taarifa kuhusu Visimbuzi**

**Mheshimiwa Spika**, Katika vikao vya mwezi Agosti, 2018 Kamati ilikutana na wadau mbalimbali wanaomiliki vyombo vya habari na wale wanaotoa huduma ya habari kupitia visimbuzi wakiwemo Startmedia, ZUKU, AZAM Media kwa ajili ya kujadili kusitishwa kwa urushaji wa maadhui

kupitia baadhi ya vituo vya ndani ya nchi (*local channels*) vya kurushia matangazo kufuatia tamko la Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliona busara ya kukutana na wadau hao pamoja na Serikali ili kupata taarifa kutoka kwa pande zote mbili ili Bunge kupitia Kamati kuweza kuwa katika nafasi nzuri ya kuishauri Serikali namna ya kutatua changamoto hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na wadau kwa wakati wake na baadae ikakutana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambayo ndiyo yenye dhamana ya Habari kwa maana ya Maudhui pamoja na Wizara ya Uchukuzi na Mawasiliano (TCRA) ambao ndiyo Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano kwa maana ya miundombinu ya Habari.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kulitafutia ufumbuzi suala hili ili.**

## **2.6 Uchambuzi wa Miswada na Mikataba ya Kimataifa (Maazimio)**

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi hiki, Kamati ilichambua Muswada mmoja wa Sheria kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane (7) biliyo chini ya kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016. Muswada huo uliojulikana kama Muswada wa Sheria ya Bodi ya Taaluma ya Ualimu Tanzania wa Mwaka 2018 (*The Tanzania Teacher's Professional Board Bill, 2018*) ulichambuliwa kwa takribani siku 5 zilizojumuisha kukutana na wadau.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu wa Sheria ya Bodi ya Taaluma ya Walimu Tanzania ulichambuliwa na Kamati katika vikao vya mwezi Agosti, 2018 kwa kufuata taratibu zote za ushirikishwaji wa wadau mbalimbali wa masuala ya taaluma ya ualimu ili kuisaidia Kamati katika kufanya uchambuzi ulio makini ili kuweza kutunga sheria yenye tija.

Baada ya uchambuzi wa Muswada, Kamati iliwasilisha taarifa ya Maoni na mapendekezo kuhusu Muswada huo mbele ya Bunge lako Tukufu mnamo tarehe 5 Septemba, 2018.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa uwepo wa Sheria hii utasaidia kusimamia taaluma ya ualimu kwa weledi mkubwa na kuimarisha taaluma ya ualimu na kuipa heshima yake. **Ni maoni ya kamati kuwa Serikali itafanya jukumu lake la kuhakikisha Waziri mwenye dhamana anatunga Kanuni mbalimbali ili iweze kuanza kutumika kwa manufaa ya wenye taaluma ya ualimu pamoja na taifa zima kwa ujumla.**

## **2.7 Semina kwa Wajumbe wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa majukumu ya Kamati unategemea ushirikiano wa Ofisi ya Bunge, Serikali na taasisi mbalimbali za Serikali na za Binafsi katika kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati katika masuala mbalimbali ili waweze kutoa ushauri wa kujenga na wenye tija kwa Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati, semina kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na Sekta ya Elimu, Afya na maendeleo ya Jamii pamoja na tasnia ya Habari zilitolewa na wadau mbalimbali wakiwemo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee wakishirikiana na Mfuko wa Fedha wa Dunia (Global Fund), EngenderHealth, SIKIKA na TCRA kwa kushirikiana na Wizara ya habari, Utamaduni, Sanaa na michezo, HAKI ELIMU , STIPTRO, Umoja wa wawekezaji wa shule binafsi Tanzania (Tanzania Private Investors in Education-TAPIE), Ofisi ya Bunge kuititia Mradi wa **Parliamentary Legislative Support Programme II (LSP II)**, Voluntary Service Overseas - VSO Tanzania na Legal Service Facility.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inawashukuru wadau wote kwa namna walivyowezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kutohana na elimu nzuri waliyoipata kuitia semina hizo.

## **SEHEMU YA TATU**

### **3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo kuhusu shughuli zilizotekelawa na Kamati kwa kipindi cha Machi, 2018 hadi Januari, 2019, Kamati inatoa Maoni, Ushauri na Mapendeleko yafuatayo:-

#### **3.1 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika Wizara**

**Mheshimiwa Spika**, KWA KUWA utekelezaji wa majukumu ya Wizara zote kwa ajili ya kuwalettea watanzania maendeleo unategemea uwepo wa bajeti ya kutosha ya fedha zilizotengwa na Serikali na kupitishwa na Bunge lako Tukufu. Haitoshi uwepo wa bajeti pekee bali na upelekaji wa fedha hizo za bajeti katika Wizara husika kwa wakati ili kuwawezesha watendaji wa Wizara hizo kutekeleza mipango iliyopangwa kwa mwaka wa Fedha husika,

**NA KWA KUWA** bado mwenendo wa bajeti siyo wa kuridhisha hali inayoathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inazidi kusisitiza Serikali iendelee kupeleka fedha zote zilizoidhinishiwa na Bunge kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

#### **3.2 Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, KWA KUWA, Katika Bajeti ya Mwaka 2017/2018 Serikali iliidhinishiwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Wizara tatu ambazo Kamati inazismamia,

**NA KWAKUWA**, Katika Miradi yote ambayo Kamati ilifanya ukaguzi mwezi Machi, 2018, hakuna mradi hata mmoja ambao ulikuwa umepelekewa fedha. Baadhi ya miradi iliyokuwa inaendelea kutekelezwa ilikuwa inatumia bakaa za fedha za miaka iliyopita,

**KWA HIYO BASI** Kamati inaendelea kusisitiza kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo zitolewe kwa wakati ili kuепusha kutekelezwa

kwa hasara kutokana na kupanda kwa thamani ya fedha kulingana na tofauti za nyakati.

### **3.3 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Wizara hii, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

#### **3.3.1 Asasi Zisizo za Kiserikali (AZAKI)**

##### **a) Kanzi data (*Database*) ya AZAKI zote**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** kwa mujibu wa taarifa za Wizara kuna zaidi ya AZAKI 8,000 nchini zilizojikita katika nyanja za afya, maendeleo ya jamii kwa maana ya watoto, wazee na hata masuala ya kijinsia hasa kwa wanawake,

**NA KWA KUWA** pamoja na AZAKI hizi kufanya shuguli zake katika maeneo mbalimbali ya nchi mijini na vijijini lakini Wizara kama wasimamizi wa AZAKI haina taarifa za uhakika wa wapi zilipo na hata wakati mwingine Wizara hazifahamu shughuli maalumu zinazotekelezwa na AZAKI hizo na kuifanya Serikali kushindwa kufuatilia utekelezaji wa shughuli zake,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Wizara kutengeneza kanzidata ambayo itaonesha jina la AZAKI, mahali inapotekeleza majukumu yake, wafadhili wa fedha wa AZAKI husika, aina ya majukumu yanayotekelawa. Kwa kufanya hivyo Wizara itakuwa imesaidia kufanya uratibu na usimamizi wa AZAKI zote nchini.

##### **b) Wizara ianzishe Kitengo cha Udhibiti ubora wa AZAKI**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** uanzishwaji wa AZAKI unafanyika kwa mujibu wa Sheria na miongozo yake lakini pia zinahitaji udhibiti wa ubora wa shughuli inazofanya,

**NA KWA KUWA** zipo asasi ambazo zinafanya vizuri na baadhi zinakwenda kinyume na sheria na miongozo ya Serikali hali ambayo inaleta ukakasi kwenye jamii,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inapendekeza Wizara kuanzisha kitengo cha udhibiti ubora wa AZAKI ili kuweza kuzisimamia na kuhakikisha zinatекееза majukumu yake ipasavyo na kuzichukulia hatua kali ikiwemo onyo na hata kupelekwa mbele ya vyombo vya sheria ikithibitika zimekwenda kinyume na sheria za nchi. Kwa kufanya hivyo zitaongeza uwajibikaji na usimamiaji wa sheria na miongozo ambayo Serikali imewekwa kwa maslahi mapana ya nchi na wananchi kwa ujumla.

### **3.3.2 Bajeti ya Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Utekelezaji wa majukumu ya Idara Kuu Maendeleo ya Jamii unategemea sana kiasi cha fedha kinachotengwa,

**NA KWA KUWA** kwa muda mrefu Idara hii haijawahi kutengewa zaidi ya shilingi **Bilioni 50** kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake ikiwemo miradi ya Maendeleo, Kamati inaona ni kikwazo kikubwa katika utendaji wa majukumu ya Idara hiyo na ukizingatia kwamba Idara hii inabeba kundi kubwa la watoto, wazee na Jinsia zote (watanzania wote),

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali ianze kubadili mtazamo wake na kuipa umuhimu Idara hii kwa kuitengeta bajeti ya kutosha ili iweze kutatua changamoto za Sekta mbalimbali, ikiwemo ya Kilimo, afya, maji, miundombini, utalii na nyingine kwa kuwa kila jambo linaanzia katika jamii kupitia maafisa Maendeleo ya Jamii walio katika kila kata hapa nchini ili kuweza kuwaletaa maendeleo wananchi.

### **3.3.3 Ukatili wa Kijinsia na Watoto**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, imeainisha kwamba nanukuu "*Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake kwa mujibu wa sheria,*"

**NA KWA KUWA** hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la ukatili wa kijinsia na watoto hususan katika Mkoa wa

Njombe ambapo watoto wanaendelea kuuwawa jambo ambalo ni kinyume na Katiba ya nchi yetu na matakwa ya makubaliano ya kimataifa lakini pia ni kinyume na haki za binaadamu,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inapendekeza Serikali ifanye uchunguzi wa haraka na kuwachukulia hatua kali wale wote watakaobainika kuhusika na vitendo hivi ya kinyama.

### **3.3.4 Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)**

a) **Muswada wa Sheria ya Bima ya afya kwa wote**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** afya ni mtaji mkubwa katika kujiletea maendeleo kwa nchi husika na kwa muda mrefu Serikali imekuwa ikishauriwa na kupokea mapendekezo ya Kamati kwamba ni wakati sasa umefika kukawepo na Bima ya Afya kwa watu wote (*Universal Health Coverage*) lakini inashindikana kwa kuwa hakuna Sheria ambayo itaweza kusimamia aina hiyo ya bima,

**NA KWA KUWA** Kamati inaona umuhimu mkubwa wa aina hii ya Bima kwa wananchi wote ambayo itaondoa ubaguzi wa nani awe na bima na nani asiwe nayo. Hali ilivyo sasa ni wale walio katika ajira rasmi tu ndiyo wanufaika kwa asilimia kubwa na Bima ya taifa ya afya ambao hawazidi asilimia 27 ya watanzania wote,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kuharakisha Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote (*Universal Health Coverage Bill*) ili kuiwezesha NHIF kutekeleza jukumu la kutoa bima ya Afya kwa wananchi wote na kuwapa uhakika wa upatikanaji wa huduma za afya.

b) **Maboresho ya Huduma za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ni mfuko wa umma unaotoa huduma zake kwa wananchi hasa kwa watu ambao wapo katika ajira rasmi (Utumishi wa Umma) na sasa imepanua huduma zake

kwa kuwaingiza wale ambao wapo katika sekta binafsi kwa maana ya kujajiri na hata kuajiriwa na Sekta binafsi,

**NA KWA KUWA**, Licha ya kufanya hivyo bado wananchi wengi hawafahamu umuhimu wa kuwa na bima ya afya na namna gani kama mtu binafsi au vikundi wanaweza kupata huduma ya bima ya afya kutokana na kukosekana kwa baadhi ya mambo ikiwemo uhamasishaji mdogo wa jamii, vifurushi vichache au visivyovutia vinavyotolewa na bima ya afya ambavyo vinampa uwanja mdogo mteja wa kuweza kuchagua nini anahitaji pamoja na gharama zake. Kamati inaona kuwa vifurushi vinavyopangwa vinatokana na maamuzi ya Mfuko wa Bima ya Afya wenyewe na siyo mahitaji ya wateja wake jambo linalopelekea wananchi kutoona umuhimu wake,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inapendekeza kuwa:-

i) Serikali kupitia NHIF iendelee kufanya uhamasishaji kwa wananchi kuhusu umuhimu wa Bima ya afya ili kuwawezesha kuwa na uhiari wa kujunga na Bima ya afya kulingana na mahitaji yao kama vile uwezo wa kiuchumi (Social stratification), ambapo kuna baadhi ya wahitaji wanataka huduma ya kwenda kutibiwa nje ya nchi ili mradi akubaliane na gharama za ulipaji wa bima hiyo ambapo mashirika ya kimataifa na taasisi kama Benki ya Dunia watakuwa tayari kujunga na Bima hii ili mteja apate kile anachohitaji. Aidha, NHIF iwe inafanya utafiti mara kwa mara na kuona ubadilikaji wa mahitaji ya wateja kutokana na maoni yao ili kuweza kutengeneza vifurushi vinavyoendana na mahitaji ya wateja hao; na

ii) NHIF ifanye mchakato wa kutafuta wateja badala ya kusubiri kuletewa wateja kwa mujibu wa sheria kama ilivyokuwa awali kwamba watumishi wa Umma wote ni wateja wao na sasa wameongezewa mashirika na taasisi zote za umma ambazo ziliikuwa zinapata huduma ya bima ya afya kutoka kwa watoa huduma wengine, hali hii isipelekee kushindwa kufanya shughuli za kutafuta wateja wengine.

c) **Tathmini (Actuarial Valuation) ya Mfuko wa Taifa Bima ya Taifa**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ni mfuko wa wananchi ambao wanahudumiana kwa kuchangishana (*Risk Pooling Strategy*) kila mwezi ili kuweza kupata huduma za afya kwa maana ya kwamba anayeugua anahudumiwa na walio wazima. Fedha hizi zinapaswa kuwepo na mteja aone kama zipo anatarajia kupata huduma za afya wakati wowote na mahali popote alipo bila kikwazo chochote cha kutokuwepo kwa dawa, mto huduma ya afya, vifaa tiba kwa maana ya kupata vipimo ili kutambua ugonjwa unaomsumbu na masuala mengine yanayoendana na hayo,

**NA KWA KUWA** Kamati imekuwa ikishuhudia Mfuko huu ukifanya uwekezaji wa aina mbalimbali na hata kutoa mikopo kwa taasisi za Serikali kwa ajili ya kufanya uwekezaji ambao baadhi haiendani na hata na masuala ya afya hali ambayo inaweza kupelekea Mfuko kutofanya majukumu yake ya msingi,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inapendekeza kuwa, Mfuko huo utekeleze majukumu yake ya msingi ambayo ni malengo mahsus ya kuundwa kwake. Aidha, Serikali ifanye tathmini ya mfuko (*Actuarial Valuation*) huo ili kuweza kufahamu uhai na nguvu ya Mfuko baada ya kufanya uwekezaji huo mkubwa kwa nyakati tofauti. Kwa kufanya hivyo, Serikali itafahamu changamoto zake na namna gani ya kuweza kuzikabili kisha kuona namna bora ya kuendelea kuuimarisha Mfuko kwa manufaa wa wanachama wake.

**3.3.5 Bohari Kuu ya Dawa (MSD)**

a) **Serikali kutolipa deni la MSD kwa wakati:**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Bohari Kuu ya Dawa ndiyo yenye jukumu la kununua na kusambaza dawa hapa nchini na imekuwa ikitekeleza majukumu yake katika mazingira magumu sana licha ya kuwa Serikali imeongeza fedha za dawa katika Wizara ya Afya na kuendelea kudaiwa kiasi cha Zaidi ya Bilioni 200. Bohari Kuu ya Dawa imekuwa

ikitoa huduma hiyo licha ya Serikali kutolipa madeni hayo kwa wakati huku ikiendelea kutaka kupatiwa huduma. Hali hii inafanya Bohari kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Maelezo ya Serikali ni kwamba bado inahakiki deni hili,

**NA KWA KUWA** MSD imeongeza wigo wa utekelezaji wa majukumu yake hadi kwa nchi nyingine licha ya kwamba haitatumia fedha za Serikali kusambaza dawa hizo katika nchi jirani lakini bado zitatumika katika kuwawezesha watendaji kusimamia majukumu hayo yaliyoongezeka,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kwamba fedha zilizotengwa kiasi cha shillingi Bilioni 50 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kikatolewa haraka wakati uhakiki huo ukiwa unaendelea kwani kwa vyovoyote vile deni halitapungua kiasi hicho cha shillingi Bilioni 50. Aidha, mpaka Septemba 2018 deni la Serikali lilikuwa limefikia kiasi cha Shilingi Bilioni 200 ingawa Taarifa imeonesha ni shillingi Bilioni 114 nalo lipo katika uhakiki.

**b) Mkakati wa kuwawezesha wawekezaji katika uzalishaji wa dawa hapa nchini**

**Mhesimiwa Spika, KWA KUWA** nchi yetu ina kauli mbiu ya Uchumi wa Viwanda na moja ya eneo ambalo Serikali inaweza ikafanya vizuri sana ni katika uwekaji wa mazingira bora ya viwanda vya uzalishaji wa dawa za binadamu hapa nchini,

**NA KWA KUWA** ili kufanikiwa katika uzalishaji wa dawa hapa nchini, ushirikishwaji wa Sekta binafsi ni muhimu ili ziweze kuzalisha dawa hizo hapa nchini kwa gharama nafuu,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali iharakishe mchakato wa mpango wa kuziwezesha sekta binafsi katika kuzalisha dawa hapa nchini ili kuendelea kupunguza gharama za dawa kama ilivyo sasa. Kwa kufanya hivi, Serikali itakuwa imetimiza Sera yake ya Uchumi wa Viwanda, itapunguza gharama zinzotumiwa na MSD katika manunuzi

ya dawa nje ya nchi kwa gharama kubwa lakini pia katika kuwawezesha wawekezaji na wananchi katika kupata dawa za uhakika hapa nchini.

### **3.3.6 Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA)**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Mamlaka ya chakula na Dawa ndiyo yenyeye jukumu la kuhakikisha usalama wa mlaji wa chakula, vipodozi pamoja na dawa nchini,

**NA KWA KUWA**, katika vikao nya Kamati, iliyasilishwa taarifa ya kuwepo kwa bidhaa ambazo hazifai kwa matumizi ya binadamu zikiwemo chakula, dawa na vipodozi hali iliyopekea mamlaka kiviteketeza ambavyo vilikuwa na jumla ya uzito wa **tani 453.6** zenyeye thamani ya shilingi **6,940,348,743**. Bidhaa hizi ni pamoja na zile zilizokwisha muda wake na kutolewa taarifa na wateja wenyewe, zinazothibitika kuwa ni duni na bandia baada ya uchunguzi wa kimaabara au bidhaa zinazokutwa katika maeneo ambayo hayajasajiliwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaishauri Serikali kutengeneza Alama maalum ya utambuzi wa ubora wa bidhaa (*Barcode*) itakayomilikiwa na Mamlaka kama ambavyo ilivyo kwa Shirika la viwango Tanzania (TBS) wanayo alama ya utambuzi wa ubora wa bidhaa. Kwa kufanya hivyo kutasaidia kupunguza matumizi ya vyakula, dawa na hata vipodozi ambavyo havina uhakiki wa mamlaka ya Chakula na Dawa.

### **3.3.7 Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Sera ya Afya inaelekeza huduma za afya kwa watoto, wajawazito na wazee wa kuanzia miaka sitini (60) kupewa huduma hizo bila malipo,

**NA KWA KUWA**, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete ni miongoni mwa Taasisi inayotoa huduma hizo kwa makundi maalumu bila malipo na kupelekea taasisi kuingia gharama kubwa ya shilingi **607,444,779.93** kwa kipindi cha nusu mwaka (Juni-Disemba, 2018) kuweza kufidia gharama hizo hali inayopelekea Taasisi kushindwa kujidesha vizuri,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaishauri Serikali kutoa ruzuku kwa taasisi hii na taasisi za Afya zote nchini kwa ajili ya kufidia gharama za matibabu kwa makundi maalumu yaliyotajwa ili kuzisaidia kuendelea kutekeleza huduma zake za kutoa huduma za afya.

**3.4 Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

**3.4.1 Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA)**

**a) Kuongeza idadi ya Wakalimani**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Lugha ya Kiswahili ni lugha ambayo inatambulika kitaifa na kimataifa, ambapo hata nchi jirani kama Rwanda zimerasimisha lugha hii kutumika kama lugha ya mawasiliano ndani ya nchi hiyo,

**NA KWA KUWA** lugha hii imeanza kutumika katika mikutano mikubwa ya ndani na nje ya nchi ya Tanzania lakini kuna changamoto ya wakalimani kwani wakalimani waliopo wanaojuua lugha mbalimbali hawazidi 10 idadi ambayo ni ndogo sana ikilinganishwa na uhitaji wake,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaishauri ili lugha hii iweze kutambulika Kimataifa ni vyema Serikali ikaweka mkakati madhubuti wa kuongeza idadi ya Wakalimani ili waweze kuzitumia fursa zilizopo. Aidha, mkakati huo ujielekeze pia katika kuhakikisha wakalimani hawa wanakuwa na uelewa wa lugha nyingi zaidi kama vile Kifaransa, Kireno, Kijerumani na hata Kichina.

**b) Tuzo ya Kiswahili**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Serikali ina mikakati mbalimbali ya kukuza lugha ya Kiswahili ikiwemo kuheshimu michango ya watu/nchi mbalimbali katika kuikuza lugha hiyo kwa kuwapa Tuzo ya Kiswahili ijulikanayo “Tuzo ya Shaban Robert”,

**NA KWA KUWA** baadhi ya watu/nchi kama vile Afrika ya kusini na Rwanda zimekuwa mstari wa mbele kuhamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika nchi zao,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inapendekeza watu/nchi hizo na nyingine zitambuliwe na kupewa Tuzo ya Shaban Robert, kwa kufanya hivi kutaifanya lugha ya Kiswahili kuendelea kutangazwa na kutambulika kote ulimwenguni.

### **3.4.2 Sheria ya Huduma za Habari**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Mwaka 2016 Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya Huduma za Habari (The Media Services Act, 2016) kwa ajili ya kusimamia masuala yote ya Habari ikiwemo weledi wa wanataaluma ya uandishi wa Habari, wamiliki wa vyombo vya habari ikiwemo magazeti, redio na Televisheni,

**NA KWA KUWA**, Kamati imekuwa ikishuhudia baadhi ya magazeti yakikiuka maadili, taaluma na weledi wa kupasha habari hapa nchini,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaishauri Serikali isimamie kikamilifu Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016 kwa kuvichukulia hatua vyombo vyote vya habari, wamiliki wake wanaokiuka Sheria kama ambavyo ilikusudiwa uundwaji wake ili kuweza kuitunza heshima ya nchi yetu.

### **3.4.3 Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA)**

**a) Uibuaji wa vipaji mbalimbali vya wasanii katika jamii**

**KWA KUWA** kuna vipaji vingi ambavyo viro kwenye jamii lakini Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) halijaweza kuvitambua,

**NA KWAKUWA** kuibuliwa kwa vipaji hivyo kutaongeza idadi ya wasanii waliopo nchini na hivyo kuongeza mapato ya nchi kutohana na kazi watazokuwa wanafanya,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kuitia BASATA iandae mkakati maalumu wa kuibua vipaji hivyo kuanzia ngazi ya chini ya jamii ili kuweza kuwa na wasanii wengi ambao kwa namna moja ama nyingine wataendelea kuipeperusha bendera ya Tanzania, ikumbukwe sanaa ni ajira.

**b) Wasanii**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** moja ya kazi za BASATA ni kutoa ushauri na misaada ya kiufundi kwa wasanii na wadau wa Sanaa nchini na hivi karibuni kumekuwa na fungia fungia ya nyimbo za wasanii na matamasha ya wasanii,

**NA KWA KUWA** wasanii hawa wamekuwa wakipata mapato mengi kutoka na HITS wanazopata kuititia mitandao ya jamii kama Youtube na Serikali imekuwa haipati chochote kutokana na mahusiano yasiyordhisha kati yao na wasanii,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inapendekeza;

i) BASATA kutekeleza jukumu la kuwalea kwa kuwashauri wasanii kuandaa nyimbo zinazoendana na maudhui na kuwaonya pale wanapokosea;

ii) Kuboresha mahusiano na wasanii ili kuweza kufaidika na mapato yatokanayo na hits za mitandao ya jamii; na

iii) BASATA kuhakikisha wanaandaa kanzidata (*Database*) ya kuwafahamu wateja wao (Wasanii wote) nchi nzima kwa kuwa na aina maalumu ya utambuzi (Special Identification) ikiainisha jina, aina ya kazi anazozifanya na masuala mengine yanayoambatana na hayo. Hili linawezekana kwa kuwatumia maafisa utamaduni wa Wilaya, Mkoa na mwisho Baraza la Sanaa la Taifa.

**3.4.4 TASUBA**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** TASUBA licha ya kuwa ni Kituo cha Ubora uliotukuka (Centre of Excellency) lakini bajeti inayotengwa hususani fedha kwa ajili ya miradhi ya maendeleo kwa Taasisi hii pamoja na miundombinu iliyopo haviendani na hadhi yake,

**NA KWA KUWA** pamoja na kufanya Tamasha la 37 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni lakini matangazo hayakuwa mengi kutokana na ukosefu wa fedha na hivyo kuathiri idadi ya washiriki pamoja na mapato,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri: -

a) Bajeti ya TASUBA iongezwe hususan ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ikiwemo Miundombinu, na vifaa ili iweze kuboreshwa; na

b) TASUBA ianze kujitangaza hasa inapokuwa na matamasha ili yafanane na yale ya Sauti za Busara au Tamasha la Kimataifa la Filamu Zanzibar (ZIFF) kwani itasaidia kupata washiriki wengi na mapato ya Serikali kuongezeka.

#### **3.4.5 Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)**

a) **Chaneli ya Utalii**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** TBC imeanzisha chaneli ya Utalii kwa lengo la kutangaza vivutio vyta utalii, maliasili, mali kale na utamaduni wa Mtanzania ili kuvutia watalii wa ndani na nje ya nchi,

**NA KWA KUWA** Chaneli hii bado inaonekana ndani ya nchi pekee licha ya mpango wa TBC kutaka ioneckane hadi nje ya nchi ili kuweza kuvutia watalii wa nje ya nchi na hivyo kuongeza pato la Taifa,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri TBC kuandaa mpango mkakati ambaao utahakikisha chaneli hii inaonekana nje ya nchi mapema ili kuwavutia watalii wengi na hatimae kuongeza pato la Taifa kutokana na ujio wao.

b) **Mapato ya TBC**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** ili TBC iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kama zilivyo Televisheni nyingine za Umma katika nchi mbalimbali duniani inahitaji kuwa na uwezo wa kifedha,

**NA KWA KUWA** kwa muda mrefu sasa TBC inashindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo kutokana na ufinyu wa fedha ili hali kuna uwezekano wa kutumia vyanzo vingine vyta mapato kama vile tozo za ving'amuzi na ada za leseni za Televisheni nyingine,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaishauri Serikali iweke utaratibu utakaowezesha TBC kupata sehemu ya mapato yatokanayo na malipo ya muda wa hewani wa visimbuzi pamoja na ada za leseni za Televisheni nyingine ili kuiweseha kifedha katika utekelezaji wa majukumu ya Umma.

#### **3.4.6 Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF)**

**Mheshimiwa Spika**, KWA KUWA Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) ndiyo yenyeye jukumu la kusimamia mchezo wa mpira wa miguu nchini,

**NA KWA KUWA**, kumekuwa na changamoto nyingi katika usimamizi na uratibu wa mpira wa miguu nchini,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri

- a) Wizara yenyeye dhamana na Michezo ishirikiane na TFF kuhakikisha kuwa hakuna mabadiliko ya mara kwa mara ya ratiba za Ligi Kuu ili kuondoa dhana ya upangaji wa matokeo;
- b) Wizara ishirikiane na TFF kuondoa migogoro katika vilabu na vyama vya michezo;
- c) Serikali iandae program za mafunzo kwa makocha wa mpira wa ndani ili kuinua soka letu; na
- d) Serikali iachane na ratiba za michezo ya ligi ya wanawake inayochewa nyumbani na ugenini na badala yake ichezwe kwenye vituo ili kupunguza gharama kwani timu nyingi hazina uwezo.

#### **3.5 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

##### **3.5.1 Mkakati wa kuboresha miundombinu ya Vyuo**

**Mheshimiwa Spika**, KWA KUWA utoaji wa elimu bora kwa wanafunzi wa chuo kikuu unategemea na uwepo wa Miundombinu bora inayotosheleza kama Mabweni ya wanafunzi yenyeye huduma zote ikiwemo maji safi na salama, Ofisi za Wahadhiri, Maabara, maktaba vikianishwa kwa uchache,

**NA KWA KUWA** kumekuwa na changamoto ikiwemo upungufu wa baadhi ya miundombinu kama vile mabweni

katika baadhi ya vyuo mfano Chuo Kikuu Kishiriki cha Mkwawa na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere hali inayoathiri utekelezaji mzuri wa majukumu ya chuo na usalama kwa wanafunzi hasa kwa watoto wa kike,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali iandae mkakati wa maksudi na wa haraka, ili kuweza kuwasaidia wanafunzi wanaokaa nje ya chuo kwa maana ya **Off - Campus** kwenye nyumba za watu binafsi. Ni imani ya Kamati kuwa Serikali itafanya juhudhi hizo za maksudi kama ambavyo ilifanyika kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salama kwa kujenga mabweni ya wanafunzi hali ambayo imemaliza kabisa changamoto ya wanafunzi kukaa nje ya chuo.

### **3.5.2 Chuo cha Kumbukumbu ya Mwl J.K Nyerere kiendane na jina**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ndiye muasisi wa Taifa linaloitwa Tanzania leo, ndiye Rais wa kwanza wa nchi ya Tanzania, ndiye aliyeongoza harakati za kujipatia uhuru kutoka kwa wakoloni waliotutawala katika Nyanja zote za kiuchumi, kiutamaduni, kisasa na hata kifikra, ndiye aliyeifanya nchi hii ikatambulika ndani na nje ya Bara la Afrika. Si hivyo tu, jina lake pia linatambulika nje ya nchi kwa mchango wake katika kujipatia uhuru na hata usuluhishi wa migogoro mbalimbali katika nchi nyingine duniani,

**NA KWA KUWA**, kutokana na sifa chache zilizotajwa hapo awali, Serikali iliona umuhimu wa kumuenzi Baba wa Taifa kwa kutoa jina na kukiita Chuo kilichopo Kigamboni Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, ambacho wakati Kamati ikipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu yake ilibaini kwamba jina ambalo Chuo limepewa (Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere) ni kubwa na haliendani na shughuli ambazo Chuo inatekeleza,

**KWA HIYO BASI**, ili kutunza hadhi ya jina la mwalimu na hata kuweza kutambulika katika nchi nyingine na kuwafanya watu kutoka nchi hizo kutamani kuja Tanzania na kusoma katika Chuo chenye jina la muasisi wa Taifa na ili

kuondoa hali ilivyo kwa sasa, kwamba wanafunzi wanaokosa sifa za kujunga na vyuo vingine hapa nchini ndiyo wanaokwenda kujunga na masomo katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, ambayo Kamati inaona si sawa hata kidogo. Kamati inashauri: -

- a) Chuo Kijielekeze katika kutoa mafunzo ya uongozi ili iweze kuwa "*Centre of Excellency*". Hii itasadia kuvutia watu wengi kujunga na chuo lakini wahadhiri wengi bora wenye kufundisha masuala ya uongozi kwenda kufundisha katika Chuo hicho na kuondokana na changamoto ya upungufu wa watumishi; na
- b) Chuo kianzishe mafunzo ya muda mfupi ya uongozi na yatolewe kwa viongozi mbalimbali kuanzia ngazi ya kijiji mpaka Taifa ili waweze kufahamu kwa kina misingi ya uongozi bora na uzalendo.

### **3.5.3 Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu**

#### **a) Vigezo vyaa upatikanaji wa Mkopo**

**Mheshimiwa Spika, KWAKUWA,** Serikali inatenga fedha kwa ajili ya kusomesha wanafunzi katika ngazi ya elimu ya juu zaidi ya kiasi cha shilingi **Bilioni 400** kila mwaka kwa njia ya kuwapa mikopo ambayo inapaswa kurejeshwa na wafaidika hao mara wamalizapo masomo,

**NA KWAKUWA,** Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ndiyo inayosimamia utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa kuzingatia vigezo mbalimbali vilivyoainishwa na Bodi ikiwemo hali ya uchumi, historia ya shule mwanafunzi alizosoma ikiwemo sekondari, hali ya wazazi (*death status*) vikitajwa wa uchache wake ambavyo Kamati inaona ni vichache,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuvipitia tena vigezo hivyo na ikibidi kuboreshwa na kuongezwa kwa vigezo vingine kama vile ufaulu wa mwanafunzi bila ya kujali hali ya uchumi wa familia, jinsi ya kike lakini pia kwa wanafunzi wenye ulemavu na wana ufaulu

mzuri wapewe mkopo bila kuangalia vigezo vingine ikiwemo historia yake.

**b) Mwenendo wa Ukusanyaji wa madeni ya Mikopo kutoka kwa wanufaika**

**KWAKUWA**, Serikali imekuwa ikitoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa muda mrefu tangu mwaka 1994/1995 mpaka Desemba 2018 jumla ya shilingi **Trilioni 3.87** kwa **wanufaika 478,548** zimetolewa,

**NA KWA KUWA**, katika kiasi kilichotolewa (Trilioni 3.87) na Serikali kwa wanufaika mbalimbali ni takribani shilingi **Bilioni 291.538** bado hazijarejeshwa ambazo ni sawa na **asilimia 70** ya bajeti ya fedha (**Bilioni 412.4**) ya Bodi ya mikopo kwa wanufaika kwa mwaka **2018/2019** zipo mikononi mwa wanufaika zinapaswa kurejeshwa kwa Bodi ya Mikopo kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wengine kwani wahitaji wanazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo;

i) Bodi ya mikopo iimarishe mifumo ya taarifa za wanufaika wa mikopo kwani kumekuwepo na malalamiko ya baadhi ya wanufaika kudaiwa deni zaidi ya mara moja ili hali mtu huyo ameanza kurejesha au amemaliza malipo ya mkopo;

ii) Kuandaa utaratibu rahisi na wa kisasa kwa mnufaika kuweza kupata taarifa za deni lake na kuweza kulipa kuitia mfumo wa simu za mikononi kwa kuwa wanufaika wengi wanao uwezo wa kumiliki simu za mikononi, kwa kufanya hivyo kutarahisisha ukusanyaji wa madeni hayo; na

iii) Bodi ya Mikopo iandae orodha ya wadaiwa wote wanaostahili kulipa madeni (madeni yaliyoiva Bilioni 291.538) hayo na kuyasambaza kwa waajiri, taasisi mbalimbali na kwenye vyombo vya habari ili kuweza kuwahamasisha na kuwakumbusha wadaiwa hao kuweza kulipa madeni hayo ya mkopo.

### **3.5.4 Miradi ya Lipa kulingana na Matokeo (EP4R) kusimamiwa na Wizara ya ELIMU**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Mradi wa EP4R umekuwa na tija chini ya usimamizi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Kamati imeshuhudia uwepo wa thamani ya fedha katika maeneo yote ambayo mradi umekuwa ukitekelezwa,

**NA KWA KUWA**, hivi karibuni kumekuwa na minong'ono ya kutaka Mradi huu uanze kusimamiwa na watendaji wa TAMISEMI jambo ambalo Kamati inaona sjema kwa kuwa TAMISEMI inashughuli nyingi za kufanya zikiwemo barabara, maji, elimu na afya,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaendelea kusisitiza Miradi yote inayohusu uboreshaji wa miundombinu ya elimu chini ya EP4R iendelee kutekelezwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

### **3.5.5 Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM)**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** malengo ya chuo kikuu cha Dodoma ni kudahiri **wanafunzi 40,000**,

**NA KWA KUWA**, Mpaka kufikia mwaka 2018/2019 Chuo kimedahiri jumla ya **wanafunzi 28,776** kutokana na changamoto ya fedha za miradi ya maendeleo zikiwemo za ukamilishaji wa ujenzi wa chuo lakini pia kutokana na uhaba wa wafanyakazi hasa wanataaluma katika ngazi za madaktari na maprofesa wa kufundisha wanafunzi hao,

**KWAHIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali ikipatie chuo fedha hizo za miradi ya maendeleo ili kikamilishe ujenzi wa chuo utakaowezesha udahiri wa wanafunzi wengi zaidi lakini pia iweke mkakati madhubuti utakaohakikisha chuo kinakuwa na walimu wa kutosha wa kufundisha lengo la wanafunzi hao 40,000.

### **3.5.6 Vyuo vya Ufundu**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA**, Serikali ya awamu ya Tano imejikita katika kukuza uchumi wa viwanda na

kuipeleka nchi katika uchumi wa viwanda katika sekta mbalimbali ikiwemo viwanda vinavyohitaji ufundi wa aina tofauti tofauti kwa manufaa ya nchi yetu,

**NA KWA KUWA**, idadi ya mafundi mchundo na mafundi sadifu wanaozalishwa na vyuo vya ufundi nchini ni kidogo ikilinganishwa na mahitaji halisi,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kuandaa mpango mkakati wenyе tija na wa muda mrefu wa kuimarisha vyuo vya ufundi kwa kuongeza miundombinu bora, walimu wa kutosha na ikiwezekana kuwapa mikopo wanafunzi hao kama ambavyo wanafunzi wa elimu ya juu wanapata kwa ajili kuzalisha mafundi mchundo na mafundi sadifu wa kutosha kwa ajili ya kuendeleza Sera ya Viwanda na kuimarisha uchumi wa viwanda kwa maslahi mapana ya Taifa.

### **3.5.7 Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)**

#### **a) Asilimia 1 ya Pato la Taifa (GDP) kwenda COSTECH**

**KWAKUWA**, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ilianzishwa kwa lengo la kuwa Mshauri Mkuu wa Serikali katika masuala yote yanayohusiana na Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa maendeleo ya Taifa zima,

**NA KWA KUWA**, Taarifa ya tume inaonesha kuwa katika utekelezaji wa majukumu yake kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini ambapo katika uchambuzi wa Kamati ilibainika kuwa Tume hii ilipaswa kupokea fedha kutoka Serikalini kiasi cha **asilimia moja** ya Pato zima la Taifa (1% of GDP) yakiwa ni makubaliano ya Nchi zote za Umoja wa Afrika (*African Union*) kwa lengo la kusaidia utafiti jambo ambalo limekuwa halifanyiki kwani upatikanaji wa fedha umekuwa ni **asilimia 0.034** ya Pato la Taifa kwa muda mrefu,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kutekeleza makubaliano yaliyofanywa na Umoja wa nchi za Afrika za

kutenga **asilimia 1** ya Pato la Taifa kwa mwaka ili kwanza kutimiza makubaliano ya nchi za Umoja wa nchi za Afrika lakini pia kuisaidia Tume kutekeleza majukumu yake ya utafti.

**b) Fedha za Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano ya Simu (Telecommunication Traffic Monitoring System – TTMS)**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** moja ya chanzo cha mapato ya Tume ni fedha za Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano ya Simu (*Telecommunication Traffic Monitoring System –TTMS*),

**NA KWAKUWA**, chanzo hicho cha mapato kwa sasa Kimeondolewa hali inayopelekea utekelezaji wa majukumu ya Tume kuwa mgumu,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kuona namna bora ya kurudisha chanzo hiki cha mapato kwa Tume ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

#### **SEHEMU YA NNE**

##### **4.0 HITIMISHO**

##### **4.1 SHUKRANI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Pamoja nawe napenda kumshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge, kwa kuliongoza vyema Bunge letu.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Mawaziri wote 3 na Manaibu Waziri 3 ambaotunafanya kazi nao kwa karibu kwa ushirikiano mkubwa, nasema asante sana Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mhe. Ummy Mwalimu (Mb), Naibu Waziri Dkt. Faustine Ndugulile (Mb), Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Dkt. Harrison G. Mwakyembe (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Juliana D. Shonza (Mb), Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Joyce Ndalichako (Mb) na Naibu Mhe. William T. Ole Nasha (Mb) wamekuwa karibu na Kamati na kuielewa

Kamati inapotoa hoja za msingi katika kuendelea kuboresha utendaji mzuri wa Serikali. Aidha, napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Wizara hizo wakiongozwa na Makatibu Wakuu wao kwa utendaji mzuri wa kazi zao licha ya changamoto nyingi wanazokumbana nazo lakini bado wameendelea kufanya kazi kwa weledi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika**, namshukuru Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Juma S. Nkamia, Mb kwa ushirikiano anaonipa mimi binafsi pamoja na Kamati katika kutekeleza majukumu yetu. Kipekee naomba kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano mzuri ambao wamekuwa wakinionesha katika kutekeleza majukumu yangu lakini pia kutoa michango yenye tija kwa Taifa.

Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Peter J. Serukamba, Mb	Mwenyekiti
2. Mhe. Juma Selemani Nkamia, Mb	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb	Mjumbe
4. Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb	Mjumbe
5. Mhe. Peter Ambrose Lijualikali	Mjumbe
6. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Grace Victor Tendega, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Bernadeta K. Mushashu, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Vicky Paschal Kamata, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Deogratius Francis Ngalawa, Mb	Mjumbe
12. Mhe. Amina Nassoro Makilagi, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Kabwe Zuberi Ruyagwa Zitto, Mb	Mjumbe
14. Mhe. Susan Anselm Lyimo, Mb	Mjumbe
15. Mhe. John Peter Kadutu, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Mgeni Jadi Kadika, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Khamis Yahya Machano, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Mch. Dkt. Getrude P. Rwakatare, Mb	Mjumbe
20. Mhe. Selemani Said Bungara, Mb	Mjumbe
21. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb	Mjumbe
22. Mhe. Joseph Leonard Haule, Mb	Mjumbe
23. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb	Mjumbe

24. Mhe. Maulid Said Mtulia, Mb Mjumbe
25. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, kipekee zaidi napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila vikwazo. Nawashukuru pia wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge akiwemo Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman B. Hussein, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati hii Ndg. Dickson M. Bisile pamoja na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Pamela E. Pallangyo na Ndg. Agnes Nkwera kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati.

#### 4.2 HOJA

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuwasilisha Taarifa hii, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Peter Joseph Serukamba, Mb

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA**

**MAENDELEO YA JAMII**

**7 Februari, 2019**

**SPIKA:** Ahsante sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Kila Mheshimiwa Mbunge anayo nakala na kwa kweli humu ndani yapo maoni mazuri sana, naomba kila mmoja ajaribu kuititia na kuona Kamati inatushauri nini kama Bunge. (*Makof*)Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa. Anakuja Mwenyekiti mwenyewe, Mheshimiwa Rweikiza karibu sana, una robo

saa jitahidi. mwenyewe, Mheshimiwa Rweikiza karibu sana, una robo saa jitahidi.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati. katika kipindi cha kuanzia Januari 2018/2019, Kamati ilikutana na kutembelea Wizara, Taasisi na Idara zilizo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa miradi, Mfuko wa Maendeleo ya *TASAF*. Utekelezaji wa mradi huu umejikita katika kuzisaidia kaya maskini kukuza uchumi na hivyo kupunguza umaskini wa kipato na kuzipatia ruzuku ya fedha ili kuboresha maisha kwa kupata chakula, kuwezesha watoto kuhudhuria shulen na kliniki kwa walio chini ya miaka mitano. Ukiwa katika hatua ya tatu ya utekelezaji wake mpango huu umefikia takriban Watanzania 5,900,000 ambao wamepokea ruzuku ya kiasi cha shilingi billioni 147.6 katika awamu mbalimbali za malipo.

Mheshimiwa Spika, Mkoani Simiyu Kamati ilitembelea Mtaa wa Nalikungu na Kijiji cha Shanwa katika Wilaya ya Maswa ambapo ilibaini kwamba katika Kijiji cha Shanwa, jumla ya kaya za walengwa 248 zilinufaika na mpango huu wa ruzuku na tayari zilikuwa zimepokea malipo ya awamu 16. Miiongoni mwa wanufaika hao ni Bibi Monica Katambi Gwilasa, miaka 60 ambaye ametumia ruzuku kama chachu ya kujenga nyumba ya tofali ya vyumba vitatu na kuezeka kwa bati. *TASAF* imeshiriki kwa kiasi kikubwa katika kuboresha elimu ya sekondari kwa kuchangia ujenzi wa

vyumba viwili katika Shule ya Sekondari Nalikungu kwa kutoa jumla ya shilingi milioni 30. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kupitia mpango huu wa MKURABITA wananchi wanyonge wanawezeshwa kurasimisha ardhi na biashara zao wanazozimiliki kwa kuzitumia kujikwamua kiuchumi. Kamati ilitembelea Vijiji vya Segese, Lunguya katika Halmashauri ya Msalala ambavyo vimefanyiwa mpango wa matumizi bora ya ardhi chini ya uwezeshaji wa MKURABITA. Pamoja na mafanikio hayo, kuna changamoto ya ubaha wa wataalam wa ardhi sambamba na kutenga bajeti ya kutosha ili kuwezesha MKURABITA kuyafikia maeneo mengi zaidi ambayo hayajarasimishwa.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Ukusanyaji Mapato kwa njia ya Kielektroniki. Mfumo huu ambao sasa unatumika katika Halmashauri zote 185 nchini, umewezesha Serikali kuachana na matumizi ya vitabu na mawakala katika ukusanyaji wa mapato na hivyo kuepuka upotevu mkubwa wa mapato kutokana na upotevu wa vitabu na kumbukumbu. Kamati ilibaini changamoto ya mtandao kutopatikana kikamilifu na hivyo kuishauri Serikali kuboresha upatikanaji wake ili kuondoa usumbufu kwa walipaji. Aidha, kuwe na makubaliano ya pamoja baina ya Benki ya *NMB* na *TAMISEMI* namna kuufanya mtandao huu kuwa rahisi na rafiki kwa watumiaji.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Wanawake. Mradi huu ni sehemu ya jitihada za Serikali za kuwawezesha kiuchumi wanawake na vijana kupitia asilimia 10 ya mapato ya ndani ya kila Halmashauri. Kamati ilitembelea kikundi cha vijana ambacho kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Maswa kimeanzisha Kiwanda cha Chaki kilichopo Maswa Mjini. Vijana hawa wanamiliki asilimia 40 ya hisa katika mradi huo wenye thamani ya shilingi milioni 100.

Mheshimiwa Spika, kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji. Kuanzishwa kwa Wakala wa Barabara Vijijini na Mjini (*TARURA*) ni mwendelezo wa utekelezaji wa mabadiliko

(reforms) kwenye sekta ya ujenzi wa barabara yaliyoanza mwaka 1998 ambayo ni pamoja na marekebisho ya *Roads Tolls Act*, kwa kuanzishwa kwa Mfuko wa Barabara (*Roads Fund*), *TANROADS* na sasa *TARURA*. *TARURA* ambayo inahudumia mtandao wa barabara wenge jumla ya kilomita 108,000 ina majukumu makubwa ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara vijijiini na mijini, pamoja na madaraja na mpango mkakati wa kuondoa vikwazo ili barabara ziweze kuitika muda wote. Kamati inafikiria njia mojawapo ya kuongeza uwezo wa *TARURA* kifedha ni kuongeza mgao wa fedha kutoka Mfuko wa Barabara (*Road Fund*) kutoka asilimia 30 hadi asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa ukarabati wa shule kongwe za sekondari nchini. Mkakati huu unalenga kurudisha shule kongwe katika ubora wake baada ya miundombinu yake kuchakaa na kuharibika kwa kiwango kikubwa. Ni ushauri wa Kamati kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI, irejee upya (review) mkataba yote ambayo imeingia na *TBA* kuhusu ujenzi na ukarabati wa shule kongwe na iwapo itabainika kasoro za utekelezaji basi hatua stahiki zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kusitisha au kuvunja mikataba kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Usambazaji Majisafi na Salama Vijijiini. Utekelezaji wa programu hii uko katika awamu ya pili na unalenga kuongeza na kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo ya vijijiini. Hatua ya Bunge kutunga sheria ambayo imeanzisha Wakala wa Maji Vijijiini ambacho kitakuwa ni chombo chenye dhamana ya kusimamia masuala yote ya maji maeneo hayo ni dalili nzuri ya juhudhi za Serikali. Kamati inaomba chombo hiki kitakapoanza kazi kiwezeshwe kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa hospitali za Halmashauri na Vituo vya Afya. Utekelezaji wa mpango huu unalenga kuboresha hali ya utoaji wa huduma za afya kwa kuzingatia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Kamati inapongeza dhamira ya Serikali katika ujenzi wa

vituo vyा afya 350 katika kipindi cha muda mfupi kwa gharama ya zaidi ya shilingi bilioni 137.35. Hata hivyo, uzoefu umebaini kwamba bajeti ya kulingana (*flat rate*) inayotengwa kwa vituo vyote nchini siyo halisi kwani gharama za ujenzi hazifanani kote nchini. Kamati pia inatambua na kupongeza hatua ya Serikali kutenga na kuidhinisha shilingi bilioni 105 katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali za Halmashauri 67 katika Halmashauri ambazo hazikuwa na hospitali hizo. Hadi kufikia Novemba, 2018 fedha hizo zilikuwa zimetolewa zote na kupelekwa kwenye Halmashauri husika ili kuanza mchakato wa ujenzi na ambao Serikali imeelekeza ukamilike ndani ya miezi sita.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA). Mpango huu umeendelea kuandaa na kusimamia Mfumo wa Kitaifa wa Umiliki wa Rasilimali na Uendeshaji wa Biashara unaotambulika na kukubalika kisheria. Kupitia mpango huu, wanyonge wanawezeshwa kurasimisha mali walizonazo ardhi na biashara na kuzitumia kujikwamua kiuchumi. Kwa kuzingatia umuhimu wa kazi zinazotekelawa na MKURABITA, ni mtazamo wa Kamati kwamba Serikali iongeze bajeti ya MKURABITA kwani inayotengwa ni kidogo sana na inaathiri mpango huu kusambaa katika maeneo mengine nchini.

Mheshimiwa Spika, mpango wa *TASAF*. Mfuko huu unatekelezwa katika awamu tatu tangu ulipoanzishwa mwaka 2000. *TASAF* Awamu ya III ambayo ilizinduliwa Agosti 2013 inatekeleza mpango wa kunusuru kaya maskini kwa kuziwezesha kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu. Zaidi ya walengwa 1,005,000 waliopo katika vijiji, mitaa na shehia 10,000 wanunuifaika na mpango huu wa ruzuku ambao zaidi ya shilingi bilioni 706 zimetolewa na kutumika katika ngazi zote za utekelezaji. Ni maoni ya Kamati kwamba ni vyema Serikali ikatathmini ushiriki wake katika mpango huu na kuanza kutoa fedha

kikamilifu ili kujenga mazingira ya kugharamia mpango huu kwa fedha za ndani iwapo wahisani watajiondoa.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria wa Tamko la Kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi uliletwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ili kufanyiwa kazi. Muswada huu ulipendekeza kutungwa Sheria ya Tamko la Makao Makuu ya mwaka 2018 kwa madhumuni ya kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kamati ilitimiza wajibu wake kwa kushughulikia Muswada huo katika tarehe 21 na 28 Agosti mwaka 2018, ambapo ulifanyika uchambuzi wa kitaalamu ulioboresha Muswada huo kwa kuzingatia maelezo ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo, Wakala wa Barabara Vijijiini na Mijini (*TARURA*). Kwa kuwa Wakala hii imebainika kukabiliwa na changamoto kadhaa, ikiwa ni pamoja na ufinyu wa bajeti, uhaba wa watumishi na ofisi. Na kwa kuwa hali hiyo inaathiri utekelezaji wa majukumu ya Wakala na kuifanya ishindwe kusimamia kikamilifu matengenezo ya miundombinu ya barabara inazozisimamia. Kwa hiyo basi, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuitaka Serikali kutenga fedha za kutosha na kuzitoa kikamilifu kwa *TARURA* ili iweze kuhudumia kikamilifu mtandao wa barabara unaosimamia ambao una zaidi ya kilomita 108,000.

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari. Kwa kuwa mkakati huu unasuasua kutokana na mkandarasi Wakala wa Majengo (TBA) kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Na kwa kuwa hali hiyo si kwamba inatia doa mkakati huo wa Serikali na kuchelewesha kikamilifu ukamilikaji wa ukarabati wa shule hizo. Hivyo basi, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuitaka Serikali, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia upya (*review*) mikataba

yote ambayo imeingia na *TBA* kwa ajili ya ukarabati wa shule hizo kongwe.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Usambazaji Maji Vijijini. Kwa kuwa ukomo wa bajeti, upatikanaji wa fedha usioridhisha kutoka Hazina na upungufu wa wataalam wa maji na mafundi mchundo umeathiri usimamizi wa utekelezaji huo vijijini. Na kwa kuwa hali hiyo imesababisha vituo 40,000 ya kuchotea maji kushindwa kufanya kazi na hivyo kuwanyima wananchi wa maeneo ya vituo hivyo huduma ya maji. Hivyo basi, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuitaka Serikali kuongeza bajeti ya upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Hospitali za Halmashauri. Kwa kuwa Serikali imetenga na kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali za Halmashauri 67. Na kwa kuwa kiasi hicho kitagharamia ujenzi wa hospitali hizo kwa asilimia 20 tu. Hivyo basi, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali itenye na kutoa kiasi cha fedha kilichobaki cha shilingi bilioni 6 kwa kila hospitali ili ujenzi ukamilike.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa vituo vya afya. Kwa kuwa Serikali inatekeleza Mpango wa Ukarabati na Ujenzi wa Vituo vya Afya 350 nchini katika hatua mbalimbali tangu mwaka 2017. Na kwa kuwa mpango huo unakabiliwa na ufinyu wa bajeti ambao umesababisha vituo vingi kutengewa kiasi sawa cha fedha. Hivyo basi, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuongeza bajeti inayotengwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya nchini.

Mheshimiwa Spika, ufinyu wa bajeti na kuathiri Mpango wa MKURABITA. Kwa kuwa bajeti ya maendeleo inayotengwa na kupatikana kwa ajili ya MKURABITA ni finyu. Na kwa kuwa hali hiyo inasababisha wananchi wa maeneo mengi kutofikiwa na MKURABITA. Kwa hiyo basi, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuongeza bajeti ya maendeleo ya MKURABITA.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Kumbukumbu za Taifa. Kwa kuwa shughuli za Idara ya Kumbukumbu za Taifa hazifahamiki kwa jamii. Na kwa kuwa hali hiyo inasababisha wananchi wenyewe hazina ya taarifa hizo kutoona umuhimu wa kujitokeza na kuziwasilisha. Hivyo basi, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuitaka Serikali kuiwezesha Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa kutumia vyombo vyaa habari kujitangaza.

Mheshimiwa Spika, *TASAF*. Kwa kuwa asilimia 30 ya maeneo (vijiji/mitaa/shehia) nchini haijafikiwa na awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango wa *TASAF*. Na kwa kuwa hali hiyo inasababisha walengwa kati ya 300,000 na 400,000 wenyewe sifa katika maeneo hayo kukosa huduma. Hivyo basi, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kutafuta pesa ili kuhakikisha utekelezaji wa awamu ya tatu ya mpango huo unakamilika.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Ninapohitimisha napenda kuzungumzia kidogo kuhusu dhana ya ugatuvi wa madaraka na upelekaji wa madaraka kwa wananchi (*Devolution by Decentralization – D by D*). Jambo hili msingi wake ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 146 inasisitiza kwamba vyombo vyaa Serikali za Mitaa (Halmashauri, Kata, Vijiji, Vitongoji na Mitaa) vitakuwa na haki na mamlaka ya kuwashirikisha wananchi katika mipango na shughuli za utekelezaji wa maendeleo. Dhana hiyo Kikatiba kuitia sera iliyotungwa mwaka 1998 imekuwa na manufaa kadhaa ikiwa ni pamoja na kusogezwa kwa huduma karibu na wananchi na ushiriki wa wananchi katika kutathmini, kupanga, kuamua na kutekeleza mipango mbalimbali kwa kuzingatia matatizo yaliyonayo na ni kwa mantiki hiyo wananchi kwa nguvu zao na uungwaji mkono wa Serikali...

*(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, dakika moja umalizie.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba taarifa hii iingie katika Kumbukumbu zetu za *Hansard* na Waheshimiwa Wabunge wanayo.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kutoa hoja.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KWA KIPINDI CHA KUANZIA JANUARI, 2018 HADI JANUARI, 2019 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## **SEHEMU YA KWANZA**

### **1.0        UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2018 hadi Januari, 2019.

Taarifa hii imejikita katika kuelezea shughuli mbalimbali zilizotekelawa na Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, katika kipindi cha mwaka mmoja wakati ikitekeleza majukumu ya kuisimamia na kuishauri Serikali ambayo ni majukumu yake ya kikanuni.

### **1.1 Majukumu**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 6(4) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari,2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, inasimamia shughuli za Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Aidha, kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Kanuni, 2016 kinaweka bayana kuwa majukumu ya Kamati hii yatakuwa: -

- a) Kushughulikia Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
- b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Maazimio na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Ofisi ya Rais;
- c) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na
- d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais.

### **1.2 Njia zilizotumika kutekeleza Majukumu**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitumia njia mbalimbali kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo: -

- a) Vikao na Wizara, Taasisi na Idara zilizo chini ya Ofisi ya Rais ili kufahamu Muundo na Majukumu na shughuli zinazotekelzwa;
- b) Uchambuzi wa Taarifa mbalimbali za kutendaji kutoka Ofisi ya Rais;

c) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari,2016; na

d) Mafunzo na Semina za kuwajengea uwezo (capacity building) Wajumbe wa Kamati.

Lengo la kutumia mbinu hizo tofauti ni kuwawezesha Wajumbe wa Kamati kujielimisha kwa kiwango cha kutosha katika nyanja ambazo wana wajibu wa kuisimamia na kuishauri Serikali.

### **1.3 Shughuli zilizotekeliza na Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha masharti ya kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge yanazingatiwa ipasavyo, Kamati ilipanga na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

#### **1.3.1 Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari ,2016 Kamati ilifanya ziara za ukaguzi Miradi ya Maendeleo inayotekeliza na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Miradi iliyohusika ni ambayo ilitengewa fedha katika mwaka wa fedha 2017/2018 na inatekelezwa katika Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Simiyu kama ifuatavyo: -

##### **i) Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

- Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF);
- Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA); na
- Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC).

ii) **Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

- Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA);
- Mfuko wa Maendeleo wa Vijana na Wanawake (Asilimia 10 ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri; na
- Ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kieletroniki.

**1.3.2 Kuchambua Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitekeleza jukumu hili ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Lengo la uchambuzi huo lilikuwa kuiwezesha Kamati kufanya ulinganisho kuhusu makadirio ya matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**1.3.3 Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Januari,2018 hadi Januari, 2019 Kamati ilipokea na kujadili Taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais. Madhumuni ya kujadili taarifa hizo za utekelezaji ni kuzingatia jukumu la kikanuni la kuksimamia na kuishauri Serikali ambalo pia msingi wake ni Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Mijadala ya taarifa hizo iliibua masuala mbalimbali ambayo ufanuzi wake unapatikana katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

### 1.3.4 Kushiriki katika Semina za Ndani

**Mheshimiwa Spika**, Wajumbe wa Kamati walishiriki katika semina mbalimbali zilizoandalifi na Ofisi ya Bunge (Legislative Support Programme), Wizara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais (TARURA) pamoja na Taasisi zisizo za Kiserikali ambazo zimekuwa zikifanya kazi na Kamati. Semina hizo zililenga kuwaongezea uelewa Wajumbe wa Kamati katika nyanja mbalimbali pamoja na kuwakumbusha kuhusu majukumu na wajibu wa Kibunge walio nao katika kuvisimamia na kuishauri Serikali.

### 1.3.5 Ziara za Ukaguzi wa Shughuli za Ofisi ya Rais

**Mhehimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua shughuli mbalimbali zinazotekeliza na Ofisi ya Rais, kupitia Taasisi na Idara zake. Ziara hizi zilitoa fursa kwa Wajumbe kujiridhisha kuhusiana na utekelezaji ikilinganishwa na Taarifa za utekelezaji ambazo ziliwasilishwa na Serikali kwenye Kamati.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

#### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii ya taarifa inaelezea kwa ufasaha, majukumu yaliyotekeliza na Kamati kwa kipindi chote cha mwaka mmoja. Uchambuzi wa kina wa matokeo ya shughuli hizo umefanyika kwa kuanisha Wizara, Taasisi na Idara iliyo husika na kuonesha mafanikio na changamoto. Aidha, ili kufafanua zaidi na kuongeza uelewa katika baadhi ya maeneo ya uchambuzi wa matokeo, sehemu hii itatumia takwimu na **vielelezo/michoro**.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Januari,2018 hadi Januari,2019 Kamati ilikutana na kutembelea Ofisi ya Rais kama ifuatavyo: -

**2.1.1 Ofisi ya Rais, Menejimet ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

- a) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF);
- b) Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC);
- c) Mfuko wa Kujitegemea wa Rais (PTF);
- d) Wakala wa Mafunzo kwa njia ya Mtandao (TaGLA);
- e) Mpango wa Kurasimisha Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)
- f) Taasisi ya Kupambana na kuzuia Rushwa (TAKUKURU); na
- g) Tume ya Utumishi wa Umma.

**2.1.2 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)**

- a) Wakala wa Barabara Mijini na Vijiji (TARURA);
- b) Mikoa Ishirini na Sita (26) ya Tanzania Bara;
- c) Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC);
- d) Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART);
- e) Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa;
- f) Wakala wa Barabara Mijini na Vijiji (TARURA);
- g) Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa (LGTI) – Hombolo; na
- h) Mfuko wa Pensheni wa LAPF.

**Mheshimiwa Spika**, mambo yatakayochambuliwa katika sehemu hii kuhusu Wizara, Taasisi na Idara zilizoanishwa hapo juu yamegawanyika kama maeneo yafuatavyo: -

- a) Uguzi wa Miradi ya Maendeleo;
- b) Uchambuzi wa Bajeti;
- c) Taarifa za Utekelezaji; na
- d) Ziara za uguzi wa shughuli za kiutendaji; na
- e) Uchambuzi wa Miswada.

## 2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati

### 2.2.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, ukaguzi wa miradi ya maendeleo ni mionganini mwa majukumu ya Kamati na hutekelezwa kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Ili kutekeleza jukumu hili, Kamati ilitembelea na kukagua miradi iliyotengewa na kuidhinishiwa fedha katika mwaka wa fedha 2017/2018 ambayo inatekelezwa na Ofisi ya Rais, katika Mikoa ya Simiyu, Shinyanga na Tabora.

Lengo la ukaguzi huo ni kuwawezesha Wajumbe wa Kamati kujiridhisha iwapo utekelezaji wa miradi hiyo unaendana na thamani halisi ya Fedha "*value for money*" iliyotolewa. Aidha, ukaguzi huo utasaidia Wajumbe wa Kamati kuwa na uelewa wa kutosha na hivyo kuweza kuishauri vyema Serikali wakati wa uchambuzi wa bajeti ya mwaka wa fedha unaofuata. Ifuatayo ni baadhi ya miradi iliyokaguliwa na Kamati: -

#### a) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu uko chini ya kifungu 1003 cha Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na utekelezaji wake umejikita katika kuzisaidia kaya maskini kukuza uchumi na hivyo kupunguza umaskini wa kipato. Kaya hizo zinawezeshwa kwa kupatiwa ruzuku ya fedha ili kuboresha maisha kwa kupata chakula, kuwezesha watoto kuhudhuria shulenii na kliniki kwa walio chini ya miaka mitano.

Ukiwa katika hatua ya tatu ya utekelezaji wake, mpango huu umeweza kufikia takribani Watanzania milioni 5.9 ambaao wameandikishwa ili kunufaika na uratatibu wa ruzuku. Idadi hiyo inatokana na kaya 1,118,751 ambazo kwa ujumla wake zimepokea ruzuku ya kiasi cha shilingi bilioni 147.6 katika awamu mbalimbali za malipo.

Aidha, katika kipindi hicho Kamati ilielezwa kuwa mpango huu umeweza kaya za walengwa 288,385

kuajiriwa katika utekelezaji wa miradi 3,682 yenyé thamani ya **shilingi billioni 13.3**. Miradi hiyo inatekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (42) na wilaya zote za Zanzibar kwa kuhusisha Vijiji 2,091, Mitaa 331 na Shehia 168.

**Mheshimiwa Spika**, mkoani Simiyu Kamati ilitembelea Mtaa wa Nyalikungu na Kijiji cha Shanwa katika Wilaya ya Maswa. Kamati ilibaini kwamba, katika kijiji cha Shanwa jumla ya kaya za walengwa 248 zinanufaika na mpango wa ruzuku na tayari zilikuwa zimepokea malipo kwa awamu kumi na sita (16).

Idadi hiyo ya kaya imepungua kwa asilimia 19 (kaya 60) kutoka kaya 308 za awali ambazo zilikuwa zinanufaika na mpango wa ruzuku. Kaya zilizoondolewa zilikosa sifa kufuatia zoezi la uhakiki ambalo liliendeshwa na mamlaka za usimamizi.

Aidha, Kamati ilibaini kwamba, mpango wa ruzuku kwa kaya masikini katika Kijiji cha Shanwa umekuwa na mafanikio makubwa kwani walengwa wameweza kutumia vizuri kiasi kidogo cha fedha wanachopata kuanzisha miradi ambayo imewawezesha baadhi yao kuboresha makazi yao.

Miongoni mwa wanufaika hao ni Bibi Monica Katambi Gwilasa (miaka 60), ambaye ametumia ruzuku kama chachu ya kujenga nyumba ya tofali ya vyumba vitatu na kuezeka kwa bati.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile TASAF imeshiriki kwa kiasi kikubwa katika kuboresha elimu ya Sekondari kwa kuchangia ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika Shule ya Sekondari Nyalikungu kwa kutoa jumla ya **shilingi milioni 29.6**.

Aidha, kupitia utaratibu wa kuwezesha mahudhurio ya shulenii kwa watoto wanaotoka kaya maskini, mfuko huu umeweza Wanafunzi 49 wa kidato cha I- IV kushiriki kikamilifu katika masomo ya sekondari kwa kupatiwa mahitaji muhimu kama vile sare za shule, madaftari, kalamu, viatu na matumizi mengine. Mahitaji hayo muhimu

yamesaidia kuboresha mahudhurio shulenii, na hivyo kupunguza utoro na mdondoko (drop out) kwa wanafunzi hao.

Aidha, wanufaika wengine wameweza kuboresha maisha yao kwa kuinua kipato cha kiuchumi kuitia shughuli wanazozifanya kama vile ufugaji wa mbuzi na kuku, kupika na kuuza chakula, biashara ndogo za kuuza nguo na kilimo cha mbogamboga.

Vile vile, kuitia utaratibu huu, wanufaika wameendelea kuhimizwa kutumia sehemu ya fedha za ruzuku wanazopokea kuijunga na mfuko wa bima ya afya ya jamii (CHF), ili waweze kupata huduma ya afya.

**b) Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

**Mheshimiwa Spika**, MKURABITA unatekelezwa chini ya kifungu 1003 *Policy and Planing* cha Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Mpango huu unaandaa na kusimamaia mfumo wa kitaifa wa umiliki wa raslimali na uendeshaji wa biashara unaotambulika na kukubalika kisheria. Kuitia mpango huu wananchi wanyonge wanawezeshwa kurasimisha ardhi na biashara wanazomiliki na kuzitumia kujikwamua kiuchumi.

Vilevile, mpango huu unahamasisha na kuchangia ujenzi wa Masijala za Ardhi katika Vijiji/Mitaa ili kuwezesha uhifadhi madhubuti na salama wa Nyaraka '(Hati za Hakimiliki za Kimila na Nyaraka nyingine) za urasimishaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea vijiji vya Segese na Lunguya katika Halmashauri ya Msalala ambavyo vimefanyiwa mpango wa matumizi bora ya ardhi chini ya uwezeshaji wa MKURABITA. Katika vijiji hivyo ambavyo ni asilimia 2.17 ya vijiji vyote 92 vya halmashauri hiyo, MKURABITA imeweza kushirikiana na halmashauri kupima jumla ya mashamba 2,158 na kutoa hati za hakimiliki

za kimila 274 (Kijiji cha Segese – 205 na Kijiji cha Lunguya - 69).

Aidha, miongoni mwa mafanikio ya kuigwa katika maeneo haya ni wanawake kuwezesha kumiliki ardhi peke yao au kwa ubia na waume zao. Vilevile, urasimishaji umewezesha mpango bora wa matumizi ya ardhi katika vijiji hivyo kwa kutengwa maeneo ya makazi, kilimo, ufugaji, hifadhi za misitu, malisho na huduma nyingine za jamii.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo ambayo yalishuhudiwa na Kamati, ilibainika kwamba mgawanyo wa halmashauri uliofanyika umechangia kwa kiasi kikubwa katika upotevu wa takwimu na upungufu wa Wataalamu wa ardhi jambo linaloathiri mwendelezo wa zoezi la urasimishaji.

Kamati inaishauri Serikali ihakikishe inatatua changamoto ya uhaba wa wataalam wa ardhi kwa kuajiri wataalam zaidi, sambamba na kutenga bajeti ya kutosha ili kuwezesha MKURABITA kuyafikia maeneo mengi zaidi ambayo hayajarasimishwa.

c) **Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)**

**Mheshimiwa Spika**, chuo hiki kilianzishwa kwa ajili ya kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika nyanja za uongozi, menejimenti na utawala. Pia chuo kinajihuisha na utafiti na kutoa ushauri wa kitaalam na kutoa machapisho ya kitaalam katika utumishi wa umma.

Kutokana na umuhimu wa chuo hiki, Serikali imekiwezesha kuanzisha Kampasi Sita (6) ambazo ziko Dar es Salaam, Mtwara, Singida, Tabora, Tanga na Mbeya.

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhisha kuhusu utendaji wa chuo hiki na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Kamati ilitembelea Kampasi ya Tabora ambayo ilikuwa ikitekeleza ukarabati wa jengo la Shaban Robert. Kukamilika kwa ukarabati huu kutawezesha chuo kuwa na ofisi za kutosha

kwa Watumishi wake na kupunguza changamoto ya uhaba wa vyumba vyataga madarasa.

Hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba, ukarabati wa jengo hili umechukua muda mrefu sana kutohakana na bajeti finyu inayotengwa pamoja na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Kwa mantiki hiyo, ni ushauri wa Kamati kwamba Serikali iongeze bajeti kwa ajili ya mradi huu na zipatikane kwa wakati ili kukamilisha ukarabati huo na hivyo kuleta thamani ya fedha katika utekelezaji wa mradi huo.

**d) Local Government Own Source Project (Mfumo wa Ukusanyaji Mapato kwa njia ya Kieletroniki - (LGRCIS)**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatekelezwa chini ya Kifungu 8091 cha Fungu 85 – Mkoa wa Tabora. Lengo la mradi huu ni kuiwezesha Serikali kuongeza mapato kwa kuboresha njia na mfumo wa ukusanyaji wa mapato (*revenue collection system*).

Mfumo huu umeiwezesha Serikali kuachana na matumizi ya vitabu na mawakala katika ukusanyaji wa mapato, na hivyo kuepuka upotevu mkubwa wa mapato kutohakana na upotevu wa kumbukumbu na mawakala wasio waaminifu.

Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wa kuanzisha na kusimamia kikamilifu mfumo wa ukusanyaji mapato kwa njia ya kieletroniki ‘*Local Government Revenue Collection Information System*’ ambao sasa unatumika katika Halmashauri zote 185 nchini, ikiwa ni miaka miwili tu tangu ulipoanzishwa rasmi katika mwaka wa fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ilianza na ununuzi wa mashine za kukusanya mapato katika mwaka wa fedha 2015/2016 na hadi Kamati inafanya ziara tayari mashine hamsini na tisa (59) zilikuwa zimenunuliwa na hivyo kubakiza hitaji la mashine ishirini na sita zaidi ili kufikia lengo la mashine themanini na tano (85) zinazohitajika.

Vile vile, ili kujiridhisha na matumizi ya mfumo huu Kamati iliweza kutembelea na kukagua maeneo ya biashara katika Soko Kuu la Tabora lenye jumla ya mashine 9 za kukusanya mapato (POS), na Stendi ya Mabasi yaendayo mikoani ambayo inatumia mashine mbili tuu za POS.

Kamati ilibaini changamoto ya mtandao na hivyo kushauri Serikali iboreshe upatikanaji wa mtandao huu ili kuondoa usumbufu kwa walipaji. Aidha, kuwe na makubaliano ya pamoja baina ya Benki ya NMB na TAMISEMI kuhusu namna ya kuufanya mtandao huu kuwa rahisi na rafiki kwa watumiaji.

**e) Programu ya Uimarishaji Miji (Urban Local Government Strengthening Programme -ULGSP).**

**Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa barabara za manispaa kwa kiwango cha lami unatekelezwa chini ya Programu ya Uimarishaji Miji (ULGSP) ambapo Manispaa ya Shinyanga ni mionganii mwa wanufaika wapatao 18. Katika Manispaa hii Kamati ilitembelea na kukagua barabara zenye urefu wa kilomita 4.370 ambazo zilikuwa zimeweka lami, sawa na asilimia 33.36 ya kilomita 13.1 zilizo katika mkataba uliosainiwa kati ya Manispaa na Mkandarasi Jassie & Co. Ltd (JASCO) wa Mwanza kwa gharama ya **shilingi bilioni 15.438**(bila VAT).

Aidha, hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu tayari Mkandarasi alikuwa amelipwa jumla ya **shilingi bilioni 5.61** kiasi ambacho ni sawa na asilimia ya 36.34 ya fedha yote ya mradi.

Utekelezaji wa mradi huu umekuwa na manufaa kwa kuongeza mtandao wa barabara za lami katikati ya Mji wa Shinyanga, jambo ambalo limechangia kuongeza thamani kwa maeneo ya makazi yaliyo jirani na barabara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya mafanikio yaliyoshuhudiwa na Kamati, zipo changamoto kadhaa ambazo zilibainika na hivyo kuathiri utekelezaji na usimamizi mzuri wa mkataba. Mionganini mwa changamoto hizo ni mahusiano hafifu baina ya Wataalam wa Manispaa ya Shinyanga na Wakala wa Barabara Mijini na Vijiji (TARURA) ambayo yamesababisha kutosimamiwa kikamilifu mkandarasi anayetekeleza mradi huo.

Kamati inashauri pande mbili hizi kujenga mahusiano mazuri ya kikazi ili kuwezesha usimamizi mzuri wa miradi ya barabara katika Manispaa ya Shinyanga. Aidha, mkataba baina ya mkandarasi na Manispaa ya Shinyanga upitiwe upya ili kurekebisha na kuondoa kasoro zilizobainika na hivyo kuwezesha mradi kutekelezwa kwa tija na thamani halisi ya fedha.

**f) Local Government Own Source Projects (Mfuko wa Maendeleo kwa Vijana na Wanawake)**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ultengewa jumla ya Shilingi milioni 471.45 na ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 8091 cha Fungu 47 - Mkoa wa Simiyu. Mradi huu ni sehemu ya jithiada za Serikali za kuwawezesha kiuchumi Wanawake na Vijana kuititia asilimia (10%) ya mapato ya ndani ya kila Halmashauri nchini. Kuititia utaratibu huu Wanawake na Vijana wamejengewa uwezo wa kubuni miradi na kupata mitaji ya kuitekeleza na hivyo kujikwamua kiuchumi.

Kamati ilitembelea Kikundi cha Vijana ambacho kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Maswa kimeanzisha Kiwanda cha Chaki kilichopo Maswa Mjini. Katika Kiwanda hicho, Kamati ilipata fursa ya kujionea shughuli za uzalishaji na ufungashaji (*production and packaging*).

Aidha, Kamati ilielezwu kwamba kikundi hicho cha vijana kinamiliki asilimia 40 ya hisa katika mradi huo wenye thamani ya shilingi milioni 100 na ambao unamilikiwa kwa ubia na Halmashauri ya Wilaya ya Maswa.

**Mheshimiwa Spika**, Vijana hao walianza na mtaji wa Shilingi milioni moja (1,000,000) kabla ya kupata fedha kutoka mfuko wa uwezeshaji wa Vijana wenye thamani ya shilingi milioni 30.

Kutokana na mafanikio yaliyobainika, mradi huo umeingizwa katika kundi la miradi ya kimkakati ya halmashauri na umetengewa kiasi cha **shilingi bilioni 4** kwa ajili ya upanuzi wa kiwanda hicho ili kiweze kuzalisha bidhaa nyingine za kimkakati kama vile vifaa tiba na vifaa vya ujenzi.

Aidha, licha ya mafanikio hayo bado kuna changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na vijana kukosa elimu ya ujasiriamali na kushindwa kurudisha kikamilifu marejesho ya fedha walizokopeshwa na mfuko.

**Mheshimiwa Spika**, ni ushauri wa Kamati kwamba, Halmashauri ziwatumi Maafisa Maendeleo ya Jamli kutoa elimu ya kutosha kuhusu ujasiriamali kwa vikundi vya Wanawake na Vijana ili kuwezesha vikundi vinavyoanzishwa kukua na kuimarika kiuchumi na hivyo kusaidia makundi hayo.

## 2.2.2 Uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kukamilisha ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ilijikita katika uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais ili kutimiza masharti ya Kanuni ya 98 (2), ikisomwa pamoja na kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Bajeti ya Ofisi ya Rais inahusisha Mafungu 28 kutoka Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na Mafungu 8 kutoka Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Uchambuzi ulijikita katika kuititia Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali, kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Vikao vya Uchambuzi wa Bajeti vilifanyika kama ifuatavyo: -

### 2.2.3 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa bajeti katika Ofisi hii ulihusisha mafungu yafuatayo:-

- 1) Fungu 56 – Ofisi ya Rais – TAMISEMI
- 2) Fungu 2 - Tume ya Utumishi wa Waalimu (TSC)
- 3) Fungu 70 – Mkoa wa Arusha
- 4) Fungu 78 – Mkoa wa Mbeya
- 5) Fungu 79 – Mkoa wa Morogoro
- 6) Fungu 88 – Mkoa wa Dar es Salaam
- 7) Fungu 63 – Mkoa wa Geita
- 8) Fungu 90 – Mkoa wa Songwe
- 9) Fungu 89 – Mkoa wa Rukwa
- 10) Fungu 80 – Mkoa wa Mtwara
- 11) Fungu 81- Mkoa wa Mwanza
- 12) Fungu 84 – Mkoa wa Singida
- 13) Fungu 85 – Mkoa wa Tabora
- 14) Fungu 75 – Mkoa wa Kilimanjaro
- 15) Fungu 71 – Mkoa wa Pwani
- 16) Fungu 36 – Mkoa wa Katavi
- 17) Fungu 73 – Mkoa wa Iringa
- 18) Fungu 87 – Mkoa wa Kagera
- 19) Fungu 54 – Mkoa wa Njombe
- 20) Fungu 74 – Mkoa wa Kigoma
- 21) Fungu 76 – Mkoa wa Lindi
- 22) Fungu 47 – Mkoa wa Simiyu
- 23) Fungu 95 – Mkoa wa Manyara
- 24) Fungu 77 – Mkoa wa Mara
- 25) Fungu 72- Mkoa wa Dodoma
- 26) Fungu 82 – Mkoa wa Ruvuma
- 27) Fungu 83 – Mkoa w Shinyanga
- 28) Fungu 86 – Mkoa wa Tanga

**Mheshimwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ulizingatia makusanyo ya maduhuli kwa kulinganisha na malengo na mwenendo wa upatikani wa fedha za matumizi kutoka Hazina kwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa

i)      **Ukusanyaji Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2018 jumla ya **shilingi bilioni 9.95** zilikuwa zimekusanywa na Fungu 56, kiasi ambacho ni sawa na asilimia 43.7 ya mapato yaliyotarajiwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2017/18. Pamoja na kwamba, kiwango cha ukusanyaji kilikuwa chini, kiasi kilichopatikana kwa wakati huo kiliongezeka kwa zaidi ya asilimia 15 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 28 ambacho kilikusanywa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, baadhi ya sababu ziliochangia kutofikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa maduhuli ni pamoja na mauzo machache ya nyaraka za zabuni na vifaa chakavu vyta ofisi, halmashauri nyingi kushindwa kuwasilisha michango yao kwenye Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa na Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa kushindwa kupata shilingi bilioni 1.2 ilizotarajia kuzipata kutoka CRDB. Aidha, hakuna ubunifu wa vyanzo vipyta vyta mapato pamoja na kukosa uhalisia wakati wa kupanga malengo ya ukusanyaji.

**Mheshimiwa Spika**, taswira inayopatikana kutokana na uchambuzi wa Kamati ni kwamba, pamoja na ukusanyaji kutofikia angalau asilimia 70 ambayo ingepaswa kuwa imefikiwa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha, kuna ongezeko katika ukusanyaji wa maduhuli.

Hata hivyo, ni maoni ya Kamati kwamba utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na Ofisi hii kwa kutegemea fedha za ndani utaendelea kusuasua kwa kuwa bajeti ya shughuli hizo hupangwa kwa kuzingatia malengo ya makusanyo yaliyowekwa.

Ni vyema Ofisi ya Rais – TAMISEMI ikazingatia makadirio halisi ya makusanyo kutokana na vyanzo vilivyopo ili kuweza kuwa na makusanyo halisi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Mikoa na Serikali za Mitaa hadi kufikia mwezi Februari, 2018 makusanyo yalikuwa ni **shilingi bilioni 347.19**, kiasi ambacho ni sawa na asilimia 50 ya lengo. Ingawa kiasi hiki kiko chini ya lengo la angalau asilimia 70 hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka wa fedha, kiwango cha makusanyo katika Serikali za Mitaa ni kikubwa. Sababu inaweza kuwa ni vyanzo vingi vya makusanyo na wingi wa watu katika halmashauri ikilinganishwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Taasisi zake.

ii) **Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, umebaini kwamba hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 na kiasi kinachotolewa na Hazina.

Kutokana na uchambuzi huo imebainika kwamba, fedha iliyotolewa ni kidogo ikilinganishwa na mpango wa upatikanaji fedha (*cash flow plan*) uliowekwa, kiasi cha fedha kinachotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni kikubwa ikilinganishwa na matumizi ya maendeleo; na fedha hazikupatikana kwa wakati, jambo ilioathiri utekelezaji wa mipango ya bajeti kwa Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2018 Ofisi ya Rais – TAMISEMI pamoja na Taasisi zilizo chini yake, ilikuwa imepokea **shilingi bilioni 245.18** kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 53 ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii.

Mwenendo wa upatikanaji wa fedha unaonesha kwamba, kiasi hicho kilichopatikana katika kipindi hicho kimepungua kwa takribani asilimia 4 ikilinganishwa na kipindi kama hicho katika Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 ambapo ilikuwa ni asilimia 57.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida hadi kufikia Februari, 2018 kiasi kilichopokelewa ni **shilingi bilioni 29** sawa na asilimia 69 ya fedha iliyoidhinishwa. Kiasi hicho ni ongezeko la asilimia 5 ikilinganishwa na asilimia 64 katika mwaka wa fedha 2016/17.

Aidha, hadi kufikia mwezi Februari, 2018, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi bilioni 216.1** kutoka Hazina kwa ajili ya maendeleo, sawa na asilimia 52 ya fedha yote iliyoidhinishwa. Kiasi hicho kimepungua kwa takribani asilimia 4 ikilinganishwa na asilimia 56 iliyopokelewa katika mwaka wa fedha 2016/17.

**Mheshimiwa Spika**, wastani wa upatikanaji wa fedha za fedha (Matumizi ya Kawaida na Maendeleo) katika Mwaka wa Fedha 2017/18 ulikuwa ni asilimia 60.5, sawa na kiwango kilichoshuhudiwa katika kipindi kama hicho mwaka wa Fedha 2016/17.

### **iii) Utekelezaji wa Maoni ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi ulibaini kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilizingatia maoni na ushauri wa Kamati kwa kiwango cha kuridhisha kwa kutatua changamoto zilizobainishwa na Kamati wakati wa uchambuzi wa bajeti.

Kuzingatiwa kwa maoni na ushauri wa Kamati kumechangia uboreshaji wa huduma za msingi kwa maendeleo ya jamii. Hata hivyo, bado Kamati iliitaka Serikali kufanya kazi maoni ambayo yalikuwa hayajatekelezwa ili kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya maeneo yaliyoboreshwa kwa kuzingatia ushauri na maoni ya Kamati ni pamoja na: -

i. Halmashauri kubuni vyanzo vipya vyaa mapato ili kuepuka utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu. Hadi kufikia Februari, 2018 Halmashauri 21 ziliweza

kubuni miradi mbalimbali ya kimkakati kama vile ujenzi wa stendi za mabasi, masoko, maeneo ya maegesho, machinjio na kilimo cha umwagiliaji. Miradi hiyo ilikidhi vigezo na Serikali ilitenga shilingi **bilioni 131.5** katika mwaka huu wa fedha ili iweze kutekelezwa; na

ii. Serikali ihakikishe Halmashauri zote zinatumia mfumo wa kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ya ndani (*Local Government Revenue Collection Information System - LGR CIS*), ambapo hadi kufikia Disemba, 2017 Halmashauri zote 185 sawa na asilimia 100 zilikuwa zinatumia Mfumo huu.

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya maoni yamefanyiwa kazi, lakini Kamati iliona kuna umuhimu wa Serikali kuendelea kuyaboresha zaidi ili kuleta ufanisi katika utendaji. Maoni hayo ni pamoja na:

i. Kuhakikisha Halmashauri zinaandaa na kutunza takwimu sahihi kuhusiana na idadi ya vikundi vyta Wanawake na Vijana, vinavyopokea na kurejesha fedha zinazotokana na asilimia kumi (10%) ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri;

Aidha, Halmashauri zitenge kikamilifu fedha na kuzipeleka kwa wahusika. Uchambuzi ulibaini kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2018 wastani wa kutenga fedha hizo ulikuwa ni asilimia 25.5 tu. Kiwango hicho ni kidogo sana na jambo hili linahitaji msisitizo wa Serikali;

ii. Halmashauri kushirikiana na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi, kwa kuainisha maeneo ya kilimo, ufugaji na matumizi mengine, jambo litakalosaidia kuepusha migogoro ya ardhi baina ya Wakulima na Wafugaji; na

iii. Serikali kutoa fedha za Miradi ya Maendeleo kwa wakati ili kuwezesha Halmashauri kulipa madeni ya watoa huduma na Wakandarasi kwa wakati na hivyo

kuepusha ongezeko la gharama katika miradi inayotekelizwa. Hadi mwezi Februari, 2018 Halmashauri zilikuwa zimepokea asilimia 51 tu ya fedha za maendeleo, kiasi ambacho ni kidogo na kingesababisha utekelezaji wa miradi kuathirika.

**iv) Makadirio ya mapato kwa mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza malengo yaliyokusudiwa, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Halmashauri, ziliomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 6,582,946,851,733/=**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 4,522,965,704,000/=** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **Shilingi 1,799,436,057,500/=** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Aldha, katika fedha hizo **Shilingi 4,134,200,811,930/=** sawa na asilimia 62.8 ni kwa ajili ya Mishahara, na **Shilingi 649,309,982,303/=** sawa na asilimia 9.8 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi umebaini kwamba, bajeti hiyo iliongezeka kwa **shilingi bilioni 14.1** (sawa na asilimia 0.07) ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018. Hata hivyo ongezeko hilo ni kidogo ikilinganishwa na ongezeko katika mwaka wa fedha 2016/2017 ambalo lilikuwa ni asilimia 8.5. Tafsiri inayojitokeza hapa ni kwamba, kumekuwa na ongezeko kwa kiwango cha kupungua (*increasing at decreasing rate*) kutoka asilimia 12 katika mwaka wa fedha 2016/2017, asilimia 8.5 katika mwaka wa fedha 2017/2018 na sasa asilimia 0.07 katika mwaka wa fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa makusanyo katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, ilikadiria kwamba jumla ya **Shilingi 758,362,711,799** zitakusanywa. Kiasi hicho ni ongezeko la asilimia 5.9 ikilinganishwa na **Shilingi 44,778,191,187** zilizokusanywa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Uchambuzi ulibaini kwamba, ongezeko la makusanyo hayo linatarajiwaka kuchangiwa kwa kiasi kikubwa na Halmashauri nchini ambazo zimeendelea kuimarisha matumizi ya mashine za kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato.

**Mheshimiwa Spika**, ingawa uchambuzi ulibaini ongezeko la jumla la **asilimia 5.9** katika ukusanyaji wa mapato ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka uliotangulia, makusanyo ya Mikoa yilibainika kushuka kwa kiwango cha kutisha cha asilimia 96.2 (**shilingi bilioni 3.38**) sababu kubwa ikiwa ni Hospitali za Rufaa za Mikoa kuhamishiwa Wizara ya Afya na hivyo makusanyo yote yaliyokuwa yakikusanywa kwa mfumo wa GoT – HoMIS kuondoka. Ni wazi kwamba utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika mikoa umeathirika kutokana na kuondolewa kwa vyanzo hivyo vya mapato.

**Mheshimiwa Spika**, ulinganisho wa bajeti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI na Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 unaonesha kwamba, wakati bajeti ya Taifa iliongezeka kwa asilimia 2.53 kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2017/2018, bajeti ya TAMISEMI katika kipindi hicho imeongezeka kwa asilimia 0.07 tu, ongezeko ambalo ni dogo sana.

Aidha, uchambuzi umebaini zaidi kwamba, bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ni sawa na **asilimia 20.27** ya bajeti ya Taifa. Uwiano huo umepungua katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, kutoka uwiano wa **asilimia 24** mwaka wa fedha 2015/16.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kupungua huko, bado ni jambo lisilopingika kwamba, Ofisi ya Rais TAMISEMI ndiyo inabeba sehemu kubwa ya bajeti ya nchi yetu ikilinganishwa na Wizara nyingine, kutokana na kusimamia kila sekta katika ngazi za Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Ni kwa mantiki hiyo, Kamati inashauri bajeti ya ofisi hii iendelee kuongezwa, badala ya kupungua.

#### 2.2.4 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

**Mheshimiwa Spika**, katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utawala Bora, Kamati ilifanya uchambuzi wa mafungu yafuatayo: -

1. Fungu 20 – Ikulu;
2. Fungu 30 – Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;
3. Fungu 32 – Menejimenti ya Utumishi wa Umma;
4. Fungu 33 – Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
5. Fungu 67 – Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;
6. Fungu 94 – Tume ya Utumishi wa Umma;
7. Fungu 09 – Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma; na
8. Fungu 04 – Idara ya kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

##### a) **Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, umebaini kwamba hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa Fedha 2017/2018 na kiasi kilichotolewa na Hazina. Aidha, mtiririko wa fedha iliyo tolewa haukuwa mzuri kwa sababu kiasi kilichoidhinishwa kilikuwa kinatolewa kidogo ikilinganishwa na mpango wa upatikanaji wa fedha (cash flow plan) ulioandaliwa.

Uchambuzi umebainisha kwamba hadi kufikia mwezi Februari, 2018 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, pamoja na mafungu yaliyo chini yake, ilikuwa imepokea kutoka Hazina jumla ya **shilingi bilioni 417.7**, kiasi ambacho ni sawa na asilimia 50.89 ya Fedha yote iliyo idhinishwa.

Kamati ililinganisha hali hiyo ya upatikanaji wa Fedha kwa mwaka 2017/2018 na mwaka 2016/2017 na kubaini kuwa kiasi hicho cha Fedha kilipungua kwa takribani **shilingi bilioni 109.3** sawa na asilimia 20.74 ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2016/2017 ambacho kilikuwa ni shilingi bilioni 527.1

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa fedha za maendeleo uchambuzi ulibaini kwamba hadi kufikia mwezi Februari, 2018 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mafungu yake ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi bilioni 206.72** kutoka Hazina, kiasi ambacho ni sawa na asilimia 52.87 ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya maendeleo. Kiasi hicho kilipungua kwa asilimia 16.26 ikilinganishwa na kiasi kilichopokelewa kwa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2016/2017 ambacho kilikuwa ni **shilingi bilioni 246.78**.

Kamati imebaini kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ujumla haukuwa mzuri, kwani fedha zilizopatikana ziliikuwa ni takribani asilimia 50.37 ya fedha zote zilizoidhinishwa. Aidha, mtiririko wa fedha kutoka hazina haukuwa mzuri ikilinganishwa na miaka iliyopita kwani, kiasi kinachotolewa kiliendelea kupungua. Vile vile, kasumba ya fedha za matumizi ya kawaida kuwa nydingi ikilinganishwa na fedha za maendeleo imeendelea kujitokeza.

#### **b) Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ilizingatia kikamilifu baadhi ya maoni ya Kamati, na ilikuwa inaendelea kuzingatia yaliyosalia. Baadhi ya maoni na ushauri vilivyozingatiwa ni kuhusu: -

i) Serikali kutoa mchango wake wa fedha katika utekelezaji wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, ambapo katika mwaka uliopita ilitoa jumla ya **shilingi milioni 750** kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huo;

ii) Serikali kuelimisha taasisi za kifedha uhalali wa hati za hakimiliki za kimila kutumiwa kama dhamana kwa ajili ya mikopo. Aidha, MKURABITA inatumia taasisi hizo za fedha kuwaelimisha wamiliki wa ardi wenye hati hizo namna ya kuandaa mpango kazi kuhusu mikopo watakayoichukua. Tayari wakulima 105 kutoka Halmashauri ya Wilaya za Kilosa na Mji wa Njombe wamekopeshwa **shilingi bilioni 3.8** kutoka Benki ya Kilimo kwa dhamana ya hati hizo;

iii) Kuongeza bajeti ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, ambapo katika mwaka huu wa fedha Serikali imeongeza jumla ya **shilingi bilioni 2.95** kwa chombo hiki.

iv) Serikali iajiri watumishi ili kuziba pengo lilllosababishwa na kuondolewa kwa watumishi wasio na sifa baada ya uhakiki wa Watumishi, ambapo Serikali imeanza na inakamilisha utaratibu wa kuajiri watumishi 52,436.

**c) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza malengo yaliyokusudiwa, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, iliomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 669.09** kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 473.12** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 195.97** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, bajeti iliyoombwaa kuidhinishwa katika mwaka huu wa fedha ilipungua kwa **shilingi bilioni 152.23** (sawa na asilimia 18.53) ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 ambayo ilikuwa **shilingi bilioni 821.32**. Upungufu huo ni mkubwa sana kwani ni takribani mara tatu ya upungufu ulioshuhudiwa katika mwaka wa fedha uliomalizika ambaao ulikuwa ni asilimia 6.89.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa bajeti ya maendeleo, uchambuzi ulibaini kwamba, kiasi kilichoombwa kuidhinishwa kilipungua kwa **shilingi bilioni 194.99** (sawa na asilimia 49.88) ikilinganishwa na kiasi cha **shilingi 390.97** kilichoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2017/18.

Uchambuzi umebaini zaidi kwamba, kiasi kilichopungua ni kikubwa sana kwani ni zaidi ya mara tatu ya kilichobainika kupungua katika mwaka wa fedha unaomalizika ambacho kilikuwa **asilimia 16.13**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ili kubaini ni kwa kiasi gani ongezeko la Bajeti ya Taifa linaathiri mwenendo wa bajeti ya ofisi hii, katika mwaka huu wa fedha. Mambo yallyobainika ni haya yafuatayo:-

i) Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2018/19 ambayo ni **shilingi bilioni 669** ni sawa na asilimia 2.06 ya Bajeti ya Taifa ambayo ni **shilingi trilioni 32.476**;

ii) Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2018/19 unaonesha ongezeko la bajeti kwa asilimia 2.45, ikilinganishwa na Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2017/18; lakini bajeti ya jumla ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2018/19 imepungua kwa asilimia 18.59 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa fedha 2017/18;

iii) Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaonesha ongezeko la asilimia 0.06 katika fedha za maendeleo, kwa mwaka wa fedha 2018/19, wakati bajeti ya maendeleo kwa Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambayo ni sawa na asilimia 0.60 ya Bajeti ya Taifa, imepungua kwa asilimia 49.88 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2017/18.

## 2.2.5 Kupokea na kujadili taarifa za Utekelezaji

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitekeleza jukumu hili ikiwa ni uzingatiaji wa masharti ya Kifungu cha 7 (1) (c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari,2016.

### a). Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA)

**Mheshimiwa Spika**, Wakala huu ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala za Serikali, Sura 245 na kuanza kutekeleza majukumu yake tarehe 2 Julai, 2017. Kuanzishwa kwa wakala huu ni muendelezo wa utekelezaji wa mabadiliko (*reforms*) kwenye sekta ya ujenzi na barabara yaliyoanza mwaka 1998 ambayo ni pamoja na marekebisho ya Road Tolls Act, kuanzishwa kwa Mfuko wa Barabara (RF), TANROADS na sasa TARURA.

TARURA ambayo inahudumia mtandao wa barabara wenyewe jumla ya **kilomita 108,946** ina majukumu makubwa ya ujenzi, ukarabati na matengenezo barabara za Vijijini na Mijini pamoja na madaraja na mpango mkakati wa kuondoa vikwanzo ili barabara ziweze kupidika muda wote. Aidha, TARURA inatarajiwa kuimarisha barabara zinazopita kwenye maeneo muhimu yenye viwanda na kilimo na hivyo kusaidia shughuli za kiuchumi na kijamii.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya utekelezaji wa kazi za matengenezo ya barabara inaonesha kwamba, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali kupitia Mfuko wa Barabara ilitenga **shilingi bilioni 247.70** kwa TARURA. Hadi kufikia Juni 30, 2018 fedha iliyokuwa imetolewa ilikuwa **shilingi bilioni 179.3** ambayo ni sawa na asilimia 72.4. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 **shilingi bilioni 243.2** zimetengwa na Serikali kupitia Mfuko wa Barabara kwa ajili ya TARURA kutekeleza majukumu yake.

Kamatii inatambua kazi nzuri inayofanywa na TARURA katika maeneo mbalimbali nchini, kwa lengo la kuhakikisha barabara hizo zinapitika wakati wote. Hatua hiyo inaondoa

keru kwa wananchi na hivyo kuwawezesha kutekeleza shughuli za kiuchumi na uzalishaji kama vile kilimo, biashara n.k

**Mheshimiwa Spika**, ni mtazamo wa Kamati kwamba ili TARURA iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi inapaswa kuondokana na changamoto zinazoikabili ambazo ni pamoja na ufinyu wa bajeti ikilinganishwa na mtandao wa barabara nchini, upungufu wa watumishi na vitendea kazi (hasa magari) na majengo ya ofisi.

Kamati inafikiri njia mojawapo ya kuongeza uwezo wa kifedha wa wakala hii ni kuongeza mgawo wa fedha kutoka Mfuko wa Barabara (RF) kutoka asilimia 30 ya sasa hadi asilimia 50.

Aidha, Serikali iwezeshe wakala huu kutunga sheria ndogo ndogo kwa lengo la kuzuia uharibifu wa miundombinu ya barabara na kuwezesha barabara hizo kudumu kwa muda mrefu.

**b). Mkakati wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari za Serikali Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, mkakati huu unalenga kurudisha shule kongwe katika ubora wake baada ya miundombinu yake kuchakaa na kuharibika kwa kiwango kikubwa. Mkakati huu ulianza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 na unagharamiwa na Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (Education Program For Results – EPSR).

Jumla ya shule 89 kongwe zitakarabatiwa kwa awamu ambapo awamu ya kwanza yenye shule 49 ilianza kutekelezwa mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha, maandalizi kwa ajili ya awamu ya pili yenye shule 17 yameanza.

Jumla ya **shilingi bilioni 35.58** zilitengwa kutumika katika awamu ya kwanza ya ukarabati, na hadi Oktoba, 2018 wakati Kamati inapokea taarifa kuhusu mkakati huu

tayari **shilingi billioni 22.43** (sawa na asilimia 63.04) zilikuwa zimetumika na ukarabati kukamilika kwa baadhi ya shule, huku ukiendelea katika shule nyingine.

Kamati ilitembelea Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Ihungo iliyoko Mkoani Kagera ambayo ni miongoni mwa shule zilizokarabatiwa ili kujionea kazi iliyofanyika.

**Mheshimiwa Spika**, shule hii imejengwa upya na Serikali kwa kushirikiana na Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (*Deparment for International Development - DfID*) kufuatia kuathiriwa vibaya na tetemeko lilitotokea mkoani Kagera, mwezi Septemba, 2016.

Kiasi kilichotengwa kwa ajili ya ujenzi wa shule hii ni **shilingi billioni 10.5** kwa ajili ya ujenzi wa majengo matatu ya madarasa yenye vyumba 24 na ofisi 8, Jengo la vyoo lenye ghorofa moja, majengo matatu ya mabweni yenye jumla ya vyumba 288, nyumba thelathini (30) za Walimu na mifumo ya maji taka.

Wakati Kamati inatembelea shule hii mwezi Juni, 2018 ujenzi ulikuwa umefikia asilimia 80.5 na ultarajiwaa kukamilika mapema ili kuruhusu shule kuchukua wanafunzi wa kidato cha tano, jambo ambalo lilitifanyika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza kwa dhati hatua ya Serikali kukarabati shule kongwe nchini, kwani itawezesha kurejesha heshima ya shule hizo pamoja na kuongeza ari ya utendaji kwa Walimu kutokana na mazingira mazuri ya kazi.

Pamoja na kazi nzuri inayofanyika, bado kuna changamoto iliyoshuhudiwa na Kamati na ambayo inatia doa juhudi za Serikali katika mkakati huu. Changamoto hiyo ni Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ambaye amepewa kadhi katika shule kadhaa nchini, kushindwa kutimiza majukumu yake kikamilifu na hivyo kukiuka masharti ya mikataba aliyosaini ili kutekeleza ujenzi au ukarabati.

Ni ushauri wa Kamati kwamba, Ofisi ya Rais – TAMISEMI irejee (*review*) mikataba yote ambayo imeingia na TBA kuhusu ujenzi na ukarabati wa shule kongwe, na iwapo itabaini kasoro za utekelezaji basi hatua stahiki zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kusitisha au kuvunja mkataba kwa mujibu wa sheria.

**c). Programu ya Usambazaji Maji safi na salama Vijijiini**

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Programu hii uko katika awamu ya pili na unalenga kuongeza na kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo ya vijijiini. Malengo hayo yanaenda sambamba na Sera ya Maji ya Taifa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015, ambazo mionganoni mwa mambo mengine zinalenga kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira unafikia asilimia 85 katika maeneo ya vijijiini na asilimia 90 katika maeneo ya mijini ifikapo mwaka 2020.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inasimamia programu hii kwa sababu ndiyo yenyeye jukumu la kuratibu na kusimamia sera ya ugatuaji wa madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda Mamlaka za Serikali za Mitaa na huko ndiko programu za maji zinafanyika kwa kiwango kikubwa kwa kushirikisha wananchi. Aidha, ni muhimu kukumbuka kwamba, Ofisi ya Rais – TAMISEMI inafanya kazi kwa karibu na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kupongeza juhudzi za Serikali katika kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama kwa kutenga fedha za kutosha kugharamia Mpango wa Usambazaji Maji Safi na Salama Vijijiini.

Katika mwaka huu wa fedha Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 254.87** kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maji, kutekeleza kampeni ya usafi wa mazingira na usimamizi wa miradi. Ili kuhakikisha kunakuwa na usimamizi madhubuti Ofisi ya Rais – TAMISEMI

Makao Makuu iliidhinishiwa **shilingi milioni 332** kwa ajili ya uratibu na usimamizi wa miradi ya maji na Sekretarieti za Mikoa ziliidhinishiwa **shilingi bilioni 2.77** kwa ajili ya usimamizi wa miradi ya maji katika Mamlaka za serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika**, ingawa kiasi kilichotengwa ni kikubwa, bado kuna changamoto kubwa kuhusiana na upatikanaji wa fedha hizo kutoka Hazina. Hadi kufikia mwezi Disemba, 2018, ni **shilingi bilioni 31.53** tu sawa na asilimia 12.23 ndio zilipokelewa kwa ajili ya usimamizi na utekelezaji wa miradi ya maji.

Kamati inasikitishwa na mwenendo wa upatikanaji wa fedha hasa kwa kuzingatia kwamba, katika kipindi hicho Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikuwa na miradi 482 ya maji ambayo utekelezaji wake unaendelea.

Aidha, utekelezaji wa programu hii unakabiliwa na uhaba wa Wataalam wa maji na uchakavu wa miundombinu ya vituo vyta kuchotea maji ambao umesababisha vituo 39,509 sawa na asilimia 30.62 ya vituo vyote vyta kuchotea maji 128,991 vilivyopo nchini kushindwa kufanya kazi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza hatua ya Bunge kutunga sheria ambayo imeanzisha Wakala wa Maji Vijijini (RUWA) ambacho kitakuwa ni chombo chenye dhamana ya kusimamia masuala yote ya maji. Hata hivyo, ni rai ya Kamati kwamba, chombo hiki kitakapoanza kazi kiwezeshwe kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu.

#### **d). Ujenzi wa Hospitali za Halmashauri na Vituo vyta Afya**

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa vituo vyta afya unalenga kuboresha hali ya utoaji wa huduma za afya kwa kuzingatia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka mitano, Awamu ya Pili wa 2016/17 kwa lengo la kuchangia: -

- kupunguza vifo vya mama wajawazito kutoka 432 mwaka wa fedha 2014/15 hadi 250 kwa kila vizazi hai 100,000 ifikapo mwaka 2020/21;
- kupunguza vifo vya watoto wachanga kati ya watoto 1,000 waliozaliwa kutoka 43 mwaka 2014/15 hadi 42 ifikapo mwaka 2020/21 na;
- kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano kati ya watoto 1,000 kutoka 67 vilivyokuwepo mwaka 2014/15 hadi 45 ifikapo mwaka 2020/21 kwa Mpango huu wa ujenzi wa vituo vya kutolea huduma ya afya unatekelezwa kwa kushirikisha wananchi, wadau mbalimbali wa maendeleo, sekta binafsi na mashirika ya dini. Kwa sasa Serikali imeweka kipaumbele katika kukamilisha maboma yaliyoanza kujengwa kwa kutumia nguvu za wananchi ili miradi hiyo ikamilike na kuanza kutoa huduma na kutowavunja moyo wananchi waliojitelea kuitekeleza.

Ukarabati na ujenzi wa vituo vya afya uliana Oktoba, 2017 na unahusisha vituo 350 nchi nzima ambavyo utekelezaji wake unafanyika katika awamu tano tofauti chini ya usimamizi wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa gherama ya zaidi ya **shilingi bilioni 137.35**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza dhamira ya Serikali katika ujenzi wa Vituo vya afya vingi katika kipindi cha muda mfupi. Hata hivyo, uzoefu umebaini kwamba bajeti ya kulingana (*frat rate*) inayotengwa kwa vituo vyote nchini siyo halisi kwani gherama za ujenzi hazifanani kote nchini. Aidha, bajeti hiyo ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji ya ujenzi wa kituo cha afya na upatikanaji wa vifaa tiba na vitendanishi.

Ni maoni ya Kamati kwamba, Serikali iongeze bajeti ya ujenzi wa kituo cha afya ili kiweze kukamilika. Aidha, mkakati wa kuandaa wataalam wa tiba uanze mapema ili vituo vinapokamilika viweze kuanza kutoa huduma na

kuwapunguzia wananchi adha na usumbufu wa kukosa huduma ya afya.

**Mhehimwiwa Spika**, Kamati pia inatambua na kupongeza hatua ya Serikali kutenga na kuidhinishiwa **shilingi bilioni 100.5** katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali za Halmashauri 67 katika halmashauri ambazo hazikuwa na hospitali hizo.

Hadi kufikia Novemba, 2018 fedha hizo zilikuwa zimetolewa zote na kupelekwa kwenye Halmashauri husika ili kuanza michakato ya ujenzi na ambao Serikali imeelekeza ukamilike ndani ya kipindi cha miezi sita kuanzia Disemba, 2018.

Kiasi hicho cha fedha kimekadiriwa kuwezesha ugharamiaji wa ujenzi wa jengo la utawala, jengo la wagonjwa wa nje, stoo ya dawa, maabara, jengo la vipimo vyta mionzi, jengo la kufulia nguo na jengo la wazazi.

Ni ushauri wa Kamati kwamba, pamoja na nia njema ya Serikali ya kuhakikisha halmashauri ambazo hazina hospitali za wilaya zinaanza ujenzi, gharama ya **shilingi bilioni 1.5** iliyotengwa kwa kila hospitali ni ndogo (sawa na asilimia 20 ikilinganishwa na lengo la **shilingi bilioni 7.5**) hivyo Serikali ianze kuandaa bajeti ambayo itaongezwa kwa halmashauri husika ili kuendeleza ujenzi uliokusudiwa.

Aidha, Serikali ianze maandalizi ya kupata na kuajiri watumishi wa sekta ya afya sambamba na ununuzi wa vifaa tiba na vitendanishi ili kuwezesha hospitali hizi kutoa hudumia kikamilifu mara zitakapokamiliika.

#### e). Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)

**Mshimiwa Spika**, Tume hii ilianzhishwa kwa Sheria Na. 25 ya Mwaka 2015 ili kuweza kusimamia utumishi wa Walimu nchini kwa lengo la kukabili changamoto zilizokuwepo katika kusimamia utumishi wa Walimu.

Hiki ndicho chombo chenye jukumu la kuendeleza na kusimamia utumishi wa Walimu kwa kuhakikisha Walimu wanatimiza wajibu wao na kupata stahili zao kikamilifu.

Hata hivyo, TSC imekuwa iikabiliwa na changamoto kadhaa katika utendaji wake. Mionganini mwa changamoto hizo ni ufinyu wa bajeti inayotengwa na kiasi kinachotolewa kuwa kidogo. Mfano katika mwaka wa fedha 2018/19 Tume ya Utumishi wa walimu iliidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 12.52**, hata hivyo katika kipindi cha Julai hadi Disemba ,2018 Tume ilikuwa imepokea **shilingi bilioni 4.71** kati ya lengo la **shilingi bilioni 6.62** ambazo zilipaswa kupokelewa. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 74.5 ya lengo.

**Mheshimiwa Spika**, shughuli ambazo ziliweza kutekelezwa na Tume ya Utumishi wa Walimu ni pamoja na kuthibitisha kazini Walimu 2,793 wakiwemo wa shule ya msingi 547 na shule ya sekondari walimu 2,246. Aidha, Walimu wa Sekondari 2,536 walipandishwa daraja.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya umuhimu wake chombo hiki kimekuwa kikabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na bajeti finyu inayokwamisha utekelezaji wa majukumu ya kisheria ya chombo hiki. Aidha, TSC ina upungufu wa ofisi, samani na watumishi kuanzia ngazi ya makao makuu hadi katika wilaya 139 ambazo zinahitaji watumishi 179 ili kukidhi mahitaji ya ikama.

Ni ushauri wa Kamati kwamba, kutokana na mamlaka ya chombo hiki iwapo kitapatiwa bajeti inayojitosheleza kinawenza kufanya utafiti na kumshauri Waziri mwenye dhamana juu ya namna nzuri za kushughulikia masuala yanayowahusu Walimu. Aidha, TSC inaweza ikafanya utafiti na kushauri kuhusu namna ya kuwa na uwiano ulio sawa baina ya Walimu wa masomo ya sayansi na masomo ya sanaa; na baina ya walimu wa mijini na vijijini.

**f). Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

**Mheshimiwa Spika**, mpango huu umeendelea kuandaa na kusimamia mfumo wa kitaifa wa umiliki wa rasilimali na uendeshaji wa biashara unaotambulika na kukubalika kisheria. Kupitia mpango huu wanyonge

wanawezeshwa kurasimisha mali walizonazo (ardhi na biashara) na kuzitumia kujikwamua kiuchumi.

Ili kufanikisha utekelezaji wa shughuli za urasimishaji nchini, MKURABITA inazijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Wizara za kisekta kwa upande wa Zanzibar, kwa kutoa mafunzo kwa watendaji wa Halmashauri za Miji na Wilaya, Manispaa, Kata, na Shehia ili kuendeleza urasimishaji katika maeneo yao.

Katika kipindi cha kuanzia Aprili hadi Septemba,2018 mpango huu umefanya utafiti wa sekta isiyo rasmi nchini, kupitia radio na television kuhusu MKURABITA na uvezeshaji wananchi kiuchumi, na wameingia makubaliano na Shirika la Utangazaji la Zanzibar - ZBC ya kuandaa vipindi vyenye tija ya urasimishaji rasilimali na biashara Zanzibar.

Katika kipindi cha Oktoba ,2018 hadi Juni,2019 MKURABITA imepanga kuanzisha vituo vitano (5) vya urasimishaji biashara katika halmashauri tano (5) za Wilaya ya Geita, Njombe, Singida, Tanga na Singida; na kutoa mafunzo kwa watu 5,000 kuhusu fursa na matumizi bora ya Hati Miliki za Kimila.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia umuhimu wa kazi zinazotekelawa na MKURABITA ni mtazamo wa Kamati kwamba, Serikali iongeze bajeti ya MKURABITA kwani inayotengwa ni kidogo sana na inaathiri mpango huu kusambaa katika maeneo mengine ya nchi.

#### **g). Idara ya kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha kuwa kumbukumbu na nyaraka za umma zinahifadhiwa na zinapatikana haraka kwa watumiaji, idara imefanikiwa kuanzisha, kusimika na kusimamia matumizi ya mifumo ya kieletroniki ya uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka kama Mfumo wa masijala ya kieletroniki (*e – file management system*) katika Taasisi za Umma. Hadi sasa jumla ya Watumishi 179 kutoka Taasisi 44 wamepatiwa mafunzo, na kati ya Taasisi hizo Taasisi za Umma

thelathini na tisa (39) zimeunganishwa na zinatumia mfumo huo.

Vile vile, mfumo wa utunzaji wa taarifa za kumbukumbu tuli katika kituo cha taifa (*The National Records Centre Management System*) unahifadhi taarifa za majalada yanayohamishiwa katika kituo cha Taifa Dodoma kutoka katika Taasisi za umma na kurahisisha uhifadhi na upatikanaji wake zinapohitajika kwa ajili ya utoaji maamuzi mbalimbali Serikalini

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Septemba, 2018 jumla ya Taasisi 55 zikiwemo Wizara, Mikoa, Wilaya, Idara, Wakala na Mamlaka mbalimbali za Serikali zilikuwa zimehamishiwa na kuhifadhiwa majalada yake takribani 124,476.

Idara ya kumbukumbu na nyaraka za Taifa imekuwa ikihifadhi nyaraka mbalimbali toka kipindi chote cha utawala wa kikoloni na baada ya uhuru. Inakadiriwa kwamba, Idara ina nyaraka zenye kurasa 9,487,000 ambazo ziko kwenye mfumo wa karatasi na mikanda na baadhi yake zimeanza kuchakaa kutokana na kukaa kwa muda mrefu.

Ni ushauri wa Kamati kwamba kwa kuwa wananchi wengi hawajui shughuli zinazotekelezwa na idara hii, ni vyema ikajitangaza kupitia vyombo vya habari ili shughuli zake ziweze kufahamika. Aidha, idara itoe matangazo ya kukaribisha watu wenye hazina ya taarifa za kale kwa ajili ya kuzihifadhi.

#### **(h) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)**

**Mheshimiwa Spika**, mfuko huu umetekelezwa katika awamu tatu tangu ulipoanzishwa mwaka 2000. Awamu ya kwanza iliyotekelezwa mwaka 2000 – 2005 katika maeneo 42 (halmashauri za Tanzania Bara, na Unguja na Pemba) ililenga kuwapatia wananchi huduma muhimu katika sekta za maji, elimu, miundombinu, afya n.k ambapo miradi 1,704 ilitekelezwa kwa **shilingi bilioni 72**.

Serikali iliamua kueneza mafanikio yaliyopatikana katika awamu ya kwanza kwenye halmashauri zote 124 za wakati huo Tanzania Bara, pamoja na Unguja na Pemba na kwa kuanzisha awamu ya pili (TASAF II) iliyotekelawa kwa kipindi cha miaka nane (2005 – 2013) ambapo miradi 12,347 ilitekelezwa kwa **shilingi bilioni 430**.

**Mheshimiwa Spika**, TASAF Awamu ya Tatu ambayo ilizinduliwa mwezi Agosti, 2013 inatekeleza Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini kwa lengo la kuziwezesha kaya maskini kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu.

Tangu kuanza kutekelezwa kwa awamu hii zaidi ya walengwa milioni moja na elfu tano (1,005,495) waliopo katika Vijiji/Mitaa/Shehia 9,968 wananaufaika na mpango wa ruzuku ambao zaidi ya shilingi bilioni 706 zimeishatolewa na kutumika katika ngazi zote za utekelezaji.

Kutokana na utekelezaji wa mpango huu zaidi ya asilimia 95 ya watoto walio chini ya miaka 5 kutoka kaya za walengwa wanahudhuria kliniki, huku zaidi ya asilimi 97 ya watoto wanaotoka kaya za walengwa wakihudhuria shulenii. Kuimarika kwa mahudhurio hayo ni ishara njema ya kujenga nguvu kazi yenye uelewa kwa kizazi kijacho.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo mpango wa kunusuru kaya maskini umekuwa ukikabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na ufinyu wa bajeti kutokana na Serikali kushindwa kuchangia kikamilifu theluthi moja (1/3) kwa mujibu wa makubaliano na wadau wengine wa mpango huu.

Kwa mfano katika kipindi cha miaka mitano ya bajeti kuanzia 2013/2014 – 2017/2018 Serikali iliweza kuchangia **shilingi bilioni 4.35** tu kati ya **shilingi bilioni 63.5** zilizoidhinishwa na Bunge. Kiasi hicho ni sawa na takribani asilimia 7 tu. Mchanganuo zaidi wa uchangiaji wa Serikali ni kama unavyoonekana katika jedwali hapa chini.

Mwaka	Kiasi idhinishwa (Tsh)	Kiasi tolewa (Tsh)	Bakaa
2013/14	18,500,000,000	3,000,000,000	15,500,000,000
2014/15	14,000,000,000	600,000,000	13,400,000,000
2015/16	14,000,000,000	0.00	14,000,000,000
2016/17	14,000,000,000	0.00	14,000,000,000
2017/18	3,000,000,000	750,000,000	2,250,000,000
<b>Jumla</b>	<b>63,500,000,000</b>	<b>4,350,000,000</b>	<b>59,150,000,000</b>

**Maelezo:** Uchangiaji wa Serikali katika Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini kwa kipindi cha miaka mitano 2013/14 – 2017/18.

**Mheshimiwa Spika**, tafsiri ya takwimu katika jedwali hilo ni kwamba, mpango wa kunusuru kaya maskini kwa takribani asilimia 93 umekuwa ukitekelezwa kwa fedha za mikopo na misaada kutoka kwa wahisani. Hali hii inaashiria kwamba, mpango huu hautaweza kutekelezwa iwapo ushiriki wa wahisani utafikia ukomo.

Ni maoni ya Kamati kwamba, ni vyema Serikali ikatathmini ushiriki wake katika mpango huu na kuanza kutoa fedha kikamilifu ili kujenga mazingira ya kugharamia mpango huu kwa fedha za ndani iwapo wahisani watajiondoa.

#### 2.2.6 Semina kwa Wajumbe wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka mmoja cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati, Wajumbe walipata fursa ya kushiriki katika semina mbazo zililenga kuwajengea uwezo kama ifuatavyo: -

##### a) **Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji kwa Awamu ya Tatu (2017 -2022)**

**Mheshimiwa Spika**, semina hii iliandaliwa na kuendeshwa na African Parliamentarians Network Against Corruption (APNAC) kwa kushirikiana na Mradi wa Legislative Support Program (LSP) unaotekelizwa na Ofisi

ya Bunge chini ya ufadhilli wa Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP).

Kupitia semina hii Wajumbe waliweza kupata uelewa wa kutosha juu ya Awamu ya Tatu ya Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa (2017 – 2022), na hivyo kuwa na wigo mpana wa uelewa katika kusimamia na kuishauri Serikali katika masuala yanayohusu mapambano dhidi ya rushwa nchini.

Kwa namna ya pekee nichukue fursa hii kuushukuru Mradi wa LSP kwa kugharamia semina hii na kuwezesha wajumbe kupata uelewa wa kutosha kuhusu masuala ya rushwa. Ni matumaini yangu kwamba, LSP itaendelea kufadhilli semina za jinsi hii ili kuendelea kuongeza uelewa wa Wabunge katika mapambano dhidi ya rushwa, hasa kwa kuzingatia kwamba wao ni viongozi wa wanapaswa kuongoza mapambano dhidi ya rushwa.

**Mheshimiwa Spika**, madhara ya rushwa ni mabaya sana kiasi cha kufananishwa na ugonjwa wa saratani, kama alivyowahi kunukuliwa Makamu wa Rais wa 47 wa Marekani (2009 – 2017), Joe Biden kwamba; *“Corruption is a cancer: ... it wastes the talent of entire generations. It scares away investments and jobs”*.

Kwa tafsiri isiyo rasmi anachosema kiongozi huyo ni kwamba, *“Rushwa ni saratani: ... Inapoteza kipaji cha vizazi vyote. Inafukuza uwekezaji na kazi”*.

**Mheshimiwa Spika**, sote tunajua madhara ya ugonjwa wa saratani kwamba ni kifo kwa binadamu. Hali kadhalika, hatua ya rushwa kufananishwa na ugonjwa huu, ni ishara kwamba nayo ina madhara makubwa kwa jamii, hivyo tunapaswa kuipiga vita kwa nguvu zote.

b) **Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGS) Utekelezaji Ufuatilaji na Mapitio, Tanzania mwaka 2017**

**Mheshimiwa Spika**, semina hii iliandaliwa na kuendeshwa na shirika lisilo la kiserikali la Policy Forum kwa

lengo la kuwaongezea Wajumbe uelewa kuhusu mchakato wa uchambuzi wa bajeti kwa kuangalia Mpango wa Maendeleo endelevu katika utekelezaji na ufuutiliaji na mapitio ya Bajeti.

Semina hii ilijikita katika maeneo ambayo yanashabihiana na elimu au afya, na uwiano wa kiasi cha fedha kinachotengwa katika sekta hizo ikilinganishwa na bajeti ya Taifa ambapo ilibainika kwamba, kiasi kinachotengwa bado ni kidogo.

Aidha, uwiano wa kiasi cha fedha kinachopatikana ikilinganishwa na kiasi cha fedha kilichotengwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya maeneo hayo uliangaliwa, ambapo ilibainika kwamba, kiasi kinachotolewa ni kidogo na hakitiki kwa wakati hivyo kuathiri mipango ya utekelezaji ilioandaliwa.

**c) Uchambuzi wa bajeti kwa ajili ya sekta ya elimu**

**Mheshimiwa Spika**, semina hii iliandaliwa na kuendeshwa na shirika lisilo la kiserikali la HakiElimu kwa lengo la kuwaongezea Wajumbe wa Kamati uelewa wa namna ya kuchambua bajeti inayoelekezwa kwenye sekta ya elimu.

Semina hiyo ilizingatia uhalisia kwamba, sehemu kubwa ya bajeti ya elimu inatekelezwa chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambako Kamati hii imekasimiwa jukumu la kuisimamia na kuishauri Serikali. Sote tunatambua kwamba, elimu msingi kwa maana ya elimu ya msingi (darsa la I – VII) hadi elimu ya sekondari (kidato cha I – IV), na elimu ya sekondari ya juu (kidato cha V – VI) inasimamiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na semina hiyo Wajumbe wa Kamati walibaini kwamba kwa ujumla bajeti inayotengwa kwa ajili ya sekta ya elimu imepungua katika miaka miwili ya bajeti 2017/2018 na 2018/2019) ikilinganishwa na miaka mitatu ya bajeti ya 2014/2015, 2015/2016 na 2016/2017 ambapo bajeti iliongezeka kutoka shilingi bilioni 3,465 hadi shilingi bilioni 4770.

Aidha, Wajumbe waliweza kubaini kwamba mwenendo wa kupungua kwa bajeti ya sekta ya elimu ni tofauti na mwenendo wa bajeti ya taifa ambayo iliongezeka kutoka **shilingi trilioni 29, 540 hadi shilingi trilioni 32,700** katika kipindi cha miaka mitatu ya fedha iliyopita.

Vilevile, Wajumbe walielewa kwamba, ingawa bajeti ya sekta ya elimu inagawanywa katika Wizara tatu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ndiyo inachukua kiasi kikubwa (asilimia 69.4) na zilizobaki ni Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo inachukua asilimia 30.4, na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inayopata asilimia 0.2.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupata sehemu kubwa ya bajeti ya sekta ya elimu, sehemu kubwa ya bajeti hiyo inaelekezwa kwenye matumizi ya kawaida na siyo maendeleo. Kwa mfano katika bajeti ya mwaka huu wa fedha (2018/2019) asilimia 93 ya bajeti ya sekta ya elimu katika TAMISEMI imemelekezwa kwenye matumizi ya kawaida, na asilimia 7 tu ndiyo imemelekezwa katika maendeleo. Hii ni ishara kwamba, utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta ya elimu utaendelea kusucasua.

Hali hii itachangia kuathiri mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwani shule nyngi miundombinu yake inahudumiwa na TAMISEMI. Hii inaunga mkono taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka wa fedha 2016/17 ambayo ilibainishwa kwamba, shule za msingi zina upungufu wa: - vyumba vya madarasa kwa asilimia 85, matundu ya vyoo kwa asilimia 83, nyumba za walimu kwa asilimia 66 na madawati kwa asilimia 14.

Aidha, kwa upande wa sekondari ripoti hiyo ilionesha kuna upungufu wa: - vyumba vya madarasa kwa asilimia 52, maabara kwa asilimia 84, madawati kwa asilimia 86, nyumba za walimu asilimia 85, na matundu ya vyoo asilimia 53.

**Mheshimiwa Spika**, ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali iongeze zaidi bajeti ya sekta ya elimu mwaka hadi

mwaka hasa kwa kuzingatia ukweli kwamba, uamuzi wa Serikali kutoa elimu bila malipo umewezesha wazazi wengi kipeleka watoto wao shule na hivyo kusababisha ongezeko kubwa la hitaji la miundombinu ya elimu.

## 2.2.7 Ziara za Ukaguzi wa Miradi

### (i) Mkakati wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari

**Mheshimiwa Spika**, ili kujionea kazi iliyofanyika na kulinganisha na thamani halisi ya fedha "value for money" katika ukarabati wa shule kongwe nchini, Kamati ilitembelea Shule za Sekondari za Ihungo na Nyakato, mkoani Kagera.

Serikali ililazimika kujenga upya shule hizi baada ya miundombinu ya majengo yake kuathiriwa vibaya na tetemeko liliotokea mkoani Kagera, mwezi Septemba, 2016.

Shule ya Ihungo imejengwa upya na Serikali kwa kushirikiana na Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (*Department for International Development – DfID*) kwa ghamama ya shilingi bilioni 10.5, ilihali shule ya Nyakato imejengwa kwa fedha za Serikali pekee jumla ya shilingi bilioni 2.45.

Ujenzi wa shule ya Ihungo umehusisha majengo matatu ya madarasa yenye vyumba 24 na ofisi 8, jengo la vyoo lenye ghorofa moja, majengo matatu ya mabweni yenye jumla ya vyumba 288, nyumba thelathini (30) za Walimu na mifumo ya maji taka. Aidha, ulifanyika ukarabati wa majengo mawili ya maktaba na maabara, na bwalo la chakula na jiko.

**Mheshimiwa Spika**, wakati Kamati inatembelea shule hizi mwezi Juni, 2018 ujenzi ulikuwa umekamilika kwa asilimia 100 katika shule ya Nyakato na asilimia 80.5 (shule ya Ihungo) na ulitarajiwa kukamilika mapema ili kuruhusu wanafunzi wa kidato cha tano, kuijunga na masomo kuanzia mwezi Julai, 2018.

Kamati inapongeza kwa dhati hatua ya Serikali kujenga upya majengo ya shule hizi kwa kutumia teknolojia ya kisasa ambayo itayawezesha kuhimili matetemeko ya ardhi. Kukamilika kwa ujenzi wa shule hizo, mbali na kutoa fursa kwa Wanafunzi wengi kujiunga na masomo ikilinganishwa na idadi ya awali, umeboresha mazingira ya kusomea kwa wanafunzi na mazingira bora ya kufundishia na makazi kwa Walimu.

Aidha, ni hatua chanya kwa Serikali katika mkakati wake wa kurejesha heshima ya shule za Serikali na kuongeza ari ya utendaji kwa Walimu kutokana na mazingira mazuri ya kazi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo Kamati ilibaini changamoto ambayo inatia doa juhudzi za Serikali katika mkakati huu. Changamoto hiyo ni Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ambaye amepewa kazi ya ukarabati katika shule kadhaa nchini, kushindwa kutimiza majukumu yake kikamilifu na hivyo kukiuka masharti ya mikataba aliyosaini na wateja wake.

Ni ushauri wa Kamati kwamba, Ofisi ya Rais – TAMISEMI irejee (*review*)mikataba yote ambayo imeingia na TBA kuhusu ujenzi na ukarabati wa shule kongwe, na iwapo itabaini kasoro za utekelezaji basi hatua stahiki zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kusitisha au kuvunja mikataba kwa mujibu wa sheria.

## **ii. Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP)**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (*Dar es Salaam Metropolitan Development Project*) una lenga kutatua changamoto zinazolikabili Jiji la Dar es Salaam kwa kuboresha huduma za jamii, miundombinu na kujenga uwezo wa Manispaa za Jiji la Dar es Salaam katika utoaji wa huduma za jamii.

Mradi huu unatekelezwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia wenye thamani ya dola za Marekani milioni 300 kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2015/2016. Aidha, Mfuko wa Maendeleo wa nchi za Nordic (NDF) umechangia dola za kimarekani milioni 5 ili kusaidia kukabili changamoto za mabadiiliko ya tabia nchi, huku Idara ya Maendeleo ya Kimataifa nchini Uingereza (DfID) ikichangia kupitia Benki ya Dunia shilingi bilioni 42 ili kuboresha Bonde la Mto Msimbazi. Serikali ya Tanzania imechangia shilingi bilioni 55.6 kwa ajili ya kulipa fidia katika maeneo ambayo yatapitiwa na mradi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea utekelezaji wa Mradi wa DMDP katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ambayo katika kipindi cha mwaka 2015 – 2020 inatarajia kutumia shilingi bilioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji na mifereji ya maji, vituo vya mabasi, uwekaji taa za barabarani, masoko, ununuzi wa vifaa vya kuboresha ukusanyaji na usafirishaji wa taka ngumu, vyoo vya umma, uwanja wa mpira, na kituo cha Afya.

Halmashauri hiyo imechangia gharama za mradi kwa kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi kwa fedha za mkopo shilingi bilioni 19.6 kutoka Benki ya CRDB. Jumla ya wananchi 2,198 wameishalipwa fidia (shilingi bilioni 18.4) na taratibu za malipo ya shilingi bilioni 1.9 zinaendelea kwa wananchi 430.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanikiwa kutembelea barabara ya Kijichi – Toangoma (3.3 km) katika Kata ya Kijichi na kushuhudia ujenzi wa Daraja la Toangoma; barabara Mwanamtoti (1.8 km) na Jengo la Ofisi za DMDP ambalo limegharimu shilingi bilioni 21.67

Aidha, Kamati ilikagua ujenzi wa barabara zenyet urefu wa kilomita 16; Stendi ya Mabasi na soko ambavyo vimetumia jumla ya shilingi bilioni 22.28.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza hatua madhubuti ambazo Serikali inazichukua ili kubadilisha sura

ya jiji la Dar es Salaam kwa uboreshaji wa miundombinu ambayo licha ya kurahisisha huduma za usafiri, itaboresha madhari ya Jiji la Dar es Salaam na kusaidia kukabili matukio ya dharura kama majanga ambayo yanaweza kutokea.

## 2.2.8 Muswada wa Sheria

**Mheshimiwa Spika**, ulileta Muswada wa Sheria ya Tamko la Kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Mwaka 2018 *[The Dodoma Capital City (declaration) Bill, 2018]* kwenye Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa ili iweze kuufanyia kazi.

Muswada huu ulipendekeza kutungwa kwa Sheria ya Tamko la Makao Makuu ya Mwaka 2018 kwa madhumuni ya kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kamati ilitimiza wajibu wake wa kushughulikia Muswada huo kati ya Tarehe 21 hadi 28 Agosti, 2018 ambapo ilifanya uchambuzi wa kitaalam ulioboresha Muswada huo kwa kuzingatia maelezo na hoja zilizowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kuhusu vifungu vya Muswada, hoja za Wadau mbalimbali na kufanya tathmini na kuanda maoni ambayo yalilisaidia Bunge kutunga Sheria ya Tamko la Makao Makuu iliyokidhi viwango.

**Mheshimiwa Spika**, kutungwa kwa sheria hii kuliwezesha nchi yetu kuwa na tamko la kisheria kuhusu Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jambo ambalo lilikosekana kwa takribani miaka 45 iliyopita.

Aidha, ni dhahiri shahiri kwamba, Wajumbe wa Kamati ya Utawala na Bunge lako kwa ujumla tumeingia katika historia ya nchi yetu kwa kuwezesha kutungwa kwa Sheria ya Tamko la Makao Makuu ya nchi yetu ikiwa ni baada ya zaidi ya miongo minne. Kazi hii tulioifanya itadumu kuwa

kumbukumbu isiyosahaulika kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa kadri nchi yetu itakavyodumu kuwepo katika ulimwengu huu.

## **SEHEMU YA TATU**

### **3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO**

#### **3.1 Maoni**

**Mheshimiwa Spika**, yafuatayo ni maoni ya Kamati kuhusiana na shughuli zilizotekelawa katika kipindi cha kuanzia Januari, 2018 hadi Januari, 2019 ambayo yanabainisha mtazamo wa kile kilichojiri wakati wa kamati ikitimiza majukumu yake. Maoni hayo ni haya yafuatayo: -

**(a) Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

- i. Ufinyu wa bajeti inayotengwa kwa ajili ya TARURA ikilinganishwa na mtandao wa barabara ambao inausimamia, unaathiri utendaji wa wakala hiyo;
- ii. Upungufu wa watumishi, uhaba wa ofisi na vitendea kazi unaifanya TARURA ishindwe kutimiza majukumu yake kikamilifu;
- iii. Ukosefu wa sheria ndogo ndogo kwa lengo la kulinda na kuzuia uharibifu wa barabara zinazosimamia na TARURA kunachangia matumizi yasiyo sahihi ya barabara;
- iv. Ukarabati wa shule kongwe za Sekondari nchini unaboresha mazingira ya kusomea kwa wanafunzi na mazingira ya kufundishia na makazi bora kwa Walimu na hivyo kuinua ari ya utendaji;
- v. Hatua ya Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kushindwa kutekeleza kazi za ukarabati wa shule kongwe za Sekondari kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba kunaathiri mkakati wa Serikali wa ukarabati wa shule kongwe za Sekondari;

vi. Uhaba wa Wataalaam wa maji katika ngazi za halmashauri unaathiri utekelezaji wa miradi ya Programu ya Usambazaji Maji Safi na Salama Vijijini;

vii. Mwenendo usioridhisha wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa ajili ya Programu ya Usambazaji Maji Safi na Salama Vijijini unakwamisha utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa;

viii. Ujenzi wa Hospitali za Wilaya katika Halmashauri 67 ambazo hazikuwa na hospitali za ngazi hiyo, kutasaidia kuondoa usumbufu kwa wananchi ambao walikuwa wanakosa huduma hiyo;

ix. Ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya 350 ambao unaendelea nchini utasaidia kuboresha upatikanaji wa huduma ya afya kwa wananchi na hivyo kusaidia kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto;

x. Hatua ya Serikali kutenga bajeti inayolingana (flat rate) kwa ajili ya ujenzi/ukarabati wa Vituo vya afya na ujenzi wa hospitali za Wilaya unaweza kuathiti utekelezaji wa miradi hiyo kwa baadhi ya maeneo;

xi. Hatua ya baadhi ya Halmashauri kuendelea kuvutana kuhusu maeneo ya ujenzi wa hospitali za Wilaya wakati fedha za kuanza ujenzi zimetolewa na Serikali, kunaathiri juhudhi za Serikali za kuwafikishia wananchi huduma ya afya; na

xii. Bajeti finyu, upungufu wa ofisi na watumishi kunasababisha Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ishindwe kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

**(b) Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

(i) Bajeti finyu inayotengwa kwa ajili ya Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) unakwamisha jitihada za kuongeza wigo na kuyafikia maeneo mengi zaidi nchini;

(ii) Hatua ya baadhi ya Viongozi wa Halmashauri kutoshirikiana na Waratibu wa MKURABITA katika ngazi ya halmashauri kunaathiri jitihada za mpango huo kuenea katika maeneo mengi nchini;

(iii) Hatua ya MKURABITA kushirikiana na taasisi za kifedha kuelimisha wananchi juu ya umuhimu wa hati za haki miliki za kimila kutumiwa kama dhamana ya mikopo katika taasisi hizo, kumesaidia kujenga uelewa wa wananchi na wameanza kutumia fursa hiyo na kupata mikopo;

(iv) Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa inapaswa kutumia vyombo vyaa habari kujitangaza ili wananchi waweze kufahamu shughuli zake;

(v) Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa iandae utaratibu wa kutafuta na kukaribisha watu wenye hazina ya taarifa za kale ili wajitokeze na kuwasilisha taarifa hizo kwenye idara hiyo kwa ajili ya kuhifadhiwa;

(vi) Hatua ya Serikali kushindwa kuchangia kikamilifu mchango wake katika mpango wa kunusuru kaya maskini kunafanya mpango huo kutegemea zaidi fedha za wahisani; na

(vii) Upungufu wa fedha unakwamisha mpango wa TASAF kuzifikia kaya maskini katika vijiji, mitaa na shehia ambazo hazijafikiwa na hivyo kuibua malalamiko kutoka mionganini mwa wananchi wa maeneo hayo.

### **3.2 Mapendekezo**

#### **3.2.1 Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA)**

**KWA KUWA,** Wakala hii imebainika kukabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na ufinyu wa bajeti, uhaba wa watumishi, ofisi na vitendea kazi vingine;

**NA KWA KUWA;** hali hiyo inaathiri utekelezaji wa majukumu ya wakala na kuifanya ishindwe kusimamia

kikamilifu matengenezo ya miundombinu ya barabara inazozisimamia;

**KWA HIYO, BASI,** Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kutekeleza mambo yafuatayo: -

i. Kutenga fedha za kutosha na kuzitoa kikamilifu kwa TARURA ili iweze kuhudumia kikamilifu mtandao wa barabara inaousimamia ambao una zaidi ya kilomita 108,000. Njia mojawapo ya kuongeza uwezo wa kifedha za Wakala hii ni kuongeza mgawo wa fedha kutoka Mfuko wa Barabara (RF) kutoka asilimia 30 ya sasa hadi kufikia asilimia 50;

ii. Serikali iiwezeshe TARURA kupata ofisi katika maeneo mbalimbali ya nchi, magari na vitendea kazi vya kutosha pamoja na kuajiri watumishi illi kupunguza uhaba uliopo; na

iii. Kutunga sheria ndogo ndogo (by laws) ili kuiwezesha TARURA kusimamia na kuhakikisha matumizi sahihi ya barabara zilizo chini yake, na kukusanya tozo na ushuru kwa shughuli zinazofanyika katika barabara hizo ili kuongeza mapato.

### **3.2.2 Mkakati wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari**

**KWA KUWA,** mkakati huu unasuasua kutokana na mkandarasi (Wakala wa Majengo-TBA) kushindwa kutekeleza kikamilifu kazi za ukarabati wa shule ilizoingia mkataba na Serikali;

**NA KWA KUWA,** hali hiyo si kwamba inatia doa mkakati huo wa Serikali na kuchelewesha kukamilika kwa ukarabati uliokusudiwa, bali pia inakiuka makubaliano ya kimkataba;

**HIVYO BASI,** Kamati inalishauri Bunge kuitaka Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia (*review*) upya mikataba yote

ambayo imeingia na TBA katika ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari na iwapo itabaini ukiukwaji wa makubaliano basi ifuate taratibu za kisheria na kuvunja mikataba hiyo;

### **3.2.3 Programu ya Usambazaji Maji Safi na Salama Vijijini**

**KWA KUWA**, ukomo wa bajeti, upatikanaji wa fedha usioridhisha kutoka hazina na upungufu wa Wataalam wa maji na mafundi mchundo umeathiri usimamizi na utekelezaji wa miradi ya maji vijijini;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo imesababisha vituo 39,509 (sawa na 30.62%) ya vituo vya kuchotea maji 128,991 nchini kushindwa kufanya kazi, na hivyo kuwanyima wananchi wa maeneo ya vituo hivyo huduma ya maji;

**HIVYO BASI**; Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuongeza kiwango cha ukomo wa bajeti (*ceiling*) na upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa kutoka Hazina kwa ajili ya utekelezaji wa programu ya usambazaji wa maji safi na salama vijijini na kukarabati vituo vya kuchotea maji ambavyo havifanyi kazi ili kuongeza upatikanaji wa maji; na

ii. Kuajiri wataalam wa maji ili kupunguza upungufu wa asilimia 49.49 na mafundi mchundo ili kupunguza upungufu wa asilimia 66.13, ambao unaathiri usimamizi na utekelezaji wa miradi ya maji.

### **3.2.4 Ujenzi wa Hospitali za Halmashauri na Vituo vya Afya**

#### **3.2.4.1 Ujenzi wa Hospitali za Halmashauri**

**KWA KUWA**, Serikali imetenga na kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa hospitali za halmashauri 67 (**Tsh. bilioni 1.5 kwa kila hospitali**) katika halmashauri ambazo hazina hospitali hizo;

**NA KWA KUWA**, kiasi hicho kitagharamia ujenzi wa hospitali kwa asilimia 20 tu, jambo linaloweza kusababisha kuwa na maboma mengi ya hospitali yasiyokamilika na hivyo wananchi kuendelea kukosa huduma tarajiwa;

**HIVYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali itenye na kutoa kiasi cha fedha kilichosalia (**Tsh. bilioni 6** kwa kila hospitali) ili kukamilisha ujenzi uliokusudiwa. Aidha, mipango ya kupata watumishi na vifaa kwa ajili ya hospitali hizo ianze ili ujenzi utakapokamilika, wananchi waanze kupata huduma.

### **3.2.4.2 Ujenzi na Ukarabati wa Vituo vya Afya**

**KWA KUWA**, Serikali inatekeleza mpango wa ukarabati/ujenzi wa vituo vya afya 350 nchini nzima katika hatua mbalimbali tangu mwaka 2017;

**NA KWA KUWA**, mpango huo unakabiliwa na ufinyu wa bajeti ambao umesababisha vituo vingi kutengewa kiwango sawa cha fedha (*flat rate*) bila kujali mazingira ya ujenzi na upatikanaji wa malighafi za ujenzi;

**HIVYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuongeza bajeti inayotengwa kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya ili kukamilisha ujenzi na kuepuka kuwa na maboma yasiyokamilika kama ilivyokuwa awali. Aidha, ni vyema kujenga na kukamilisha vituo vya afya vichache kuliko kufanya ujenzi wa vituo vingi ambavyo vitachelewa kukamilika

### **3.2.5 Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)**

**KWA KUWA**, Tume ya Utumishi wa Walimu imekuwa ikikabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na ufinyi wa bajeti na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina, upungufu wa ofisi na Watumishi;

**NA KWA KUWA**, changamoto hizo zinaathiri utendaji wa majuku ya Tume hii na hivyo kuifanya ishindwe kutoa

huduma na kushughulia masuala mbalimbali ya utumishi wa Walimu;

**HIVYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kutekeleza mambo yafuatayo: -

i. Kuongeza bajeti na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina ili kuiwezesha Tume kutimiza wajibu wake kikamilifu kwa Walimu;

ii. Kuiwezesha Tume kupata ofisi, samani na Watumishi wa kutosha kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Makao Makuu.

Aidha, chombo hiki kikitumiwa vyema kinaweza kutafiti na kuishauri Serikali namna bora ya kuwa na uwiano baina ya Walimu wa masomo ya sayansi na masomo ya sanaa, na baina ya Walimu wa mijini na vijijini.

### **3.2.6 Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

#### **3.2.6.1 Bajeti finyu na upatikanaji wa fedha usioridhisha kutoka hazina**

**KWA KUWA**, bajeti finyu ya maendeleo inayotengwa na upatikanaji wa fedha usioridhisha kutoka hazina vinaathiri utendaji wa MKURABITA na hivyo kuathiri juhudzi za kuongeza wigo wa shughuli za urasimishaji katika maeneo mengi ya nchi;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inasababisha wananchi wa maeneo mengi kutofikiwa na MKURABITA na hivyo kukosa fursa ya kurasimisha ardhi na biashara zao;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuongeza bajeti ya maendeleo ya MKURABITA ili mpango huu uweze kuongeza wigo wa urasimishaji na hivyo kutoa fursa kwa wananchi wengi kurasimisha ardhi na biashara zao.

**3.2.6.2 Halmashauri kutomiliki ajenda ya urasimishaji**

**KWA KUWA**, Halmashauri nyingi hazijapokea na kumikili ajenda ya urasimishaji wa ardhi na biashara inayotekelzwa na MKURABITA;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo imezifanya halmashauri kutoona umuhimu wa kutenga fedha za urasimishaji na kushirikiana na Waratibu wa MKURABITA katika maeneo yao;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuzihimiza halmashauri kupokea na kumiliki ajenda ya urasimishaji kwani mbali na kunufaisha wananchi pia ni njia mwafaka ya kutatua au kuепusha migogoro ya ardhi baina ya makundi ya kijamii. Aidha, Serikali iangalie namna ya kuweka mfumo wa kisheria wa utekelezaji wa MKURABITA katika halmashauri.

**3.2.7 Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa**

**KWA KUWA**, shughuli za Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka hazifahamiki katika jamii kutohana na kutojitangaza vyta kutosha,

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inasababisha Wananchi wenyе hazina ya taarifa za kale kutoona umuhimu wa kujitokeza na kuwasilisha taarifa hizo kwenye idara hii ili zihifadhiwe;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuiwezesha Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa kutumia vyombo vyta habari kujitangaza ili wananchi waweze kufahamu shughuli zake. Aidha, Idara hii iandae utaratibu wa kutafuta na kukaribisha watu wenyе taarifa za kale ili waweze kuziwasilisha kwa lengo la kuhifadhiwa.

**3.2.8 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)**

**3.2.8.1 Baadhi ya maeneo kutofikiwa na Mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini**

**KWA KUWA**, asilimia 30 ya maeneo (vijiji/mitaa/shehia 5,693) nchini haijafikiwa na awamu ya kwanza ya utekelezaji

wa mpango wa kunusuru kaya maskini unaotekelawa na TASAF,

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inasababisha walengwa kati ya **355,000 – 426,000** wenyе sifa katika maeneo hayo kukosa fursa ya kunufaika na mpango huo ili waweze kujiletea maendeleo na hivyo kupunguza kiwango cha umaskini,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kutafuta pesa ili kuhakikisha utekelezaji wa awamu ya pili ya mpango wa kunusuru kaya maskini ambao utaanza katika mwaka ujao wa fedha, unahuishisha maeneo yote yaliyobaki ili kuwapa wananchi wa maeneo hayo fursa ya kunufaika.

#### **3.2.8.2 Mchango wa Serikali katika Mpango wa kunusuru Kaya maskini**

**KWA KUWA**, katika kipindi cha miaka mitano (2013/2014 – 2017/2018) Serikali ilichangia **shilingi bilioni 4.35** tu sawa na asilimia 6.68 ya kiasi kilichotengwa na kuidhinishwa cha **shilingi bilioni 63.5**;

**NA KWA KUWA**, kiasi hicho ni kidogo sana na hakifiki thiellathi moja (1/3) ambayo Serikali inapaswa kuchangia na hivyo kufanya mpango wa kunusuru kaya maskini kutegemea zaidi fedha za mkopo na msaada wa wahisani;

**HIVYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuongeza kiasi inachotoa ili kufikia thiellathi moja (1/3) ambayo ni makubaliano ya uchangiaji katika mpango wa kunusuru kaya maskini. Aidha, hali hiyo inatoa taswira kwamba, iwapo wahisani watajiondoa katika kuchangia mpango huu, basi hautaweza kuendelea kwa kutegemea fedha za Serikali.

#### **SEHEMU YA NNE**

#### **4.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, ninapohitishwa napenda kuzungumza kidogo kuhusu dhana ya ugatuzi wa madaraka

au upelekaji wa madaraka kwa wananchi (*Devolution by Decentralization – D by D*). Jambo hili msingi wake ni Ibara ya 145 na 146 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Ibara ya 146 (1) inasitiza kwamba, vyombo vya Serikali za Mitaa (Halmashauri, Kata, Vijiji, Mitaa na Vitongoji) vitakuwa na haki na mamlaka ya kuwashirikisha wananchi katika mipango na shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika sehemu zao na nchini kote kwa ujumla.

Utekelezaji wa dhana hiyo ya kikatiba kupitia sera iliyotungwa mwaka 1998 umekuwa na manufaa kadhaa ikiwa ni pamoja na kusogezwa kwa huduma karibu na wananchi, na ushiriki wa Wananchi katika kutathmini, kupanga, kuamua na kutekeleza mipango mbalimbali kwa kuzingatia matatizo yanayowakabili kwa kutumia mbinu ya fursa na vikwazo kwa maendeleo.

Ni kwa mantiki hiyo wananchi kwa nguvu zao na uungwaji mkono wa Serikali wamefanikiwa kujenga shule za msingi, shule za sekondari za kata, zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, miradi ya maji, uhifadhi endelevu wa misitu, n.k

**Mheshimiwa Spika**, hivi karibuni kumekuwa na uhamishaji wa baadhi ya majukumu kutoka Serikali za Mitaa kwenda Serikali Kuu (*centralization*) kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wake bila hata kuwashirikisha wananchi katika ngazi za Serikali za Mitaa. Hatua hiyo inawanyang'anya wananchi madaraka na mamlaka ya kushiriki kwenye maendeleo yao na Taifa kwa ujumla kwa kuwafanya waamini kwamba kila kitu kitatekelezwa na Serikali Kuu. Aidha hatua hiyo itaondoa ukaribu na urahisi wa upatikanaji wa baadhi ya huduma kwa wananchi kwa kuwa mamlaka ya usimamizi na maamuzi yatakuwa katika ngazi za wizara.


**Mheshimiwa Spika**, ni mtazamo wa Kamati kwamba, Serikali Kuu inaweza ikakumbana na ugumu katika

kusimamia shughuli za maji, hospitali za mikoa na sekta nyingine zitakazohamishwa kutoka Serikali za Mitaa kwenda Serikali Kuu kama hakutakuwa na ushirikishaji wa vyombo vyaa Serikali za Mitaa.

Aidha, Kamati inafikiri ni vyema Serikali Kuu ikajikita katika kujenga mfumo imara wa kumhudumia mwananchi ambao utazingatia misingi ya upelekaji wa madaraka kwa wananchi ambao Ibara ya 8(a) ya Katiba inawataja kuwa wao ndiyo misingi wa madaraka yote na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi.

Vile vile, Serikali inapaswa kuhakikisha inagatua rasilimali fedha za kutosha na kuzipeleka kikamilifu kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa ambako utekelezaji unafanyika ili kuziwezesha mamlaka hizo kutimiza wajibu wake kwa wananchi.

Kielelezo kifuatacho kinaonesha tofauti ya kuwa na kutokuwa na ugatuzi wa madaraka



**Ufunguo:**

■ **Mchoro A** unaonesha kwamba, mamlaka na utoaji wa huduma vinahodhiwa sehemu moja. Ni sawa na kusema kwamba, hakuna ugatuzi wa madaraka kwa Serikali za Mitaa, hivyo mamlaka na utoaji wa huduma vinahodhiwa na Serikali Kuu. Changamoto iliyopo ni kwamba, wananchi wote watalazimika kufuata huduma sehemu moja, tena mbali na kunaweza kuwa na urasimu.

■ **Mchoro B** unaonesha kwamba, mamlaka na utoaji wa huduma vimekasimiwa katika maeneo mbalimbali. Ni sawa na kusema hapa kuna ugatuzi wa madaraka kwa mamlaka mbalimbali (Mamlaka za Serikali za Mitaa) ili ziweze kuamua na kusimamia utoaji wa huduma. Faida yake ni kwamba, huduma hizo huwa karibu zaidi na wananchi na kunakuwa na kiwango kidogo cha urasimu huku wananchi wakishirikishwa kikamilifu kuamua na kutekeleza mambo yanayohusu mustakabali wao.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mhe. George Huruma Mkuchika, (Mb) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Selement Said Jafo (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Naibu Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI Mhe. Josephat Sinkamba Kandege (Mb) na Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara (Mb) na Naibu Waziri wa Nchi Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Dkt. Mary Mwanjelwa (Mb) kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Aidha, nawashukuru watendaji wote wa ofisi ya Rais – TAMISEMi wakiongozwa na Mhandisi Joseph Nyamuanga, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na Watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wakiongozwa na Dkt. Laurian Ndumbaru, kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote wa kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa ushirikiano walionipatia katika kipindi chote cha mwaka mmoja cha utekelezaji wa shughuli za Kamati. Aidha, natambua na kuthamini mchango wao adhimu na kujitoa kwao kikamilifu katika kuhakikisha Kamati yetu inatekeleza wajibu wake.

Ni wazi kwamba, bila weledi na ushirikiano wao Kamati isingetekeleza kwa ufanisi shughuli ilizojipangia katika kipindi cha kuanzia Januari, 2018 hadi Januari, 2019. Kwa heshima kubwa ningetamani kuwataja majina yao, hata hivyo, kutohana na ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina hayo ni haya yafuatayo:

1. Mhe. Jasson Samson Rweikiza, Mb – Mwenyekiti
- 2.Mhe. Mwanne Ismail Mcemba,Mb–Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb,
4. Mhe. Angelina Adam Malembeka Mb
5. Mhe.George Malima Lubeleje, Mb
6. Mhe.Hamad Salim Maalim, Mb
7. Mhe.Innocent Sebba Bilakwate,Mb
8. Mhe.Mwatum Dau Haji,Mb
9. Mhe.Saada Mkuya Salum,Mb
10. Mhe.Salum Khamis Salum,Mb
11. Mhe.Venance Methusela Mwamoto,Mb
12. Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb
13. Mhe. Jerome Dismas Bwanausi, Mb
14. Mhe. Martha Moses Mlata, Mb
15. Mhe. Lusia Ursula Michael, Mb
16. Mhe. Rehema Juma Migilla, Mb
17. Mhe. Joseph Raman Selasini, Mb
18. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb
19. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb
20. Mhe. Khatib Said Haji, Mb
21. Mhe. Njalu Daudi Silanga, Mb
22. Mhe. Daniel Edward Mtuka, Mb
23. Mhe. Hamidu Hassan Bobali, Mb
24. Mhe. Mansoor Hilan Shaniff, Mb

25. Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchembba, Mb
26. Mhe. Ibrahim Hassanaly Mohamedali Raza, Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai kwa ushirikiano wake kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake. Pia, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati hii Ndg. Chacha Nyakega na Ndg. Eunike Shirima, wakisaidiwa na Ndg. Grace Mwenye, kwa uratibu mzuri wa shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii. Vilevile, nawashukuru Watumishi wote wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge, wakiongozwa na Bi. Hanifa Masaninga, kwa kuandaa na kutoa vitabu vya taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo ya kina kuhusu shughuli zilizotekelzeza na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo, maoni na mapendekezo ya Kamati, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kuikubali taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Jasson S. Rweikiza (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA  
NA SERIKALI ZA MITAA**

7 FEBRUARI, 2019

**SPIKA:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Rweikiza. (*Makofii*)

Sasa nimwite Mheshimiwa wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi. Anakuja Mwenyekiti mwenyewe, tafadhali, una robo saa.

**MHE. OSCAR R. MUKASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii na nakushukuru kwa kunipa nafasi kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati kwa kufanya kazi iliyo mbele yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, nikuombe taarifa yote iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, kwa sababu nitasoma kwa muhtasari ili kukimbizana na muda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, muundo wa taarifa hii umezingatia masharti yote ya Kanuni za Bunge na imeangalia masuala Wizara mbili ambazo Kamati inazisimamia, TACA/DS, Tume ya Taifa ya Masuala ya Ukimwi na Tume ya Kupambana na Madawa ya Kulevyta. Kwa ufupi baada ya majadiliano tumegundua mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Tume ya Ukimwi, tumegundua:-

(i) Ufinyu wa bajeti na ucheleweshwaji wa fedha kutoka Serikalini ambapo mpaka sasa zaidi ya asilimia 90 ya bajeti ya Tume inategemea fedha za wafadhili.

(ii) Kukinzana kwa Sheria ya UKIMWI na baadhi ya sheria. Kwa mfano, mpaka sasa kisheria watu wenye umri wa chini ya miaka 18 hawaruhusiwi kupima virusi vya UKIMWI kwa hiari, isipokuwa tu kama ana ridhaa ya mzazi lakini wakati huo Sheria ya Ndoa inaruhusu mtoto kuolewa akiwa na miaka 14 kama ana ridhaa ya mzazi. Kwa hiyo, kuna mgongano ambao unaleta shida kwenye utekelezaji wa baadhi ya mambo.

(iii) Mapungufu ya usimamizi wa Sera ya UKIMWI ya mwaka 2001 ambapo mpaka sasa sera iko Ofisi ya Waziri Mkuu, sheria iko Wizara ya Afya ambapo mlolongo unakuwa mrefu pale ambapo baadhi ya mambo yanatakiwa kuamuliwa kwa haraka.

(iv) Kuwepo kwa tofauti kwa baadhi ya takwimu zinazotolewa na wadau ukilinganisha na takwimu zinazotolewa na taasisi rasmi ikiwemo *TACAIDS* na *National Bureau of Statistics*.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi (*Aids Trust Fund*) umeanzishwa kwa Sheria ya Bunge ya mwaka 2015 lakini mpaka sasa haujaweza kutimiza malengo yake ya kutoa asilimia 7 ya fedha za ndani mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 30 ya mahitaji ifikapo 2018. Mpaka sasa asilimia 95 ya fedha yote ya masuala ya UKIMWI nchi hii bado inatoka kwa wafadhili.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya kupambana na Madawa ya Kulevyta, masuala ya msingi tuliyoyaona ni:-

(i) Kukosekana kabisa kwa fedha za miradi ya maendeleo. Kwa hiyo, suala hili linatazamwa kwa hali ya shughuli ya kawaida lakini siyo kwa mtazamo wa maendeleo ambao ni wa kimkakati zaidi.

(ii) Kutokuwepo kwa Sera ya Taifa ya Kupambana na Dawa za Kulevyta ambalo ni suala zito. Sheria tumesikia inafanya kazi vizuri sana lakini nije ya mazingira ya kisera. Kwa hiyo, kuna haja ya kuwa na sera haraka iwezekanavyo.

(iii) Kukosekana Kwa mfumo maalum kwa ngazi ya jamii Kwa ajili ya kuwatambua waraibu. Kama ambavyo inafanyika upande wa UKIMWI, Serikali imeweza kufanya kazi na wadau kuna Mabaraza ambayo yanawatambua huko kwenye ngazi ya chini, kwa hiyo, wanapata taarifa na wanaweza wakafikiwa na afua kwa urahisi.

(iv) Kuwepo kwa baadhi ya *NGOs* na taasisi zisizo za kiserikali ambazo zinajjhishisha na mapambano dhidi ya Madawa ya Kulevyta lakini kwa namna ambayo haijaratibiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, tulipata taarifa kutoka kwenye baadhi ya Wizara kuhusiana na utekelezaji wa kisheria wa

kupambana na UKIMWI sehemu za kazi na magonjwa yasiyoambukiza. Tulipata taarifa kutoka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Wizara ya Mambo ya Nje, Wizara ya Madini, TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa ujumla, kuna tatizo la hizi Kamati za UKIMWI sehemu za kazi ambazo zipo kwa mujibu wa sheria ama kutokuwepo ama kuwepo lakini hazifanyi kazi ipasavyo na kuchukuliwa kwamba ni jambo la ziada.

Mheshimiwa Spika, lakini mahususi kwa Wizara ya Fedha na Mipango, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

(i) Serikali kushindwa kutumia kwa asilimia 100 fedha zinazotoka *Global Fund* na hivyo kuathiri mgao wa fedha kutoka *Global Fund* kwa mwaka unaofuata; kwa sababu kwa kawaida kama hazikutumika zinaathiri mgao wa mwaka unaofuata hivyo kupunguza nguvu ya kifedha ya mapambano ya ukimwi hapa nchini.

(ii) Mpaka sasa hakuna mkakati endelevu wa uhakika wa upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara kadhaa lakini moja ambayo tuliona jambo mahsusni Ifakara ambapo Kituo cha Utafiti wa Afya Ifakara kina *Viral Load Machine* ambayo ina uwezo wa kuhudumia sampuli 13,000 kwa mwaka, lakini kinazuiiliwa kupata vitendanishi kutoka *MSD* kwa sababu tu kwamba umiliki wa mashine haupo kwenye taasisi ya umma ilhalii Mkoa mzima wa Morogoro unatumia mashine moja iliyoko Hospitali ya Mkoa ambayo inahudumia sampuli 9,000. Kwa hiyo, kama Taasisi ya Ifakara ingepata fursa ya kuunganisha nguvu na hiyo Serikali ya Mkoa, Mkoa wa Morogoro ungeweza kupata sampuli 22,000 kwa mwaka na hivyo kuondoa mlolongo wa huduma ya upimaji wa *viral load* kwa wagonjwa wetu na hivyo kusaidia kupunguza mzigo.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine muhimu ambayo tuliyaona wakati wa ziara ni kwamba pamoja na

tatizo la wanaume kutokujitokeza kwenye kushiriki katika upimaji wa *VVU*, sasa zinaonekana dalili za wanaume pia kutokushiriki kwenye vikundi vya watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI, kwa sababu wanapenda kutumia fedha vile isivytakiwa ukilinganisha na wanawake. Kwa hiyo, ni muhimu jambo hili likatazamwa kwa ukaribu zaidi kwa sababu sasa wanaume wanaanza kutengwa kwenye kupima, tiba na hata kwenye huduma za kijamii ambazo wanazipata kama wanakuwa kwenye vikundi.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2017 na mchakato wa bajeti wa mwaka 2018/2019. Kamati imechambua taarifa za utekelezaji na kugundua kwamba Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania katika mwaka wa fedha 2017/2018 ilitengewa shilingi Bilioni 5.9 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake lakini hadi kufikia Februari, 2018 ilipokea asilimia 57 tu. Kamati imebaini kuwa kumekuwepo na changamoto kwa Taasisi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI kupelekewa fedha kama zilivyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya matumizi. Katika mwaka wa Fedha wa 2018/2019, Tume ya UKIMWI iliomba jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 12 ikiwa ni makadirio ya matumizi yake. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi bilioni 10 sawa na asilimia 79 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 2 sawa na asilimia 20 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya maduhuli. Mwaka wa Fedha wa 2018/2019, *TACA/DSh*ai kupata maduhuli kama yalivyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy. Kwa Mwaka 2018/2019 ilikadiriwa kufanya matumizi ya shilingi bilioni 5.7. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 4 ambayo ni asilimia 85 iliombwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi milioni 800, sawa na asilimia 14 ni kwa ajili ya mishahara. Makadirio haya yameongezeka kwa kiasi cha shilingi bilioni 1.7 sawa na

asilimia 30 ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Katika uchambuzi wa Kamati ilibainika kwamba mamlaka hajitatenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa 2018/2019 ndio jambo ambalo Kamati imelibaini.

Mheshimiwa Spika, mafunzo na semina yalifanyika kutoka taasisi mbalimbali kwa ajili ya kujenga uwezo wa wanakamati na inatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa nitoe maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati, kama ifuatavyo:-

(i) Tume ya Kudhibiti UKIMWI (*TACAIDS*), kukinzana kwa sera, mipango na sheria mbalimbali. Hili linahusiana na miaka 18 kuwa ndiyo ukomo wa mtu kupima virusi vya UKIMWI kwa hiari bila ridhaa ya mzazi, ikilinganishwa na miaka 14 ambayo kisheria mtoto anaweza kuolewa. Kwa kuwa ukinzani huu unakwamisha juhudzi za mapambano dhidi ya UKIMWI hasa kwa kuzingatia kwamba asilimia 40 ya maambukizi mapya yapo mionganini mwa vijana wa umri wa miaka 15-24, na kwamba asilimia 80 ya maambukizi haya mapya katika kundi hili ni mionganini mwa watoto wa jinsia ya kike. Hivyo basi, Kamati inapendekeza, Shelia ya UKIMWI ifanyiwe mapitio ili kuzingatia hali halisi inayodhihirishwa na takwimu zilizopo, hasa katika kuwalinda zaidi vijana wetu wa kike. (*Makofii*)

(ii) Utegemezi wa fedha za wahisani kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kama tulivyojenga hoja, Kamati inaishauri Serikali ionye umuhimu wa kutenga fedha zake za ndani kwa ajili ya udhibiti wa UKIMWI kwa wananchi wake, na hii ni kwa kutumia mfuko wa *ATF* ambao tayari sheria ipo. Tunaiomba Wizara ya Fedha ifanye haraka mchakato wa kuweka tozo maalum ya kikodi kwa ajili ya Mfuko huu kupata fedha ya uhakika. Pia kushirikiana na wadau wa maendeleo na sekta binafsi kwa ajili ya kuanzisha mfuko unaoitwa *Endowment Fund* ambao unaweza ukaongeza nguvu kwenye mfuko wetu wa *ATF*.

(iii) Wanaume kutojitekeza kupima na kutokujinga kwenye vikundi vinavyowahusu hasa wale walioambukizwa Virusi vya UKIMWI. Kamati inashauri kuwa Serikali ifanye utaratibu wa haraka wa kuanzisha afua za kuhamasisha wanaume katika upimaji na katika kuhakikisha wale ambao wamekutwa na maambukizi wanashiriki kama ambavyo wanawake wanafanya kwa ajili ya kuongeza nguvu kwenye mapambano hayo.

(iv) Utekelezaji wa afua za UKIMWI kuwa maalumu. Huduma za tiba kwenye vituo vya afya umaalum wa utoaji wa huduma hizi mara nyingine unashiriki pia katika kuongeza unyanyapaa. Kwa hiyo basi, Kamati inashauri Serikali ifanye mapitio ya matokeo ya utafiti uliofanyika kwa muda mrefu sasa juu ya faida au hasara ya kutoa huduma ya UKIMWI katika maeneo mseto na kutumia matokeo ya utafiti huo katika kufanya maamuzi juu ya huduma ya Ukimwi kutolewa ama katika mazingira mseto au ya kipekee.

(v) Taasisi za Umma kutokuzingatia kikamilifu Sera na Sheria ya Ukimwi Katika Utekelezaji wa Afua za UKIMWI Mahala pa Kazi. Katika hili, Kamati inashauri Serikali kuimarisha uratibu na utekelezaji wa afua za UKIMWI kama zilivyoainishwa katika Sera na Sheria. Kamati inashauri kuwa Kitengo Maalum ndani ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI (*TACAIDS*) kinachoshughulika na uratibu wa shughuli za UKIMWI ndani ya Wizara na taasisi nyingine zote za umma kiimarishwe na kuhakikisha kwamba kinafanya kazi ipasavyo.

(vi) Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevyta, umuhimu wa Serikali kutenga fedha kwa ajili ya bajeti ya miradi ya maendeleo. Kamati inashauri Serikali kuiwezesha Mamlaka hii kuweza kutenga fedha kwenye bajeti yake kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa sababu mapambano dhidi ya madawa ya kulevyta ni suala la kimkakati zaidi kuliko vinginevyo.

(vii) Mfumo wa taasisi Katika utekelezaji wa shughuli za masuala ya dawa za kulevyta, kuna haja ya kuwa na mfumo kwenye ngazi ya chini kwa ajili ya kuratibu waraibu

na watu wote wanaoshughulika na mambo hayo kama ambavyo Serikali imefanya vizuri sana kwenye upande wa kuratibu watu kwa ngazi ya jamii kwenye suala la UKIMWI.

(viii) Sheria za Kupambana na Dawa za Kulevy ya mwaka 2015 inatekelezwa vizuri sana kwa ushahidi uliopo na kwa taarifa tunazozipata lakin kuna malalamiko kwamba kuna kukosekana kwa uwiano wa mapambano haya kati ya pande zetu mbili za Muungano. Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali kuitazama tena Sheria hii ili iweze kutoa fursa ya ushirikiano baina ya Mamlaka za Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy katika pande zote mbili za Muungano.

(ix) Mapambano ya dawa za kulevy kwenye maeneo ya viwanja vya ndege. Katika hili, Kamati inashauri Serikali iwekeze katika vitendea kazi vya kisasa vitakavyorahisisha zoezi zima la upekuzi na ukamataji wa dawa za kulevy kwenye viwanja vyetu vya ndege.

(x) Kutokuwepo kwa Sera ya Madawa ya Kulevy. Kwa kuwa mpaka sasa Tanzania haina Sera ya Taifa ya Kupambana na Dawa za Kulevy ambayo kwa umuhimu wake ingechagiza zaidi mapambano yaliyopo dhidi ya matumizi na biashara ya dawa za kulevy. Na kwa kuwa sera hii ina umuhimu mkubwa katika kuweka misingi na mwelekeo wa Taifa katika vita dhidi ya mapambano ya dawa za kulevy. Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali kuongeza kasi ya mchakato wa kuandaa Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, napenda kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu yake hadi kufikia Januari, 2019. Naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Walemavu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Naibu Waziri, Mheshimiwa Antony Mavunde na Naibu Waziri, Mheshimiwa Stella Ikupa. Aidha, nampongeza pia Mkurugenzi Mtendaji

wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Dkt. Leonard Maboko na Kamishna wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti.

**MHE. OSCAR R. MUKASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, naomba kuwashukuru Wajumbe wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza shughuli zilizotekelizwa, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali na kupokea ripoti yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee ripoti ya Kamati. (*Makofii*)

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI  
TAARIFA YA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA KWA KIPINDI CHA  
JANUARI, 2018 HADI JANUARI, 2019 KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

### **SEHEMU YA KWANZA**

#### **1.0      UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati, kukushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Mwaka kuhusu majukumu na shughuli zilizotekelizwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI.Taaria hii ya kipindi

cha mwaka 2018/2019 ni kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika**, Muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 123 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, hivyo imegawanyika katika sehemu kuu tatu (3). Sehemu ya Kwanza ni ya Utangulizi unaofafanua muundo, majukumu pamoja na maelezo ya jumla kuhusu utekelezaji shughuli za Kamati. Sehemu ya Pili ni Uchambuzi na Matokeo ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati. Katika Sehemu ya Tatu Kamati imetoa, mapendekezo na hitimisho.

### **1.1 Muundo na Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane ya Kanuni ya 118 (10) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Masuala ya UKIMWI inasimamia shughuli za Taasisi mbili ambazo ni Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*) na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyा.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kusimamia majukumu ya Taasisi hizo, Kanuni hiyo pia imeipa Kamati jukumu la kuratibu masuala yote yanayohusu UKIMWI katika sekta zote ikiwemo kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na udhibiti wa dawa za kulevyा. Hivyo Kamati inatekeleza majukumu yafuatayo:-

- a) Kuratibu masuala yanayohusu UKIMWI katika sekta zote Tanzania Bara;
- b) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na udhibiti wa Dawa za Kulevyा;
- c) Kujadili na kutoa mapendekezo na ushauri kuhusu hatua za kudhibiti dawa za kulevyा; na
- d) Kushughulikia Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyा.

## **1.2 Utaratibu uliotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, taratibu zifuatazo zimekuwa zikitumika katika kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake:-

- (a) Kufanya vikao na Wizara na Taasisi kwa kuwaomba kufika mbele ya Kamati ili kutoa taarifa juu ya jambo au suala mahususi ambalo Kamati ilipenda kupata taarifa zake kutoka kwa Watendaji wa Wizara na Taasisi hizo;
- (b) Kufanya ziara ili kukagua shughuli zinazozekelezwa katika kushughulikia masuala ya UKIMWI na Dawa za Kulevyta
- (c) Kushiriki semina, tamasha na warsha mbalimbali zilizohusu Masuala ya UKIMWI na Dawa za Kulevyta; na
- (d) Kufuatilia utekelezaji wa Majukumu ya Wizara na Taasisi hizo.

## **1.3 Shughuli zilizotekelzwa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kutekeleza majukumu yake kwa kipindi cha Januari, 2018 hadi Januari, 2019, Kamati ilikuwa na shughuli zifuatazo:-

- (a) Kufuatilia utekelezaji wa Afua mbalimbali za UKIMWI na Dawa za Kulevyta katika Wizara na Taasisi balimbali;
- (b) Mafunzo mbalimbali kuhusiana na masuala ya UKIMWI na Dawa za Kulevyta;
- (c) Ziara za Kamati katika sekta mbalimbali zinazojihusisha na mapambano ya UKIMWI na Dawa za Kulevyta kwa lengo la kuona na kutoa ushauri kuhusiana na maeneo hayo.
- (d) Kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

(e) Kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyia kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

## **SEHEMU YA PILI**

### **2.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii inaelezea utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa kipindi cha Januari, 2018 hadi Januari, 2019 kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 hususan Kanuni ya 117 inayohusu utaratibu katika Kamati za Kudumu za Bunge. Hivyo, Kamati iliandaa Mpango Kazi uliotekelizwa katika kipindi hicho ambao Matokeo ya utekelezaji wake yamefanyiwa uchambuzi katika Sehemu hii.

### **2.1 KUFUATILIA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilianza utekelezaji wa majukumu yake kwa kufuatilia kwa ukaribu utendaji kazi wa Taasisi zilizo chini yake pamoja na utekelezaji wa Sera na Mpango inayohusu Udhibiti wa UKIMWI na Dawa za Kulevyia katika Wizara na Taasisi za Umma nchini kama ifuatavyo:-

#### **2.1.1 TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA**

**Mheshimiwa Spika**, katika kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

a) Ufinyu wa Bajeti na ucheleweshwaji wa fedha kutoka serikalini ambapo kwa sasa zaidi ya asili 90 ya bajeti ya Tume inategemea fedha za wafadhili wa nje hali inayopunguza ufanisi wa Tume katika mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI.

- b) Kukinzana kwa Sheria ya UKIMWI na Sheria mbalimbali hususan katika umri wa mtu kupima kwa hiari au kwa ridhaa ya mzazi kwa mtoto (chini ya miaka 18) ilihali Sheria ya Ndoa inaruhusu mtoto chini ya miaka 14 kuolewa kwa ridhaa ya mzazi. Ukinzani huu unakwamisha juhudzi za mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI hususan katika kundi la watu wenye umri mdogo.
- c) Mapungufu ya kiusimamizi katika Sera ya UKIMWI ya Mwaka 2001. Sera hii ipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na utekelezaji wa Sheria ya UKIMWI upo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Hali hii inapelekea mlolongo wa kufanya maamuzi kwa jambo moja pale panapohitajika rejea ya Sera na Sheria kwa pamoja.
- d) Kuwepo kwa tofauti kubwa kwenye takwimu za masuala ya UKIMWI baina ya zile zinazotolewa na Tume ya Taifa ya UKIMWI, Ofisi ya Takwimu ya Taifa dhidi ya Taasisi nyingine za umma na wadau mbalimbali. Hali hii inasababisha mkanganyiko katika matumizi ya takwimu hizo na na hivyo kusababisha vikwazo katika kujenga hoja na kutekeleza shughuli mbalimbali.

#### **2.1.2 MFUKO WA TAIFA WA KUDHIBITI UKIMWI (AIDS TRUST FUND (ATF)**

**Mheshimiwa Spika**, mwaka, 2015 Bunge lilipitisha Sheria ya Mfuko wa UKIMWI (Aids Trust Fund - ATF). Lengo la Mfuko ni kuhakikisha Serikali inatenga fedha zake za ndani kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI. Mfuko ulijiwekea malengo ambayo ni kuongeza rasilimali fedha za ndani kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI kutoka asilimia **7** mwaka 2015 hadi kufikia asilimia **30 ya mahitaji** ifikapo mwaka 2018 sambamba na kuongeza mchango wa sekta binafsi katika udhibiti wa UKIMWI kutoka asilimia 8 hadi asilimia 15 kufikia 2018. Mpaka sasa malengo haya hayajafanikiwa na **asilimia 95** ya fedha zote za mapambano dhidi ya UKIMWI bado ni kutoka kwa wafadhili.

Pamoja na mipango na malengo ya kuanzisha Mfuko huu, Kamati imebaini kuwepo kasi ndogo ya utekelezaji wake, kwani hadi sasa Mfuko haujaanza kufanya kazi iliyokusudiwa. Hivyo Kamati inasisitiza kukamilisha taratibu stahiki ili Mfuko ukamilike. Aidha, inasisitiza kuwa ni vema Serikali ikaweka tozo maalum ya kikodi ili Mfuko uweze kuwa na chanzo cha uhakika cha mapato. Aidha, upo umuhimu sasa kwa Serikali kubuni uwekezaji kwa kushirikisha sekta binafsiili kuwekeza katika miradi ambayo sehemu ya faida itakua chanzo cha mapato kwa ajili ya Mfuko (Endowment Fund).

#### **2.1.3 MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

**Mheshimiwa Spika**, Katika utekelezaji majukumu ya Mamlaka ya Kudhibiti Kupambana na dawa na Kulevya, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

(a) Kukosekana kabisa kwa fedha za Miradi ya Maendeleo ni tatizo kubwa ikizingatiwa kuwa ajenda ya kupambana na dawa za kulevya ni kubwa na pana kuliko inavyochukuliwa kwa sasa;

(b) Kutokuwepo kwa kwa Sera ya Taifa ya Kupambana na Dawa za Kulevya ni suala lenye uzito mkubwa na hivyo linahitaji msukuo wa ziada.:

(c) Kukosekana kwa Mfumo maalum kwa ngazi ya Jamii kwa ajili ya kuwatambua waraibu wa dawa za kulevya. Kwa sababu hiyo kunakua na upungufu wa mwitikio wa Kitaifa wa kupambana na tatizo hilo; hii ni pamoja na kukosekana kwa elimu ya kutosha kuhusu matumizi na madhara ya dawa za kulevya kama ilivyofanyika kwa mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU/UKIMWI;

(d) Kuwepo kwa baadhi ya NGOs na Taasisi zinazojihusisha na mapambano dhidi ya Madawa ya Kulevya nchini ambazo hazina muundo na mifumo rasmi kwa jinsi zinavyowasaidia waathirika wa dawa za kulevya.

#### **2.1.4 TAASISI ZA UMMA ZA KISEKTA ZINAZOTEKELEZA SERA ZA UKIMWI NA DAWA ZA KULEVYA**

##### **(a) Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ili kujadili hatua iliyofikiwa katika Utafiti wa Upatikanaji wa Chanjo ya UKIMWI nchini. Kamati ilibaini kuwa wataalamu wa utafiti wa tiba bado wapo kwenye hatua za awali za utafiti wa chanjo na tiba. Hata hivyo, kutokana na changamoto ya rasilimali fedha, rasilimali watu na teknolojia ya juu inayohitajika katika utafiti. Kwa sababu hiyo Tanzania, kama ilivyo katika nchi nyingine za Afrika, inategemea tafiti zinazofanywa na nchi zilizoendelea kama Ulaya na Marekani. Ipo haja ya Serikali kuweka mkazo katika kuhakikisha uwepo wa rasilimali kwa ajili ya tafiti.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee Na Watoto kuhusu utendaji wa Bohari Kuu ya Dawa Nchini (MSD) kuhusu upatikanaji wa Dawa za ARV na Kifua Kikuu, taarifa ya Utekelezaji wa shughuli za Programu ya Taifa ya Kupambana na UKIMWI (NACP) pamoja na taarifa kuhusu Mashirika yasiyo ya kiserikali yanayojihusisha na uratibu wa masuala ya UKIMWI Nchini.

Kwa ujumla, Kamati ilibaini na kutoa ushauri kuhusu mambo ya msingi yafuatayo:-

i) Kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa dawa za kufubaza makali ya virusi vya UKIMWI (ARV's) unategemea Wafadhili wa Global Fund na USAID. Kamati ina maoni kuwa, mwenendo huu wa kutegemea wafadhili kupata ARV's bila ya kuweka mipango madhubuti ya kupata fedha za bajeti ya ndani kwa ajili ya kununua dawa hauhakikishi mapambano endelevu dhidi ya UKIMWI. Ni vema Serikali ikaanza kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa UKIMWI (ATF) ili kuwa na uhakika wa fedha za ndani, ili ziweze kutumika pindi ikihitajika.

ii) Kwa mujibu wa utafiti wa Tanzania HIV impact Survey (THIS 2017), takwimu zikuonyesha kuwa **asilimia 40** ya maambukizi mapya yapo katika umri wa miaka 15-24, na **asilimia 80** ya hao ni wasichana. Kwa kuwa kundi la vijana walio katika umri huu ni kubwa na kwa kiwango kikubwa wako katika shule za Sekondari na Vyuo, Kamati inaona kuna umuhimu wa Serikali kuweka juhudii kubwa katika kukabiliana na maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI katika Taasisi za Elimu.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonesha kuwa Tanzania haijafanikiwa kwa kiwango cha kutosha katika Mkakati wa 90 90 90 hususan kwenye 90 ya kwanza inayotaka asilimia 90 ya watanzania wanaokadirwa kuwa na maambukizi ya VVU wawe wamepima afya zao ifikapo Mwaka 2020. Pamoja na maelezo yaliyotolewa na Wizara sambamba na takwimu za maambukizi mapya miongoni mwa vijana wa umri wa miaka 15-24, Kamati ilitaka kujua hatua iliyofikiwa katika marekebisho ya Sheria ya UKIMWI ili kuongeeza wigo wa upimaji na kuendana na makubaliano ya Kimataifa. Kamati inashauri Serikali kuongeza kasi kukamilisha marekebisho ya Sheria ya UKIMWI. Aidha Kamati ianaipongeza Serikali kwa hatua iliyofikiwa katika utafiti juu ya matumizi ya dawa za kukabiliana na maambukizi ya VVU kwenye makundi maalum (PREP). Kamati inasistiza umuhimu wa kukamilika kwa utafiti huu kwa ajili ya hatua zinazofuata.

**b) Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasilino**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasilino ili kujadili Udhhibit wa Uingizwaji wa Dawa za Kulevyta kwenye maeneo ya Bandari, Fukwe, Reli, Barabara Kuu na Viwanja vya Ndege, ambapo Kamati ilibaini yafuatayo:-

i) Uhaba wa vitendea kazi kwa ajili ya kupambana na dawa za kulevyta kwa baadhi ya viwanja vya ndege kama mashine za kukagua abiria ;

ii) Baadhi ya viwanja vya ndege nchini havina vifaa na Mbwa maalum wa kunusa na kubaini dawa haramu za kulevyia ili kupambana na tatizo hilo;

iii) Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) kukosa vitendea kazi kama mashine za kisasa za (*X - Ray Backscatter*) zenyet uwezo wa kung'amuia dawa za kulevyia kwenye mizigo ya abiria na vituo vya malori ya mizigo pamoja na mbwa maalum wa kunusa.

c) **Wizara ya Madini**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Wizara ya Madini ili kujadii hali ya Virusi vya UKIMWI kwenye Migodi ya Tanzania, ambapo ilibaini yafuatayo:-

i) Takwimu za hali ya Maambukizi ya VVU na UKIMWI Migodini hazikuweza kubainisha ukubwa wa tatizo na hatua zitakazochukuliwa za kukabiliana na janga hilo kwa kuzingatia muktadha wa 90 90 90;

ii) Hakuna utaratibu wa kuhamasisha matumizi ya kondomu za kike pamoja na upatikanaji wake kwa ajili ya kuwezesha wanawake kuzitumia na kujikinga dhidi ya Maambukizi ya VVU;na

iii) Kukosekana kwa mwongozo na mikakati ya namna ya kuratibu afua za UKIMWI katika maeneo ya Migodi pamoja na waratibu wa kusimamia ipasavyo Madawati ya UKIMWI katika kila Mgodi ambao wananchi watakuwa wanapata taarifa na huduma wanazostahili.

d) **Ofisi ya Raisi - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Ofisi ya Raisi - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kupoea taarifa kuhusu utekelezaji wa Afua za UKIMWI mahala pa kazi pamoja na uratibu wa Asasi sizizo za Kiserikali zinazojihusisha na masuala ya UKIMWI kwenye ngazi ya Wilaya, Kata na Vijiji. Taarifa ya Wizara ilieleza Mikakati iliyopo na inayotekelizwa katika kupambana na maambukizi ya VVU na UKIMWI kwa jumla.

Taarifa pia ilainisha malengo mahsus ya Wizara, utekelezaji wake, mafanikio, pamoja na changamoto zilizopo katika kila hatua zinazochukuliwa. Aidha taarifa ilifanua kuhusu uratibu wa asasi zisizo za kiserikali (NGO's) zinazotekeleza Afua za UKIMWI katika ngazi mbalimbai za Serikali za Mitaa.

Kufuatia Taarifa iliyowasilishwa, Wajumbe walijadili na kuibua hoja mbalimbali ambazo zilihitaji ufanuzi, kisha kutoa Ushauri wa namna ya kuimarisha Mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI kama ifuatavyo:-

i) Ni hatua gani zinachukuliwa na Wizara katika kuratibu na kusimamia upaikanaji wa lishe bora kwa wanafunzi walioathirika na VVU walio katika shule za sekondari, hususan za bweni

ii) Ni vigezo gani vinatumika katika kugawa fedha za *Global Fund* katika Sekretarieti za Mikoa na Hamashauri. Kamati haikuweza kupata ufanuzi kuhusu tofauti kubwa ya fedha za Global Fund zinazopelekwa katika Halmashauri mbalimbali. Ni muhimu kanuni za mgawanyo huo zikawa na uwazi zaidi kwa ajili ya ufanisi hasa kwa kuzingatia kwamba mapambano dhidi ya UKIMWI ni lazima yazingatie kinga pamoja na matumizi ya dawa za kufubaza.

iii) Kamati inasilitiza kuwa ni vyema Wizara ikaimarisha uratibu kwa kutambua Asasi gani inafanya nini, inafanya wapi, kwa muda gani, kwa gharama kiasi gani na kwa matoeo gani. Aidha Wizara iwe na malengo na vipaumbele vya afua, kisha kuzitaka Asasi hizo kufuata Mpango wa Serikali katika kutekeleza Afua za UKIMWI, badala ya kila Asasi kutaka kutekeleza vile inajvyojipangia yenye.

**e) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na kupokea taarifa kuhusu utekelezaji wa Afua za UKIMWI mahala pa

kazi pamoja na hatua na namna inavyoshirikiana na Mataifa mengine katika mapambano dhidi ya madawa ya kulevy. Kwa ujumla Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

i) Pamoja na mikakati mingi inayoelezwa kutekelezwa na Wizara katika mapambano dhidi ya mambukizi ya VVU na UKIMWI mahala pa kazi zilizochukuliwa na Wizara haionyeshi matokeo mahsus. Aidha changamoto zinazoelezwa na Wizara kama sababu za utekelezaji hafifu wa Afua ikiwa ni pamoja na ufinyu wa bajeti na mwamko mdogo mionganoni mwa watumishi wanaoishi na VVU kujitokeza zinaashiria kutokuwepo kwa hatua madhubuti za kupambana na maambukizi ya VVU na UKIMWI. Kwa mfano Kamati ilibaini kuwa, Wizara ilikua imeunda Kamati ya UKIMWI na magonjwa yasiyo ya kuambukiza mahala pa kazi, wiki chache tu kabla ya kukutana na Kamati ya Masuala ya UKIMWI.

ii) Katika suala la mapambano dhidi ya madawa ya kulevy, taarifa imeainisha namna ambavyo Tanzania imekua ikishirikiana na Mataifa mengine katika mapambano dhidi ya madawa ya kulevy. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua inazozichukua katika kuhakikisha kunakuwepo na ushirikiano wa Tanznnia na Jumuia ya Kimataifa katika mapambabo dhidi ya janga hili.

f) **Wizara ya Fedha na Mipango.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Wizara ya Fedha na Mipango na kupokea Taarifa kuhusu Mwenendo wa kupokea na kutumia fedha za Global Fund katika kipindi cha miaka mitano, Mipango na Mikakati endelevu ya Upatikanaji wa Fedha za ndani kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI pamoja na Utekelezajii wa Afua za UKIWI mahala pa kazi ndani ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Taarifa ya Wizara ilieleza mwenendo wa kupokea na matumizi ya Fedha za Mfuko wa Global Fund kwa Tanzania

kuanzia Julai 2012 hadi Disemba 2018.Na kwamba Tanzania ni nchi ya pili barani Afrika (baada ya Nigeria) inayonufaika zaidi na Fedha za Mfuko wa Dunia wa kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria. Kati ya Julai 2012 na Disemba 2018 Tanzania imepokea na kutumia kiasi cha **Dola za Marekani 555.6** kutoka katika Mfuko wa Global Fund. Kwa ujumla fedha hizo zimeimarisha utoaji wa huduma za afya ikiwa ni pamoja na kuweza kufikia kiwango cha asilimia 90 katika kutoa tiba ya Kifua Kikuu, kupunguza vifo vitokanavyo na malaria na kupunguza maambukizi ya VVU.

Uchambuzi wa Kamati umebaini na kuhoji mambo ya msingi yafuatayo: -

. Serikali kushindwa kutumia kwa asilimia 100 kiasi cha fedha zinazotolewa na *Global Fund* kutohana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na; kukosekana watumishi wa kutosha katika sekta ya Afya kwa ajili ya kusimamia na kufuatalilia matumizi ya Fedha za Global Fund pamoja na ucheleweshaji wa marejesho ya msamaha wa kodi hivyo kuathiri utekelezaji wa program za *Global Fund* katika nyakati tofauti. Kamati haikiridhishwa na kasi ndogo ya matumizi (*low burning rate*) ya fedha za *Global Fund*. Hivyo Kamati inasilitiza Serikali kuweka mazingira wezeshi ili kutumia fedha za Mfuko wa *Global Fund* kwa asilimia 100, hasa ikizingatiwa kuwa fedha zinazotolewa zisipotumika kwa wakati uliopangwa huathiri mgao kutoka *Global Fund* kwa mwaka unaofuatia.

. Mpaka sasa hakuna Mkakati endelevu wa uhakika wa upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya kupambana na UKIMWI.Bado kwa kiasi kikubwa mapambano dhidi ya UKIMWI yanategemea fedha za wafadhili. Pamoja na hatua nzuri ya Serikali kuanzisha Mfuko wa Taifa wa UKIMWI (ATF) lakini bado hakuna vyanzo maalum mahsus kwa ajili ya kupata fedha za Mfuko. Kamati inashauri Serikali kukamilisha mchakato wa kuanzisha tozo maalum kwa ajili ya mfuko wa ATF. Aidha Kamati inapendekeza Serikali kuwa na Uwezekano wa kuwa na endowment fund.

Kutokuwepo kwa ukaguzi wa CAG katika fedha zinazokuja nchini kwa kuitia Taasisi zisizo za Serikali. Kikwazo hiki ni kwa mujibu wa Sheria ambayo inamzuia CAG kufanya ukaguzi kwenye taasisi ambazo Serikali ina hisa kidogo. Suala hili lina umuhimu wa pekee kwa sababu fedha hizi ni nyingi kwa ujumla wake na zinakuja kwa jina la Wanzania.

Aidha Kamati ilibaini kukosekana kwa umadhubuti wa Kamati ya UKIMWI na magonjwa yasiyo ya kuambukiza mahala pa kazi.

## **2.2 ZIARA ZILIZOFANYWA NA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki, Kamati ilifanya ziara ya kikazi katika Taasisi ya Afya Ifakala (*Ifakara Health Center - IHI*) na Hospitali ya St. Francis zilizopo Mkoani Morogoro kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa afua na Sera ya UKIMWI na Dawa za Kulevyा.

Kamati ilibaini kuwa, pamoja na huduma za kupima VVU na kukabiliana na magonjwa nyemelezikama TB, vile vile Taasisi hizi zinatoa huduma ya Kliniki Mseto (*One-Stop Clinic and Chronic disease clinic*) ambapo imeunganisha kliniki ya mama, baba na motto wenye maambukizi ya VVU pamoja na ile inayojumuisha huduma za UKIMWI na magonjwa mengine ya kudumu kama Kisukari na Shinikizo la damu.

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia ziara hii Kamati ilibaini mambo yafuatayo: -

(a) Kuwepo changamoto ya upatikanaji wa vitendanishi vyta kupima wingi wa VVU katika Maabara ya Taasisi ya Afya ya Ifakara (IHI) ambayo kwa makubaliano ya kimkataba inatoa huduma kwa wagonjwa wa Hospitali ya Mt. Fransis-Ifakara na Wilaya nzima ya Kilombero.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa, kwa sasa IHI haipatiwi vitenganishi kwa ajili ya upimaji wa *Viral load* wakati Taasisi hiyo inayo mashine ya kufanya vipimo hivyo. Mashine hiyo aina ya **Abbott m2000** ina uwezo wa kupima sampuli 13,545 kwa mwaka ilihali Mkoa mzima wa Morogoro unayo mashine inayoweza kupima sampuli 9,000 tu kwa mwaka. Kwa maana hiyo endapo Taasisi ya IHI itapata mgawo wa vitendanishi vyta Serikali kutoka Bohari ya Taifa ya Madawa (MSD), Mkoa utakua na uwezo wa kupima sampuli 22,000 kwa mwaka na hivyo kufanya ongezeko la upimaji kwa asilimia 60. Kwa sasa Wilaya imekuwa ikipokea sampuli za damu kutoka katika vituo mbalimbali na kuzisafirisha kwenda maabara ya Hospitali ya Mkoa wa Morogoro kwa ajili ya kupimwa. Kutokana na umbali na miundombinu mibaya ya barabara hususana wakati wa masika, majibu ya wagonjwa huchukua muda mrefu na hivyo kukosesha wagonjwa huduma bora ya haraka na kwa wakati.

Katika Mkoa mzima wa Morogoro, Hospitali ya mkoa ina uweezo wa kuhudumia sampuli 9,000 kwa mwaka. Kwa maana hiyo Serikali ina fursa ya kujumuisha huduma kutoka Taaisisi ya IHI na Hospitali ya Mkoa na hivyo kuweza kuhudumia sampuli zipatazo 22,000 badala ya 9,000 za sasa.

Kwa maelezo hayo, Kamati haikuridhishwa na sababu za IHI kutopatiwa vitendanishi.

(b) Kuwepo kwa malalamiko ya wananchi juu ya ghamama kubwa za matibabu zinazotozwa na Hospitali ya St Francis, ilihali ikiwa inapata ruzuku ya Serikali. Hali hii inapelekea wagonjwa walio wengi kutokumudu ghamama hizo na kutafuta njia nyingine za kupata matibabu. Kamati iliwasilisha suala hili kwa Mamlaka husika na hatua zilichukuliwa.

(c) Kuwepo takwimu zinazoashiria kwamba, idadi kubwa ya wanaume hawajitokezi katika kupima VVU na kuijunga na vikundi vyta watu wanaoishi na maambukizi

ya VVU. Kamati inaishauri Serikali kutafuta afua maalum za kupunguza ushiriki mdogo wa wanaume.

(d) Lipo tatizo la kukosekana Sera na mwongozo wa kuwapatia huduma bila malipo WAVIU dawa za magonjwa nyemelezi na hali nyingine zenyenye gharama kubwa ya tiba kwa mfano, figo na kisukari kama ilivyo kwa dawa za kufubaza virusi vya Ukimwi (ARV). Kamati inasisitiza umuhimu wa bima ya afya kwa watu wanaoishi na maambukizi ya VVU.

(e) Lipo tatizo kubwa la usugu wa utumiaji dawa kwa watoto kuliko wakubwa kwa sababu ya kukosekana uelewa na umakini wa wasimamizi wa watoto ambao wanategemea kupewa dawa na watu wanaowasimamia. Kamati inashauri Serikali kufanya tafiti na kutoa taarifa juu ya hatua zinazofaa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitoa ushauri kwamba, Ili kutoa huduma bora ya kupima wingi wa virusi, ni vema Serikali ikaongeza ushirikiano na Taaisi zisizo za Kiserikali katika tafiti na utoaji wa huduma.

### **2.3 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA WA 2017/2018 NA MCHAKATO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri ilioutoa kuhusu Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Taasisi hizo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Taarifa hizo ziliwasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) Toleo la Januari, 2016, mnamo mwezi Machi, 2018.

#### **2.3.1 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania**

##### **a) Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Tume ilitengewa

kiasi cha shilingi **Bilioni 5.983** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Hadi kufikia tarehe 28, Februari 2018 Tume ilipokea kiasi cha shilingi **Bilioni 3.462**, sawa na **asilimia 57.8** tu ya fedha zote zilizotakiwa kutolewa na Serikali kwenda katika Tume hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa kumekuwepo na changamoto kwa Taasisi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI ya kupelekewa fedha zilivyoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inasisitiza Serikali kuimarisha upelekaji wa fedha Tume ya Kudhibiti UKIMWI ili Tume iweze kutekeleza mipango iliyojiwekea, kwani ni dhahiri kwamba kila mwaka unakuwa na mipango na malengo yake ambayo huwa ni endelevu.

**b) Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi**

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa Fedha wa 2018/2019 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS)-**Fungu 92**, iliomba jumla ya kiasi cha shilingi **Bilioni 12.909** ikiwa ni makadirio ya matumizi yake. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi **Bilioni 10.300** sawa na **asilimia 79.7** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na shilingi **Bilioni 2.609** sawa na **asilimia 20.2** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha mishahara ya watumishi.

**c) Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**katika Mwaka wa Fedha wa 2018/2019 Tume ya Kudhibiti UKIMWI - Fungu 92 haikuwa na makadirio ya makusanyo ya maduhuli yaliyoidhinishwa na Bunge.

### **2.3.2 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyा**

**a) Uchambuzi wa makadirio na matumizi**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyा ilikadiriwa kufanya matumizi ya kiasi cha Shilingi **Bilioni 5.755**


kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni **4.948** sawa na **asilimia 85.9** ya fedha yote inayoombwani kwa ajili ya Matumizi mengineyo (Jedwali namba 1) na Shilingi **806.549** sawa na **asilimia 14.1** ni kwa ajili ya Mishahara. Makadirio haya yameongezeka kwa kiasi cha shilingi **Bilioni 1.74** sawa na **asilimia 30.2** ikilinganishwa na makadirio ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi wa Kamati, ilibainika kwamba Mamlaka haijatenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa Fedha wa 2018/2019 kama ambavyo ilijitokeza kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, kama inavyoonyeshwa katika **Jedwali namba 2**. Muendelezo huu wa kutotenga fedha za maendeleo unaashiria kutolitazama tatizo hili kimkakati na baade kutakuwa na madhara makubwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua majukumu ya Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevyaa ambayo ni udhibiti wa matumizi ya dawa za kulevyaa, kufanya uelimishaji kwa jamii na kufanya afua za kupunguza madhara ya dawa za kulevyaa kwa jamii. Ni dhahiri kwamba jukumu la pili na la tatu ni ya kimkakati kuliko vinginevyo

**Mheshimiwa Spika**, ni maoni ya Kamati kuwa kuna umuhimu wa Mamlaka ya kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyaa kuanza kutenga fedha kwenye Bajeti yake kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kwa kufanya hivyo, kutasaidia kujenga mfumo bora wa kudhibiti na kupambana na dawa za kulevyaa nchini kwa upana wake ikiwa ni pamoja na kujenga jamii ya Watanzania isiyotumia dawa za kulevyaa na kutoshiriki katika biashara na matumizi ya dawa za kulevyaa.

**Jedwali namba. 1**



**Jedwali namba 2.**



**Chanzo:** Bajeti za Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevyaa kwa miaka ya fedha 2011/12, 2012/13, 2013/14, 2014/15, 2015/16, 2016/17, 2017/18. 2018/19

**b) Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2018/2019 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyia (Fungu 91) haikuwa na Makadirio ya makusanyo ya maduhuli yaliyoidhinishwa na Bunge.

**2.4 MAFUNZO NA SEMINA KWA WAJUMBE WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha Wajumbe wa Kamati wanajengewa uwezo katika maeneo mbalimbali lakini pia wanashirikiana na wadau katika kubadilishana mawazo na uzoefu, Kamati ilipata mafunzo kwa njia ya semina kutoka kwa Taasisi mbalimbali kama ifuatavyo: -

**a) Semina kuhusu Muundo na Majukumu ya Tume na Mamlaka zinazosimamiwa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Wajumbe walipata elimu kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu Shughuli za Kamati ikiwemo muundo na majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyia.

**MWENENDO WA FEDHA ZA MERADI WA MAFUNZO KWA FUNGU 91 KUANZA MWAKA WA FEDHA 2011/12 HADIA**

**2018/19**

**Ashiria ya Fedha**

**Ukumbi wa Kulevyia kasihi. Mbalibali nafasi data uelewa juu ya**

**mapambano na kilichotolewa na hubu na mamlaka** na Mamlaka

**Uliyoidhinishwa kakeleza Serikali** na Serikali

**ufahamu jigu ya hali ya maambukizi ya UKIMWI na udhibiti**

**wa Dawa za Kulevyia kwa mwaka 2015/2016 pamoja na**

**wajibu wa mwananchi katika mapambano hayo. Semina**

**350,000,000/- tera 125,000,000/-chi, 2018 85%**

**Zalendo ya Zamani Ofisi Bunge, Dodoma.**

**b) 0 Semina ya Ugonjwa wa UKIMWI katika Sekta**

**ya Kilimo 0 0 0%**

**Semina hii iliendeshwa na Taasisi 0% Action Aid kwa ajili ya kukuza uelewa kwa Wajumbe wa Kamati kuhusu umuhimu wa mapambano ya UKIMWI katika Sekta ya Kilimo**

na changamoto zake kwa maendeleo ya Taifa. Wajumbe walipata fursa ya kufahamu umuhimu wa serikali kutenga bajeti ya kutosha katika mapambano dhidi ya UKIMWI, kwa kuwa kilimo ni sekta ya uzalishaji ambayo huchangia kukuza pato na kuimarisha uchumi wa Taifa. Kwa mujibu wa Tafiti za Viashiria na Matokeo ya UKIMWI Tanzania (*THIS*) ya Mwaka 2016/2017 vinaonyesha kuwa vijana wenyе umri wa miaka 15-24 wanapata maambuki ya ugonjwa wa UKIMWI kwa **asilimia 1.4**. Aidha wanawake wenyе umri wa miaka 15 hadi 64 wana maambukizi ya juu kwa **asilimia 6.5**. Semina hii ilitolewa hapa Mjini Dodoma, tarehe 27 Machi, 2018 katika Ukumbi ulioko African Dreams.

c) **Semina ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy Na. 5 ya Mwaka 2015 na Marekebisho yake ya Mwaka 2017**

Semina ilitolewa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy kwa ajili ya kuwapa wajumbe uelewa wa umuhimu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy, makosa yanayohusiana na mazao ya dawa za kulevy na umiliki wake pamoja na kemikali zinazotumiwa kutengenezea dawa za kulevy. Aidha, semina hii iliwavezesha Wajumbe kuelewa umuhimu wa marekebisho ya Sheria hii kwa kuzingatia hali ya uingizwaji wa dawa hizo na mbini mbalimbali wanazotumia pamoja na ongezeko kubwa la vijana wanaojingiza katika matumizi ya dawa za kulevy aambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa. Semina hii ilifanyika terehe 26 Mei, 2018 katika Ukumbi wa Zahanati ya Zamani, Ofisi ya Bunge Dodoma.

d) **Semina ya hali halisi ya Kifua Kikuu (TB), pamoja na mwingiliano wake na UKIMWI, mafanikio na changamoto katika udhibiti wake hapa nchin.**

Semina hii iliendeshwa na Shirika la KNCV Tuberculosis Foundation kwa ajili ya kuwapatia Wajumbe uelewa kuhusu Hali ya Kifua Kikuu nchini pamoja na Azimio la AZAKI katika Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Kifua Kikuu, Mafanikio na Changamoto zinazoikabili jamii katika utekelezaji wa

shughuli za Kifua Kikuu. Wajumbe walifahamishwa kuwa Kifua Kikuu ni ugonjwa wa kuambukiza na unaongoza kwa kusababisha vifo vingi Duniani na Tanzania ni mionganini mwa nchi 30 zenyet tatizo kubwa la Kifua Kikuu. Kila mwaka inakadiriwa kuwa watu 160,000 wanaugua Ugonjwa wa Kifua Kikuu hapa nchini. Semina hii ilifanyika mara mbili kuhakikisha Wajumbe wa Kamati wanapata fursa ya kuweza kujadili na kuishauri vizuri serikali katika mapambano ya Kifua Kikuu (TB). Semina hii ilifanyika terehe 30 Mei, 2018 katika Ukumbi wa St. Gaspar Hotel na tarehe 21 Juni, 2018 ilifanyikia katika Zahanati ya Zamani, Ofisi ya Bunge Dodoma.

**e) Semina kuhusu Takwimu za Maambukizi ya UKIMWI na mwitikio wa Kitaifa wa kukabiliana na maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI**

Semina ilitolewa na Taasisi ya JHPIEGO chini ya Mradi wa Sauti Yetu kwa ajili ya kuwapa wajumbe uelewa kuhusu takwimu halisi za hali ya maambukizi ya UKIMWI Kitaifa na Kidunia pamoja na uhamasishaji wa wananchi kupima Virusi vya UKIMWI kwa hiari hususan wanaume.

Wajumbe walifahamishwa kuwa, takwimu za utafiti wa hali na viashiria vya UKIMWI Tanzania kwa mwaka 2016/2017 zinaonesha kuwa idadi ya raia wa Tanzania inakisiwa kuwa ni **50.9** milioni. Ukubwa wa maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI (VVU) kitaifa mionganini mwa jamii yenye umri wa miaka 15 – 49 ni wastani wa asilimia **4.7** Kitaifa; wanawake wakiwa asilimia **6.2** na wanaume ni asilimia **3.1**. Inakadiriwa kuwa jumla ya watanzania **milioni 1.4** wanaishi na Virusi vya UKIMWI na kwa vijana wa umri wa miaka kati ya 15 na 24 ni asilimia **1.4**. Wavulana asilimia **0.6** na wasichana ni asilimia **2.1**. Semina hii ilifanyika terehe 23 Juni, 2018 katika Ukumbi wa Zahanati ya Zamani, Ofisi ya Bunge Dodoma.

**f) Kongamano la Wadau wa Masuala ya UKIMWI na Bunge**

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake ya kufuatilia utekelezaji wa Sera za UKIMWI na Dawa

za Kulevyta, tarehe 20 Juni, 2018, Kamati ilipata fursa ya kushiriki katika Tamasha ambalo pia lilihusisha Wabunge wote akiwemo Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano Tanzania. Maudhui ya Tamasha hilo yalihu nafasi ya viongozi katika kufikia azma ya 90-90-90 ifikapo mwaka 2020. Aidha, Tamasha hili lilitibiana Taasisi zisizo za Kiserikali na Asasi za Kiraia chini ya mwamvuli wa Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na VVU na UKIMWI (*NACOPHA*). Katika Tamasha hilo Wabunge walipata uelewa zaidi kuhusu umuhimu wa ushiriki wa viongozi katika kuhamasisha mapambano dhidi ya Ugonjwa wa UKIMWI. Katika Tamasha Wabunge wakiongozwa na Mheshimikwa Spika, walishirki kupima afya zao ikiwa ni njia mojawapo ya kuhamasisha Watanzania kupima afya kwa lengo la kujua hali zao kuhusu na maambukizi ya VVU. Aidha katika Kongamano hilo wajumbe na wabunge kwa ujumla walipata fursa ya kujadilana na wadau wa masuala ya UKIMWI juu ya maswala mbalimbali ya kisera na kiusimamizi

## **SEHEMU YA TATU**

### **3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na shughuli za Kamati zilizofanyika katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Januari 2018 – Januari 2019, kumekuwa na changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika Taasisi zinazosimamiwa na Kamati hii ambazo Kamati inazitolea maoni na ushauri ufuatao:-

#### **3.1 TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA (TACAIDS)**

##### **a) Kukinzana kwa Sera, Mipango na Sheria mbalimbali za UKIMWI**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kukinzana baina ya Sheria ya UKIMWI ambayo katika suala la umri wa mtu kupima kwa hiari sharti awe na miaka 18 au kwa ridhaa ya mzazi kwa walio chini ya miaka 18, wakati sheria ya Ndoa

inaruhusu mtoto chini ya miaka 14 kuolewa kwa ridhaa ya mzazi.

**NA KWA KUWA** Ukinzani huu unakwamisha juhudzi za mapambano dhidi ya UKIMWI hasa kwa kuzingatia kwamba asilimia 40 ya maambukizi mapya yapo miongoni mwa vijana wa umri wa miaka 15-24.

**HIVYO BASI** Kamati inapendekeza, Sheria ya UKIMWI ifanyiwe mapitio ili kuzingatia hali halisi inayodhihirishwa na takwimu zilizopo.

**b) Utegemezi wa Fedha za Wahisani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kuwa kwa kiasi asilimia kubwa Bajeti ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania imekuwa ikitegemea fedha za wahisani, ambapo uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa katika mwaka wa Fedha wa 2017/2018 Serikali haikutenga kiasi chochote cha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ilihali mwaka wa Fedha wa 2018/2019, imetenga kiasi cha shilingi **Bilioni 3** tu sawa na **asilimia 29.1** ya fedha yote iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Tume.

**NA KWA KUWA**, kuendelea kutegemea wafadhili wa nje hakutoi uhakika wa mapambano endeevu dhidi ya maambukizi ya VVU na ugonjwa wa UKIMWI ambayo yanahitaji rasilimali fedha za uhakika za kutosha.

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali ione umuhimu wa kutenga fedha zake za ndani kwa ajili ya udhibiti wa UKIMWI kwa wananchi wake. Aidha, Serikali iweke mpango mkakati wa kupata vyanzo vingine vya mapato vya kuijwezesha kutenga fedha zaidi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Itakuwa jambo jema endapo bajeti ya UKIMWI angalau asilimia 50 ya fedha ya maendeleo ya Tume iwe ni fedha za ndani na asilimia 25 tu itokane na wafadhili wa nje kwa kuwa tatizo hili ni la wananchi wote na si wale wenye maambukizi pekee.

c) Kuanzisha Tozo kwa Mfuko wa UKIMWI wa Taifa (AIDS Trust Fund - ATF)

**KWA KUWA** Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya kuanzisha Mfuko wa UKIMWI (Aids Trust Fund - ATF) ambao lengo lake ni kuhakikisha Serikali inatenga fedha zake za ndani kwa ajili ya kupambana na ugonjwa wa UKIMWI.

**NA KWA KUWA** Mfuko ulijiwekea malengo ya kuongeza rasilimali fedha za ndani kutoka **asilimia 7** mwaka 2015 hadi kufikia **asilimia 30** ifikapo mwaka 2018, pamoja na kuongeza mchango wa sekta binafsi katika udhibiti wa UKIMWI kutoka **asilimia 8** hadi **asilimia 15** kufikia 2018.

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali ianzishe kisheria chanzo mahususi cha kutunisha Mfuko huu kama ilivyo kwenye mifuko mingine. Kamati inapendekeza Serikali iharakishe mchakato wa tozo maalum kwa ajili ya Mfuko wa ATF. Aidha, Serikali ibuni uwekezaji kwa kushirikisha na Sekta binafsi ili kuwekeza katika miradi ambayo sehemu ya faida itakua chanzo cha mapato kwa ajili ya Mfuko (*Endowment fund*).

d) Usimaizi na Utekelezaji wa Sera ya Masuala ya UKIMWI

**KWA KUWA**, Sera ya Masuala ya UKIMWI ipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na utekelezaji wa Sheria ya UKIMWI upo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**NA KWA KUWA** utaratibu uliopo unapelekeea mlolongo mrefu katika kufanya maamuzi kwa jambo moja pale panapohitajika rejea ya Sera na Sheria ambazo zipo chini ya mamlaka mbili tofauti.

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashuri kuwa, Sera na Sheria ya UKIMWI ziwekwe chini ya mwamvuli mmoja wa maamuzi na utekelezaji ili kuharakisha utekelezaji wa mpango na mikakati mbalimbali ya UKIMWI.

e) **Ukaguzi wa Fedha za UKIMWI**

**KWA KUWA, rasilimali fedha za mapambano dhidi ya UKIMWI** ni fedha za umma ambazo upatikanaji wake unahusisha Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa nje na ndani ya nchi.

**NA KWA KUWA,** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Ukaguzi ya Mwaka 2008 hana mamlaka kufanya ukaguzi wa fedha za UKIMWI katika mashirika mbalimbali ya ndani na nje zilizopatikana kwa jina la watanzania hasa ambazo haziingii katika mfuko mkuu wa Serikali.

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri, fedha zote zinazoingia nchini kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya UKIMWI licha ya kutoingia katika mfuko mkuu wa Serikali zikaguliwe na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Fedha za Serikali. Na kwamba Sheria inayomnyima mamlaka Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Fedha za Serikali irekebishwe ili impe Mdhibiti na Mkaguzi wa Serikali mamlaka ya kufanya ukaguzi katika taasisi hizo zisizo za kiserikali ili kuona kilichotekelawa ikilinganishwa na Mawasilisho yaliyowasilishwa kwa wafadhili. Kwa kufanya hivi kutaongeza uratibu wa usimamizi wa fedha zinzoelekezwa katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

f) **Takwimu za Utekelezaji wa Afua mbalimbali za UKIMWI**

**KWA KUWA,** utekelezaji wa afua mbalimbali za UKIMWI unatokana na takwimu ambazo zinapatikana kutoka katika vyanzo tofauti tofauti ikiwemo Serikali pamoja na wadau wake.

**NA KWA KUWA,** kumekuwa na matukio ya mkinzano wa takwimu katika jambo moja,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inishauri Serikali kuwa na utaratibu utakaoondoa migongano ya takwimu kwani

migongano hiyo inaathiri shughuli za watumiaji wa takwimu hizo.

**g) Mabadiliko ya Sheria ya UKIMWI kuhusiana na Umri wa mtu Kuweza Kupima VVU na Upimaji wa mtu binafsi**

**KWA KUWA**, takwimu zinaonyesha kuwepo kwa asilimia 40 ya maambukizi mapya ya VVU kwa vijana wenye umri wa kuanzia miaka 15-24, na kwamba 80% ya maambukizi haya mapya ni mionganoni mwa jinsia ya kike.

**NA KWA KUWA**, Tanzania haijafanya vizuri katika malengo ya 90 ya kwanza ya mapambano ya UKIMWI (Kwa mujibu wa takwimu) ipo haja ya Serikali kufanya taafakari juu ya mchakato wa upimaji wa mtu binafsi (*Self Testing*).

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kufanya mabadiliko katika Sheria ya UKIMWI ili kuzingatia mahitaji mapya kwa mujibu wa takwimu.

**h) Wanaume Kutojitokeza Kupima UKIMWI**

**KWA KUWA**, Kamati imebaini takwimu zinaonyesha wanaume wamekuwa hawajitokezi kwa wingi kupima na kutambua hali zao za maambukizi ya UKIMWI ikilinganishwa na wanawake.

**NA KWA KUWA**, wanaume wanashiriki katika vikundi vya WAVIU na wakati huo huo upo ushahidi unaoonyesha kuwa vikundi hivi vina msaada mkubwa kwa wanachama wake.

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaishauri kuwa, Serikali ijikite katika kuendeleza afua za kuhamasisha wanaume katika upimaji wa VVU na ushiriki katika vikundi vya watu wanaoishi na VVU.

**i) Shughuli za Kiuchumi na Maambukizi ya UKIMWI**

**KWA KUWA**, Utafiti unaonesha kwamba sababu ya maambukizi kupanda katika baadhi ya maeneo ni pamoja na shughuli za kiuchumi na maendeleo ikiwemo ujenzi wa barabara, uchimbaji wa madini, ujenzi wa reli, kilimo cha

kisasa, wavuvi, maeneo ya viwanda na migodini, ambazo hupelekea watu kuhama kutoka maeneo mbalimbali kwenda katika maeneo hayo.

**NA KWA KUWA**, uchambuzi wa Kamati umebaini katika maeneo hayo kutokuwepo mkakati maalumu na wa maksudi wa kuhaikisha maeneo hayo yanapewa elimu ya kutosha ya namna ya kujikinga na maambukizi ya VVU.

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali iweke mkakati maalumu na wa maksudi wa kuhaikisha maeneo hayo yanapewa elimu ya kutosha ya namna ya kujikinga na maambukizi ya VVU na Tiba ya UKIMWI ili kuwawezesha kuendeleza utekelezaji wa shughuli hizo za maendeleo. Aidha, Serikali pamoja na wadau wake waelekeze nguvu kubwa pia katika kuhamasiha jamii ili kuweza kubadili tabia (Behavioural Change Programmes) ambayo inawalenga **asilimia 95** ya watu ambao hawaishi na VVU ili kuweza kuwakinga wasipate maambukizi ya UKIMWI.

**j) Utekelezaji wa Afua za UKIMWI Kuwa Maalumu**

**KWA KUWA**, utekelezaji wa afua za UKIMWI umepewa umaalumu mkubwa hasa kwenye vituo vya kutolea huduma.

**NA KWA KUWA**, Kamati imebaini kuwa katika baadhi ya maeneo ya kutolea huduma umaalum huo umekuwa ni sehemu ya unyanyapaa,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali ifanye utafiti wa kuangalia faida na hasara za kufanya utoaji wa huduma za masuala ya UKIMWI kuwa maalumu na kutumia matokeo ya tafiti hiyo kuamua kama kuna ulazima sa kuendelea na umaalum uliopo au vinginevyo.

**k) Tafiti kwa ajili ya upatikanaji chanjo ya UKIMWI**

**KWA KUWA**, Kamati imebaini kuwepo kasi ndogo ya utafiti wa chanjo na tiba ya UKIMWI, ambapo bado wataalamu wetu, kama nchi wapo kwenye hatua za awali

za utafiti wa chanjo hiyo kutokana na changamoto ya rasilimali fedha, rasilimali watu na teknolojia ya juu inayohitajika katika utafiti wa chanjo hiyo.

**NA KWA KUWA**, suala la kupata chanjo ya tiba ya UKIMWI lina umuhimu mkubwa katika mapambano dhidi ya UKIMWI, lakini pia ni suala la ustawi wa jamii na uchumi.

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kuwekeza katika utafiti wa chanjo ya UKIMWI, kama hatua muhimu katika kukabiliana na UKIMWI.

**I) Taasisi za Umma kutozingatia kikamilifu Sera na Sheria ya UKIMWI katika utekelezaji wa Afua za UKIMWI mahala pa kazi**

**KWA KUWA**, Kamati imebaini kuwa, baadhi ya Taasisi za umma hazizingatii ipasavyo matakwa ya Sera na Sheria ya UKIMWI katika kutekeleza Afua za UKIMWI katika ofisi. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, katika Ofisi nydingi za uma hakuna mwamko wa watumishi kupima maambukizi ya VVU, watumishi hawako tayari kuweka wazi hali ya afya zao ili kuweza kunufaika na huduma za walioathirika, bajeti zinazotengwa kwa ajili ya kutekeza afua za UKIMWI ni kiasi kidogo, hazitolewi kwa wakati, na pale zinapotolewa hazitumiki.

**NA KWA KUWA**, mwenendo huu wa kukosekana chachu ya mapambano dhidi ya UKIMWI mahala pa kazi ni hatarishi kwa ustawi wa Taifa,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kuimarisha uratibu na utekelezaji wa Afua za UKIMWI kama zilivyoainishwa katika Sera na Sheria kwa kutenga bajeti ya kukidhi mipango na mikakati ya kupambana na UKIMWI mahala pa kazi, kuhamasisha watumishi kupima maambukizi ya VVU, kubuni mbinu za kuwafanya watumishi kuweka wazi hali zao za afya ili watakaoonekana wana maambukizi waweze kuanza kutumia dawa. Aidha Kamati inshauri Kamati za UKIMWI katika Taasisi mbalimbali za uma,

ziimarishwe ili zitekeleze majukumu yake pamoja na kutakiwa kutoa taarifa kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI. Kitengo maalum ndani ya TACAIDS kinachoshughulika na uratibu wa shughuli za UKIMWI ndani ya Wizara na Taasisi za Umma kiimarishwe na kusimamiwa ipasavyo.

### **3.2 MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

**a) Umuhimu wa Serikali kutenga fedha kwa ajili ya bajeti ya miradi ya Miradi ya Maendeleo.**

**KWA KUWA**, kwa kuzingatia majukumu ya Mamlaka ya Kudhibiti na kupambana na Dawa za Kulevya ambayo ni udhibiti wa matumizi ya dawa za kulevya, kufanya uelimishaji kwa jamii na kufanya afua za kupunguza madhara ya dawa za kulevya kwa jamii.

**NA KWA KUWA**, jukumu la pili na la tatu ni ya kimkakati zaidi ikilinganishwa na jukumu la kwanza, na utekelezaji wake unahitaji rasiliali fedha za kukidhi ukubwa wa tatizo la athari za biashara na matumizi ya dawa za kulevya, ilihali bado elimu kuhusu matumizi na madhara ya dawa za kulevya haijawafikia wanajamii kwa kiasi kikubwa.

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kuiwezesha Mamlaka hii kwa kutenga fedha kwenye Bajeti yake kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha hizo zitaiwezesha mamlaka kuimarisha program za kuhamasisha na kutoa elimu ya madhara ya biashara na matumizi ya dawa za kulevya kwa wananchi ili waweze kushiriki kikamilifu katika kupambana na kudhibiti dawa za kulevya kwani vita hii ni ngumu na endelevu. Hivyo ni wakati muafaka kwa Serikali kuchukua hatua za haraka kuhakikisha Mamlaka na wadau wengine wa dawa za kulevya wanatoa elimu jamii ya kutosha kuanzia ngazi ya Kaya, Vijijini, Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa zima kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kufanya hivyo, kutasaidia kujenga mfumo bora wa kudhibiti na kupambana na dawa

za kulevya nchini pamoja na kujenga jamii ya Watanzania isiyotumia dawa za kulevya na kutoshiriki katika biashara na matumizi ya dawa za kulevya. Kwa hali ilivyo, dawa za kulevya ni tatizo linaloongezeka kwa kiwango kikubwa katika jamii yetu siku hadi siku na linaathiri vijana wengi ambaao ndiyo nguvu kazi ya Taifa.

**b) Mfumo wa Taasisi katika Utekelezaji wa shughuli za Masuala ya Dawa za Kulevya**

**KWA KUWA**, Serikali imekuwa ikiendeleza mapambano dhidi ya udhibiti na upambanaji wa Dawa za kulevya nchini ikishirikiana na wadau mbalimbali zikiwemo taasisi zisizo za kiserikali.

**NA KWA KUWA**, uchambuzi wa Kamati umebainilka kuwa, zipo baadhi ya NGOs na Taasisi zinazojihusisha na masuala ya dawa za kulevya nchini ambazo hazina muundo na mifumo rasmi wa jinsi gani zinawasaidia watumiaji wa dawa za kulevya. Badhi zikitekeleza shughuli zake kwa kuwabagua watumiaji wa dawa hizo, mfano zinazo wahudumia wanawake peke yake, wale wanaojidunga kwa sindano na mara nyingine wale wanaotumia kwa kuvuta. Ikizingatiwa kuwa, watumiaji wengi wanaotumia kwa kujidunga ni wale ambaao wamepitaa katika hatua ya kuvuta kwanza na ndipo anakwenda katika hatua ya kujidunga, ubaguzi huu hauna tija katika mapambano dhidi ya matumizi na athari ya watumiaji wa dawa za kulevya.

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri kuwa, kuititia Mamalaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya pamoja na Wizara ya Afya, Jinsia, Wazee na Watoto kuititia kitengo chake cha uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali wafanye zoezi la utambuzi na uratibu wa asasi zote zinazojishughulisha na Dawa za Kulevya ili kuangalia malengo yao pamoja na kazi zinazofanywa na asasi hizo na kuwawekea mfumo rasmi wa utekelezaji wa shughuli zao ili kuhakikisha kuwa walengwa wanafaidika na uwepo wa asasi hizi kwani fedha zinazotolewa ni kwa jina la

watanzania. Aidha mfano mzuri wa uratibu wa aina hiyo ni ule wa wadau wa mwitikio wa UKIMWI nchini.

**c) Uanzishwaji wa Vikundi vyta Watu walioathirika na Dawa za Kulevyta**

**KWA KUWA**, tafiti zinaonesha kuwa, watu wanaoishi na Virusi vyta UKIMWI (WAVIU) wamefanikiwa kuitia mabaraza yao yajulikanayo kama (KONGA) ambayo yalianzishwa kuanzia ngazi ya Kata hadi Wilaya.

**NA KWA KUWA**, kuitia mfumo huo wameweza kupata taarifa na kupokea afua mbalimbali za Masuala ya UKIMWI kwa urahisi,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kushirikiana na Asasi zisizo za kiserikali kubuni namna sahihi na ya kimkakati ya kuwafikia watu walioathirika na Dawa za Kulevyta ili iwe njia rahisi ya kuwatambua, kuwashirikisha na kuwasaidia waathirika wa dawa za kulevyta katika mwitikio wa kitaifa wa janga hili. Njia hii inaweza kusaidia kuwafatilia kwaukaribu mienendo yao ili kuacha matumizi ya dawa hizo, kupunguza unyanyapaa mionganii mwa jamii, kuwawezesha kufanya shughuli nyingine za kiuchumi pamoja na kupata takwimu sahihi ya warahibu.

Kwa kufanya hivi tutajenga Taifa ambalo ni imara na haya yote yanaweza kufanywa chini ya uratibu wa uongozi wa Halmashauri husika kama ambavyo imefanikiwa kwa upande wa UKIMWI.

**d) Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevyta ya Mwaka 2015 kutumikaka pia Tanzania Zanzibar.**

**KWA KUWA**, Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevyta inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevyta, chini ya Kifungu Namba 4 na 5 ya Mwaka 2015. Ikizingatiwa kuwa, Sheria hii ni mionganii mwa Sheria ambazo

zimetambulika na nchi nyingine kuwa ni Sheria nzuri ya Kupambana na Dawa za Kulevya.

**NA KWA KUWA**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwepo changamoto ya ushirikiano baina ya Mamlaka za Kupambana na Madawa ya Kulevya kwa pande mbili za Muungano,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kutafuta njia bora ya kutoa fursa ya ushirikiano ya baina ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya katika pande zote mbili za Muungano.

**e) Mapambano ya Dawa za Kulevya kwenye maeneo ya Viwanja vya Ndege**

**KWA KUWA**, juhudzi za Mapambano dhidi ya Uingizwaji wa Dawa za Kulevya kwenye maeneo ya Viwanja vya Ndege zinafanywa na Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa nje na ndani ya nchi.

**NA KWA KUWA**, utekelezaji wake unaonekana kuwa mgumu kutokana na ukosefu wa vitendea kazi vya kisasa kwa baadhi ya viwanja vya ndege kukosa mashine za ukaguzi wa abiria na mizigo kikamilifu.

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali iwekeze katika vitendea kazi vya kisasa vitakavyorahisisha zoezi zima la upukuzi na ukamataji wa dawa za kulevya zinazoingizwa nchini kuitia njia mbalimbali lakini pia vitakavyolinda afya za watumishi. Aidha, Wizara ishirikiane na vyombo vya dola katika kuandaa kampeni endelevu ambazo mbali nakuwepo vifaa madhubuti itawajengea uwezo watumishi kutumia kikamilifu vifaa na teknolojia ya kisasa katika kudhibiti dawa za kulevya.

**f) Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu Na Majini (SUMATRA)**

**KWA KUWA**, tafiti zinaonyesha kuwa, zipo mbinu mbalimbali zinazotumika kusafirisha dawa za kulevya ikiwa

ni pamoja na kubeba mizigo ya kawaida na kuficha ndani ya bidhaa nyingine kama magunia na viroba na hata kwa kutumia maiti.

**NA KWA KUWA**, jukumu la kupambana na dawa za kulevyta linahitaji ushirikiano na wadau mbalimbali ikiwemo sekta ya usafirishaji wa anga, barabara, reli na bandari.

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kuititia Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) kuweka mikakati maalum ya kuhakisha wanaboresha na kusimamia viwango vya usalama kwa kufunga mashine za kisasa za (*X - Ray Backscatter*) zenye uwezo wa kung' amua dawa za kulevyta kwenye mizigo ya abiria, vituo vya malori ya mizigo pamoja na mbwa maalum wa kunusa.

**g) Kutokuwepo kwa Sera ya Madawa ya Kulevyta**

**KWA KUWA**, Mpaka sasa Tanzania haina Sera ya Taifa ya Kupambana na Dawa za Kulevyta, ambayo kwa umuhimu wake ingeimaridha mapambano yaliyopo dhidi ya matumizi na biashara ya dawa za kulevyta.

**NA KWA KUWA**, Sera ina umuhimu mkubwa katika kuweka misingi na mwelekeo wa Taifa katika vita dhidi ya madawa ya kulevyta kwa ujula wake.

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kuongeza kasi ya mchakato wa kuandaa Sera ya Taifa ya kudhibiti na kupambana na Madawa ya Kulevyta Nchini.

**SEHEMU YA NNE**

**4.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu yake hadi kufikia Januari, 2019.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Walemavu, Mhe. Jenista Mhagama, Mb na Naibu Waziri Antony Mavunde na Stella Ikupa, Mb. Aidha, nampongeza pia Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Dkt. Leonard Maboko na Kamishna wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyा, Ndг. Rogers Siyan'ga na Watendaji wote wa Tume na Mamlaka kwa ushirikiano walioipa Kamati kwa kipindi cha mwaka mzima, kwa kufika mbele ya Kamati na kutoa ufanuzi mara zote ulipohitajika.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa uchapakazi wao wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Kamati kwa mwaka mzima. Wajumbe wamefanya kazi kubwa katika kuhakikisha Kamati inaisimamia na kuishauri Serikali ipasavyo. Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa majina kama ifuatavyo:-

1.Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa	-	Mwenyekiti
2.Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa Bunga, Mb	-	M/Mwenyekiti
3.Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb	-	Mjumbe
4.Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb	-	Mjumbe
5.Mhe. Dkt. Haji Hussein Mponda, Mb	-	Mjumbe
6.Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb	-	Mjumbe
7.Mhe. Edward Franz Mwalongo, Mb	-	Mjumbe
8.Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb	-	Mjumbe
9.Mhe. Prof. Norman Adamson Sigalla King, Mb	-	Mjumbe
10.Mhe. Kemirembe Julius Lwota, Mb	-	Mjumbe
11.Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb	-	Mjumbe
12.Mhe. Mattar Ali Salum, Mb	-	Mjumbe
13.Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb	-	Mjumbe
14.Mhe.Oliver Daniel Semuguruka, Mb	-	Mjumbe
15.Mhe. Susan Anselim Lyimo, Mb	-	Mjumbe
16.Mhe. Zainab Matitu Vullu, Mb	-	Mjumbe
17.Mhe.Omary Ahmed Badwel, Mb	-	Mjumbe
18.Makame Mashaka Foum, Mb	-	Mjumbe
19.Munde Tambwe Abdallah, Mb	-	Mjumbe
20.Mhe Amina Nassor Makilagi, Mb	-	Mjumbe

- |                                   |   |        |
|-----------------------------------|---|--------|
| 21.MheYussufu Haji Khamisi, Mb    | - | Mjumbe |
| 22.Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb    | - | Mjumbe |
| 23.Mhe. Ester Nicholas Matiko, Mb | - | Mjumbe |
| 24.Mhe. Fratei Gregory Massey, Mb | - | Mjumbe |
| 25.Mhe. Godfrey W. Mgimwa         | - | Mjumbe |
| 26.Mhe.Mwigulu L. Nchomba, Mb     | - | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, kwa ushirikiano ambao amekuwa akiutoa kwa Kamati. Pamoja na yeye, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge – Ndg. Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi – Ndg. Dickson Bisile, Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Asia Msangi, Ndg. Happiness Ndalu, Ndg. Virgil Mtui pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Grace Mwenye, kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa, Uchambuzi wa Matokeo ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati, Maoni na Mapendekezo mbele ya Bunge lako Tukufu, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa lipokee, lijadili na kuikubali Taarifa ya mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo kwa ajili ya utekelezaji wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

.....  
Oscar Rwegasira Mukasa, Mb  
**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI**

**FEBRUARI, 2019**

**SPIKA:** Nakushukuru sana MwenyeKITI wa Masuala ya UKIMWI kwa hotuba yenu kama Kamati. Mheshimiwa Nsanzugwanko nimekuona umesimama.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Nashukuru kabisa, hoja imeungwa mkono. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia upande wa uchangiaji na tunazichangia Kamati zote tatu kwa wakati mmoja kutegemeana na Kamati ipi ambayo wewe mwenyewe umejipanga ama zote kutokana na hali itakavyokuwa, dakika zetu ndiyo hizo inabidi ujipange vizuri. Nani atufungulie leo, Mheshimiwa James Mbatia hebu tuanzishie leo dakika 10, atafuatia Mheshimiwa Edward Mwalongo na wengine waendelee kuwepo.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, nitajikita zaidi kwenye Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii na mapendekezo yao na ushauri wao ni mzuri sana, nawapongeza Kamati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa wamefafanua baadhi ya malengo na mwelekeo wa elimu yetu Tanzania. Lengo la Nne la Maendeleo Endelevu Duniani ni elimu bora, sawa, shirikishi kwa wote. Tunajiuliza leo hii, je, Sera yetu ya Elimu Tanzania na mitaala, muhtasari na vitabu vinaakisi mahitaji ya kusudio hili au lengo hili la dunia? Je, mahitaji ya msingi ya wanafunzi wetu, marupurupu ya walimu wetu, mazingira rafiki katika shule zetu, yanaweza yakaakisi lengo hili la dunia?

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu ukiangalia Sera yetu ya Elimu ya sasa hapa Tanzania na Mheshimiwa Waziri aliwahi kusema hapa Bungeni kwamba ina matatizo, tunajiuliza leo hii Tanzania tunafuata sera ipi ya elimu? Ni Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 au ni Sera ya Eimu ya mwaka 1995? Hii ni kwa sababu Sera ya Elimu ya sasa inasema elimu msingi ni miaka sita baadaye miaka minne

lakini kuna *pre-primary* ambayo inakuwa ni miaka 11. Leo tunafata Sheria ya Elimu ya mwaka 1978, kwa hivyo elimu yetu inakuwa haina mfumo ambao ni shirkishi, bora na unaelekeza usawa kwa wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu tumekuwa tunafanya elimu yetu *sample* na majoribio ya mara kwa mara, kwa mfano, suala la *Big Results Now*, ninayo nakala yake hapa, ukiangalia yaliyokuwa yameainishwa humu ndani yalikuwa ni mazuri sana. Hata hivyo, kisoma taarifa hii ya Katibu Mkuu ya utafiti ya Wizara ya Elimu, ambayo ilikuwa inaeleza elimu yetu kwa miaka mpaka 2024, ukurasa ule wa pili inasema, tatizo kubwa tulilonalo katika elimu yetu ni masuala ya kimfumo, kuna upungufu mkubwa wa kimfumo. Ni Wizara inasema yenye. Ukienda mbele zaidi ukurasa wa 62 inasema: "Usimamizi na uendeshaji wa elimu, ultiotajwa kwa kiwango kikubwa, ni chanzo cha matatizo ya elimu Tanzania."

Mheshimiwa Spika, sasa hii ni Serikali yenye inasema hivyo, leo hii tunajiliza, hivi kweli mfumo wetu wa elimu, taarifa ya Serikali za Mitaa hapa, ya Mheshimiwa Rweikiza ameiwasilisha vizuri; hivi masuala ya kisera, Kimuundo, Kiuendeshaji yako TAMISEMI au yako kwenye Wizara yenye ya Elimu? Je, Waziri wa Elimu au Katibu Mkuu wa Elimu na Katibu Mkuu wa TAMISEMI wanaingilia vipi katika usimamiza wa Maafisa Elimu katika ngazi za Mikoa, ngazi za Halmashauri na Wilayani na kwingineko?

Mheshimiwa Spika, tatizo hili kwa kiasi kikubwa, ndiyo maana maandiko matakati fu yanasema, watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa. Ninasema hivyo kwa sababu, ukiangalia Tanzania ya leo, *product* ambayo tunazalisha sasa hivi; ukichukua Elimu ya Msingi, Sekondari, mpaka Vyuo Vikuu, kwa mwaka tunazalisha watu zaidi ya 1,200,000. Ifikapo miaka kumi ijayo, tutakuwa na vijana zaidi ya milioni 12, hawajui waende wapi, kwa sababu elimu yetu haimfanyi huyu kijana akawa mbunifu, awe *skilled* akajua kabisa ninamaliza elimu kwa kiwango hiki, naenda wapi.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu ni mara nyingi na nime-check kwenye *Hansard* ya Bunge ya mwaka 2013, niliwahi kusema kwamba udhaifu ulioko katika Sekta ya Elimu hapa Tanzania ndijo unaosababisha tabia ya Watanzania walio wengi wa kutokujiamini katika kufanya majukumu yao, kupotea kwa mila na desturi za Kitanzania, kumomonyoka kwa uadilifu mionganoni mwa wafanyakazi wetu, kuperomoka kwa uwajibikaji, yako mengi ambayo yaliainishwa.

Mheshimiwa Spika, athari zake sasa nini? Zinasababisha nini katika elimu yetu? Athari zake ni pamoja na ugumu wa elimu yenyewe, huduma mbovu zinazotokea katika sekta mbalimbali, viwango duni vya ubora wa bidhaa hii inayozalishwa hapa Tanzania, uharibifu wa mazingira yetu, udhaifu katika kukabiliana na majanga ya aina mbalimbali hata namna gani tunasimamia TEHAMA yetu.

Mheshimiwa Spika, hii ripoti ukiisoma tufanye nini kwenye utafiti ili tujue tunaenda wapi, ukurasa wa 55 unasema, nchi za Afrika zimekubaliana kwamba 1% ya *GDP* yake iwekezwe kwenye utafiti, lakini taarifa ya Kamati inaonyesha hapa inasema ni asilimia 0.034 ndijo inayotolewa kwenye utafiti, ambapo kutokana na *GDP* yetu utafiti peke yake, *COSTECH* wangetakiwa wapate *one point two trillion* kwa sababu ndio tunajijua tunataka twende wapi; lakini leo hii, wanapata shilingi billioni 40 tu. Kwa hiyo, hapa kitakwimu ni kwamba tunaiua elimu yetu sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, sasa ukiangalia Vyuo Vikuu, mathalan, nilikuwa naangalia kwenye utafiti, ukiangalia Vyuo Vikuu 28,000 duniani, kwenye *Ranking Web of Universities*; 28,077. Tanzania tuko wapi? Tanzania kitakwimu kati ya Vyuo Vikuu 28,000 mpaka 10,000 hapo katikati, Tanzania ndijo tunaingia hapo kwenye *University* zetu tano tu. Tuko kati ya 5,000 mpaka 10,000. Ni kwamba sasa tuko kwenye dunia gani Tanzania? Yaani katika 5,000 bora hatumo duniani.

Mheshimiwa Spika, naomba tu kwa unyenyekevu mkubwa, Vyuo vyetu Vikuu ukiangalia mfumo wenyewe wa

utoaji mikopo, hauoani na mikopo inarudishwa. Je, ule utaratibu ambaa tulishawahi kuusema Benki, tukawa hata na Benki ya mikopo, watu wanaenda kukopa kule kwenye Benki moja kwa moja na mkaweka mfumo wa namna gani wa kurudisha hizo fedha ili mikopo yetu iweze ikawa ni endelevu umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ubunifu uko wapi? Vyuo Vikuu vya Umma viko hoi bin taaban. Kwa mfano, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tangu mwaka 2014 wale wanataluma; kinaidai Serikali zaidi bilioni 16.1 na Wahadhiri hao, Wanataluma wako kwenye hali ambayo ni ngumu sana, ambayo inaleta matatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ajira, zimefanyika teuzi mbalimbali kutoka kwenye Vyuo Vikuu, *replacement yake ikoje?* Ndiyo maana unakuta Vyuo Vikuu vyetu leo hii zaidi ya watu wenye umri wa wanataluma Wahadhiri wenye miaka 70 na kuendelea, bado wanapewa ajira za mikataba katika Vyuo Vikuu na *efficiency* inakuwa kwenye hali ya namna gani?

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mazingira, kuna mtaalam mmoja aliwahi kusema kwenye dunia ya leo “*with technology things are changing faster than we can imagine, knowledge is for free for those who loves it, an educated person is the one who loves knowledge and seek it.*”

Mheshimiwa Spika, nimelisema hilo kwa sababu kama hatutakubali, tukarudi miaka ya 1980 ambako kwenye Kamisheni ya Jackson Makwetta, ambayo alipendekeza tufanye nini Tanzania; na mpaka miaka 13 baadaye ndiyo ikatoka sera ya kwanza ya mwaka 1995.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa kabisa, niiombe Serikali ya Awamu ya Tano, Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli, aunde Kamisheni ya Elimu Tanzania kabla ya Taifa letu la Tanzania halijaangamia. Kamisheni ya Elimu ambayo itatuambia sisi humu ndani tunataka nini, Kamisheni ya Elimu

itakayojadiliana kama Watanzania tunataka mfumo wa namna gani vijana wetu wajiedeleze; Kamisheni ambayo tutajua duniani kuko namna gani; Kamisheni itakayotuonyesha mfumo wetu wa elimu uwe namna gani; Kamisheni ambayo itatuonyesha Tanzania ya leo tunataka iende upande gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia kwa maneno ya Yeremia 22:29 inasema, "Ee nchi, nchi, nchi lisikie neno la Bwana."

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunisikiliza.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango wako. Nadhani Wapinzani wengine wanaweza wakajifunza kutoka kwako. Siyo lazima mtu ukashifu au udharau. Hawa ma-senator wanachangia vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Edward Mwalongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa name niweze kuchangia Kamati mbalimbali ambazo zimewasilisha taarifa zake leo ikiwemo Kamati ya UKIMWI, ambayo mimi pia ni Mjumbe katika Kamati hiyo. Awali ya yote nimpongeze sana Mwenyekiti wangu, kwa wasilisho lake lillo zuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, mapambano dhidi ya UKIMWI yana utata mwangi sana, lakini sisi kama nchi, nadhani sasa imefika wakati tuweze kuona kwamba ni nini tufanya ili tuweze kupambana na UKIMWI vilivyo. Kwanza kabisa nianze na jambo moja, uko ukinzani wa kisheria ambao unatuletea shida sana katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ndoa, inasema, mtoto anaweza akaolewa kwa ridhaa ya mzazi, akiwa na miaka 14, lakini Sheria ya UKIMWI inamtaka mtoto huyu apime kwa hiyari vizuri vya UKIMWI akiwa na miaka 18. Maana yake nini? Maana yake binti au kijana au hawa wanandoa, wakitaka

kupima na hata kama wameshaoana, maana yake wafunge safari warudi kwa wazazi, wakawaambie wazazi wao kwamba sasa tunaomba mtusindikize Hospitali au kwenye kituo cha kupima, tukapime UKIMWI. Ni jambo ambalo linaleta utata sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali iangalie tufanye nini haraka iwezekanavyo ili hizi sheria zisikinzane. Haiwezekani mtoto huyu mwenye miaka 14 aende kwa mzazi akaombe kwenda kupima. Kwa hiyo, nayo inaleta shida katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo linaleta shida katika mapambano dhidi ya UKIMWI, liko tatizo kubwa sana, ukisoma kwenye bajeti za Wizara UKIMWI ipo kwenye kipaumbele. Hata ukienda kwenye Halmashauri, mapambano ya UKIMWI yako kwenye kipaumbele, lakini ikija kwenye utekelezaji, liko tatizo kubwa. Ni kwamba haya mambo yanapitishwa na Bunge hapa, bajeti inatengwa, lakini ikifika kule Wizarani au ama kwenye Taasisi za Umma inawekwa tu, hakuna anayefanya kazi.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia kwenye Kamati yetu ya UKIMWI, tukiita Taasisi za Umma, kuja kueleza afua za UKIMWI mahala pa kazi, unakuja kuta ndiyo Kamati imeundwa. Maana yake ni nini? Wito wa Bunge kuja kujibia afua za UKIMWI kwenye Taasisi zao za Umma ndiyo imewafungua macho kwamba kumbe liko jambo tunatakiwa kulijadili katika ngazi ya Wizara au kwenye ngazi ya Taasisi yetu ya Umma.

Mheshimiwa Spika, Taasisi nyingi kwa lugha ya kawaida hazikuweza kufika kwa wakati kwa sababu hazikuwa na cha kusema mbele ya Kamati. Kwa hiyo, wanakwambia tumeunda Kamati na ndiyo tumeanza. Unafuliza Wizara nzima, kuna Watumishi wangapi kwa hiyari yao wamesema wao wana virusi vyta UKIMWI, wanakwambia mmoja; wengine wanasema hakuna. Kwa hiyo, unaona kabisa kwamba kumbe jambo hili katika jamii linazoleka na linaonekana ni jambo la kawaida. Kama

linazoeleka na linakuwa jambo la kawaida madhara yake ni kwamba mapambano haya hatutafanikiwa. Kwa sababu hatuchukulii kama ni jambo hatari na linahatarisha maisha yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kutoa wito kama Mjumbe wa Kamati ya UKIMWI kwamba Wizara na Taasisi za Umma zote mahala pa kazi, zihakikishe kwamba suala la UKIMWI, linajadiliwa na wale wote ambao wanaohusika wapime na waweze kupata majibu kujua kwamba hali zao za afya zikoje? Baada ya kujua hali zao za afya, basi waanze kufuata hizo afua za UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo linatusumbua sana kwenye mapambano dhidi ya UKIMWI ni usiri. Usiri ndiyo unaoathiri sana katika mapambano dhidi ya UKIMWI. Usiri huu sasa hivi inaelekea umetengenezwa na Taasisi zinazotoa huduma za Afya. Zamani hapo ilikuwa kuwawekea wagonjwa wa UKIMWI mahali maalum pa kutibiwa, pa kuchukua dawa na Mganga Maalum, ilikuwa ni jambo linaloonekana ni jambo la faragha na jambo linalowasaidia wagonjwa wa UKIMWI. Leo, hali hiyo imebadilika imekuwa sasa huo ndiyo unyanyapaa wenyewe, kwamba mtu hayuko tayari kwenda kule kwenye kituo cha kutolea huduma za dawa na vipimo, *CTC*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishauri sana Serikali, hebu tuufute ule utaratibu wa *CTC*, wagonjwa wote sasa waende kwenye huduma ya kawaida; tukikaa kwenye mstari pale hospitalini, mimi mwenye virusi na mwingine asiye na virusi tukae pale tumwone Mganga huyo huyo, tutibiwe tuondoke. Tuache ile kwenda kuwaficha wagonjwa wa virusi mahali kwenye *CTC* na kuwapangia siku maalum, kwa sababu hiyo inasababisha sasa watu wengi zaidi; moja, waende hospitali za mbali sana kutafuta huduma, au vituo vya mbali sababu ya aibu, lakini pili, akikosa nauli ama uwezo wa kwenda huko mahali, matokeo yake anakuwa hawesi kwenda kupata zile dawa na anaacha kutumia dawa. kwa hiyo, nafikiri, tuondoe huo usiri na ugonjwa wa UKIMWI tuuone ni ugonjwa wa kawaida. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, hali za afua za UKIMWI zilipofikia sasa, zimefanya ugonjwa wa UKIMWI uonekane wa kawaida kabisa. Nampongeza sana Dkt. Maboko na Taasisi yake ya TACA/IDS wanajitahidi sana kufanya vizuri na wanatoa elimu vizuri, lakini kikubwa hali ya bajeti ya Taasisi hii iko chini sana. Kwa hiyo, hiyo nayo itakuwa ni kikwazo kwa maana ya mapambano dhidi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, suala la madawa ya kulevyta; Taasisi ya Kupambana na Madawa ya Kulevyta katika nchi yetu kwa kweli imefanya kazi kubwa sana, chini ya Dkt. Sianga. Tunatakiwa wote kama Watanzania tuwapongeze, lakini vile vile tuwaunge mkono. Hali tuliyokuwa tunaenda nayo kama nchi ilikuwa ni mbaya sana. Ilikuwa kila mahali unapokwenda, hukosi wanaoitwa mateja, lakini leo hii kumkuta teja ni kazi ngumu kidogo. Kwa hiyo, hii ni dalili kwamba Taasisi hii inafanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hii maana yake nini? Maana yake ni kwamba Taasisi ya Kupambana na Madawa ya Kulevyta peke yake, haiwezi. Sisi kama Watanzania, kama Wabunge ni lazima tuisaidie hii Taasisi. Serikali nayo iwekeze katika miundombinu ya kisasa ya kuhakikisha kwamba vifaa vya kisasa vya kupima na kutambua madawa ya kulevyta vinakuwepo ndani ya nchi na vinawenza kusaidia Taasisi hii, kuweza kufanya kazi vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwas Spika, jambo lingine ambalo ningeweza kuliungelea ni suala la elimu. Tunafahamu kabisa kwamba sasa tunatekeleza elimu bila malipo, lakini suala hili bado lina mkanganyiko mkubwa sana katika jamii yetu. Utakuta kwamba miundombinu mingi wananchi wamejenga; wamejenga madarasa, wamejenga mabweni kwa ajili ya wanafunzi, lakini hayana samani mle ndani. Linapokuwa suala la samani inakuwa ni shida sana. Naomba sana Serikali itoe muongozo vizuri. Nafahamu kabisa kwenye mwongozo uliotolewa mara ya mwisho juu ya elimu bila malipo ilieleza kabisa kwamba jukumu la miundombinu ni jukumu la wananchi, lakini inapofika mahali

fulani kuna mkanganyiko unatokea, baadhi ya sehemu hawatambui kwamba dawati ni sehemu ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, anapoambiwa mzazi achangie dawati, lakini hapo kunatoa ukinzani; wako Maafisa wa Serikali wanasema hapana, hatakiwi kuchangia. Unajiliza, mtoto anakwenda shulen, atakalia nini? Fedha ya dawati iko wapi? Kwa hiyo, naomba sana, hili litolewe ufanuzi mzuri ili kusudi tusiende kule tukakanyagana kati ya Watendaji na wananchi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la Ikama ya Walimu. Hali ya Walimu katika nchi yetu imekuwa mbaya sana. Shule nydingi hazina Walimu. Mimi nafikiri kupanga ni kuchagua. Kama tunaamini kabisa kwamba elimu ndiyo msingi wa kulifanya Taifa letu liwe bora. Naomba sana sasa Serikali ifanye maamuzi magumu kwamba ikamilishe Ikama ya Walimu. Inapokuwa inakamilisha Ikama ya Walimu kwenye shule zetu, vile vile iangalie, liko tatizo linajitokeza, Walimu wanastaafu, kwa sababu tunajua kabisa Mwalimu akistaafu maana yake atakuwa hayuko kwenye Utumishi, pale panakuwa na pengo.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri inafika mahali wanastaafu Walimu zaidi ya 30, hakuna hata Mwalimu mmoja anayeajiriwa katika Halmashauri ile. Mara ya mwisho tukaambiwa kwamba ikiwa walipatikana na vyeti bandia, walikuwa 15, basi Halmashauri hiyo inarejeshewa Walimu 15. Kwa uhakika kabisa katika Halmashauri yangu ya Njombe Mjini, hilo halikufanyika. Walitolewa Walimu kati ya 15 na 18 lakini walioletwa ni Walimu wanne, kitu ambacho nimejaribu kuulizia na kufuatilia imeonekana ni tatizo kabisa.

Mheshimiwa Spika, shida ya Walimu ni kubwa sana na ni shida ya nchi nzima. Kwa hiyo, naomba sana, tukamilishe idadi ya Walimu katika shule zetu, kwa sababu wananchi wanajenga miundombinu, wanajitahidi.

Mheshimiwa Spika, upande wa Sekondari hakuna shida kubwa sana, shida tu kwa Walimu wa Sayansi, hasa

Shule za Msingi kuna shida kubwa sana. Inafika mahali ambapo wananchi wanaambiwa jamani, sawa mmeleta watoto shulenii, liko Darasa la Awali, hili darasa sasa hatuna Mwalimu, tunajadiliana sisi kama wazazi tunafanyaje? Sasa kunatokea upinzani, wengine wanasema ni elimu bure, wengine wanasema tuchangie jamani watoto wasome, mazingira kama hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana ikama ya Walimu iangaliwe sana na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Edward Mwalongo, nakushukuru sana kwa mchango wako. Alipoanza hii shughuli Mheshimiwa Mwalongo, alikuwa mkali sana, kwamba haya mambo ya UKIMWI njombe haya, nikaone nimpeleke kwenye Kamati hiyo. Nashukuru sasa unayazungumzia tena vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Profesa nilishakutaja, Mheshimiwa Jumanne Maghembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Selasini.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, nitoe mchango wangu katika hoja ambazo ziko Mezani.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuzipongeza sana Kamati zote ambazo zimewasilisha ripoti zao leo asubuhi. Napongeza ushirikiano mkubwa ambao Serikali inaendelea kutupa katika kufanya kazi yetu ya Uwakilishi hapa Bungeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia mambo machache tu kwa sababu na muda wenyewe ni mfupi sana. La kwanza nianzie hapa alipoishia rafiki yangu Mbunge wa kutoka kule Njombe, ambaye amemaliza kuongea, kwamba katika Wilaya yangu kule Mwanga kuna upungufu mkubwa sana wa Walimu. Leo asubuhi Mwalimu Mkuu wa Shule ya Kijijiini kwangu kule Kirongaya,

ameniambia kuanzia Jumatatu ijayo kutakuwa na Walimu wawili tu katika Shule ya Msingi ya Kamwala ambayo ndiyo shule ya kijijini kwangu.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Mwanga Walimu watatu ndiyo wastani wa Walimu katika Shule za Msingi. Nimepiga kelele hapa kweli kweli, leo niongeze tena kelele hiyo. Nimemwandikia rafiki yangu Mheshimiwa George Mkuchika, Waziri wa Utumishi, nimemweleza Waziri wa Elimu, nimemweleza Waziri wa TAMISEMI. Sielewi ni kwa sababu gani tatizo hili halijaweza kutatuliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Walimu ambao wamepungua ni wale ambao wamestaifu; na kwa sababu hiyo mishahara yao ipo. Sasa inachukua je mwaka mzima kutatua tatizo dogo namna hiyo wakati Walimu mtaani wako wamejaa tele na shulenii Walimu watoto wako wenye hawana Walimu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naendelea kuihimiza Serikali iliangalie jambo hili kwa huruma kabisa ili watoto wasiendelee kupoteza maisha yao wakiwa shulenii wanacheza peke yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nimeliona huku kwenye mitandao yetu kama Wabunge, kuna mjadala unaendelea, Waheshimiwa Wabunge wanajadili kwamba labda tubadilishe lugha ya kufundisha katika ngazi ya sekondari na ngazi ya Chuo Kikuu, tufundishe kwa Kiswahili. Ukiangalia matokea ya Mtihani wa *Form IV* wa mwaka 2018 haya yaliyotoka wiki iliopita, utakuta tatizo kubwa kabisa katika shule zetu ni watoto kutojua Hesabu. Ukienda mbele, ukiangalia vizuri zaidi utakuta watoto wetu hohehahe kabisa katika Kiswahili chenyewe. Wanasesma niletee ugari na wari, akuna shida badala ya hakuna shida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, watoto wetu wana shida kabisa katika ufahamu wa Kiingereza, anasema *I will come yesterday*. Watoto wana tatizo kubwa kabisa, ukienda utakuta watoto wetu wana matatizo makubwa sana katika

sayansi; biolojia, fizikia na kemia. Sasa huko mbele Madaktari na Wachumi tutapata wapi? Kwa hiyo, tushughulikie tatizo lenyewe, tuwapeleke Walimu ambao wanafundisha masomo haya tuwajengee umahiri wa kufundisha masomo haya ya Hesabu, Kiswahili na Kiingereza sio kubadili lugha ya kufundishia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tuwapeleke Walimu tuwafundishe kwa sababu huko shulen i hawa watoto ambao wanasema *I will come yesterday* ndio wanapata *degree*, wanakwenda kufundisha *English* na wakiwa wanafundisha wanafundisha hiyo hiyo *I will come yesterday*. Kwa hiyo, tufanye juhud tuwafundishe Walimu wajengee umahiri katika masomo yao, ili tuweze kuacha Taifa ambalo litawenza kushindana katika uchumi wa dunia, litawenza kupambana katika masuala ya utafiti, litawenza kupambana katika kujenga nchi yetu, tusifanye mambo *cosmetic* yaani tusifanye vitu hivi kama vile mtu unaweka vipodozi mwilini, tusifanye mambo *cosmetic*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tufundishe Walimu vizuri ili wapate umahiri wa kufundisha Kiingereza, Hesabu na Kiswahili na watoto waanze kujua zile KKK (Kusoma, Kuandika, Kuhesabu); wajue *table* na wabebe hata vile vijiti vya kuhesabia ili wajenge kabisa umahiri katika hesabu. Hakuna Taifa ambalo linawenza kuendelea watu hawajui hesabu, wamefika *form fourwanajua* hesabu kwa asilimia 19, mambo magumu haya. Hili ni janga kabisa, kwa hiyo tulichukulie kwa nguvu inayotakiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda nirudie jambo ambalo nimelisema tena huko nyuma kwamba, watoto wanaokwenda kwenye vyuo vikuu wanahangaika sana na suala la mikopo. Katika mwezi huu uliopita wa Oktoba watoto wamefungua vyuo vikuu, nilikuwa kule Jimboni kwangu, nimeletewa watoto 15 ambao ni watoto yatima, wengine na mimi nafahamu ni watoto yatima, lakini hawakupewa mkopo. Sio kwamba lile baraza lina shida hapana, mikopo yenye haitoshi, kwa hiyo kuna watakaopata na wataokosa; wanafanya kila kitu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna siku moja nimekwenda pale, nimeongea na wale vijana wa Bodi ya Mikopo nimeona mazingira ambayo wanafanyia kazi. Serikali katika bajeti iliopita ilitoa shilingi bilioni 500, jamani shilingi bilioni 500 sio kidogo, ni pesa nyingi sana. Kwa hiyo, Serikali ina dhamira thabiti kabisa ya kusaidia watoto wapate mikopo. Sasa sisi ndio lazima tuwe wabunifu, Serikali ikishatupa shilingi bilioni 500 tuwe wabunifu. Tusifanye mambo *business as usual*, tuwe wabunifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumejata bilioni 500, tumewapa watoto hao tuliojata lakini pia mwaka kesho tutapewa tena labda bilioni 600 kwa sababu watoto wataongezeka, bilioni 700; hivi tunaweza, hatuwezi. Kwa hiyo, lazima tubadilishe gia, tuziambie benki zetu zitoe mikopo ili kila mwanafunzi wa chuo kikuu apate mkopo. Akishaingia chuo kikuu kama anataka mkopo apate mkopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali kazi yake kuangalia ile mikopo, benki zina...

**SPIKA:** Ahsante sana Profesa.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, ngoja nimalize kitu kimoja. Benki zinataka riba kiasi gani, Serikali ihangaike na riba na watoto wahangaike na mkopo wakati watakapomaliza shule zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango wako wa kiprofesa. Kazungumzia hesabu, ni kweli hesabu za shule ya msingi zinafundishwa kwa Kiswahili, ufaulu wa hesabu kwenye elimu ya msingi uko chini. Kwa hiyo, kama tatizo ni lugha kwa nini *primary* wanafeli hesabu? Hata hivyo, shule nyingi za sekondari kama zina Walimu wengi wa hesabu ni Mwalimu mmoja, zile zetu za Kata; *form one* mpaka *form four* mmoja au hakuna. Kwa hiyo, lazima ufaulu utakuwa chini sana. (*Makofi*)

Kongwa peke yake sina Walimu 1,000 wa shule ya msingi, lakini hatuwezi kuilaumu Serikali peke yake maana yake kule Kongwa kama wamemaliza 50 darasa la saba kwenye shule hiyo hiyo, wanaoandikishwa darasa la kwanza 200. Sasa kama wametoka 50 wameingia 200, Serikali ikishughulika na 200 ya mwaka huu, mwakani tunaingiza 300, shughuli ipo hapo.

Tunaendelea na Mheshimiwa Selasini, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Nkamia.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa niseme mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Utawala na TAMISEMI na kwa sababu hiyo naunga mkono taarifa ya Kamati yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, mimi niko hapa mbele ulizoea kumwona Mbewe pale na Lissu hapa na wengine, sasa nipo peke yangu hapa kwa muda mrefu, kweli naumia na hivi nichukue nafasi hii kuwapa pole wenzangu Lissu, Mbewe na Matiko na kuwaombea Mwenyezi Mungu kwamba mitihani inayowakabili, basi waipokee na Mwenyezi Mungu ajalie siku moja tuweze kuwa pamoja tena hapa na najua itakuwa hivyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichangie kwenye utawala bora na nitazungumza kuhusu sheria mbili ambazo naona ni muhimu katika kipindi cha sasa nizzungumze. Sheria ya kwanza ambayo ningependa nizungumze kidogo ni *The Regional Administration Act, 1997* ambayo ndio inawapa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa mamlaka ya kuweza kuwaweka kizuizini Watanzania kwa masaa 24 au 48.

Mheshimiwa Spika, kabla sijasema hayo kwa sababu mimi ni muhenga, nimekaa nimeona utawala tangu Awamu ya Kwanza mpaka sasa ni kwamba zamani kulikuwa na utaratibu mzuri wa kuwapata viongozi hawa; Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa. Zamani kulikuwa na *promotion* walikuwa *promoted* kutoka kwenye miongoni

mwa Makatibu Tarafa au Maafisa Ustawi wa Jamii na kadhalika. Sasa siku hizi wanapatikana namna gani sielewi, kwa sababu inavyoelekea wengi uzoefu wa kazi hiyo hawana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niseme kwa kweli Mzee Mkuchika Waziri amejitahidi sana kuwafunda na Katibu Mkuu TAMISEMI aliyestaafu Mzee lyombe naye alijitahidi sana kuwafunda, lakini mambo haya yanaendelea na nayasema kwa sababu ni mambo ambayo yanaweza yakaleta chuki mionganoni mwa jamii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sheria ile kifungu cha 7(2) na 15(2) pia vinaweka masharti ya namna viongozi hawa wanavyopaswa watumie ile sheria. Kwamba ili kumweka mtu ndani, Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa masharti manne lazima yazingatiwe. Jambo la kwanza, ni lazima kuwe na kosa la jinai; jambo la pili, kosa hilo lifanyike mbele ya kiongozi; jambo la tatu, kosa liwe linatishia na jambo la nne, kuwe hakuna njia nyingine yoyote ya kufanya zaidi ya kumweka ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wananchi, viongozi hata na wawekezaji wamekuwa wakikamatwa kwa chuki. Mfano mdogo sana Iringa, waliwekwa ndani Diwani mwanamama Celestina Johansen kwa kosa ambalo lilitanywa na halmashauri kwa kuagiza nyumba ya mkazi mmoja ikavunjwe, mama kwa sababu ni Diwani wa eneo lile Mkuu wa Mkoa akaamua awekwe ndani kwa kosa ambalo sio la kwakwe. Mkuu wa Mkoa huyu huyu juzi alimkamata mwekezaji mmoja kwa kutolipa Cess, lakini polisi walivyochunguza wakagundua kwamba yule mwekezaji hana kosa lakini ameshawekwa ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, huko Ukonga pia Diwani Nancy Disunte naye alikwishawekwa ndani. Hai ndio usiseme, ni kila kukicha Madiwani wanawekwa ndani, Arumeru Mheshimiwa Diwani Elisa Mungure, Mbozi Mheshimiwa Pascal Haonga. Juzi Mkuu wa Mkoa wa Mara alimweka ndani Diwani wa Kata ya Mwema kisa alikunja nne akiwa kwenye mukutano wake.

Mheshimiwa Spika, mambo haya sio mazuri na nayasema kwa dhati kabisa kwa sababu naipenda hii nchi. Kwa maana mambo haya yanaweka chuki mionganini mwa wale wanaowekwa ndani na tuisahau wale wana jamaa zao na chuki hii ikiendelea kuvimba itazaa kisasi, upendo kwenye jumuiya utakosekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali kwanza ifanye *vetting* ya kutosha kuhusu viongozi hawa, lakini pili iwape mafunzo ya kutosha kwa sababu haya wanayofanya mwisho wa siku ni Serikali inaaibika. Hii ni kwa sababu hawa wote na wengine sikupenda niwataje, wakienda mahakamani watashinda kesi zao.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema tangu mwanzo, utawala bora ni utawala wa sheria na sisi viongozi tunalumbana na mambo yallyo chini ya sheria. Kwa mfano jana tulisikia hapa juu ya upelelezi wa kesi ya Mheshimiwa Lissu, Waziri alisimama hapa akaeleza lakini Waheshimiwa viongozi humu ndani wana sheria mko wengi sana.

Mheshimiwa Spika, kuna ya *The Mutual Assistance in Criminal Matters Act* ambayo ina uwezo kabisa ikitumika wa kuchukua maelezo popote na hatua zikachukuliwa. Lissu hawezi kushindwa kufuatwa Nairobi, Ubelgiji au popote alipo kwa kutumia sheria hii ambayo tulitunga wenyewe hapa Bungeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa tukitoa matamko ambayo yanakinzana na hii sheria, watoto wetu wanakuja kusoma *Hansard*, watoto wetu wanakuja kufanya mitihani yao kwa kufanya *reference* ya haya tunayosema tunaonekana sijui ni Wabunge wa namna gani. Kwa hiyo, ombi langu kwa viongozi wa nchi yetu na Wabunge wote kwa pamoja tufuate sheria ambazo tunazitunga hapa itatusaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika...

**SPIKA:** Mheshimiwa Selasini japo unamlamu Waziri lakini kwa mfano dereva, kwa nini sheria hiyo ifuate si arudi tu aje atoe ushahidi?

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, wote hawa wawili wapo kwenye matibabu na wanaoweza kueleza kiwango cha namna milli yao imepokea matibabu ni Madaktari wao, lakini hii sheria Serikali, Wizara ya Mambo ya Ndani inaweza ikaitumia hata huyo dereva popote alipo akahojiwa.

**SPIKA:** Hao madaktari wameshaandika chochote kile kuleta huku?

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, lakini unaniwekea muda wangu eeh?

**SPIKA:** Muda wako nautunza kwa sababu...

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, ninachosema illi kuondoa hizi sintofahamu na kelele mionganoni mwa jamii sheria hii ifuatwe popote pale walipo na haki itatendeka tu.

**SPIKA:** Lakini pia Madaktari si waandike ripoti ije?

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, sawa...

**SPIKA:** Mtunzieni muda wake, endelea Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumza ni kuhusu uteuzi wa Wakurugenzi wetu. Zamani na nasema hili kwa sababu uliniweka kwenye LAAC katika kipindi chote cha Ubunge wangu kipindi kilichopita na tulipoanza Bunge hili uliniweka tena kwenye LAAC. Niligundua kwamba utaratibu uliokuwa unatumika ni kwamba Wakurugenzi walikuwa wanateuliwa mionganoni mwa Wakuu wa Idara ambao tena wametumikia idara zao kwa sio chini ya miaka saba na kwa sababu hiyo Wakurugenzi walikuwa wana uzoefu mkubwa sana katika kazi zao, walizielewa halmashauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uteuzi ambao unafanyika sasa hivi tumewapata Wakurugenzi ambao sio wazoefu na matokeo

yake imekuwa ni kama *trial and error*. Kwa mfano, Halmashauri ya Moshi (*Moshi DC*) miaka mitatu hii tayari imeshakuwa na Wakurugenzi watano na matokeo yake ni kwamba yaani ule utendaji unakuwa sio sawasawa na wengine ndio hawa tunaowasikia kwamba wanafanya kazi zao kibabe. Juzi tulisikia kwamba Mkurugenzi kapiga mtu risasi kanisani na mambo kama hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, eneo hili pia ningeliomba Serikali iwe makini katika kuangalia kwamba ni nani tunawateua...

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Selasini upokee taarifa, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhalli.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa kwa Mheshimiwa Joseph Roman Selasini kwamba tunachozungumzia mamlaka ya Rais ndio mwenye mamlaka ya kuteua hao, ni wateule wa Mheshimiwa Rais. Ni kweli kwamba anaweza akawa na mapendekezo na kama alivyosema ilikuwa ni mazoea ya huko nyuma. Hawezi kumlazimisha atue anaowataka yeye, kama kuna upungufu umetokea katika maeneo kadhaa, huo ni upungufu wa mtu mmoja mmoja lakini hatuwezi kuhoji mamlaka ya Rais kwamba apangiwe watu wa kuwateua. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Selasini pokea taarifa hiyo.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, kabla sijaipokea nimweleze yeye kama Waziri anajua kwamba moja kati ya kazi za Bunge hili ni kumshauri Rais na kitu ninachofanya hapa ni kushauri. Kama yeye ni Waziri wa namna hii ina maana hamsaidii Rais, ndio maana anaogopa kumshauri. Mimi sijasema kwamba Rais apoke ushauri wangu, lakini ninachosema mamlaka za uteuzi

zinazomsaidia Rais zihakikishe kwamba watu hawa wamekuwa *vetted* vizuri ili tupate watumishi wa kufaa katika kutumikia hii nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la mwisho ambalo ningependa kuzungumza naona nimepigiwa kengele...

**SPIKA:** Ooh kengele ya pili imeshalia. Ahsante sana Mheshimiwa Selasini. (*Makof*)

Nilikutaja Mheshimiwa Juma Nkamia na Mheshimiwa Charles Mwijage atafuatia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nichangie machache kwenye kamati hizi tatu. Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu *Subhanahu-wataala* kwa kutupa afya njema.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, niipongeze sana Serikali kwenye ujenzi wa vituo vya afya vinavyosimamiwa na TAMISEMI na Wizara ya Afya, wamefanya kazi kubwa sana. Mheshimiwa Rais kwa hili hata uchaguzi ujao kama ni 2020 au 2022 anatereza tu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri iliyofanywa ya ujenzi wa vituo vya afya, zipo kasoro ndogondogo kwenye maeneo yetu, zinaweza kurekebishwa. Rai yangu na ushauri wangu kwa Serikali ni kuandaa watumishi wa kutosha watakaofanya kazi kwenye vituo hivi vya afya. Leo tutajisifu tumetengeneza vituo vya afya vizuri, vifaa vitakavyowekwa kwenye vituo hivi ni vifaa vya kisasa, je, tumejijandaa vya kutosha kuwa na programu ya kupeleka watumishi huku? Hili ni jambo ambalo nadhani kwamba ipo haja sasa Wizara ya Afya, TAMISEMI na Utumishi kuanza kuchukua hatua za haraka kwa sababu *MSD* tayari wameshaanza maandalizi ya kununua vifaa, nani atakwenda kuvipokea kule na hao wataalam watakaopokea wana ujuzi huo? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la pili, nije kwenye elimu. Kwa mtazamo wangu mimi nafikiri tumepoteza *plot somewhere*. Elimu yetu ya sasa imekuwa ni ya biashara zaidi. Vyuo vikuu karibu vyote vinaandaa *extension officers* na tunawafundisha vijana kwa kuwafahamisha kabisa kwamba tunawaandaa kwa ajili ya ajira, ajira zenyewe hazipo.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri, leo pale Chemba wanafanya mahojiano ya kupata Watendaji wa Vijiji nafasi sita lakini walioomba ni 870, walioitwa 220. Juzi Chamwino hapa, walikuwa na nafasi nne za Watendaji wa Vijiji lakini walioomba walikuwa 1,500. Jeshini nimeona siku moja wameenda kwenye uwanja wa mpira wanagombea nafasi nane. Kwa hiyo, elimu yetu inawajenga watu kwa ajili ya ajira badala ya kujajiri. Nadhani tuangalie namna gani tunaweza kufanya kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye utawala bora, lakini naomba nizungumzie mwisho kwa sababu lina changamoto yake. Kwenye walimu, siamini kama kweli tuna matatizo makubwa ya walimu ila tuna tatizo la *reallocation* ya walimu. Mfano ni hapa Dodoma Mjini, kuna *excess* ya walimu 371 lakini shule za pembezoni huko Chemba, Kongwa, Mpwapwa zina matatizo ya walimu. Kwa hiyo, TAMISEMI wakae chini waangalie, hivi tatizo ni nini? Nadhani tatizo liko hapohapo TAMISEMI, wakae chini waangalie namna gani *reallocation* ya walimu ilivyo, walimu wanapelekwa lakini hawakai, wanarudi kwenye shule za mjini.

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kushauri ni kwenye michezo. Niombe sana Serikali lazima tuwe na programu ya walimu wa michezo. Kwenye mpira wa mguu Taifa hili ni kubwa sana, ni aibu sana kuwa na walimu wa mpira wa mguu *qualified* kutoka Burundi wanakuja kufundisha mpira wa mguu Tanzania. Ni aibu kwa sababu hatuna programu ya kuwa-*train* wachezaji wetu wanaostaafu mpira na wenye uelewa ili waje wafundishe vilabu vyetu, kutwa kucha timu zetu za Taifa hazitafanya vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, angalia hata ligi ya wanawake leo inachezwa nyumbani na ugenini. Timu imetoka Njombe inakwenda kucheza Mwanza hawana mahali hata pa kulala halafu mnasema waende *home and away* akina dada wale. Leo asubuhi Timu ya Majimaji ya Songea imekwama Dar es Salaam inashindwa kwenda Tanga, kocha wao anasema vijana wamekula jana, usiku hawajala tunategemea msaada ili tuweze kwenda Tanga, hatuwezi kuendesha mpira hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kakoso ananiambia Yanga imetoka Tanga ika-*drawikaja* Singida ika-*draw*, ndiyo matatizo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nkamia, siyo timu za akina dada peke yake zinazotembeza bakuli, zipo na timu zingine mnatembeza mabakuli tu. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli. Sikutaka kuitaja timu hiyo kwa sababu rafiki yangu Mheshimiwa Mwigulu yeye ni mfadhili wa timu zote mbili. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie suala la utawala bora. Utawala bora siyo uchaguzi na hili naomba niliseme kwa dhati sana na wewe juzi ultania hapa. Naomba niliseme kwa dhati sana utawala bora siyo uchaguzi kwamba tukifanya uchaguzi kila baada ya miaka miwili, mitatu ndiyo utawala bora, siamini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sina elimu ya kutisha sana lakini ni *philosopher* na sifanyi mambo bila kufanya utafiti. Nchi zote zilizoendelea duniani hazikuendelea kwa sababu ya kufanya uchaguzi kila baada ya miaka mitatu. Wajerumani wale leo ndiyo *the leading country* katika uchumi Ulaya, Angela Merkel yule mama pale amekaa miaka 16. Rwanda tunayoipigia mfano hapa ndani, tunasema inafanya vizuri sana kwenye uchumi, Kagame amekaa miaka mingapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo Lionel Messi huwezi kumuweka nje eti kwa sababu amecheza mechi kumi. Tupo kwenvye siasa za ushindani, ukiwa na mchezaji mzuri acha aende. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa sisi kama Taifa lazima tufanye maamuzi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nkamia, nakuongeza dakika tatu uhitimishe vizuri. (*Makofi*)

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Hata hao Wazungu tunaokimbilia kwao, tunakwenda kulalamika unajua hivi na hivi na wao pia wameendelea nchi zao kwa kufanya utafiti. Ukiniruhusu nipo tayari kuleta hoja yangu hapa ndani ya Bunge. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kuna watu hawapigi makofi lakini wanaipenda hii hoja. (*Makofi/Kicheko*)

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, mwongozo wako.

**SPIKA:** Ngoja kidogo Mheshimiwa Juma tusikie Mwongozo wa Spika hapa unatakiwa, Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, hapa Bungeni na Taifa letu kwa ujumla tunaendeshwa kwa mujibu wa Katiba. Katiba yetu imetuweka hapa kukaa vipindi vitano. Maneno anayoongea Mheshimiwa Nkamia ni *very dangerous* kwa Taifa letu kama hayatarudi kwa wananchi kama ambavyo tulionomba maoni ya wananchi wakati wa Katiba. Kwa hiyo, analielekeza Taifa...

**SPIKA:** Hebu rudia tena, umesema vipindi vingapi?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, vipindi vitano.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walishangilia)*

**MBUNGE FULANI:** Nzuri, nzuri, nzuri, vipindi vitano.

**MBUNGE FULANI:** Pepo lishindwe hilo.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, labda sijakuelewa swali lako, nimesema tunakaa miaka mitano, ndiyo mkataba tulionao.

**MBUNGE FULANI:** Kaa chini.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Sasa maneno anayoyazungumza haya ni mambo ambayo katika nchi mbalimbali Afrika yameleta migogoro sana kwa sababu haya mambo lazima turudi kwa wananchi waliotuleta hapa. Hii ni tamaa ya uongozi, tunatakiwa turudi kwa wananchi kwanza kwa sababu haya mambo yanahatarisha amani.

**MBUNGE FULANI:** Tutarudi usiogope.

**SPIKA:** Lakini unayemtuhumu hajasema hoja yake, ile anataka kusema wewe umeshawahi tayari, hajasema.  
*(Makofifi)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, amesema.

**SPIKA:** Kwa hiyo, kaa kwanza ili aseme, Mheshimiwa Nkamia tumekutunzia muda wako.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mchungaji Msigwa anapenda huyo, hana lolote.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, mmoja kati ya watu ninaowaheshimu sana ni Mheshimiwa Mchungaji na mmoja kati ya watu wanaonisumbua sana nilete ile hoja ya miaka saba ndani ya Bunge ni pamoja na yeze. Katika kudhihirisha hilo, hata yeze mwenyewe amekosea amesema nchi yetu inaongozwa kwa vipindi vitatu wakati siyo kweli. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba unilindie muda wangu, nilichokuwa nataka kusema ni kwamba sisi kama Taifa hata tukifanya *amendment* ya Katiba si tunakwenda kwa wananchi. Leo Baba Mtakatifu yuko Uarabuni, anafanya *study* Uarabuni kwamba hii hali ya dunia inavyokwenda sasa ikoje? Wakatoliki wengi wanahama sasa kwenda kwenye Ulokole, lazima tutafute njia nyngine ya kujua kwa nini wanahama.

Mheshimiwa Spika, mimi hoja yangu haina maana kwamba Rais Dkt. Magufuli aendelee miaka saba, hoja yangu ilikuwa na maana ukomo wa Bunge ambaye Rais ni sehemu ya Bunge. Kwa hiyo, hata waandishi wengi na ninyi wengine mliokuwa mnalalamika hapa ndani baadhi yenu, hakuna mahali nilikotaja Rais Dkt. Magufuli akae miaka saba ila ukomo wa Bunge uwe miaka saba.

**MBUNGE FULANI:** Rais ni sehemu ya Bunge.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mchungaji Msigwa hiyo ndiyo anaipenda sana. Nikuhakikishie hoja hii ukiiruhusu ikaja hapa ndani ya Bunge...

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, taarifa

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Zipigwe kura za siri (*anonymous*)...

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Hata dakika mbili hapa kila mmoja ataomba karatasi. Naomba mniruhusu nilete.

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapa kwa leo, nimalizie kwa kusema nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazozifanya

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Na Serikali ya Chama cha Mapinduzi na Mawaziri chapeni kazi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Bahati mbaya mzungumzaji ameshamaliza Mheshimiwa Mbilinyi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Anatumia Bunge kufanya vitu vya...

**SPIKA:** Upo kwenye orodha yangu utachangia baadaye utaweka hayo maneno unayotaka lakini kwa sasa hivi vumilia kidogo.

#### KUHUSU UTARATIBU

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia, utaratibu upi?

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, kumekuwa kuna utaratibu, tunafahamu mchangiaji anapochangia hapa Bungeni anawasha *microphone* anachangia. Mheshimiwa Musukuma amekuwa na utaratibu wa kuwasha *microphone* na kusema maneno bila Kiti kumkemea na umekuwa ni utamaduni wake mara kwa mara na siyo utaratibu kwa mujibu wa Kanuni. (*Makofii*)

**SPIKA:** Nakushukuru kutukumbusha. Mheshimiwa Charles Mwijage nilikutaja atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Salim Maalim (*CUF*).

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia taarifa za Kamati hizi tatu na nianze kwa kuwapongeza Wajumbe wa Kamati zote tatu na Wenye viti wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuanza na suala la UKIMWI. Suala hili siyo siri. UKIMWI ulipoingia nchini kwetu miaka ya 80 ungeweza kumgundua mgonjwa wa UKIMWI kwa kumuangalia kwenye macho hivi kwamba huyu tayari, walikuwa wanasema kupandisha kenchi, unamwona mtu mabega yamepanda juu lakini kutokana na kuwepo kwa dawa za kufubaza leo ni vigumu kuweza kumgundua mgonjwa kwa macho. Mtu unamuona anakwenda anadunda kawaida amejaza vizuri lakini kumbe anaumwa, ni kwa sababu ya vile vidonge anavyokula. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, linalonituma kuzungumza suala hili ni utaratibu wa Taifa letu kutegemea wahisani katika kusaidia wagonjwa kwa asilimia 95. Hoja yangu hapa ni kwamba sasa inabidi tuijangalie. Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati, idadi ya watu hawa ni wengi na hawakutaka wenyewe, inabidi Taifa tujifikirie tutafute vyanzo. Wakati mwenzako anapokubeba Waswahili wanasema muangalie kisogo au ujikaze mwenyewe. Kuna hatari hawa watu wakaja kutukwamisha kwa kutukamatia kwenye ugonjwa huu. Napendekeza na Wabunge iwapendeze tuanze *ku-allocate* pesa nyingi zaidi kwenye tatizo hili ambalo tunalo. Ninalo hilo dogo, imebidi nilichangie. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitachangia kidogo kwenye michezo. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii ambaye amemaliza kuchangia, Mheshimiwa Nkamia, alikuwa anataka kujifanya eti ni wakala ananitafutia mimi timu za kwenda kukimbia, hapana. Hizi mbio za juzi nilikuwa na-*test* mitambo, mimi siyo mwanariadha. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo ambalo nataka kuungana naye ni kwenye dhana ya utawala bora, naazima msemo wa Rais wa Uganda, Mheshimiwa Kaguta Museveni, walipomuliza kwa nini Museveni uko madarakani, akasema

ni vitu viwili; *prosperity* na *security*. Kwa hiyo, kwa nini mtu anaweza akawa anatamani kukaa miaka saba, labda anataka kujenga shule kila kijiji. Ilikupendeza mkwe wangu, Mheshimiwa Nkamia, kama una malengo mahsus kama huyu Rais wa Uganda ambaye anatafuta *prosperity* na *security* kwenye nchi yake, basi na iwe hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nianzime maneno ya Mheshimiwa Serukamba, juzi Mheshimiwa Museveni alikuwa anapokea kiwanda kinachozalisha lita 100,000 za maziwa akawa anamkabidhi mwewewe, akasema mimi tangia mwaka 1966 nachukia umaskini akawa anaonesha hiyo. Kwa taarifa Uganda inachakata maziwa lita milioni mbili kwa siku wakati sisi tunachakata lita 150,000 lakini nilipokuwa kule waliniambia tuna fursa ya kuchakata lita milioni 4. Nimeshazungumza na Waziri anayehusika na sisi tunakwenda huko, msiwe na wasiwasi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nizungumze suala la elimu. Tumefungua neema ya elimu ambayo imekuja na changamoto. Mimi kwetu huko kwa kipindi cha miaka mitatu nimeanzisha shule mpya za msingi tano, nimshukuru Waziri wa Elimu alinisaidia *kuzi-fast track* na kusajiliwa. Changamoto niliyoiona, jengo la vyumba vinne walijitokeza watoto 300 kuanza shule.

Mheshimiwa Spika, nachotaka kuliambia Bunge na Serikali ni kwamba tunapaswa tuijandae, Mwenyezi Mungu ametujalia kupata uzao sasa hao watoto wetu wasiwe bora wingi wa watu ila watu walioandaliwa vizuri. Zitafutwe rasilimali, watafutwe walimu ili waende kufundisha huko. Mimi nakwenda zaidi kwamba ikishindikana kuwaweka kwenye majengo bora hata tutengeneze maturubali ili mradi tuwe na walimu wawafundishe wale watoto kwa sababu mtoto aliyefika umri wa kwenda shule hawezikusubiri.

Mheshimiwa Spika, Muadhama *Cardinal* Laurean Rugambwa alikoanza darasa la kwanza kule kwetu Busita alikuwa kwenye nyumba ya nyasi, *it was a shelter* ya nyasi, lakini akasoma kwenye jengo lille na akaishia kuwa Kadinali

wa kwanza Muafrika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Elimu wale Wadhibiti Ubora wadhibiti lakini wakikuta watoto wanasoma chini ya miti waruhusu wasome hata kwenye nyumba ya nyasi mpaka siku hiyo tutakapoweza kuwapatia jengo wanalohitaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine kwenye elimu, naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tukubaliane, mtoto ni wa kila mtu, kama ambavyo Mama Kikwete huwa anasema kwamba mtoto wa mwenzio ni mwanaao. Sasa huyu mzee aliyejukua na elimu bure tusichukue watoto wetu tukamuachia, yeye alikuja na dhana nzuri kwamba elimu bure sasa tusimrushie mzigo, jukumu liwe la kwetu sisi.

Mheshimiwa Spika, unakwenda kwenye maeneo mengine watu wanajenga shule, unakuta mzazi ambaye mwanaye amekosa chumba cha darasa, hakuna mbaao anataka kukuuzia mbaao. Sasa sisi Wabunge tuisaidie Serikali, tupige propaganda, tuwahimize mtu awe tayari kutoa, aone kutoa mawe ni fahari, kushirikia kujenga ni fahari kwa sababu Mwenyezi Mungu ametusaidia ametupatia huu uzao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nichangie kidogo suala la afya. Nimesikia Mheshimiwa Kapteni Mkuchika juu ya wataalam, nazijua taarifa nzuri za TAMISEMI wanapo jenga majengo. Tunapofanya *rationing* ya majengo tuangalie ni wapi tunasubiria kupeleka wataalam na wapi tunasubiria kupeleka kituo kipyta.

Mheshimiwa Spika, nikukaribishe siku moja uende kwetu Goziba, mimi nikiwa nchi kavu kwetu kwenda Ziwanji Goziba nakwenda saa nane, sasa mtu anapokuwa Dodoma anafanya uamuzi wa wapi apelike wataalam, kituo changu ambacho *drifting* kwenye maji ni saa nane unasema tunasubiri, unakuwa hufikirii kwa kuwaangalia wale wenye tatizo. Ninayo zahanati kwetu Rutoro, ni kilometra 70 kutoka kwetu nilipozaliwa, wale watu wanakwenda kilometra 72 kwenda kwenye Jimbo la Mheshimiwa Rweikiza, unapokaa Dodoma, TAMISEMI,

Utumishi wa Umma unasubiri kuja ku-*allocate* ina maana tunakuwa hatuangalii uhalsia. (*Makofi*)

Niombe TAMISEMI, Wizara ya Afya, mnapofikiria mnifikirie mimi, nahitaji wataalam Goziba kwa sababu watu wanakufa maji kila siku kule, hawawezi kupata huduma na kuna baradi kali. Keleba hakuna wataalam, tumeshajenga maboma, kwa miaka mitatu nimemaliza maboma tisa, Serikali na mimi mniunge mkono na wananchi wangu, tuna maboma tisa tayari yanahitaji kumaliziwa na yote yapo kwenye *critical points* ambazo haziwezi kufikiwa bila kutembea kilometa ndefu. Nililitaka nzungumze hilo la afya.

Mheshimiwa Spika, nzungumze na watu wa Utumishi kwamba kuna jambo unaweza kusubiri. Unaweza kusubiri kwenda shule lakini huwezi kusubiri kwenda kupata tiba. Kama tuna upungufu wa wataalam kwa mujibu takwimu tujinyime tuweze kuwaajiri watu, mgonjwa hawezi kusubiri. Utakaa uwe mjinga usijue kusoma na kuandika, sawa, utasoma ukiwa mtu mzima miaka 20 ndiyo uko darasa la kwanza unasoma 'a, e, i, o, u', hata usipojua kusoma basi utaangalia wenzako wanakwenda lakini mtu anayeumwa hawezi kusubiri. Maana yangu ni nini? Naiomba Serikali yangu sikivu m jitahidi tupeleke watu wa afya kwa sababu wagonjwa hawawezi kusubiri lakini watu wenye nguvu ndiyo wanaweza kuchangia uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja zote. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Charles Mwijage. Niliona kibonzo kimoja juzi kinasema ulipoondoka zile mbio walikuona unapishana na basi la Shabiby Kibaigwa kule. Tumekukubali kwamba wewe ni bingwa wetu wa mbio, hongera sana. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Hamad Salim Maalim, upande wa CUF mtapewa dakika tano tano kwa sababu mko watatu atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanne Mcemba.

**MHE. HAMAD SALIM MAALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kupata nafasi hii. Kwanza, naomba ni-declare interest kwamba ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na asilimia kumi ya wanawake, vijana na walemauvu. Kwa kweli Halmashauri au Mikoa yetu mingi sana kwenye asilimia kumi hii ya wanawake na vijana inaonesha kwamba hela hii inatiwa mifukoni. Naomba nitoe mfano hai wa kitabu hiki cha Mkoa wa Manyara kwa bajeti ya 2016/2017. Mkoa wa Manyara asilimia kumi ya bajeti ya 2016/2017 ilitenga Sh.1,552,261,255 lakini kati ya hizo zilizotolewa kwa vikundi ni shilingi milioni 511.3 sawa na asilimia 33.

Mheshimiwa Spika, nasema pesa hizi zinaingizwa mifuko kwa sababu ukipitia kitabu chote hiki hukuti popote hiyo Sh.1,040,000,000 ambazo hazikutumiwa zillipoelezwa kwamba zimetumiwa kwa shughuli fulani. Ukiwaauliza wao wenyewe wanapokuja na randama zao hizi wanasema kwamba zilizobakia zimetumiwa lakini unapopitia kitabu chote hiki hakuna eneo lolote linaloeleza kwamba hii shilingi bilioni moja iliyobakia imetumiwa ama katika ujenzi wa madarasa au katika ununuzi wa meza na viti au vitu vingine. Inasemekana kwamba hela hii inaingia kwenye mifuko ya wahusika. Naomba Halmashauri/TAMISEMI ifuatilie kwa kina suala hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ajenda yangu nyingine ni Mfuko wa Rais wa Kujitegemea. Mfuko huu tunajua kwamba umeanzishwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anachaguliwa na pande mbili za Muungano (Zanzibar na Tanzania Bara) na safari iliyopita najua Zanzibar alipata kura zaidi ya laki tatu, inawezekana hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa Mfuko huu wa Kujitegemea hadi leo unatumika upande mmoja tu wa Muungano. Ushauri wangu, ama mfuko huu ubadilishwe jina uwe ni Mfuko wa Rais wa Tanzania Bara au kama ni Mfuko wa Rais wa Kujitegemea kwa sababu Rais ni wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania Mfuko huu pia ufile Zanzibar kwa kusaidia Wazanzibar walioko kule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kipengele kingine ni suala zima la...

**SPIKA:** Mheshimiwa, hakuna Rais wa Tanzania Bara.

**MHE. HAMAD SALIM MAALIM:** Mheshimiwa Spika, sawa hakuna Rais wa Tanzania, sasa kama ni hivyo mfuko utumike pande mbili ijulikane kwamba ni Rais wa Jamhuri ya Muungano usitumike upande mmoja, ndiyo tunachodai.

Mheshimiwa Spika, kipengele kingine ni upande wa TASAF kwenye kunusuru kaya maskini. Naomba niseme kwamba suala hili kwa kweli kwa Zanzibar limepiga hatua kubwa sana. Wenzetu wa upande wa Bara kwa kiasi fulani tunapotembelea miradi tuki-*compare* wa kule na huku kwa kweli wenzetu wamepiga hatu kubwa sana. Katika kipindi kifupi tu kilichopita kwenye malipo ya Oktoba na Desemba imeonyesha kuna tofauti ya malipo yale waliyokuwa wakilipwa mwezi Oktoba na mwezi wa Desemba. Kwa hivyo, nitawaomba wahusika...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana, dakika tano zimeisha.

**MHE. HAMAD SALIM MAALIM:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalize tu kidogo, naomba dakika moja.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kuna wahusika ambao Oktoba walilipwa Sh.60,000 Iakini Desemba wakalipwa Sh.36,000; mwagine akalipwa Sh44,000 mwezi Desemba akalipwa Sh.32,000 bila kupewa taarifa kwamba makato haya yanatoka wapi. Naomba suala hili lifuatiliwe ili tupate ufumbuzi wa kujua watu wetu wanakatwa pesa hii kwa misingi gani?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamad Salim Maalim. Nilikwishakutaja Mheshimiwa Mwanne Mcemba utafuatiwa na Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nichangie japo machache kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati hii, pia Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii. Nimpongeze Mheshimiwa Mwenyekiti wangu kwa uwasilisho wake mzuri na pia kuipokea hii taarifa kwamba ni sahihi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utaanza na shukrani kwa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano kwa kazi nzuri anayoifanya ya utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya CCM. Ndani ya miaka mitatu ameweza kufanya mambo ya ajabu mengi sana, sina sababu ya kuyataja, lakini mionganoni mwa miradi hiyo ambayo anaifanya na sisi kama Kamati tumeona ina mafanikio ni suala la afya. Suala hili lilikuwa nyuma sana lakini Awamu ya Tano imepeleka pesa kwenye Wizara ya Afya au TAMISEMI kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali za Mikoa, Vituo vya Afya, pia Hospitali za Wilaya. Mpaka sasa kitu ambacho tumethibitisha Hospitali za Wilaya 67 na Vituo vya Afya 350 vimeshapelekewa pesa. Kwa hiyo, hayo ni mafanikio makubwa sana ambayo tumeyaona baada ya ziara zetu. Si hilo tu bali kuna ongezeko kubwa la madawa, Mheshimiwa Rais wetu ameweza kuongeza bajeti ya madawa na mafanikio yake yanaonekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hata upande wa elimu, kwa ziara tulizotembelea sekta ya elimu kwa kweli kazi kubwa imefanyika. Nimpongeze sana Mheshimiwa Jafo amesimamia miradi yote pamoja na Naibu Mawaziri wake wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, mambo haya yanaleta heshima kwa Serikali yetu, upo upungufu mdogo unaohitaji maboresho. Tuiombe Serikali itusaidie kwa mwaka wa fedha 2019/2020 bajeti iongezeke *TASAF*, Awamu ya III. Fedha

inayotolewa na Serikali ni kiasi kidogo sana, wafadhili ndiyo wanaochangia kwa kiasi kikubwa, iwapo wale wafadhili watajiondoa ina maana *TASAF* itakufa. Kazi wanayofanya *TASAF* Awamu ya III ni nzuri sana kama itaendelezwa kwa kupatiwa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni MKURABITA. Kwenye ziara za Mikoa yote tuliokwenda MKURABITA imefanya kazi nzuri sana lakini wanachopungukiwa ni fedha kwani inayopelekwa ni kidogo sana. Kama MKURABITA itapewa fedha ya kutosha katika bajeti ina maana kazi itakayofanyika itawafafikia wananchi wote kwa sababu sasa hivi tayari wananchi wameshaelewa maana ya hatimiliki za kimila na kazi inafanyika vizuri, hata kwako Kongwa tuliwahi kupita na kuhakikisha kwamba Wagogo wote sasa wameshaelewa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, suala ligine ni *TARURA*. *TARURA* inafanya kazi nzuri sana kwenye maeneo yote ya Halmashauri lakini tatizo ni fedha, mahitaji ni mengi lakini fedha haitoshi. Kazi ya *TARURA* ni kufungua barabara za Wilaya, Vijiji na Mikoa hatimaye kuwa pamoja lakini hakuna fedha za kutosha.

Mheshimiwa Spika, niipongeze sana TAKUKURU kwa kazi nzuri inayoifanya. Sasa hivi heshima imerudi Wizara ya Afya, elimu na maofisini hakuna rushwa imepungua. Watu wanachukua rushwa lakini kwa uwoga, rushwa imepungua. Tatizo lao ni fedha ndogo wanayopewa, kwa hiyo, hawawezi kufika maeneo mengi kadri inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kulichangia, Mjumbe mwenzangu wa Kamati aliymaliza kuzungumza sasa hivi amesema kuhusu asilimia kumi ya Halmashauri. Kazi kubwa imefanyika katika Awamu ya Tano kuhusiana na asilimia hii kumi. Kwa nini nasema hivyo? Sisi wenyewe Wabunge humu ndani ni Wajumbe wa Halmashauri zetu, hizi bajeti zinapita kwetu. Sasa kama zinapita kwetu kwa nini tusizue bajeti zao wakati wa Mabaraza ya kupitisha bajeti ya kila mwaka? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tutailaumu Serikali kwamba asilimia kumi watendaji wanachukua si kweli kabisa, udhaifu upo lakini na sisi kama Wabunge tunachangia kwa sababu ni Wajumbe wa Mabaraza, hususani wanawake wenzangu, Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum ni Wajumbe wa Mabaraza tupiganie tuhakikishe hii haki ambayo ni wanawake, vijana na walemavu bajeti zisipite pamoja na Wabunge wa Majimbo mtusaidie ninyi ni Wajumbe wa Kamati ya Fedha. Kama ni Wajumbe wa Kamati ya Fedha kwa nini msitambue kwamba asilimia kumi ni muhimu sana kwa maendeleo ya wanawake, vijana na walemavu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais...

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, taarifa huku.

**SPIKA:** Naomba tuvumiliane tu aongee, maana hata wanaotoa taarifa siwaoni.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, kushoto kwako.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuamua kutoa vitambulisho kwa wajasiriamali. Naomba kweli kabisa Waheshimiwa Wabunge tupambane kwani asilimia kubwa ni wanawake na ndiyo wanaopambana Mheshimiwa Rais ametuokoa. Kwa hiyo, niombe Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wawatambue wajasiriamali kwa sababu kutokutoa vitambulisho hivyo ni kumvunja moyo Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, niombe Wabunge tuchangie jinsi gani ya kusimamia kuhakikisha wajasiriamali wanapata huduma kama ilivyotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda unaniruhusu niombe, nimeona Serikali sasa hivi ina mabadiliko ya kuondoa Idara zingine TAMISEMI, kwa mfano, Serikali sasa hivi imeondoa masuala ya maji TAMISEMI, inategemea pia

kuondoa Idara ya Kilimo, kwa nini nasema kilimo ibaki TAMISEMI? Wananchi wote wako TAMISEMI na TAMISEMI ni kwenye *grassroot*, sasa unapomwondoa huyo Mkuu wa Idara aende Wizarani watu ambao anatakiwa kuwaongoza, kwa mfano Mkuu wa Mkoa wangu alitoa agizo kwamba Wakuu wote wa Idara wa Ugani hakuna kwenda likizo mwezi Novemba kwa sababu ya mvua na kilimo, alisema wote watakaokwenda atawasukuma ndani.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho ningeomba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana, malizia hiyo sentensi.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, yote yaliyoandikwa na maoni yao yachukuliwe. Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanne Mcchemba tunashukuru sana kwa mchango wako. Nilikuwa nimekutaja Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa Msongozi.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia katika hoja hizi muhimu kimsingi ndiyo ambazo zinaleta maendeleo katika jamii zetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba kuna mtaalam mmoja ambaye alikuwa Rais wa Chuo Kikuu cha Harvard, alisema hivi: "*if education is expensive, try ignorance*". Huyu siyo mwingine bali Derek Bok.

Mheshimiwa Spika, tuko hapa kwa sababu ya elimu, kama elimu yetu ni mbovu hatutapata wataalam na vyovoyote vile hatutakuwa na maendeleo. Nimesikia kilio cha watu wengi na mimi siku zote nasema elimu ni mwalimu.

Tumeshuhudia jinsi gani tumekuwa na upungufu wa walimu hususani walimu wa sayansi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, utakubaliana nami kwamba bila sayansi hatuwezi kwenda kwenye uchumi wa viwanda. Pamoja na kwamba tuna upungufu mkubwa wa walimu tukawa na lile zoezi la kupunguza walimu wa sekondari hasa wa masomo ya sanaa kwenda kwenye shule za msingi, nakubaliana nao kwamba elimu ya msingi ndiyo msingi kama pale hakuna mwalimu kabisa itakuwa matatizo lakini zoezi lile liligubikwa na matatizo makubwa na wengine wakarudishwa tena kwenye sekondari kutokana labda na fedha au sielewi ilikuwa nini?

Mheshimiwa Spika, nachotaka kuzungumza na hata ukiangalia *Goal* Na.4 la *Sustainable Development* linalozungumzia elimu bora, sawa na shirikishi kwa wote, unaona wazi kwamba lengo hili litakuwa vigumu sana Tanzania kulifikia kwa sababu ya tatizo kubwa la walimu, vilevile mazingira ya kufundishia. Hili linajionyesha kwa matokeo ya mitihani tuliyoyapata juzi.

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba Tanzania tuna shule za vipaji maalum, shule za kata na shule za binafsi. Nitoe tu *analysis* kidogo kwa *sample* ya shule tatu, tatu; shule za Serikali kwa maana ya shule za kata na shule za binafsi. Wewe mwenyewe unajua kwamba wanaopata *division four* na *division zero* siyo rahisi kabisa kuendelea na elimu inayofuata.

Mheshimiwa Spika, nimechukua shule za tatu za binafsi ambazo zina jumla ya wanafunzi 236. Katika hizi shule tatu za binafsi waliopata *division one* ni 223 sawa na asilimia 95; waliopata *division two* ni 12 sawa na asilimia tano na waliopata *division three* ni mmoja sawa na asilimia 0.6, kwa hiyo, ukiangalia hawa wote wataendelea. Ukija kwenye shule za kata kwa hiyo *sample* niliyochukua, katika shule tatu zenye jumla ya wanafunzi 368 waliopata *division zero* na *four* ni 297, sawa na asilimia 80 na waliopata *division one* mpaka

*three* ni wanafunzi 79 sawa na asilimia 20. Kwa hiyo, unakuta kwamba kundi hili linakuwa ni la wasindikizaji.

Mheshimiwa Spika, niishauri Serikali nini cha kufanya. Ni kweli elimu bure imekuja na changamoto nydingi, wanafunzi wamekuwa wengi lakini sasa nini cha kufanya kwa sababu hatuwezi kuacha hali hii iendelee. Naishauri Serikali iendelee kuboresha miuondombinu kwa sababu unakuta shule hizo hizo za kata za Serikali ndiyo hizo hizi hazina walimu wa kutosha lakini kuna suala la chakula watoto hawa nao hawapati chakula shulenii. Kwa hiyo, unakuta nyumbani anatoka kwenye familia maskini hana chakula, anafika shule nako hamna chakula, ukilinganisha na wale wa binafsi unakuta tofauti ni kubwa sana. Kwa hiyo, naomba sana kwa *sample* hii na Mheshimiwa Waziri anajua tuone ni jinsi gani ya kuwasaidia watoto hawa wanaosoma kwenye shule za kata kwa sababu nao wanastahilli kupata elimu kama wanayopata wengine. Hilo la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini ukija hata kwenye shule zile ambazo tunaziita *special schools*, unakuta kwamba shule ya kwanza ya *special school*/lboru imekuja shule ya 36. Zile nydingine za Tabora na kadhalika unakuta ziko kati ya hizo 100 bora wala haziko kwenye 50 bora. Kwa hiyo, nadhani kuna haja pia kama hizi ni *special schools* na tunaamini wanaokwenda kule ni wale waliofaulu vizuri sana darasa la saba basi wawekewe mazingira ambayo kweli yanafanya wawe *special* kuliko wale wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nirudie tena kusema kwamba kwa kuwa elimu ni mwalimu naomba maslahi ya walimu yaboreshwe, wapandishwe madaraja, wapate mishahara yao kwa wakati lakini na yale maslahi yao mengine pia wayapate. Kama ambavyo amesema Mheshimiwa Mwijage unaweza ukasomea chini ya mti au kwenye nyasi lakini kama una mwalimu bora, mwalimu mahiri utafaulu tu kuliko kusoma kwenye shule zenyе AC lakini hakuna walimu au walimu waliopo hawafai. Kwa hiyo, naomba muwekeze zaidi kwa walimu ili tuweze kuboresha elimu yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la Bodi ya Mikopo. Ni kweli kwamba Bodi ya Mikopo imeendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wengi zaidi lakini bado kuna tatizo kubwa la urejeshwaji. Pamoja na urejeshwaji naomba sana Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla inisikilize, kuna wanafunzi waliokuwa wanasoma kwenye vyuo ambavyo *TCU* iliwaondoa, wamepelekwa kwenye vyuo vingine, mpaka leo napozungumza hawajapata mikopo yao. Kuna waliokwenda *SAUT* zaidi ya wanafunzi 100 hawajapata kabisa na hawa ni wanafunzi ambaa wanasomea ualimu. Pamoja na vyuo vingine lakini hiyo *particularly* nina majina ya wanafunzi, naomba sana Serikali ifuatilie ili wanafunzi hawa wapate mikopo yao. Haiwezekani kwa miezi minne, mitano kuanzia Novemba walipohamishwa mpaka leo hawajapata *single cent* na hawa wanastahili mikopo yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka kuoanisha suala la walimu wa sayansi na *COSTECH*. Nakumbuka kwamba tulikubaliana ndani ya Bunge hili au kwa sheria, sikumbuki vizuri lakini ilikuwa 1% ya *GDP* iende *COSTECH* ili kusaidia uvumbuzi na watoto wetu wanaosoma masomo ya sayansi. Cha ajabu hela hiyo haiendi na hata kile chanzo kingine walichokuwa wanakitegemea wamekuja kwenye Kamati wamesema nacho kimeondolewa. Kwa hiyo, leo tunapozungumza hata watoto wakiwa wabunifu namna gani kama *COSTECH* haina fedha maana yake tutakuwa tunacheza danadana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Profesa Maghembe alivyosema kwamba hisabati ni jambo la muhimu sana. Ndiyo sababu wanafunzi wanaosoma sayansi wakimaliza *form six* amepata labda 'A' zote inakuwa rahisi kwenda vyuo vikuu kusoma masomo yoyote hata ya *Arts*. Tuli-test Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1998, waliosoma *PCM* wakaja kusoma *Law* na wakafaulu vizuri sana lakini huwezi mtu wa *Arts* au tunaita *Nguin* ukasome sayansi, haiwezekani. Kwa hiyo, ni vyema tukawekeza kwenye sayansi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, inasikitisha, hili ni jambo la ajabu sana, tumeambiwa kwamba Bodi ya Mikopo asilimia 66 ya wanafunzi hawa ni *Nguin per-se*. Kwa hiyo, kama hiyo asilimia nyingine 30 inakwenda kwa wale *accountant* na mainjinia au *natural sciences then tuna tatizo kubwa sana kwamba ni asilimia 30 tu na hiyo 30 sasa labda natural science inaweza ikawa asilimia 10 au 15 halafu tunategemea tutakuwa na Taifa la viwanda, haiwezekani. Nadhani ni muhimu sana kuwekeza kwa walimu wa sayansi. Hili ni tatizo kubwa kwa sababu hatujawekeza kwenye walimu wa sayansi lakini pia hatuna hata vitendeakazi. (*Makofi*)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Sera ya Elimu inazungumzia masuala ya vitendeakazi, jambo la ajabu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, mimi ni dakika 10, hazijakwisha bado.

**SPIKA:** Hiyo ni kengele ya pili, malizia tu hiyo.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, jambo linaloshangaza, sasa hivi vitendeakazi (*teaching aids*) walimu wamekuwa wagunduzi kweli kweli, wanatumia miili yao kufundishia wanafunzi. Mimi nimeshangaa na hii itasababisha matatizo huko baadaye kwa sababu Mwalimu anamfundisha mtoto ...

**SPIKA:** Mheshimiwa Susan inabidi uwe makini kidogo.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, kama unamfundisha mwanafunzi kuandika tano kwa kiuno watoto wa darasa la tatu, la pili, hili ni tatizo kubwa sana. Hii inaonyesha kwamba Serikali haina fedha ya kuwasaidia walimu kuwapa *teaching aids*. Naomba sana wasaidiwe kwa sababu utamuona mtoto wako anakuja nyumbani anatikisa kiuno unadhani ameshaanza mahusiano kumbe...

**SPIKA:** Hiyo tano inaandikwaje Mheshimiwa Mbunge. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ningekuwa nimevaa suruali ningekuonesha. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, dakika zako zimekwisha.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana, sana kwa mchango wako. Profesa, Waziri wa Elimu, ni kweli wale watoto waliohamishwa kutoka kwenye vile vyuo ambavyo vilizuiliwa hapa katikati kwenda kwenye vyuo vingine na wengi wao ni wa *education* na wengi wao ni watoto wa kike hawajapata hata senti moja. Kwa Wabunge ambao tuna baadhi ya wanafunzi waliohamishwa huko ndiyo kazi ambayo tunafanya sasa hivi kuwasaidia hao watoto na ni ngumu kweli. Sijui ni kwa nini, toka mwezi Septemba, Oktoba mpaka leo Februari hali yao ni mbaya sana. Namba sana hili ambalo amelieleza Mheshimiwa Susan tulitazame kipekee tuwaokoe watoto hawa. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwiningi wa rehema, mwiningi wa utukufu aliyenijalia kusimama hapa siku hii ya leo. Pili, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye taarifa za utekelezaji wa shughuli za Kamati za Bunge za mwaka 2018/2019 ambazo ni Kamati za Maendeleo ya Jamii, Serikali za Mitaa na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba niende kwenye suala linalohusu maboma. Katika maboma ambayo yamejengwa na wananchi kwenye suala la afya na elimu ikiwa ni madarasa pamoja na zahanati na vituo vya afya

ni mengi sana katika nchi hii. Inapotokea kwamba nguvu za wananchi ambazo zimetumika, wananchi ambao wamejitolea kwa dhati kabisa kujenga maboma yale na ikaonekana kwamba nguvu za wananchi hawa zinapotea bure wananchi hawawezi kuielewa kabisa Serikali dhidi ya nguvu zao ambazo zinapotea bure. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie namna ya kuweka mkakati wa makusudi kabisa kuhakikisha kwamba maboma yale yanamaliziwa na watoto wetu waweze kuanza kuyatumia kwa madarasa lakini pia zahanati na vituo vya afya vianze kutumika haraka iwezekanavyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la *Local Government Development Grant*. Huu mfuko ulikuwa unasaidia sana Halmashauri zetu, najiuliza ni kwa nini Serikali imeondoa Mfuko huu? Kama kulikuwa na changamoto zozote kwa nini Serikali *is-l-maintain* Mfuko huu ili mwisho wa siku uweze kuendelea kusaidia katika Halmashauri zetu?

Mheshimiwa Spika, kuna suala linahusu *TARURA*. *TARURA* ni jambo ambalo limeletwa kama ugatuaji wa madaraka katika Serikali za Mitaa. Hata hivyo, *TARURA* huyu ye ye ni kama wakala tu katika Halmashauri hizo kwa sababu barabara ni Halmashauri lakini pia hata fedha ni za Halmashauri. Mimi nashangaa sana huyu *TARURA* anaposhindwa kuwa ni mionganoni mwa wajumbe ambao wanashiriki kwenye vikao vya Mabaraza ya Halmashauri zetu ili wale Madiwani waweze kusema ni barabara ipi ambayo inatakiwa itengenezwe badala ya *TARURA* wao kukaa tu kama kakikundi pembeni wakaanza kujipangia wenyewe kwamba tunakwenda kutengeneza barabara hii, barabara hii bila kujali kipaumbele cha wananchi ambao wanawakilishwa na Madiwani ambao wanajua kipaumbele cha barabara za kutengenezwa.

Mheshimiwa Spika, nilidhani kwamba utaratibu huu ungerekibishwa. Nitole tu mfano, anakuja mtu anaingia nyumbani kwako, anaanza kuchukua sufuria jikoni, anakwenda chumbani kupika, anavuruga utaratibu. Kwa hiyo, ni vizuri hawa *TARURA* wakashirikishana na wakawa

wanaripoti kwa Halmashauri ili wawewe kubainisha vizuri zile barabara na taratibu zote ziweze kwenda sawia. Nachoamini ni kwamba Diwani wa Halmashauri au Halmashauri haitakuwa na mamlaka ya kupanga au kutafuta wazabuni lakini hata kuelekeza tu kwamba nadhani barabara hii kutoka sehemu fulani mpaka sehemu fulani ingefaa itengenezwe kwa sasa kulingana na changamoto iliyopo, nayo pia wananyimwa? Ni jambo gumu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende kwenye suala la watumishi wa Halmashauri. Kwenye suala la afya na elimu kuna changamoto ya watumishi hasa hapa kwenye suala la afya. Zahanati zetu unakuta labda kuna Daktari mmoja au sehemu nyine hakuna Daktari kabisa ni Mhudumu tu wa kawaida kama Nesi anafanya kazi za udaktari, huyo huyo azalishe na shughuli nyine, kwa hiyo, kumekuwa na shida kubwa sana. Utendaji kwenye zahanati zetu na vituo vya afya hauridhishi mwisho wa siku tutaendelea kuwaumiza wananchi wetu, watakuwa hawapati matibabu yale yanayostahili kulingana na vile ambavyo ingefaa.

Mheshimiwa Spoika, sasa naomba niende kwenye suala la UKIMWI, naomba hapa mniskilize kwa makini sana. Tanzania 90, 90, 90 inawezekana lakini inawezekana pale tu ambapo kutakuwa na ruhusa ya watu kujipima wenyewe. Kuna watu wengine wanaona aibu kwenda kupimwa kwenye vituo vya upimaji hasa wanaume. Hawa ndiyo wamekuwa wakifanya kazi ya kusema kwamba maadamu wewe umepima basi tutakuwa tuko sawa, siyo kweli. Ni kwa sababu tu wanaona aibu kwenda kupima lakini utaratibu wa kila mtu kujipima mwenyewe utakuwa ni mzuri zaidi, mnaweza mkakaa watu wawili wenyewe mkajipima, ukampima mwenzako na wewe ukampima mkapata majibu hapo hapo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia katika suala la UKIMWI kuna suala la mkono sweta. Mkono sweta kwa utafiti ambao umefanyika...

**SPIKA:** Mheshimiwa Jaqcueline, Kiswahili hiki sijui kama kila mtu anelewa ni kitu gani hicho. (*Kicheko*)

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, mkono sweta ni wale wanaume ambaao hawajatahiriwa. Hili jina wamejaribu kuliboresha sana badala ya kuliita govi wamesema mkono sweta angalau limeboreshwa boreshwa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mkono sweta ni janga.

## T A A R I F A

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline pokea taarifa.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba jambo hilo hata Bunge la Kenya ililishughulikia na likaweka wataalam mbele ya mlango wa Bunge, wale Wabunge ambaao walikaguliwa na kuona wana hali hiyo wakapata tiba mara moja. Kwa hiyo, anachokizungumza ni sahihi kabisa na Mheshimiwa Spika unaweza ukachukua utaratibu huo ili kupunguza maambukizi. (*Kicheko/Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, nimeipokea kwa mikono miwili na nashauri tuanze na Wabunge wote humu ndani ambaao pengine watabainika hawajafanya hiyo tohara basi wafanyiwe mara moja. (*Kicheko/Makofi*)

**SPIKA:** Bahati mbaya hoja yako haikuungwa mkono. Endelea Mheshimiwa. (*Kicheko*)

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nilindie dakika zangu.

Mheshimiwa spika, suala la mkono sweta ni tatizo kubwa. Ili kufikia 90, 90, 90 ni lazima tuhakikishe kwamba mikono sweta yote inaondolewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanyika unaonyesha kwamba mkono sweta umekuwa ukiambugiza magonjwa mbalimbali ikiwa ni pamoja na ugonjwa wa UKIMWI. Maambukizi ni kwa mwenye mkono sweta lakini pia kwa mwanamke kwa asilimia 60. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, labda niseme ni namna gani ambavyo unaambukiza UKIMWI lakini pia umekuwa ukiambugiza kansa. Endapo mkono sweta ule umekutwa na virusi aina ya *human papilloma virus* ni rahisi kumuambukiza mwanamke virusi hivyo ambavyo mwisho wa siku mwanamke anakuwa anapata kansa ya kizazi. Kwa hiyo, naomba sana...

## **T A A R I F A**

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline pokea taarifa.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa kwamba ile hoja ya kuomba wanaume ambao hawajapata sunna au tohara wafanyiwe ili kuondoa mikono sweta wakati anaitoa wengine tulikuwa kidogo hatumsikia vizuri. Kwa hiyo, nilikuwa naomba nimpe taarifa airudie tena ili tumuunge mkono. (*Makof/Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline, una dakika mbili umalizie.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli sasa naongea kwa masikitiko sana. Pale unapoona kwamba hawa wanaume wenyе mikono sweta wanakwenda kuwaambukiza wanawake wenzetu ikiwemo pengine na wanawake wengine kama itatokea...

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, naomba unilindie muda wangu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Musukuma.

## T A A R I F A

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, alikuwa ameomba Peter ila kwa umuhimu umeniona mimi nashukuru. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mawazo yake ni mazuri na hili ungeliunga mkono tukawekewa kipimo pale lakini takwimu zinaonyesha kwamba hata wanawake wale walioketewa nao wanaongoza kwa kuambukiza UKIMWI. Kwa hiyo, wakati wanaume wakikaguliwa hilo na Wabunge wanawake na wao wakaguliwe pale mlangoni. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline, muda wako ulishapita tunashukuru sana. Leo hii Kamati ya masuala ya UKIMWI inataka kumpa hali ngumu sana Spika ya kuanza kufanya ukaguzi ambao haujawahi kutokea, sijui tutatumia *methodology* gani. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea vizuri na wale wote ambao majina yenu ninayo hapa mtapata nafasi ya kuchangia jioni ya leo. Kwa hiyo, tuwahi tu kurudi saa 10.00 ili tutekeleze wajibu wetu kwenye Kamati hizi tatu kama ilivyo ada.

Waheshimiwa Wabunge, kwa namna hiyo basi, naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 10.00 jioni ya leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge ilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Nne; na tukisema Mkutano wa Kumi na Nne sijui kama Waheshimiwa Wabunge wengi wanatupata, kwamba ibaki mingapi? Mikutano iliyobaki ni mitano tu kwa wasiojua. Huo ndio ukweli wenyewe. Maana yake tutamaliza mikutano 19. Sasa Mheshimiwa Nkamia akisimama, mnamzomea. Ahsante sana. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Tuanze na Mheshimiwa Khatib Haji, nakupa dakika 10.

**MHE. KHATIB S. HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai wake nikaweza kusimama hapa jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuongelea suala la ugonjwa wa UKIMWI. Asubuhi hapa nilimsikia Mheshimiwa mmoja akiongea kwamba ishara za wafadhili zinazoonesha kusita kutoa misaada ambayo kwa kiasi kikubwa inatusaidia katika sekta hii ya kuwashudumia wenzetu wenyewe maradhi haya ni kiwango ambacho ni kikubwa sana, jambo ambalo mazingatio tunayopaswa kuwa nayo kwa sasa ni kuona umuhimu kama Taifa kuanza kuona jinsi gani ya kufanya kuweza kukabiliana na hali hii.

Mheshimiwa Spika, kila siku zinavyokwenda mbele masharti ya wahisani wetu yanazidi kuwa makubwa. Masharti yanapozidi kuwa mengi na makubwa na mengine yanakuwa hayatekelezeki, ni fundisho tosha la kutufundisha sisi kuona sasa kidogo tunachokipata kuangalia maeneo muhimu. Kati ya maeneo muhimu ni maeneo yanayogusa uhai wa watu moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo hili la wagonjwa wa UKIMWI ni eneo ambalo kwa kiasi fulani tumepata mafanikio ya kupunguza maambukizi mapya kutokana na msaada mkubwa wa kifedha ambao wahisani wetu walikuwa wanatusaidia. Kutokana na hii hali ambayo imeanza

kuonekana, masharti kila yanavyozidi kuongezeka yanatishia juu ya fungu hili la kusaidia wenzetu ambapo hakuna anayejjua lini litamkuta hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama kuna maeneo ambayo tunapaswa kuyazingatia sana ni kuangalia namna gani tutaweza kukabiliana na tishio la wafadhili wetu kuacha kutusaidia katika mambo mazito na muhimu ya uhai ya wananchi wetu na sisi wenyewe kwa ujumla. Kwa hiyo, angalizo langu ni kwamba aomba Serikali kuititia Wizara ya Afya, katika mipango yake, sasa ijielekeze zaidi kutathimini maeneo haya ambayo kwa kweli yanasononesha na yanatishia sana.

Mheshimiwa Spika, nataka niongelee suala la pili ambalo ni kuhusu Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Asubuhi ya leo nilluliza swali kuhusiana na namna Zanzibar tunavyonufaika na misaada kutoka *FIFA*.

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu na wote tunafahamu kwamba Tanzania ni Taifa moja na masharti ya Taasisi zile, Shirikisho la Mpira Duniani, *FIFA* na *CAF* yote kati ya masharti yao ni kwamba hawatambui, hawawezi kupokea nchi mbili kuwa wanachama wa taasisi zile.

Mheshimiwa Spika, hili lilitokea mwanzoni mwa miaka miwili iliyopita pale Zanzibar ilipobahatika kujunga na wanachama wa *CAF* kwa jithada kubwa zilizofanywa na mapenzi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kusaidiana na washirika wa kimichezo hadi kuifanikisha Zanzibar kuingia katika wananchanma wa *CAF*, lakini kwa bahati mbaya haikuchukua zaidi ya miezi minne Zanzibar ikaondolewa katika Uanachama ule kwa masharti yale kwamba haiwezekani Taifa moja likawa na wanachama wawili. Kwa hiyo, hayo ni masharti ya Katiba zao na sisi hatukuwa na la kufanya.

Mheshimiwa Spika, hapa ninaongelea ni kwamba, asubuhi jibu nililolipata ni kwamba *ZFA* ni sehemu ya *TFF*, siyo sahihi. Kama ni sahihi, naomba Mheshimiwa Waziri

tafadhalii aje aliweke sawa jambo hili nione uhalali wa jambo hili. Kwa sababu kama nilivyosema na narudia kusema, Wizara ya Habari na Michezo ya Tanzania ni Wizara inayohusika na upande mmoja wa Muungano, kama ilivyo Zanzibar, Wizara ya Habari na Michezo Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, *TFF* ni chombo cha mpira wa Tanzania Bara na Zanzibar iko *ZFA*. Kwa hiyo, linapokuja suala la misaada kutoka nje ya kimichezo kuititia *FIFA*, inapoingia *TFF*, kama kuna kilichowahi kwenda, basi iili kuwa ni huruma *TFF*. Hakuna mfumo maalum wa kuona upande wa Zanzibar ambaye siyo mwanachama wa *FIFA* wala *CAF* anafaidika vipi na fungu la mgao kutoka *FIFA*?

Mheshimiwa Spika, hili ni suala ambalo naiomba sana Serikali ili angalie kwa umakini tusije tukazalisha kero ya ovyo katika Muungano, kwa sababu masuala ya michezo ni sekta inayogusa vijana wengi; na kama tunaavyojua, vijana wana mihemuko mingi. Leo kuliacha jambo hili ambalo taarifa zipo; kwa mfano, sasa hivi tunatarajia kama hazijaingia, zitaingia muda wowote, *1.25 billion Dollar* msaada wa *FIFA* kwa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika hili, kabla haujafika huo mgao, napenda kutoa mapendekezo yangu kwa Mheshimiwa Waziri, waangalie kuititia Wizara yake na Wizara ya Michezo ya Zanzibar, ni namna gani kale kasungura ka michezo ambako kanatolewa na *FIFA* kwa nchi ya Tanzania? Tanzania ikijua ni nchi yenye Muungano wa mchi mbili vilevile, kwa hiyo, hili jambo liwekewe mfumo maalum ili Zanzibar tuone tunanufaika vipi kuititia *FIFA*.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo na ambalo limekuwa na malalamiko makubwa kwa upande wa Zanzibar. Kwa hiyo, ni vizuri sana kuzingatia moja kwa moja isiwe ni kwa bahati mbaya; leo ukiongelea habari ya msaada wa *FIFA* kwa Zanzibar siku zote jibu linakuja, "tulisaidia Uwanja wa Gombani kuweka nyasi." Hilo tu! Kuweka nyasi Uwanja wa Gombani imekuwa ni *slogan* ya kuonesha kwamba ilitosha

kwa Zanzibar kufaidika na misaada ya *FIFA*. Hiyo siyo sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tungeweka mfumo ambao hautakuwa na mgongano wa kujua katika kinachopatikana kutoka *FIFA* wao Zanzibar moja kwa moja kifungu chao *at list* kitakuwa ni hiki na tuondoe huu mgongano ambao sioni umuhimu wowote wa kuweza kufikia hali ya kuwekwa nayo kama ni kero ya Muungano. Nadhani hilo limeeleweka.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho na la muhimu sana, hapa kuna jambo linazungumzwa, lakini mara nydingi Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakilizungumza kana kwamba ni jambo la utani na ni jambo ambalo linachukuliwa kwa utani.

Mheshimiwa Spika, suala hili la tohara kwa wanaume, nilivyomsikia mchangiaji leo akisema madhara yanayopatikana kufikia kansa, siyo jambo la kulichukulia utani tena, ni jambo *serious* kwamba kwa sababu hilo jambo linagusa kila maisha ya mwanadamu, siyo jambo la kusema hapa tukawa tunacheke. Kama leo kuna ugonjwa, nilidhani labda ni kupunguza chachu ya mambo fulani, lakini sasa kuna gongwa la hatari la kansa ambalo linapatikana kutokana na wanaume ambao hawajafanyiwa tohara. Hilo siyo jambo la utani tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ingekuwa ushauri wangu, akina mama wa Tanzania wanansikiliza, ningewaambia wawagomee wanaume wowote ambao bado hawajakubali kufanyiwa tohara. Wawagomee kabisa, wawaambie bila tohara hilo jambo haiwezekani, *no!* Kwa sababu leo unaenda kumwoa mke...

**SPIKA:** Mheshimiwa Khatib siyo fitina hiyo! (*Kicheko*)

**MHE. KHATIB S. HAJI:** Mheshimiwa Spika, hapana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, siyo fitina kwa sababu leo mtu anaenda kuoa mke, kesho amegombana, anamuacha; wewe unaenda kuoa tena; kumbe ye ye alikuwa na tatizo hilo kutokana na maradhi ya kujitakia.

Mheshimiwa Spika, mara ny ingi nimewaambia wanaume ambao bado na tatizo hilo, tuulizeni tunafaidika vipi sisi ambao tulibahatika mwanzo kujaliwa kuwa na tohara? Leo nimekuja siyo faida pekee, bali ni madhara makubwa ambayo yanatokea kiasi cha kuwapatia ndugu zetu kansa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tusichukulie utani. Kama kuna ugonjwa mkubwa ambao dada yangu asubuhi ameutaja pale, hili jambo lazima tuwe *serious* kuona kwamba hili suala ni muhimu kwa tohara ya wanaume wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nasema ahsante sana, nashukuru sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mh! Leo hatari! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Ezekiel Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Papian. Mheshimiwa Maige dakika 10.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie kwenye mada iliyoko Mezani. Kwanza naomba nizipongeze sana Kamati zote tatu, wamefanya kazi nzuri sana na kimsingi nakubaliana sana na mapendekezo ambayo wameyaweka. Kwa upande mwingine pia naomba niishukuru sana Serikali, nayo kwa upande wake imefanya kazi kubwa, imetimiza wajibu. Kwa mfano, katika Sekta ya Maendeleo ya Huduma za Jamii na Elimu, yako mambo mengi mazuri ambayo yemefanyika.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwa mfano kwa upande wa Afya jinsi ambavyo Serikali imetoa fedha ny ingi kwa ajili ya kujenga Vituo vya Afya kwenye kila Kituo cha

Afya ambacho kimependekezwa kwenye Halmashauri, vile vile kuna ujenzi wa Hospitali za Wilaya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, kwa ujumla nakubaliana na mapendekezo yalitolewa. Naomba tu niongezee kidogo kwenye maeneo ambayo nadhani ni muhimu Kamati hizi zingeweza kuyatazama na kuyawekea mkazo. Nilidhani ikiwezekana nimwombe sana Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii anisaidie katika *ku-wind up*, kuboresha azimio mojawapo linalohusu upelekaji wa fedha kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya kazi kubwa sana kama ambavyo nimesema awali, lakini bado kuna maeneo ambayo tunahitaji kuongeza juhudhi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya na elimu kwa mfano, tumefanya kazi kubwa ya kuhamasisha wananchi waweze kujenga shule; na hapa nitazungumzia hasa Jimbo langu la Msalala kama mfano mmojawapo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2015 wakati tunafanya kampeni kwa kuzingatia llani yetu ya CCM, tuliwaambia wananchi kwamba tutajenga Zahanati kila kijiji na tutajenga Kituo cha Afya kila Kata na vilevile tutajenga shule kwenye maeneo yote ambayo hayakuwa na shule. Tuliwaambia wananchi kwamba mambo haya hatutayafanya sisi kama Serika peke yake na wao wananchi watashiriki; na tuliwaeleza kwamba wanapaswa kuinua maboma na Serikali itawashika mkono. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, wananchi wameitikia sana. Nilimsikia rafiki yangu Mheshimiwa Mwijage muda fulani anazungumza kwamba sisi kama Wabunge tende tukawahamasishe wananchi wetu kupiga *propaganda* ili waweze kuanzisha miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba kazi hiyo nimeshaianza. Hivi tunavyozungumza, tuna maboma 131 kwenye Jimbo la

Msalala ambayo wananchi wameshaweka nguvu zao pale, mengine yana miaka mitatu, mengine yana mwaka mmoja na mengine yana miaka mingi kidogo. Tuna maboma zaidi ya 62 ya vyumba vya madarasa. Leo hii tunawahamasisha wananchi sasa waanze kujengwa wenyewe hadi kuyakamilisha wakati walishakayakamilisha imebaki Serikali kuleta fedha za ukamilishaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tuna maboma 40 ya Zahanati na katika mpango ule tulishawahamasisha wananchi wakanza kujengwa Vituo vya Afya kwenye maeneo matatu. Kwa hiyo, kuna majengo makubwa matatu ambayo yanatosha *OPD* pamoja na vyumba vingine ikiwemo *theater* kwenye Kata tatu. Kwa hiyo, kwa ujumla tuna maboma ambayo thamani yake iliyobaki inayotakiwa kuyakamilisha ni shilingi bilioni 4,268.

Mheshimiwa Spika, wananchi wameshaweka nguvu zao pale na thamani ya fedha au nguvu ambazo wananchi wameweka pale ni zaidi ya shilingi bilioni 1,623. Kuna hatari kwamba maboma haya sasa yanaelekeea kuanza kubomoka na Serikali haijaleta fedha za ukamilishaji wakati matarajio ya wananchi yalikuwa kwamba wakishakuwa wamemaliza maboma haya, basi Serikali italeta fedha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii kama ilivyowasilisha Kamati kwenye lile azimio linalohusu kupeleka fedha, basi angalau kama unaona siyo lazima sana kwenye maeneo mengine, basi angalau lile azimio tuliboreshe tuseme kwamba Serikali ipeleke fedha za ukamilishaji wa maboma Jimbo la Msalala...

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Na Bukene.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Na Bukene kama unaona kwingine haipendezi sana. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba hili suala la kupeleka fedha za miradi lifanyiwe haraka na liwe sehemu ya maazimio ambayo tungependa kuyaweka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie kwa upande wa elimu na tatizo la ajira. Katika maeneo ambayo tuna matatizo makubwa sana ni suala zima la ajira. Alisema Mheshimiwa Nkamia asubuhi na Waheshimiwa Wabunge wengine, suala la ajira kwa sasa ni janga. Tusipochukua hatua, ninaamini kabisa kwamba linaweza likaleta madhara makubwa kwenye jamii yetu na hata utangamano na ustahimilivu na usalama wa nchi.

Mheshimiwa Spika, ninavyoona tatizo liko katika mfumo wa elimu yetu. Tuna wahitimu wengi amba wana-*graduate* kwa sasa hivi, zaidi ya *graduates* 600,000 kwenda juu, kuanzia *level* ya *Form VI* wale wanaokosa nafasi kuendelea na masomo hadi Vyuo Vikuu; wote hawa wanahitaji ajira kwenye sekta iliyo rasmi. Kwa mfumo huu tunaokwenda nao, naamini kabisa hatuwezi kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, tujaribu kujiuliza na nilitaka niwape changamoto Mawaziri wangu wawili hawa; Mheshimiwa Jenista Mhagama na hata Mheshimiwa Waziri wa Elimu, hivi katika *intervention* za Serikali zinazofanywa, hizi za kusaidia kukuza ajira, jiulize tu, tunaposema asilimia 10 ya mapato ya Hal mashauri kwenda kwa akina mama, vijana na wale mavu, hivi kuna watu wangapi wenye elimu kuanzia *Form VI* wanaotumia fursa hiyo? Ukipiga hesabu ni kama hawapo. Wanaokwenda kwenye hizo fursa ni Darasa la Saba kwenda chini.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo elimu yote aliyoipata kuanzia *Form VI* kwenda juu hawaii mii kwenda kujishughulisha kujajiri, wanawaachia wenzao wa chini zaidi na wao wanasubiri ajira za Serikalini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumetoa vitambulisho kwa wafanyabiashara, Mheshimiwa Rais ametoa karibia

vitambulisho 100,000 sasa, hivi katika hao wafanyabiashara kuna wangapi ambao wamemaliza *Form VI*, ukiangalia utakuta ni hakuna. Kwa hiyo, hawa wote kuanzia *Form VI* kwenda vyuo wote wanasubiri ajira zilizo rasmi.

Mheshimiwa Spika, tuimarishe elimu ya ufundi (*polytechnic colleges*) ambayo mtu akimaliza pale, tena ikiwezekana hata mkopo tumpatie atoke na cherehani yake, aende ajajiri, aanze kufanya kazi. Hii ya kumaliza wanagombea *boom* kule ambalo ndiyo mikopo ya Elimu ya Juu, halafu akimaliza anakaa anaanza kuomba ajira ambazo hazipo, ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie mfumo wa elimu ili iweze kuwasaidia vijana wetu waweze kwenda kwenye ajira moja kwa moja badala ya kuwaandaa kuajiriwa kwenye nafasi za *white collar jobs* ambazo hazitoshi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kujua kwamba muda unaelekea kwisha naomba nimalizei kusema naipongeza sana Serikali na Kamati zote tatu.

Mheshimiwa Spika, nimalizie sentensi kabla sijafunga kabisa, kuhusu suala la TARURA. Ni kweli, sasa hivi utengenezaji wa barabara za vijijini umepungua kuliko ilivyokuwa ukisimamiwa na Halmashauri. Kuna tatizo. Mojawapo ni fedha zinazopelekwa *TARURA* hazitoshi. Pia hili suala la ushirikishwaji; Madiwani ambao ndio wanaosimamia Halmashauri, wengi wao hawashiriki wala hawajui mipango ipi ambayo imewekwa na *TARURA* kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, nilidhani eneo hili ni vizuri likarekebishwa; mpango wa kuwaongezea fedha *TARURA* ufanyike na namna ya kuwashirikisha Madiwani ifanyike ili tuweze kufanikisha lengo la kuwa na *TARURA* na kuboresha barabara za vijijini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja zote tatu. Nashukuru sana kwa nafasi uliyonipatia. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Papian, atafuatiwa na Mheshimiwa Godfrey Mgimwa, dakika tano tano.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa dakika tano. Kwanza napongeza jitihada nyingi za Serikali ambazo inazifanya kwenye maeneo mbalimbali na kwa namna ambavyo Mawaziri wamejitätahidi kufanya kazi kwenye hizi *report* zao.

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuwajali wakulima na wafugaji kwa kupunguza maeneo ya hifadhi ili wakulima wetu na wafugaji wapate maeneo na mahali pa kukaa salama bila ugomvi kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Jambo la pili nimshukuru Rais kwa kutoa vitambulisho kwa sababu, wajasiriamali wetu sasa wameanza kutambulika na mwisho wa siku watakuwa, watakuwa ni watu ambao wana uwezo wa kutambulika na watakuwa wakubwa na watakuwa na uwezo wa kukopesheka hapo mbele.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la tatu kuna jambo ambalo nimeliona na Wabunge wengi hawajasema, Rais ameweza kufanya kazi kubwa ya kusaidia kupata matrekta NBC imetoa matrekta, mkulima analipa milioni mbili *down payment* na leo wakulima wengi wameweza kusambaziwa matrekta nchini.

Mheshimiwa Spika, kwake kuna matrekta 89 yameingia, Wabunge wenzangu mpigieni Makofi Mheshimiwa Spika wetu. Kwa Mheshimiwa Nkamia yameshaingia matrekta 52, kwangu Kiteto yameshaingia matrekta 105. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais ameshafanya kazi kubwa kwa wakulima wetu kwa kuwatambua ili wakapate kufanya kazi kwenye maeneo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili suala la *TARURA* linatupa shida kidogo. Siku za nyuma Madiwani wetu na baraza walikuwa

na uwezo wa ku-*coordinate* zile barabara na kuona wapi pana daraja na wapi pana shida. Sasa hili suala la *TARURA* kutoleta taarifa kwenye Baraza la Madiwani tunashindwa ku-*coordinate* na ku-*monitor* hizi barabara, hata kwa kujua gharama. Hili suala litaendelea kuharibu barabara nyingi, suala la hizi barabara ambazo unakuta wameleta pesa za dharura kwa ajili ya kutengeneza maeneo korofi, huwezi kujua ni kiasi gani, huwezi kujua wanatengeneza wapi, huwezi kudhibiti angalau na kujua kwamba, kilichoingia ni kipi na kilichotoka ni kipi ili kuwabana watendaji wakandarasi kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kushauri. *TARURA*, TAMISEMI iweze kutusaidia kuhakikisha kwamba, hawa watu wa *TARURA* wawe wanaripoti kwenye Baraza, watoe ripoti pesa zilizoingia, viwango vya barabara vinavyojengwa kwa wakati huo, pesa za dharura na kila kitu chote ule mchanganuo upate halafu na sisi Baraza la Madiwani tutoe ripoti na ile ripoti iwe inakuja mpaka mkoani, mkoani iweze kuja kwenye Taifa kwa mazingira ya kila wilaya kuweza ku-*monitor* barabara zilivyo na uharibifu wake.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine; watendaji wa vijiji na kata mimi napata mshangao. Utumishi wa nchi hii unafanana kama Hati Milliki ya Ndoa ya Kikatoliki kwamba, mpaka ufe au mwenzako afe hamuwezi kuachana. Hii ni shida kubwa unakwenda mahali kijiji kimechanga Sh.2,700,000/=. Juzi nimepigiwa simu hapa, wananchi wanahitaji kupauwa jengo lao, Mtendaji wa Kijiji amechukua pesa, amekwenda amenunua mizigo yake amechakachua, amerudi hapa, haitoshi, hakuna kikao, hakuna kamati, hakuna nini, wanamuuliza anasema hakuna, amekuwa mbabe. Ukienda naye sambamba ni kwamba, mbele wanasesma sasa mtumishi ukitaka kumhamisha wanakwambia awe na *cheque* mkononi, *cheque* mkononi, unafanyaje?

Mheshimiwa Spika, ukiondoka anakaa hivyo, keshokutwa mchango mwingine, wananchi wanaacha kuchangia maendeleo yao. Lazima TAMISEMI iamue mtumishi

mbadhirifu /level ya kijiji aidha apewe adhabu ya kuondolewa kazini tuajiri wengine ndio maana tuna wasomi wako mtaani. Tuamue, hii inaweza ku-*discipline* nchi hii, otherwise ni kwamba, tutaendelea kuwa na *debate*, Mkurugenzi hawezi ku-*manage* hawa watu wote, hata akim-*manage* anamhamisha anakompeleka si kuna Watanzania walewale, si kuna kijiji kilekile, si kuna kata ileile, atachangisha ataharibu. Sasa hii *contract* ya mtumishi wa Serikali ya Tanzania ambaye hawezi kumeguka akaachwa, eti *formular* sijui mpaka uajiriwe, ukaulizwe, mupeane adhabu, barua za onyo, hatutafika na wananchi chini wanaumia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naombe kushukuru jitihada nyingi za Serikali zinazofanyika. Napongeza na kuunga mkono hoja. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Emmanuel Papian. Nilishakutajwa Mheshimiwa Godfrey Mgimwa, utafuatiwa na Mheshimiwa Makilagi.

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Nitajikita zaidi kwenye Kamati yangu...

**SPIKA:** Dakika tano eeh.

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nitajikita zaidi kwenye masuala ya UKIMWI kwa sababu na mimi pia ni Mjumbe wa Kamati hii ya UKIMWI. Nipongeze juhudhi za Kamati ambazo zimefanyika, lakini vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kufanya kwa ajili ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, kwenye masuala ya UKIMWI lazima tufahamu kwamba, tatizo la UKIMWI ni kubwa katika nchi yetu, asilimia tano katika asilimia 100 ya Watanzania ndio wenye maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI, lakini tatizo tunalolipata ni bajeti ambayo tunakumbana nayo,

changamoto ya bajeti. Tumeshauri hapa kwenye Kamati kwamba, ufinyu wa bajeti sehemu kubwa au ni chanzo kikubwa sana cha kutoweza kuwafikia ndugu zetu ambao wana maambukizi ya virusi via UKIMWI. Kwa hiyo, ingekuwa vizuri zaidi kwamba, Serikali tungeweza kujikita na kuzipeleka fedha, hasa fedha ambazo zinatoka Hazina kuelekea kwenye mifuko mbalimbali, hasa huu Mfuko wa *TACAIDS* ili tunapopeleka ujumbe wetu kwa ajili ya Watanzania na kuhakikisha kwamba, tatizo hili au ugonjwa huu wa UKIMWI unapungua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, kuna mikanganyiko au mgongano kati ya Sheria ya UKIMWI na Sheria ya Ndoa, ambapo unakuta Sheria ya UKIMWI inamtaka mtoto mwenye miaka 15 aweze kuambatana na mzazi kwenda kupima, lakini Sheria ya Ndoa inasema mtoto mwenye miaka 14 kwa ridhaa ya mzazi anaweza akaolewa. Sasa ina maana mtoto huyu mwenye miaka 14 ameshaolewa, lakini vilevile arudi tena kwenda kupima akiwa na mzazi wake. Hilo jambo linaleta mkanganyiko kidogo, kwa hiyo, Sheria ya UKIMWI tuiangalie inavyokinzana na Sheria ya Ndoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna tatizo la takwimu. Kuna takwimu ambazo zinatolewa na *NBS*, kuna takwimu ambazo zinatolewa na *TACAIDS*, takwimu nyingine zinatolewa na wadau mbalimbali wa huko nje ya nchi, Ulaya na kadhalika ambao wanatoa fedha kwa ajili ya kuendelea kusaidia changamoto ya maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI. Kwa hiyo, niseme tu kwamba, ni vyema sasa ifike wakati hizi changamoto ziweze kupungua, ili kwamba, tunapopeleka takwimu tuweze kupeleka takwimu zinazoeleweka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna sehemu nyingine unakuta wanasesma Nyanda za Juu Kusini, Mkoa wa Iringa tunaongoza kwa asilimia 13, takwimu nyingine zinasema 11, takwimu nyingine zinasema 10 kwa hiyo, kuna mkanganyiko namna hiyo. Kwa hiyo, lazima tupate takwimu ambazo zinalelewaka ili tuweze kuwaambia Watanzania ukubwa wa tatizo.

Mheshimiwa Spika, lingine nieleze, tatizo la UKIMWI ukubwa wake labda kwa takwimu tu, maambukizi kwa mwaka kwa Tanzania ni maambukizi 81,000. Iha maana kwa mwezi maambukizi ni 6,750 kwa wiki ni 1,687 kwa siku ni 241 na kwa saa ina maana ni watu 10 wanapata virusi vya ugonjwa wa UKIMWI kwa saa. Kwa hiyo, ukiangalia kwa upana wake na ufinyu wa bajeti ambaao tunao bado tuko nyuma sana na tunahitaji tuweze kuweka mkazo ili changamoto hii iweze kupungua.

Mheshimiwa Spika, vilevile niseme tu kwamba, kwenye ule mkakati wa 90 90 90 ambaao tunaenda nao mpaka mwaka 2020, ni kwamba, kwenye 90 ya kwanza Tanzania bado hatujafanya vizuri, tuko kwenye asilimia 52 ya malengo ya asilimia 90 ambapo hapa ndio kwenye changamoto kubwa ambapo watu wanashindwa kwenda kupima, hasa sisi wanaume tunakuwa wagumu sana kwenda kupima. Vilevile akinamama kwa sababu wanapata nafasi ya kwenda kupima wakiwa wajawazito, inaonesha kwamba, idadi ya akinamama ndio kubwa zaidi kwenye maambukizi, jambo ambalo inaweza ikawa lisiwe sahihi kwa sababu, wanaume tumekuwa ni wazito kidogo kwenda kupima. Kwa hiyo, changamoto hii lazima tui-address kwa wanaume pia kwamba, twende sasa tukapime kwa wingi. Nami Mbunge wa Kalenga nitakuwa mionganoni mwa Wabunge wa kwanza kwenda kupima kuwaongoza Wabunge wengine wanaume katika majimbo mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwenye 90 ya pili ni kwamba, kwenye masuala ya upatikanaji wa dawa; ni kweli kwamba, tuna tatizo, lakini kwa sasa hivi tatizo limeshapungua kwa kiasi kikubwa. Niishukuru Serikali kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda naomba niunge mkono hoja na nakushukuru sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Makilagi, utafuatiwa na Mheshimiwa Mbilinyi.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia maeneo machache...

**SPIKA:** Dakika 10.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, dakika 10? Ahsante sana kwa huo muda kwa sababu nilikuwa najaribu kuangalia dakika tano hizi.

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kutoa mchango wangu katika sekta hizi tatu. Kwanza kabisa kabisa naomba nianze kuungana na Watanzania wenzangu kutoa pole sana kwa akinamama, akinababa na jamii ya Wanajombe kwa misiba mikubwa iliyotokea ya mauaji ya watoto wetu wasiokuwa na hatia. Natoa pole kwa sababu msiba huu ni mkubwa, ni msiba wa Kitaifa na hapa naomba nitoe ushauri kwamba, Serikali yetu ifanye kila jitihada inayowezekana ili wale waliohusika na mauaji yale waweze kupatikana.

Mheshimiwa Spika, mwaka fulani yalitokea mauaji ya wanawake Mkoa wa Mara, Serikali ilichukua hatua na mauaji yalikomeshwa. Mwaka fulani yalitokea mauaji ya maalbino, Serikali ilichukua hatua na mauaji yalikomeshwa. Hivi karibuni tuliona Rufiji mauaji yalikomeshwa na hivi karibuni tuliona watu wenye ulemavu wakifanyiwa ukatili, walikomeshwa, naomba na kule Njombe Serikali ichukue hatua za haraka, ili mambo haya yaishe.

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na Wajumbe wenzangu wa Kamati hizi mbili, Kamati ya UKIMWI na Kamati ya Huduma za Jamii, lakini pia niungane na wengine wote waliouna mkono hoja. Hapa nami naunga mkono hoja na kwa kuokoa muda naomba niishauri Serikali kwamba, Maoni ya Kamati ya Masuala ya UKIMWI, kama ambavyo tumeleta mapendekezo, yapokelewe na yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, tumezungumzia tozo ya kupata fedha kwa ajili ya kununua dawa za watu wanaoishi na

virusi vya UKIMWI kwa ajili ya kufubaza. Tusiendelee kutegemea wafadhili kupitia fedha na maeneo mengine kwa sababu, kuna siku hawa wafadhili watasitisha na litakuwa ni janga kwa Taifa letu. Kwa sababu, tulishaanzisha Mfuko ni vizuri sasa Mfuko huu ukaboreshw na Serikali ikaandaa utaratibu wa kuleta sheria na tukawa na tozo maalum.

Mheshimiwa Spika, pia, tumependekeza kwenye Kamati yetu ya UKIMWI kwamba, umri wa mtoto anayeweza kwenda kupima kwa hiyari bila kwenda na mzazi ufanyiwe marekebisho kulingana na wakati tulionao wa sasa. Badala ya kuwa miaka 18 mpaka kuendelea ianzie miaka 15 waweze kupima kwa sababu, taarifa ambazo Wizara imetuletea kupitia Kamati ya UKIMWI hali ni mbaya, watoto wetu kuanzia miaka 10 mpaka 15 mpaka 25 kila wananchi wanaopimwa asilimia 40 ni watoto wadogo. Kwa hiyo, naungana kabisa na Kamati kwamba, sasa Muswada uletwe hapa Bungeni tufanye marekebisho, sheria tuitunge ili sasa hata hawa watoto wadogo waweze kwenda kupima kwa hiyari kwa ajili ya kuwanusuru.

Mheshimiwa Spika, tumeleta mapendekezo, tunaishauri Serikali ilete sheria ya kuhakikisha suala la bima kwa wote linatungiwa sheria. Tumekwenda Rwanda, Kamati baadhi ya wajumbe walikwenda, wametuletea mrejesho; wenzetu katika suala la bima wako vizuri na sisi Tanzania tuige mfano wake, kuna wengine wamekwenda Ghana wametuletea mfano. Nami naomba nitoe mapendekezo hapa na niungane na Kamati kwamba, sheria ije sasa, ili wananchi wote wapate bima kwa ajili ya manufaa yetu na wewe mwenyewe juzi ulikuwa ukisisitiza, naomba niunge mkono hapo iletwe kwa ajili yetu wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie sasa suala zima la ujenzi wa hospitali za rufaa, hospitali za mikoa, hospitali za wilaya na hata vituo vya afya. Hapa naomba nilete pongezi na shukrani nyingi sana kutoka kwa wananchi wa Mkoa wa Mara. Mkoa wa Mara tulikuwa tunajenga hospitali ya kwanza ya *Mwalimu Nyerere Memorial Centre*,

hospitali hiyo ilijengwa kwa muda mrefu na ilikuwa haikamiliki, lakini kwa uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, sasa hivi hospitali inakwenda mbio na Serikali inatuletea fedha.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Waziri Mheshimiwa Ummy ameshatembea, ameshaona jithada zinazoendelea na ameshapewa gharama na ili jengo liweze kuanza zinahitajika kiasi gani. Naomba nitoe ombi tena kwa niaba ya wananchi wa Mara, hebu Mheshimiwa Ummy au Serikali ituletee hizi fedha ili jengo liweze kukamilika hasa hili la mama na mtoto ili kituo kile cha *Mwalimu Nyerere Memorial Centre* kiweze kufanya kazi na kuwahudumia Wananchi wa mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Spika, tunaleta pongezi zetu kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi tumepata fedha billioni 1.0 kwa ajili ya kujenga Hospitali ya Rorya; billioni 1.5 kwa ajili ya kujenga Musoma Vijijiini; billioni 1.5 kwa ajili ya kujenga Tarime na maeneo mengine; lakini tumepata 400 kwa ajili ya kujenga Hospitali ya Serengeti; na 400 kwa ajili ya kujenga hospitali Butiama. Ombi langu, hii Hospitali ya Butiama na hapa naomba wanisikilize vizuri, najua Mheshimiwa Waziri atakapokuwa aki-*wind up* attachangia; Hospitali ya Butiama naomba tuipe upekee wa utofauti kabisa. Hospitali ya Butiama ni hospitali ya kihistoria, ni hospitali ambayo Baba wa Taifa alikuwa anatibiwa hapo, ni hospitali ambayo Mama Maria Nyerere akiwa Kijijiini Butiama akiugua ghafla ndiko anakotibiwa na ni hospitali ambayo kwa wilaya nzima ya Butiama ndio wilaya inayohudumua wananchi wote zaidi ya watu 200,000.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Butiama ina kituo kimoja tu cha afya kwa sababu, Mwalimu Nyerere alipokuwa Rais aliangalia Watanzania wote, aliwahudumia bila ubaguzi, hakujiangalia nyumbani kwake. Naomba katika misingi ya kumuenzi Baba wa Taifa hebu tuiboreshe Hospitali ya Butiama kwa sababu hata wageni wanaokuja kutembelea Kaburi la Baba wa Taifa wanaougua wanakwenda pale, lakini hata familia ya Baba wa Taifa

yenewe akina Makongoro na wenzake na hata Madaraka anayetulindia Makumbusho ya Baba wa Taifa akiumwa anatibiwa pale Hospitali ile ya Butiama haina hadhi ya kuendana na kazi alioifanya Baba wa Taifa letu la Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Serengeti wamechangishana fedha wamefika zaidi ya milioni 300 wakaanza kujenga hospitali, kama sio ya kwanza Kitaifa inaweza ikawa ya pili kwa mfano, ni hospitali kubwa na ni nzuri wananchi wamejitelea. Tunashukuru Serikali imetuletea shilingi milioni 400, naomba na hii hospitali hebu waiongezee na yenewe ifike bilioni 1.5 kama ambavyo wamefanya kwagine.

Mheshimiwa Spika, nimesema mimi hapa leo ni shukrani maana maoni mengi kwenye Kamati yametolewa. Naomba nilete shukrani za wananchi wa Mkoa wa Mara, wametujengea na kuviboresha vituo vyta afya 10, shilingi zaidi ya bilioni 6.0, tumejepata katika mkoa wetu. Naleta shukrani za wananchi wa Mkoa wa Mara na hata kura zikipigwa leo Chama cha Mapinduzi na Rais wetu watapata ushindi wa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, ombi letu na hapa nataka niongelee kwa Tanzania nzima ikiwemo Kongwa, Mbeya na maeneo mengine; suala la wafanyakazi au watumishi katika hivi vituo vyta afya ambavyo vimeboreshwa; naomba Serikali tupeleke watumishi, kama hatukupeleka watumishi ni sawasawa na kufanya kazi bure. Hivi karibuni nimetembelea vituo vyote ambavyo vimepelekewa fedha, nimeenda kuona mafanikio na kusikiliza changamoto, nimejionea mwenyewe Kituo cha Nata nakitolea mfano, Daktari yuko mmoja peke yake wakati chumba cha *theatre* wanatakiwa wawepo Madaktari wanne; ye ye ndio anashika mkasi, ye ye ndiye anaandaa *gloves*, ye ye ndiye anafanya kila kitu, ye ye ndiye apige kaputi, Daktari mmoja!

Mheshimiwa Spika, aliniletea kilio akasema mama mnatuua, tumeboresha hospitali, tumejenga *theatre*,

tumeweka vifaa tena vya kisasa, vingine tumekuta vimesimama havifanyi kazi kwa sababu, hata wa kuviwasha na kuendesha hiyo mitambo hawapo. Nimekuta baadhi ya mashine hata kujua *pass word* ikoje mtaalam anasema hajui. Kwa hiyo, nashauri kama alivyosema Waziri wa Utumishi asubuhi kwamba, kipaumbele ni kupeleka watumishi katika zahanati mpya na katika vituo vya afya. Hapa nashauri hivi vituo vya afya 350 walivyoviboresha Serikali yetu ya CCM, naomba na vyenyewe vipewe umuhimu wa kwanza kwa sababu, bila ya kufanya hivyo itakuwa ni sawasawa na kazi bure, wagonjwa watakwenda pale hakuna huduma, hakuna wataalam na kazi ambayo tumeifanya itaishia kwa kweli, kuwa sio nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba niongezee kwamba, kama ambavyo amesema mchangiaji Mheshimiwa Maige na Mkoa wa Mara pia ni mlongoni mwa watu ambao wanafanya kazi sana. Sisi Mkoa wa Mara tunajenga majengo ya Serikali na huduma za jamii kwa kitu kinaitwa *lisagha*, yaani watu wa rika, umri wa kwangu tunapewa boma letu, umri wa mwingine wanapewa boma lao tunajenga kuanzia msingi mpaka lenta bila kutegemea msaada wa Serikali. Tumejenga maboma ya zahanati zaidi ya 100, tumejenga vituo vya afya zaidi ya 100, tumejenga sekondari zaidi ya 100... (*Makofi*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, tunaomba hivi Serikali ikijaribu kutenga fedha kukamilisha haya majengo, ili kuunga mkono nguvu za wananchi ambao sasahivi wameishiwa, naleta ombi maalum; kengele ya kwanza hiyo...

**SPIKA:** Tayari muda wako umekwisha.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Hivi tayari?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Amina Makilagi. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Joseph Mbilinyi atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kwa unyeyekevu kabisa nianze kwa kumpongeza...

**SPIKA:** Dakika 10 eeh.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, sawa na ahsante sana. Naomba nianze kwa kumpongeza sana *Chief Whip wa Opposition*, Mheshimiwa Tundu Antiphas Mughway Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki na Rais Mstaafu wa *Tanganyika Law Society – TLS*. Nampongeza kwa ziara zake za kimataifa kuelezea hali halisi ya kinachoendelea nchini kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lissu alimiminiwa risasi 38 na 16 ziliingia mwilini. Katika hali ya kawaida ilibidi alegee na kurudi nyuma, lakini pamoja na kwamba, bado yuko kwenye matibabu amechukua jukumu la kuzunguka na kupaza sauti ili dunia ijue kwamba... (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi walikuwa wanaauliza ukurasa wa ngapi wa taarifa?

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, kama wao wanavyoanza na pongezi tu kwa mtukufu. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, muda wangu. Kwa hiyo, kwa mtu ambaye risasi 16 zimeingia ambaye alitakiwa alegee, lakini amenyanyuka na anazunguka kuilezea dunia kwamba, Tanzania, Tanzania ambayo ilikuwa ni kitovu cha amani Kusini mwa Jangwa la Sahara, hivi sasa imekuwa ni *authoritarian regime*. Tuelewane kitu kimoja, Serikali siyo Taifa kuikosoa Serikali siyo kulichafua Taifa na kuikosoa Serikali siyo kuitukana Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye hoja, kwanza naunga mkono ripoti ya Kamati yetu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Nianze na habari na utawala bora. Kwanza Mungu atuondolee kabisa balaa la pepo la kuongeza muda wa utawala, ni tabia na mawazo ya kidikteta moja kwa moja, iwe kwenye Ubunge au kwenye Urais. Maana naona hii *trend* mlanza kama utani lakini sasa hili mnakuwa *serious*, naamini mnahitaji maombi na tutapiga magoti tuwaombee ili msiliingize Taifa huko mnakotaka kulipeleka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niwapongeze CCM Habari kwa kumilikishwa *Chanel Ten* na *Magic FM*. Naamini kwa hatua hii sasa mtaiacha *TBC* ibaki kuwa TV ya umma.

## T A A R I F A

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi, kuna taarifa, Mheshimiwa Keissy nilikuona.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nampa taarifa Mbunge wa Mbeya Mjini, Mheshimiwa Sugu tukiwa kule kantini mwenyewe alisema Mheshimiwa Keissy jitahidi tuongeze hata miaka kumi. Sasa nashangaa hapa anakuja kulidanganya Bunge, aombe radhi Bunge. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Anakukumbusha yale ambayo mlikuwa mnanong'ona Mheshimiwa Mbilinyi, unaipokea taarifa?

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, siipokei taarifa yake, *actually* alichoniambia Keissy ni kwamba anataka ni m-support hoja yake ya kutaka bangi iruhusiwe na nimemkatalia na hii anayo toka Bunge lililopita. Kwa hiyo, hiyo taarifa yake siichukui. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza CCM kwa kukabidhiwa *Channel Ten* na *Magic FM*. Sijui mmepewaa, mmenunua na kwa utaratibu gani kwa sababu najua makampuni yanapouzwa upo utaratibu lakini tumeona tu ghafla watu wanakabidhiwa vyombo vya habari. Tunaamini sasa mtaimba *TBC* ibaki kuwa TV ya umma ili mbaki na vyombo vyenu ambavyo mnavyo hivi sasa, muiache *TBC* kuwa televisheni ya umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimemuona Mwenyekiti wa Taifa katoa shilingi milioni 200 kuboresha *Channel Ten* na *Magic FM*, wananchi wa Mbeya Mjini wanani pigia wanasema Mheshimiwa hizo fedha shilingi milioni 200 zilizotoka ni fedha za CCM, fedha za Serikali Hazina au zinatoka wapi? Tunavyofahamu Mwenyekiti wa CCM Taifa kazi yake ya Urais mshahara wake ni shilingi milioni 9 tu. Sasa wananchi wanajiuliza anatoa wapi mamilioni anayoyagawa kila sehemu anakopita wakati mchahara wake Rais mnyonge ni shilingi milioni 9 tu. (*Makofi*)

## TAARIFA

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Pokea taarifa Mheshimiwa Mbilinyi, lakini pia uwe unaangalia sana masuala ya takwimu, huo mshahara unaoutangaza huo nikikuambia uthibitishe utatoka jasho. Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba siku ambayo Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa alikuwa anafanya shughuli hizo za kutoa hela katika vituo vile ni siku ambayo

ilikuwa ni ya maadhimisho ya Chama cha Mapunduzi kutimiza miaka 42. Nataka nimwambie kwamba CCM ni moja ya chama chenye hela nyingi sana kuliko vyama vyote dunia.

Mheshimiwa Spika, pia akumbuke kwamba siku hiyo ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi alikuwa anashughulika na mambo yake siyo Rais, Rais ana kofia mbili. Siku ile ametumia ruzuku ya chama, tuna ruzuku zaidi ya shilingi milioni 200. Kwa hiyo, nataka kumwambia sisi tuna hela nyingi sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Taarifa hiyo Bwana, unaamini CCM haiwezi kuwa na shilingi milioni 200.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, wallsema ni Rais katoa, kwa hiyo, kama ni Mwenyekiti ndiyo mnanipa taarifa basi naelewa sasa kumbe ni hela za Chama cha Mapinduzi na siyo hela za mtu binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye afya, ripoti inaonyesha kwamba rufaa za nje zimepungua kutoka 114 takribani kwa mwaka mpaka 38. Kwangu mimi na nilivyofuatilia kwenye Kamati hii siyo *success story* kwa sababu watu wanakufa sana. Hivi sasa Madaktari wanaogopa kutoa rufaa kwa sababu ya kuangalia mtazamo wa kisiasa unataka nini kwamba hatutaki kupeleka watu nje. Lazima tukubali kwamba hatuna mabigwa wala hatuna vifaa vya kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *sometime*, narudia tena *sametime* Muhibili pale nimekaa zaidi ya mwezi mmoja na nusu hata mtungi wa gesi *oxygen* inabidi ibadilishwe yaani kuna mgonjwa hapa amelala, amewekewa mtungi, mgonjwa mwingine kule anataka kuwekewa mtungi inabidi watu wamkatie *nurse* ili mtungi uhamishwe wanasema huyu amepumua kidogo tutamletea tena baadaye. Kwa hiyo, katika hali kama hiyo huwezi....

## T A A R I F A

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Mbilinyi, Waziri wa Afya amesimama.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, muda wangu lakini.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge wa Mbeya Mjini kwamba Serikali imeongeza uwekezaji mkubwa katika huduma za matibabu ya kibigwa. Wewe mwenyewe ni shahidi kwamba sasa hivi ukienda Muhimbili tumeweza kuongeza vifaa na vifaatiba. Jakaya Kikwete sasa hivi ametoka kufanya operesheni za moyo kutoka mia moja mpaka mia nne. Kwa hiyo, anayoyasema siyo sahihi anasema uwongo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Pokea hiyo taarifa Mheshimiwa Mbilinyi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anafahamu vizuri ana *struggle* na hapa tunachofanya ni kumsaidia kwa sababu ye ye hawesi kutamka haya tunayotamka atatumbuliwa. *It is not about you Madam Minister it is about the Nation*, hatukusaidii wewe tunalisaidia Taifa hapa, hakuna vifaa na wataalam wa kutosha, watu wakufa.

**MHE. ANTHONY C. KOMU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sugu naona Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia amesimama anataka kukupa taarifa. Naona ameamua kuachia, Mheshimiwa Mbunge wa Moshi Vijijini. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. ANTHONY C. KOMU:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge anayezungumza ili imsaидie katika jambo analolizungumzia. Wiki iliyopita niliomba ruhusa ya kwenda Dar es Salaam kwa sababu nina tatizo la jicho la kulia, nikaenda Muhimbili, nikatakiwa kufanyiwa kipimo fulani cha jicho, ikashindikana Muhimbili nikapewa rufaa kwenda Hindumandal na pale nikafanyiwa kipimo hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hali anayoizungumza Mheshimiwa Sugu ilinipata mimi mwenyewe. Naomba kumpa hiyo taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Hindumandal ni India?

**SPIKA:** Wanauliza hicho kipimo kilichokosekana kinaitwaje?

**MHE. ANTHONY C. KOMU:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu mimi siyo mtaalam kesho asubuhi nitawasilisha hizo nyaraka kwako.

**SPIKA:** Jamani mnakula muda wa Mheshimiwa Mbilinyi, Mheshimiwa Mbilinyi kengele ya kwanza imelia sasa jitahidi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** *No, no, no!* Mheshimiwa Spika, *that is not fair.*

**SPIKA:** Nakulindia muda wako vizuri kabisa wala usiwe na wasiwasi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, nilindie muda wangu vinginevyo sasa mimi katika hili Bunge nitakuwa sichangii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, haya mambo tunaongea tuko *serious*, kama Mzee Kingunge angepelekwa nje kutibiwa pengine leo hii tungekuwa na Mzee Kingunge. Huwezi kumweka Mzee Kingunge mwezi mzima hospitali ya rufaa,

ukishamweka wiki moja hajapata nafuu ujue kuna tatizo mpeleke kwenye weledi wa juu zaidi. Mpaka leo mnashindwaje kumpeleka Mheshimiwa Salim Mohamed Salim, Waziri Mkuu Mstaifu, Makamu wa Pili wa Rais, unashindwaje kumpeleka kutibiwa nje pamoja na wananchi wengine wenye mahitaji? (*Makofii*)

## T A A R I F A

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi, samahani nimemuona Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa mzungumzaji ambaye anaendelea kuongea kwa sababu baadhi ya mambo ambayo anayasema kwa kweli katika Bunge lako hili Tukufu ni vyema watu wakawa na uhakika wa kile anachokisema.

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza ambalo aliligusia kwamba Hospitali ya Taifa Muhimbili haina mitungi wa *oxygen* wagonjwa wote ambao tumelaza pale wanapokezana mitungi michache, taarifa hizo siyo za kweli. Sisi pale Muhimbili tuna mtambo wa kuzalisha *oxygen* na kusambaza ambao hauhitaji hiyo mtungi mojamoja kwa ajili ya kuwapatia wagonjwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili hili analoliongelea sasa rufaa kwa wagonjwa, naomba tuwapongeze watu wetu wa huduma ya afya wanajitahidi. Sasa hivi tumeweza kufanya matibabu ya kibingwa tunapandikiza figo na wagonjwa wote wako hai mpaka sasa hivi; tunapandikiza vifaa vya usikivu, watoto wote ambao walikuwa wawe viziwi zaidi ya 20 sasa hivi wanaskia na mwaka huu tunaanza kupandikiza *bone marrow* mpaka ini. Naomba mtupongeze kwa kazi kubwa ambayo tunaendelea kuifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kigezo cha mgonjwa kukaa siku moja, mbili au tatu, siyo kielelezo kwamba mgonjwa akikaa baada ya wiki moja anahitaji rufaa. Rufaa inaandikwa pale Madaktari wetu watakapothibitisha kwamba mgonjwa huyu Madaktari wetu wa ndani hawawezi kumtibu na hawa wagonjwa Madaktari wetu wana uwezo mkubwa sana tuwape moyo. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mbilinyi, taarifa hiyo.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, niwaombe sana hawa wanaosimama kutoa taarifa, hii nchi siyo ya baba yao wala hili Bunge siyo la mama yao, hili Bunge ni la Taifa na hapa tunajadili suala la Taifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi, nakuomba sana *withdraw* hayo uliyoyasema.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Kabisa.

**SPIKA:** Kwa Wabunge wenzako, ndugu zako na Waheshimiwa wenzako.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu tunaheshimiana *I am withdrawing this* lakini ujumbe umesafika, habari ndiyo hiyo.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Muda wangu haujaisha hata kengele ya pili katika mustakabali wako haujaisha Mheshimiwa.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja hizi za Wenyeviti watatu. Kwanza kabisa, nianze kuwapongeza Wenyeviti wote wa Kamati tatu ambazo wamewasilisha taarifa zao hapa Bungeni. Pia nitoe pungezi nyngi sana kwa Mheshimiwa Rais wetu John Pombe Magufuli na kwa Mawaziri wote ambao Wizara zao ziko kwenye hizi Kamati kwa kazi nzuri sana ambazo wamekuwa wakizifanya na kwa kweli wanaitendea haki nchi yetu na Chama chetu cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba niipongeze Serikali kwa utoaji wa pesa kwa ajili ya Hospitali za Wilaya 67. Kwa kweli pesa hizi hata katika Mkoa wetu tumepata Iringa DC, Kilolo na Mufindi lakini naomba nitoe ombi maalum. Katika Mkoa wetu wa Iringa tunayo hospitali ambayo ipo katika Manispaa yetu, Hospitali ya Frelimo, Iringa Mjini ambayo iliazishwa mwaka 2013, naomba Serikali yetu iwapatie pesa kwa sababu kabla ya hizi pesa hazijaenda kujenga hospitali za wilaya hizi nilizozitaja wagonjwa wanatibowi katika hospitali hii. Kwa hiyo, naomba Serikali ingeangalia kama kuna uwezekano wa kuhakikisha kwamba hizi hospitali ambazo zinafanya kazi basi zipewe kipaumbele. Hii hospitali ingejengewa wodi za akina mama, akina baba na watoto ingeweza kusaidia hata kupunguza msongamano mkubwa ambao upo katika hospitali yetu ya mkoa. Vilevile ingeweza kujengewa hata jengo la vipimo ambalo kwa kweli imekuwa ni tatizo. Kwa hiyo, niombe ombi maalum kwamba sasa hivi tumalizie hizi hospitali ambazo zipo na tayari zimeanza kusaidia maana hospitali hii imesaidia kupunguza vifo vya akina mama na watoto katika Mkoa wetu wa Iringa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna changamoto kubwa sana katika Hospitali ya Mkoa, kuna mwingiliano katika Hospitali ya Mkoa na katika Gereza la Mkoa. Mwingiliano huo kwa kweli ni mkubwa sana kwa sababu kuna wakati ambapo barabara zinafungwa, wagonjwa wanashindwa kupelekwa hospitali wakati wanapeleka wafungwa kwenye gereza. Kwa hiyo, naomba kipaumbele kitolewe kwa

sababu bale wanashindwa hata kuongeza majengo kwa ajili ya Hospitali yetu ya Mkao ambayo Serikali yetu sasa hivi imesema hizi hospitali za Mikoa zitakuwa za rufaa na zingeweza kusaidia sana katika Mkao wetu wa Iringa na Nyanda za Juu kwa suala zima la matibabu. Katika Hospitali ya Mkao hakuna nyumba za Madaktari Bigwa, kwa hiyo, wananchi wanapata shida sana, hili ni ombi maalum.

Mheshimiwa Spika, nimwombe tu kaka yetu Mheshimiwa Sugu kwenye Wizara ya Afya kazi kubwa imefanyika. Kuna vingine ambavyo Wapinzani mnatakiwa muunge mkono. Nishukuru safari hii mengi mnayaunga mkono na iwe hivyo kwa sababu ni kwa nia nzuri kabisa Serikali yetu inafanya kazi hizo. Nimpongeze Mheshimiwa Tulia anafanya kazi nzuri sana, amewatendea haki sana wananchi wa Mbeya, kwa kweli hongera zako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukienda ukurasa wa 37 na 38 wa Kamati ya Huduma za Jamii, naomba niunge mkono kabisa ushauri wa Kamati hii wa kuiwezesha Idara ya Maendeleo ya Jamii. Idara hii mara nyingi imekuwa haipatiwi pesa za kutosha na ndiyo ambayo inasaidia jamii na sasa hivi tuna tatizo kubwa sana la watoto kubakwa na vifo vyta watoto.

Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kujua Benki yetu ya Wanawake imefikia wa wapi, kwa sababu najua idara hii ipo chini yake. Kuna wakati kulikuwa na sintofahamu kwamba na yenyeche imetangazwa na Benki Kuu hata akina mama sasa wameingia wasiwasi kwamba hii benki sasa inawasaidiaje wanawake? Benki hii tulikuwa tunajua ndiyo suluhisho la akina mama kwamba hatupati zile shida za benki nyingine ambazo zimekuwa zikituzalilisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nielezee pia kuhusu bima ya afya. Niombe katika bima ya afya kuna ile *package* ya Sh.1,500,000 ambapo huduma anapata baba, mama na watoto wanne lakini utakuta kina mama wengi au familia sasa hivi ile *package* hawasaidii kwa sababu watoto wakiwa juu ya miaka 18 hawatibowi. Nashauri ingekuwa vizuri ikawepo na *package* ya mtu mmoja pengine iwe Sh.500,000 ili kama

watoto wangu wameshafikisha miaka 18 niweze kumkatia bima yake ama kama nina mzazi wangu basi niweze kumkatia bima yake au mama mwingine ni mjane, wababa wengine ni wagane inakuwa haina maana kuchukua *package* nzima. Kwa hiyo, naomba suala hili lingeangaliwa ili kuweza kusaidia wananchi ambao wanahitaji bima kwa ile *package* ya juu kwa maana ya *grade one*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niendelee kuchangia kuhusu ukarabati wa shule zetu za msingi. Kwa kweli hili ni tatizo kubwa sana. Katika Mkoa wetu wa Iringa shule nyingi sana za msingi ni za siku nyingi sana. Kwanza nipongeze Serikali kwa ukarabati shule kongwe za sekondari, Ifunda imetuhusu, shule nyingi kweli zimekarabatiwa, kwa kweli nipongeze.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe hizi shule za msingi kwa sababu katika hal mashauri zetu bado hakuna uwezo wa kuzikarabati. Mara nyingi tumekuwa tukianza kujenga madarasa kwa ajili ya hii elimu bure, kwanza nimpongeze Rais kwa elimu bure katika Mkoa wa Iringa, lakini kuna tatizo ambalo limejitokeza kutokana na ukongwe wa hizi shule za msingi basi vyoo ndiyo haviingiliki kabisa. Watoto wetu sasa wamepata hata tatizo la kubakwa sababu mojawapo ni kwamba wanakwenda kuomba kujisaidia kwenye vyoo vya jirani na shule hazina uzio. Kwa hiyo, naomba Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi iangalie kabisa hizi shule za msing kwa sababu ni tatizo kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kuhusu *capitation fund*. Wanapotoa hii *fund* wanaangalia idadi ya watoto lakini hawaagalii matatizo yaliyopo. Kwa mfano, sasa hivi shule nyingi sana wanashindwa kulipia maji, umeme na zile gharama ndogo ndogo. Kwa hiyo, kuna zile shule ambazo idadi ya watoto siyo wengi lakini wanatakiwa kugharamia huduma hizo nilizosisema, nashauri labda wangeangalia jinsi ya kuwa na mfumo mwingine.

Mheshimiwa Spika, utakuta shule zetu hizi za msingi wamekatiwe maji hivyo watoto wanapata shida sana. Kwa sababu sasa hivi ni elimu bure pengine tungewaacha watoto wasikatiwe maji kwani wamekuwa wakipata matatizo sana mfano kunapokuwa na magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu. Kwa kweli shule nyingi za msingi hata za sekondari hazina maji labda tungeangalia mfumo mwingine mzuri wa kusaidia shule hizo ili wasikatiwe maji bali shule iendelee kudaiwa au Serikali iangalie njia nzuri zaidi ya kusaidia hizi shule zetu za msingi ili kuondokana na changamoto hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nielezee kuhusiana na timu zetu ambazo zinazocheza daraja la kwanza hasa za wanawake. Kwa mfano, pale Iringa kuna timu ya Panama inashiriki hili kombe kwenye mazingira magumu sana. Nafikiri nillishamwambia hata Waziri tuone tunawasaidiaje hawa watoto wa kike na pale kuna vipaji vikubwa sana lakini utakuta wanashindwa kwenda kushiriki sehemu nyingine au wanakwenda kwa shida au wanatembeza mabakuli kiasi kwamba hawa watoto wakike wanaweza kupata masharti mengine. Naomba Wizara ya Michezo ingalie njia nzuri ya kusaidia hizi timu za wanawake ambao wanashiriki ligi kuu ya daraja la kwanza kwa sababu najua pale ndiyo tutapata vipaji vyta kuunda timu ya Taifa kutoka kwenye mikoa mingine. (*Makof*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa twende mkono wangu wa kushoto, Mheshimiwa Rehema Migilla atafuatiwa na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika dakika tano, tano.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi jioni hii nichangie kuhusu mawasilisho ya hizi Kamati tatu. Jambo la kwanza, napenda nimshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kutuwezesha jioni hii kuwepo mahali hapa kwani bila yeze sisi hatuwezi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jioni ya leo, napenda kuchangia mada zifuatazo. Suala la kwanza ni kuhusu uhaba wa vyumba vya madarasa. Hivi karibuni yalitoka matokeo ya darasa la saba hali iliyopekelea kuonekana ufaulu umekuwa mkubwa ambao hauendani na sambamba na vyumba vya madarasa. Hali hii ilipelekea watoto wengi kukosa vyumba madarasa na hatimaye wengine wakaanza kusoma wengine wamechelewa kuanza kusoma. Hali hii inakatisha tamaa wazazi hata na watoto wenyewe kwa sababu wanaona wenzao wameanza kusoma wengine hawajaanza kusoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali ili kuweza kumaliza hili tatizo ni vyema basi wafikie mahali pa kutumia takwimu kutoka kwenye Halmashauri zetu hususani takwimu ambazo ni maoteo ya watu wanaomaliza shulenii. Wakiweza kutumia hizi takwimu za maoteo watajua upungufu upo kiasi gani na mahitaji kiasi, watakapojua hivyo wataweza kuwasadia kama ni wadau wa elimu, wazazi, walezi ili kujumuika ku-cover ule upungufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine nataka niongelee kuhusu utitiri wa kodi uliokithiri katika Halmashauri zetu. Ni ukweli usiopingika kwamba uhai wa Halmashauri yoyote unategemea makusanyo ya kodi lakini kodi hizi kwa sasa baada ya Serikali Kuu kuchukua vyanzo vingi vya mapato kutoka kwenye Halmashauri zetu, Halmashauri zimebakia hazina kitu hivyo zimebuni njia mbalimbali za kupata kodi. Matokeo yake kumekuwa kuna msururu wa kodi mkubwa sana ambapo wananchi maskini hawezikulipa. Matokeo yake wanatengeza njia za kusababisha kukwepa kodi au kutokulipa kodi bila shuruti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali iweze kutengeneza mazingira rafiki au elimu itolewe kwa hao wananchi ili waweze kulipa kodi bila shuruti kwa sababu tumeshuhudia, tumesikiliza kwenye taarifa ya habari tumeona Singida kule mauaji yametokeo, raia ameuwawa kwa risasi lakini raia huyu chanzo chake tumeambiwa alikwepa kodi. Kwa hiyo, niiombe Serikali ihakikishe kunakuwa na mazingira rafiki ya ulipaji wa kodi lakini pia na hawa watu wanaokusanya kodi wawe ni marafiki kwa walipa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine napenda kuzungumzia ukatili wa kijinsia. Ukatili wa kijinsia sasa hivi umekuwa mkubwa kupita kiasi ambapo wanafunzi wetu wanabakwa, wanalawitiwa na wanafanyiwa vitendo hivi na watu tu wenye akili zao timamu lakini hata huko shulen iwanafunzi kwa wanafunzi wanalawitiana. Kwa hiyo, niiombe sasa Wizara ya Elimu na TAMISEMI tuangalie tunamalizaje suala hili, kujenga mabweni mfano ya Ihungo Sekondari, yale majengo yakijengwa vizuri wanafunzi wataepuka kufanya vitendo vya ubakaji na kulawitiana. Nishauri tena wazazi tusipeleke shule watoto wenye umri mdogo kwa sababu ndio wanaoathirika kwa kuharibiwa na kaka zao. (*Makofi*)

Suala lingine ni upandaji madaraja kwa walimu. Walimu kwa sasa wamekosa *morale* ya kufanya kazi...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana, dakika tano zimekwisha. Tunaendelea na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, dakika tano, atafuatiwa na Mussa Zungu dakika tano.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Nitajikita kwenye Wizara ya Afya hususani Bima ya Afya (*NHIF*). Kwa kweli kila mtu anahitaji kuwa na afya nyema, Taifa lilitokuwa halina afya basi halina maendeleo wala halizalishi uchumi wala hatutazaana kwa haraka, naam! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Wizara ya Afya kuhusu bima wanasema mpaka sasa hivi wanaotumia bima ni 34% tu. Hicho ni kiasi kidogo, bado Serikali hajajipanga kutoa afya kwa wote. Watu wengi hawana bima ya afya na tuna maradhi mengi yanatusumbua kama vile kansa, kisukari na maradhi mengine. Kwa hiyo, Serikali ifanye kila jitihada kutumia bima ya afya na wale waliokuwa hawajajiunga wajunge. Wizara itoe elimu na ihamasiche ili watu wote wajunge kwenye bima ya afya ili wapate matibabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilipata fursa ya kwenda Rwanda ili kuona Bima ya Afya inavyofanya kazi ni tofauti wanavyofanya hapa kwetu. Kule tajiri, maskini wote wanapata fursa sawa za kutibiwa. Wao kule wanatibiwa kwa mfumo wa daraja, tajiri anatibiwa kwa daraja lake, mwenye kipato kikubwa anatibiwa kwa daraja lake na watu wa katika wa chini wana madaraja yao na wale waliokuwa na hali zao ni duni kabisa basi wanatibiwa bure wakiwamo hao maskini, watoto chini ya miaka mitano, walemavu pamoja na wajawazito. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisemi kwamba kwa nchi yetu wajawazito watibiwe bure, watibiwe kwa daraja, wale masikini kabisa ambao hawana hata hela ya kupanda daladala basi watibiwe bure. Tulikaa na Wizara ya Afya na wakasema watafanya mazungumzo ili kuleta Muswada hapa Bungeni tuweze kutunga sheria ya watu wote wapate fursa sawa ya kupata matibabu. Naiomba Serikali iharakishe kuleta Muswada huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie sasa masuala ya UKIMWI. Katika Mkoa huu wa Dodoma kuna asilimia kubwa ya maambukizi, kwanza ilikuwa 2.3% mpaka sasa hivi waathirika wamepanda imekuwa 5%. Je, Serikali inasemaje kuhusu Mkoa wa Dodoma? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi kama viongozi hapa Bima ya Afya wanatibu Mbunge na mweza wake na watoto wanenye. Hata hivyo, kuna Wabunge wengine humu hawana wenza,

hana mke na mwagine hana mume, kwa nini asitumie fursa hii kutibu wazazi wake? (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mgeni. Tunaendelea na Mheshimiwa Mussa Azza Zungu, dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Venance Mwomoto.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nichukue nafasi hii kuunga mkono hoja za Kamati zote tatu. Pili, niwapongeze Mawaziri wa Wizara zote tatu kwa kazi nzuri wanazofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza tena Waziri wa Michezo, takribani miezi minne nilitoa hoja kuhusu Uwanja wa Taifa kutokuwa na sehemu ya kivuli kama mvua zitanyesha. *Immediately* kazi inafaywa na nafikiri mechi ya tarehe 16 watu tunaokaa katika maeneo yale hata ikija mvua tutakuwa tunasheherekea ushindi wa timu yoyote itakayojaliwa na Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *FIFA* ina *standard* ya viwanja ndiyo maana inaleta fedha kutengeneza viwanja katika miradi ya *FIFA*. Vipo viwanja vinachezewa *Premium League* vina hali mbaya sana, vinaharibu ubora na viwango. Mfano jana, kwa dhati kabisa nasema, Uwanja wa Singida ambapo jana *Club* za Yanga na Singida *United* wamecheza hauna sifa wa kuchezewa mashindano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimwa Waziri, najua *TFF* ni watu *independent* lakini ninyi ndiyo *custodian* na ndiyo mnasimamia viwango vya Watanzania. Timu ambazo zipo kwenye *Premium League* na viwanja vyao ni vibaya wahamishiwe viwanja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha sana jana kuona klabu kubwa kama *Dar Young Africans* inashindwa

kucheza kandanda yake. Naomba wanaohusika walione hili kwa sababu kwenye mpira kuna *formation*, kuna *diagonal attack*, *diagonal defence*, kama kiwanja kibaya, maana kama kule Mbondole kuna kiwanja ambapo kipa wa huku hamuoni kipa wa kule, wanaulizana vipi huko? (*Kicheko/Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Ngapi huko?

## T A A R I F A

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa nimekuona Mheshimwa tafadhali.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Spika, nitaka kumpa taarifa Mheshimiwa Zungu kwamba nimewahi kushuhudia mechii ya Ligi Daraja la Kwanza Morogoro mwaka fulani ambapo upande mmoja wa goli, golikipa akidondoka inabidi mumtafute kwanza ndiyo mpira uendelee. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Zungu.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, nafikiri Mheshimiwa Waziri amenielewa.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa umeipokea?

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Kwa Morogoro nimeipokea. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mchango wangu unajikita kwenye masuala ya viwanja ambavyo havina ubora, Serikali iingilie kati iambie *TFF* viwango vyatya wachezaji vinakufa...

## T A A R I F A

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Pokea taarifa Mheshimiwa Zungu.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba viwanja hivi vyote vinapitishwa na *TFF* na huwa kuna timu ya Wakaguzi. Kwa hiyo, Kiwanja cha Singida nacho kimekaguliwa. (*Makofii*)

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, hata usinihoji, sipokei taarifa yake. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, viwanja hivi ndiyo vinatoa ubora wa wachezaji wa Timu ya Taifa, viwanja vibovu vyote pamoja na cha Singida na viwanja vingine vyta timu zinazoshiriki *Premium League* kama Mkwakkani Tanga, vilabu vile vihamishiwe kwenye viwanja vingine ili ubora na viwango vyta mpira viweze kupatikana Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nimeshakutaja Mheshimwa Venance Mwamoto, dakika 10.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati zote waliowasilisha taarifa zao na hasa Mheshimiwa Jasson Rweikiza ambaye ni Mwenyekiti wangu wa Kamati. Pia niipongeze Serikali kwa ujumla wake kwa kazi kubwa ambayo imefanyika kwa kipindi hiki cha miaka mitatu. Najua kuna changamoto ambazo sisi inabidi tuzifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, kwanza tulikuwa na upungufu mkubwa sana wa madarasa na vituo vyta afya, zahanati pamoja na hospitali lakini Serikali kwa kujua hilo ilianza kupambana na changamoto hiyo. Changamoto kubwa ilikuwa ni majengo na sehemu kubwa majengo yamejengwa. Kwa hiyo, changamoto kubwa sasa ni upungufu wa wauguzi, walimu na kadhalika ambayo inaweza kutibika.

Mheshimiwa Spika, kwa huwa Serikali imesomesha kwenye vyuo vyetu vijana wengi kabisa na hawana shughuli

na Serikali imewakopesha, kitu ambacho naishauri Serikali wapo ambao wapo tayari kujitolea, kwa nini Serikali isikubali vijana wale badala ya kukaa wakajitolea wakafanya kazi zile kupunguza upungufu wa wauguzi na walimu kwa miaka angalau miwili na shule zetu zote zingekuwa hamna upungufu sijui kuna kigugumizi gani? Pia wale ambao watafanya vizuri maana wanadaiwa na Serikali baadhi ya fedha zikapunguzwa kwenye mikopo yao ili waweze kufanya kazi kwa kujitolea na wengi wapo tayari. Naomba hilo Serikali ilichukue na ilifanyiele kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni hili la *TARURA*. Tulipitisha wenyewe hapa Bungeni Muswada wa *TARURA* lakini leo tumeshaanza kugeuka kwa kuanza kusema Meneja wale waende wakaripoti kwenye Baraza la Madiwani. Nafikiri kikubwa tungeangalia changamoto lakini kazi inayofanyika ni kubwa, kama sisi Wabunge tutapitisha fedha kwa maana ya mgao, maana mgao uliopo sasa hivi ni 70 kwa 30, tukawaongozea *TARURA* kelele zitakuwa hazipo. Kama ilivyo *TANROADS* wanafanya kazi vizuri, ukiwaingiza kwa Madiwani au Wabunge inakuwa ni mfumo wa kisiasa, kila mmoja atataka barabara yake ijengwe hata kama ni kilomita 2 lakini unapowaachia huru, wanatoa tu taarifa kazi zitakwenda. Nafikiri tujikite zaidi kuona tunawaongezea ngapi ili kazi ifanyike kwa sababu sisi wenyewe tulipitisha kwa kuangalia changamoto nyingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, asubuhi niliuliza swalii kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na alinijibu vizuri sana. Nafikiri kuna haja Waziri wa Fedha mkawaongezea fedha wenzetu wa Wizara ya Michezo ili suala hilli lipewe umuhimu. Kama nilivyosema asubuhi, sidhani hata baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hapa wana ulewa mzuri, michezo ya *AFCON* ni michezo ya Afrika nzima *under 17* inafanyika Tanzania na hakuna matangazo ya kutosha ambayo yameshatolewa kuwapa watu uelewa waweze kuchangia pato la nchi ili fedha hizo siende kufanya kazi mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumenunua ndege ndiyo ulikuwa wakati wa kutangaza wa ndege zile hata ikiwezekana

Meneja wa Shirika la Ndege akasema kwamba kwa wale wataokwenda kuangalia michezo kutoka Iringa na sehemu nyingine watapata pungozo wakati wa mechi wakikata tiketi mapema, fedha zile zingeongezwa kwenye uchumi wetu. Rais wa *FIFA* atakuwepo hapa na kundi kubwa kabisa la watu kutoka nje ilikuwa ndiyo wakati mzuri wa kutangaza utalii wa nchi yetu na wao wakitoka hapa wangeweza kuwa Mabalozi wazuri wakatutangazia nchi yetu huko nje ili tuingize pato kwenye utalii. Nafikiri hili ni suala na Mheshimiwa Waziri wa Michezo na Waziri wa Maliasili kuangalia wanafanyaje ili kuhakikisha tunatangaza vizuri mashindano haya na kutuingizia pato kwenye nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa ni suala ambalo pia limezungumzwa na watu wengi. Mwaka jana tulikuwa na tatizo kubwa sana la mlundikano wa wanafunzi waliofaulu, ikabidi tuanze mchakamchaka kwa ajili ya kujenga madarasa, mwaka huu tatizo liko palepale. Nafikiri kuna tatizo labda kwenye takwimu au la wataalam wengine. Kwa sababu hivi leo watakaomiliza mwaka huu mwishoni idadi tunayo, kwa nini tunangoja kuja kuanza kufanya mchakamchaka wakati tunaweza tukatatua jambo hilo mapema? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niishauri Serikali kwamba kama ni kwenye bajeti liingizwe ama lishughulikiwe kwa njia yoyote lakini mapema siyo kama sasa hivi kuna wanafunzi ambao hawatakwenda shule wanesubiri mpaka mwezi wa pili, tatu, madarasa yajengwe ndipo waende, nafikiri hapo kuna tatizo. Niombe Mawaziri wafanye kazi kwa nguvu zote na kushirikiana badala ya kufanya kazi ya zimamoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nisingependa kusema mambo mengi, niunge mkono hoja kwa asilimia 100. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Mussa Mbarouk dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Jerome Bwanausi.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia afya njema tukaweza kuzungumza masuala mbalimbali ya nchi yetu. Pili, asubuhi wakati Mheshimiwa Baba Paroko Joseph Selasini akizungumza hapa kuna maneno aliyasema, niongezee kidogo katika yale aliyoyasema, nimuombe Rais wetu msikivu, kwa heshima na taadhima, haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kupitia kwa DPP wetu ambaye ana dhamana basi waweze kuwapatia dhamana Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao tumewakosa katika Bunge hili; Mheshimiwa Freeman Mbewe na Mheshimiwa Esther Matiko ili Bunge Ijalo tuweze kujumuika nao. Pili, kupitia nafasi hiyohiyo, nimwombe tena Mheshimiwa Rais wale Mashekhe wetu ambao hawajapata dhamana mpaka leo nao wapatiwe dhamana ili waweze kuhudumia jamii yetu katika huduma za kiroho. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine niipongeze TAMISEMI kwa kumaliza mgogoro wetu wa Hospitali ya Wilaya kule Tanga ambapo sasa ujenzi unaendelea. Vilevile pia nishukuru kwa Vituo vyetu vya Afya vya Makorora, Mikanjuni na Ngamiani navyo kwa kupatiwa fedha takribani shilingi bilioni 1.4 na hali inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwenye mchango wangu nizungumzie Serikali za Mitaa. Najua tunazo Serikali za namna mbili, tuna *Central Government* (Serikali Kuu) na tuna *Local Government* ambazo ni Serikali zetu za Kienyeji au Serikali za Mitaa. Mimi nilikuwa najua kazi ya Serikali za Mitaa kwanza ni kukusanya kodi, kutoa huduma bila ya kusahau kutengeneza ajira kwa wananchi wa eneo husika. Hata hivyo, sasa hivi Serikali zetu za Mitaa zimepokonywa vyanzo vya mapato kama *property tax* hata mabango ya biashara, imekwenda sasa wananyang'anywa mpaka uwakala wa barabara za vumbi, ukarabati na ujenzi wa mifereji lakini hata huduma za taa za barabarani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu shughuli hizi sasa zinapelekwa *TARURA* (Wakala wa Barabara) basi TAMISEMI ingefanya utaratibu ufuatao; hizo gharama za usafi wa mifereji na taa za barabarani nazo zingepelekwa *TARURA* ili kuzipunguzia Halmashauri zetu mzigo. Kwa sababu Halmashauri zinafanya shughuli kubwa sana, zinashughulika na masuala ya afya, elimu na masuala mengine ya huduma za kijamii. Kwa hiyo, naishauri Serikali kwamba *TARURA* ibebe mzigo wa huduma za usafi wa mifereji na taa za barabani lakini *enough is enough* hivi vyanzo vya mapato vya Halmashauri visichukuliwe vingine.

Mheshimiwa Spika, hata hili suala la uvuvi, Halmashauri zinapokea mapato katika uvuvi kutokana na ushuru wa samaki. Kwa bahati mbaya sasa katika hiyo operesheni, kumekuwa na tatizo kwamba wavuvi wanapokamatwa na nyavu ambazo haziruhusiwi wanatozwa faini mpaka shilingi milioni 2 kwa nyavu moja lakini cha kushangaza, nina mfano wa risiti hapa ambazo wametozwa wavuvi, navyojua mapato ya Serikali sasa hivi yanakusanywa kwa *EFD machine*, hizo risiti ukizitazama zimeandikwa kwa mkono. Nina mashaka inawezekana mapato haya yakavuja na ikawa ni mianya hii ya kutengeneza masuala ya rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nalotaka kulizungumza ni kwenye uteuzi wa Wakurugenzi. Baadhi ya Wakurugenzi siyo wote wamekuwa wababe na wakati mwingine wanakuwa na kiburi. Nitoe mfano wa Mkurugenzi wa Jiji langu la Tanga, mimi upande mwingine ni Diwani wa kuchaguliwa katika Kata yangu lakini ameniandikia barua kwamba eti nimepoteza sifa ya kuwa Diwani kwa kukosa *Ward Council* sita. Naamini Mkurugenzi anajua Kanuni za Halmashauri, moja ya sifa za Diwani kupoteza sifa ni kutohudhuria vikao vitatu vya Mabaraza ya Madiwani (*Full Council*) bila taarifa siyo *Ward Council* sita. Nimeiandikia barua Wizara ya TAMISEMI lakini mpaka leo sijapata majibu. Vilevile Mkurugenzi hata kuniita labda akaniambia Bwana hili jambo ulilifanya kimakosa kwa sababu Kanuni hazisemi hivyo imeshindikana. Mimi niitake TAMISEMI kwanza inipe

majibu ya barua yangu lakini Wakurugenzi nao tuwasimamie waweze kutoa ushirikiano mzuri kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jerome Bwanausi, atafuatiwa na Mheshimiwa Mchungaji Msigwa na Mheshimiwa Ester Mmasi ajiandae.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba za hizi Kamati ambazo zimewasilishwa hapa. Nianze tu kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa jinsi anavyofanya kazi na kwa kweli ni mfano wa Marais bora katika Afrika ambao wanafanya kazi nzuri sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwenye afya, pongezi hizi ambazo nimempungeza Mheshimiwa Rais na sisi sote hapa pande zote mbili, upande wa Chama Tawala na wale wenzetu wa Upinzani ni mashahidi kwamba katika miaka ya nyuma hajjawahi kutokea tukaweza kutenga fedha kwa ajili ya hospitali 67 na vituo vya afya 350. Hii hajjawahi kutokea, tunahitaji kumpongeza Mheshimiwa Rais na Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri inayoifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kama walivyochangia wengine haya majengo tunayoyajenga, hospitali 67 na vituo vya afya 350, kama havikupata watumishi, kwa kweli vituo hivi vitabaki kama *white elephant*, yatabaki majengo ambayo hayana tija. Nisisitize sana wanaohusika na maandalizi ya kuwapata watumishi wa Idara ya Afya waweze kufanya jambo hili kwa haraka sana ili tuweze kupata tija katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, pia niiombe tu Serikali, sisi wa Mkoa wa Mtwara kuna ujenzi unaoendelea wa Hospitali ya Rufaa lakini unasuasua sana. Nipongeze kazi kubwa anayofanya Mheshimiwa Waziri Ummy na Naibu wake

ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Ndungulile, mnafanya kazi kubwa sana na wala hatuna mashaka na utendaji wenu wa kazi lakini naomba sana mlitupie macho suala la ujenzi wa Hospitali ya Rufaa pale Mtwara. Kwa sasa wananchi wa Mkoa wa Mtwara na Lindi wakihitaji kumpeleka mgonjwa katika Hospitali ya Rufaa wanawajibika kuja Dar es Salaam. Kwa hiyo, naomba sana hili jambo lipewe kipaumbele, najua Mheshimiwa Waziri atakapokuja kutoa mchango wake ataeleza kuhusu jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilitaka kusema, ni kweli huu utaratibu wa Serikali tuliouanzisha wa kuwaondoa watumishi kwa mfano wa kilimo, maji na ardhi na kuwapeleka kwenye Serikali Kuu ni mzuri. Jambo hili ni jema kwa sababu inawezekana likawa linasaidia kuweka udhibiti wa watumishi wetu. Hata hivyo, kwa maana ya uwakilishi (Madiwani na Wabunge), nikuballane na hoja na Mheshimiwa Mwamoto kwamba kweli tulipitisha hapa hizo sheria lakini kuna wakati mwingine unaweza ukakuta liko jambo ambalo lina umuhimu sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa wenyе kikao pale, nawaombeni sana.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, napendekeza Usirudishwe utaratibu wa zamani wa kwamba kila jambo linaongelewa kwenye Baraza lakini lazima kuwe na baadhi ya vikao hata kama ni kwa miezi sita au kwa mwaka ambavyo vitafanyika kwenye Halmashauri ambapo mchango wa Waheshimiwa Madiwani na Wabunge kuhusu barabara, maji na kilimo unaweza kupewa umuhimu. Kwa sababu kama wataachiwa tu watendaji peke yao wakafanya maamuzi sasa ule uwakilishi wa wananchi kutoka kwenye ngazi mbalimbali hautakuwa na maana kabisa. Kwa hiyo, hili naomba sana litazamwe Serikalini na tuone mfumo gani mzuri utakaosaidia kuhakikisha kwamba na wale wawakilishi wa wananchi wanapewa fursa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa pia suala la *TARURA* kwenye Kamati ya *TAMISEMI* na mimi naunga

mkono kabisa yote yaliyomo katika taarifa ya Kamati ile. Hata hivyo, kama *TARURA* haikupata fedha za kutosha, watu watakuja kusema afadhalii ya Halmashauri kuliko *TARURA*. Kwa hiyo, ni muhimu sana kwenye bajeti ijayo *TARURA* wapate fedha za kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo kubwa sana la barabara vijijiini na madaraja ambayo yanahitaji kujengwa lakini kwa fedha wanazopata *TARURA* hawawezi kujenga madaraja hayo kabisa. Kwa hiyo, ni vizuri sana *TARURA* iweze kupata fedha za kutosha ili washirikiane na *TANROADS* kuhakikisha kwamba suala la barabara na madaraja linapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni muhimu sana ni juu ya kuziwezesha Halmashauri zetu zijiendeshe zenyewe. Halli kwenye baadhi ya Halmashauri ni mbaya sana na nitatoa mfano wa Halmashauri yangu ya Wilaya ya Masasi na Halmashauri nyingi ambazo zaidi ya asilimia 80 ya mapato yake zinategemea kutokana na ushuru wa korosho, hali ni mbaya sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Madiwani hawajapata posho zao za mwezi sasa takribani miezi nane hata posho za vikao hazijatolewa na miradi mbalimbali hakuna kinachofanyika. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshalieleza kwamba Serikali ipo kwenye mpango sasa wa kuhakikisha kwamba ushuru wa korosho kwa ajili ya Halmashauri unapelekwa, kwa kweli fedha zile zinahitajika zipelekwe haraka sana ili kunusuru hali ya Halmashauri zetu ambazo hivi sana hali ni mbaya kuliko maelezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kusisitiza ni kwenye Kamati ya UKIMWI. Wafadhili wetu wamekuwa wakitusaidia sana kwenye eneo hili lakini baadhi ya wafadhili wetu wamekuwa wakijiondoa taratibu katika kuchangia kwenye janga hili la UKIMWI. Niiombe Serikali sasa ione uwezekano wa kuanza kutenga fedha zetu za ndani ili zisaidie katika kupambana na janga hili. Kama hatuwezi kutenga fedha zetu za ndani itatusumbua sana

mbele ya safari pale wafadhili wetu watakuwa wameachia kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kulinda muda wako, niunge mkono hoja za Kamati zote zilizowasilishwa, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jerome Bwanausi. Mheshimiwa Mchungaji Msigwa atafuatiwa na Ester Mmasi na Mheshimiwa Joel Mwaka ajiandae.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa hizi dakika tano. Mara nydingi tumeambiwa kwamba upande huu hatusifu, nianze sasa kwa kutoa sifa zifuatazo. Kwanza, nimshukuru sana Mheshimiwa Mkuchika alikuja akatoa Semina nzuri ya Maadili ya Utumishi wa Umma ambapo vijana wengi pale Iringa wallifurahia. Sijui nani watakaorithi kuendelea na utaratibu ambao Mheshimiwa Mkuchika aliufanya maana wafanyakazi wengi wallifurahia. Hayo ni mambo mema ambayo tunapenda yatokee katika nchi kwa sababu ni mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nimshukuru sana Waziri wa Afya na Naibu wake pale ambapo Mkuu wetu wa Mkoa ali-*demoralize spirit* ya watendaji kazi katika Manispaa ya Iringa, alim-*harass* sana Daktari wetu ambaye ni Bingwa ambao tumewasomesha vizuri, lakini walihakikisha yale mambo wameyaweka *calm* yakaenda vizuri na Daktari anaendelea vizuri. Hilo niwashukuru sana ni mambo mema mnayoyafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo napenda nishukuru tena katika Manispaa ya Iringa ni pale ambapo Mkuu wa Mkoa alivyofika tulikuwa na machinjio; Kamati ya LAAC walifika na waliona tuna machinjio nzuri sana, ilikwama kwa sehemu na wakaiona, wakatutia moyo. Ilipaswa iwe imeanzishwa miaka mitatu, minne iliyopita lakini kukawa na vikwazo vya kisiasa, wakatupa ushauri lakini kuna mambo mengi tuliviyotaka kuanza kulikuwa na taabu sana, Mkuu wa Mkoa kajiapiza kwamba akiwa yeye Mkuu wa Mkoa

hataruhusu hela yoyote ije. Niwashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo, jana Meya wangu wamesaini, Serikali imekubali ku-release shilingi bilioni 1 ambayo itasaidia kufanya hayo machinjio iweze kufanya kazi. Haya ni mambo mema ni lazima tupongeze na kama mwakilishi wa watu ni lazima niyapongeze. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niombe Wizara kama nilivyomsifu Mheshimiwa Mkuchika tufanye kazi kwa utaratibu na Maadili ya Umma kutokana na sheria inavyosema. Hawa Wakuu wa Mikoa wengine kwa kweli wanapagawa sana, hawamjali mtu ye yoyote. Naomba kama inawezekana kwa mujibu wa utaratibu Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa TAMISEMI, tuendelee kusaidiana, muendelee kuwalea hawa vijana wenye mihemko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, haya mambo ya kuwekaweka watu ndani ina-*demoralize* utendaji wa kazi. Lile wiki alilokuja Ndugu Hapi Iringa Mjini wafanyakazi wote walikuwa *down* lakini kwa sababu na mimi nilikuwa na misuli ya kutosha, nilihakikisha napandisha ile *morale* ya utendaji kazi ili turudi kwenye utendaji kazi na kufuata masharti ya utumishi wa umma. Watendaji hawa wateule, Wakuu wa Wilaya, wanatumia vibaya madaraka yao. Hili ni Taifa la wote, tunatakiwa tufuate taratibu, kanuni na miongozo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nilishamuona Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna Bwana mmoja alikuwa ni Mkurugenzi wetu aliondolewa Iringa kwa siasa, Iringa kuna siasa nyingi sana. Hata hivyo, tunafanya kazi kama nilivyosema tunaongoza kwa kukusanya mapato, tunaongoza kwa usafi na tunapata hatisafi mfululizo. Misingi hii aliyetuwekea ni Bwana mmoja anaitwa Ahmed Sawa, mmeenda kum-*dump* sijui wapi huko Mkoani kwa kosa ambalo hana. Watumishi kama hawa hata asiporudi Iringa mtafutieni sehemu nyingine afanye kazi kwa sababu ni mchapakazi, ni mbunifu, haya mambo tunayoyapata leo ni kwa sababu ya utendaji wake mzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana, nimeona nitoe haya kwa sababu mimi ni mwakilishi wa watu na watu wengine hawayajui, watu wengine wanaonewa sana katika nchi hii kwa makosa ambayo hawayajafanya.

Mheshimiwa Spika, Nikushukuru sana.

## T A A R I F A

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika taarifa.

**WABUNGE FULANI:** Kashamaliza.

**SPIKA:** Ndiyo Mheshimiwa.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, nilitaka nimpe taarifa tu Mheshimiwa Msigwa kwamba haya anayozungumza ya watumishi, Wilaya ya Chemba zaidi ya watumishi 30 wameomba kuhama kwa sababu ya aina ya uongozi kama huo ulioko Iringa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nafikiri ulishamaliza Mheshimiwa. (*Kicheko*)

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nilitaka nipokee tu taarifa yake kwamba haya matatizo ya Wakuu wa Wilaya na Mikoa yako maeneo mengi. Kwa hiyo, Waziri Mkuu na Serikali mnasikia, sisi Wabunge tunataka tufanye kazi na wateule wa Rais kwa kupendana siyo kwa kushindana. Mtu anakuja ametukuta pale tunafanya kazi, haya mambo hayakuzuka kuna watu walifanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Mmasi dakika 10 anaifuata Mheshimiwa Joel Mwaka dakika 10.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pia naungana na wenzangu wote ambao wamepongeza Kamati zote hizi tatu kwa kazi zao nzuri lakini pia na kwa ripoti ambazo ziko *well informed*.

Mheshimiwa Spika, nitapenda kujielekeza kwenye Kamati ya Huduma za Jamii na nitajikita kama kawaida kwenye masuala mazima ya uboreshaji wa elimu ama mfumo wa elimu ambao tunao. Ni dhahiri kwamba kumekuwa na jitihada mbalimbali katika kuinua fursa za elimu kwa watoto wetu. Jitihada hizi zinaonekana pale ambapo tunaona migomo mingi imepungua au imefutika katika elimu za juu lakini pia kero nyingi ambazo walikuwa nazo wazazi mathalani masuala ya ulipaji ada kwa elimu ya awali yameondoka. Watu wengi tumetoa pongezi hizi kwa Mheshimiwa Rais hasa tukitambua mchango wa Serikali unaoongozwa na Mawaziri wake na Naibu Waziri tunawapongezeni sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika nchi mbalimbali duniani kote lakini pia katika ulimwengu wa kwanza elimu inatumika kama nyenzo kuu katika kukuza uchumi na kupelekea maendeleo ya dhati kwa Taifa husika. Misingi hii ya ujenzi wa uchumi ni dhahiri kwamba katika nchi mbalimbali haifanani.

Mheshimiwa Spika, kwa nchi ya Tanzania uchumi wa sasa tunavyouangalia, tunajitahidi kuwekeza hata katika miundombinu ya elimu, tunajikita hasa kwenye *ku-promote* uchumi wa viwanda (*Industry Economy*), lakini pia katika Mataifa yaliyoendelea, wamehama katika mfumo huu wa kusukuma uchumi kupitia *Industry Economy* kwenda kwenye *knowledge economy*. (*Makof*)

**MBUNGE FULANI:** Safi sana.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Spika, tunapoongelea *knowledge economy* tunaangalia nchi ya Tanzania inavyowekeza nguvu nyingi katika kuinua uchumi mathalan ujenzi wa *Stiegler's Gorge*, uwekezaji wa anga na uwekezaji kwenye Bahari Kuu, uwekezaji wa utalii na masuala mengineyo, bado tunaona kuna kila sababu kwa nchi ya Tanzania kuona umuhimu wa *promote* au *ku-embrace knowledge economy* kwa maana ya kwamba elimu au mfumo wa elimu uinue zaidi masuala ya ujuzi na maarifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu bila kuoanisha muktadha huu vizuri ni dhahiri kwamba hatu nguvu zinazowekezwa na Serikali zitakosa mapokeo chanya kwa vijana ambao wanaandaliwa kwa mifumo ya elimu ambayo tuko nayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kwamba kuptitia ilani bado tuna maswali mengi ya kujibu kwenye masuala ya ajira. Ninapoongelea *knowledge economy* ni dhahiri kwamba vijana wetu watashiriki rasmi kwenye kuandaa ajira zao wenyewe, watatoka kwenye kusimama kwenye nafasi ya utazamaji na badala yake wataingia na kuwa *key players* katika kuandaa ajira zao wenyewe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tunapoongelea uchumi unaojengwa na maarifa pamoja na ujuzi, ni kwamba vijana wetu kama nilivyosema wanaweza wakajandalia ajira zao. Ukiangalia sasa na niliwahi kusoma kitabu cha Henry Mintzberg ambaye aliandika kitabu kimoja kizuri sana *MBA's But Not Managers* inaeleza vizuri masuala haya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi nimetoka Kilimanjaro na dada yangu Mheshimiwa Stella Ikupa ni shahidi, tulikwenda Kilimanjaro na maelekezo kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu tukitaka kuwatengenezea ajira vijana wetu; na kwa Mkoa wa Kilimanjaro tulipata fursa za kuwatengenezea ajira vijana 800 kila Wilaya. Tulikuwa tumeponga kuboresha ajira za vijana kuptitia kilimo kwa watoto mia moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dada Stella ni shahidi, lakini pia tunaye *Eng. Kahabi* ambaye ndio alikabidhiwa jukumu hili. Nilipita kila Wilaya, nilisikitika, hakuna *graduate* hata mmoja aliyeweza ku-*respond* kwenye mradi huo wa Serikali ambao wameweka fedha, wameweka wataalam katika kuwafundisha vijana katika kuingia rasmi kwenye Sekta ya Kilimo. Kilimanjaro tuna fursa nzuri sana ya kimasoko, tumeponga na Kenya, lakini wanafunzi hawajaandaliwa kwenda kuingia kwenye ushindani wa kibiashara, wanafunzi hawajaandaliwa kwenda kuandaa ajira zao au kushiriki kwenye ajira zisizo rasmi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuongelea changamoto ambazo pia nimezisikia zimeongelewa hapa asubuhi. Tunafahamu kwamba Serikali ilifuta Vyuo 19, nia na makusudi ni kuleta tija katika mfumo wa elimu. Tunaipongeza sana Serikali na tuko pamoja na Serikali katika maamuzi haya. Katika muktadha huu wa kufuta vyuo, lakini bado kuna dosari chache ambazo zimeonekena na ninafikiri ni vizuri Serikali ikaingilia kati na kuona.

Mheshimiwa Spika, imeelezwa kwamba wanafunzi wengi baada ya kuhamishwa kwenye vyuo hivi, unaenda mtu ana-*inquire loan status* anaambiwa *loan not registered*. Siyo hivyo tu, wapo wanafunzi kwa Mkoa wangu wa Kilimanjaro ambao walitoka St. Stephano *Memorial University* ambao walipelekwa Chuo cha Mweka, lakini wengine walipelekwa Masoka na wengine walipelekwa Ushirika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mtu anasoma *let's say BBA*, lakini anapopelekwa Masoka anaenda kuingizwa kusoma *HR* akiwa tayari ana *background* ya miaka miwili amesoma *Accounts* au amesoma *BBA*. Akienda Masoka, baada ya miaka miwili kukaa kwenye Chuo kile alichofutwa, anaenda kule anaingizwa kwenye mfumo wa kusoma *HR* anaitwa ni *graduate*.

Mheshimiwa Spika, Taifa kwa lillioendelea hatuwezi kujikita kuandaa bomu kwa Taifa hili kwa maana ya kwamba tunaona kuna uwekezaji mkubwa unaofanywa na elimu ya juu kuitia Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote wa *Loans Board*. Kwa hiyo, nafikiri ni jambo ambalo inabidi liangaliwe vizuri sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester unaweza ukarudia kidogo hicho kitu? Kimefanyika cha namna hiyo?

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo. Ninao ushahidi, kuna wanafunzi ambao walitoka *St. Stephano Memorial University* ambao walipelekwa Mwika na Ushirika. Walikotoka walikuwa wamesajiliwa masomo

mengine, walipofika kwenye vile vyuo walivyokuwa *dispatched* wameenda kulazimika kusoma masomo mengine ambayo walikuwa hawana *foundation* nayo. Nasema hapa nikiwa na ushahidi wa mwanafunzi ambaye alikuwa anasoma *BBA* akaenda Mwika akalazimika kusoma *HR*. Ni Mwika kama sikosei, Ushirika, akalazimika kusoma *HR*. Nafikiri hapa inabidi pengine Wizara itusaidie.

**SPIKA:** Subiri kidogo Mheshimiwa Ester, Profesa amesimama.

## T A A R I F A

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nimpatie taarifa Mheshimiwa Ester Mmasi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa tu nataka kumpa taarifa kwamba, utaratibu ni kwamba mwanafunzi anapohama, anahama na kozi kama alivyo. Kwa hiyo, utaratibu wa mwanafunzi kwenda kubadilisha, hicho ni kitu ambacho, kama anao ushahidi naomba anipatie ili niweze kuufanya kazi. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ndiyo maana na mimi nilistuka kidogo, nikamwambia hebu rudia hilo, maana yake njipya. Endelea Mheshimiwa Ester.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Spika, nitafuatilia, nitampatia *document* Mheshimiwa Waziri ili kwa pamoja tuone ni kwa namna gani tunaweza kuboresha haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, lakini kuna changamoto ya masuala ya Bima ya Afya. Tunaona wanafunzi wanaosoma Vyuo; *Private University vis-à-vis public Universities*, yaani hivi vyuo vinafsi na vyuo vya Serikali, unakuta ulipaji wa bima hizi unatofautiana. Utakuta kwa mfano mwanafunzi anayesoma kwenye Chuo cha Serikali analipa Sh.50,400/=, lakini wale wanaosoma vyuo binafsi wanalipa shilingi 100,000/=.

Mheshimiwa Spika, napenda Wizara yako ifahamu, masuala haya yanaleta sintofahamu kubwa kwa sababu siyo wote wanaoenda kwenye *Private University* wako vizuri au wazazi wao wana uwezo wa kuwapeleka na kuhimili maelekezo yote ambayo yanaondoa masuala mazima ya *uniformity* kwenye muktadha huu.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri husika au Wizara husika itusaidie kuona hapo tunafanyaje? Kwa sababu kimsingi wanafunzi hawa wanaotoka kwenye *background* za wazazi wa wakulima, wafugaji na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, kuwa kwenye *Private University*, haimaanishi kwamba mtoto huyo au mzazi huyo alipenda kwenda pale. Wengine tunalazimika kwa kuchangiana kwenye ukoo, kukopa, kuweka rehani vitu mtoto aende kwenye hicho chuo asibaki nyuma. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri na hilo pia atusaidie kuangalia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ipo *concern* ya uporaji wa mali kuititia taasisi zetu hizi za elimu. Inafahamika na nilishawahi kumwona Mheshimiwa Waziri wa Elimu, lakini pia suala hili limewahi kuletwa na Mheshimiwa Mizengo Pinda, mwaka 2006, vile vile hapa Bungeni liliwasilishwa mwaka 2016 kwamba kuna shule ambayo inaitwa Shule ya Kolila ambayo inatokana na Kijiji cha *Old Moshi* ambacho kinaitwa Sudan.

Mheshimiwa Mweneyekiti, Shule ya Kolila ni shule ya wazawa na ni shule ya kijiji ambapo Kijiji hicho cha *Old Moshi* kilikuwa na ekari zake 40. Kijiji kilijitahidi kikajenga madarasa 10, lakini cha kusikitisha katika shule hii, Shule ya Kolila imeingia kwenye mgogoro mkubwa na mvutano mkubwa na dhehebu la Kikristo ambalo sitapenda kulitaja nisije nikaleta migongano huko ya kiimani.

Mheshimiwa Spika, Shule Kolila ni Shule ya Wanakijiji, shule ile ikaja baada ya wanakijiji kukosa nguvu ya kuiendeleza ikakodishwa kwa shirika hilo la taasisi ya kidini. Kinachosikitisha, leo hii shule ile haikuwahi kuendelezwa...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Ester, muda hauko upande wako.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Spika, nitaomba pia nikabidhi taarifa hizi TAMISEMI na kwa Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joel Mwaka, dakika tano.

**MHE. JOEL M. MAKANYAGA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nashukuru kupata nafasi nami niweze kuchangia katika hoja hii iliyo mezani inayohusu Kamati Tatu za Kudumu za Bunge. Kwa sababu ya muda naomba niende haraka haraka tu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli napongeza Kamati zote tatu, viongozi wao pamoja na Wanakamati wote kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameifanya, tumezisikia ripoti zao, zimekaa vizuri, wala hakuna shaka yoyote juu ya hiyo. Tunachokifanya hapa ni kujaribu kuongeza nyama kidogo, lakini kuweka msisitizo kwa baadhi ya mambo ambayo wameyazungumza wenzetu kwenye ripoti zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa haraka haraka niseme kwamba sasa Serikali yetu ya Awamu ya Tano iliyoko madarakani imemaliza miaka mitatu. Ni kazi kubwa ambayo imeshafanyika sasa hivi, kila mtu anaiona. Kazi hii ndiyo ilikuwa chanzo cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli kusema kwamba katika awamu hii yeche anasema Hapa Kazi Tu. Katika Serikali ya Awamu ya Tano bila kuwa na Hapa Kazi Tu, mambo makubwa yanayotendeka yasingweza kutendeka kufikia hapa tulipofika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba Serikali iliamua kwa dhati, kwa kauli moja kwamba tuijenge Tanzania ya

Viwanda ambayo itaisaidia nchi hii kuvuka toka katika uchumi wa chini kwenda uchumi wa kati. Hizi ndizo kazi kubwa zinazofanywa na Wizara mbalimbali. Kati ya Wizara hizo, ziko Wizara ambazo zinasimamiwa na Kamati hizi tatu ambazo tunajidili hapa leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikizungumzia kwa uchache kabisa, Kamati ya *TAMISEMI*, tunazungumzia masuala ya elimu. Katika elimu, Awamu ya Tano walisema Elimu Bila Malipo. Elimu Bila Malipo bila kumung'unya maneno, imekuwa na matokeo chanya sana kwa Taifa letu, tunawapongeza sana. Tulikuwa na kampeni ya kuhakikisha watoto wetu wote wanaingia darasani na wanakaa kwenye madawati, tulifanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuititia kauli hii ya Elimu Bila Malipo, sasa hivi tatizo la madawati limerudi pale pale, kwa sababu watoto walioandikishwa kuingia Darasa la Kwanza wamekuwa wengi kuliko vile ilivyotegemewa. Kazi kubwa bado tunayo mbele, tunatakiwa tuifanye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, kuna maboma mengi ya madarasa na nyumba za Walimu ambayo yanahitaji kumaliziwa. Tunafahamu Serikali inatoa rai kwa Halmashauri zetu kuhakikisha kwamba maboma yote yanakamilishwa ili yaweze kutumika inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuititia hadhara hii leo kwamba siyo Halmashauri zote ambazo zina uwezo wa kukamilisha maboma hayo kwa muda mfupi. Kwa hiyo, naiomba Serikali zile Halmashauri ambazo kwa sababu moja au nyingine zinapata shida kuyakamilisha maboma, kwa Serikali iwaunge mkono ili maboma haya yaishe, watoto waingie madarasani waweze kusoma.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo kwa haraka haraka kabisa, tunaipongeza Serikali sana kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali za Wilaya 67, ujenzi wa Vituo vya Afya 350 katika Wilaya mbalimbali na Kata mbalimbali. Hata hivyo, huko nako kuna tatizo kubwa la maboma. Naendelea kuiomba

Serikali ijaribu kuzisaidia Halmashauri ambazo haziko vizuri kuhakikisha kwamba nao wanaweza kukamilisha maboma hayo na wananchi waweze kupata huduma inayostahili kama tulivokuwa tumekusudia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kuzungumza suala zito na muhimu kabisa la majisafi na salama. Bado tatizo la majisafi na salama ni kubwa sana katika vijiji vyetu, pamoja na vijiji ambavyo kwa kweli...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Joel.

**MHE. JOEL M. MAKANYAGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja Kamati zote tatu. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Daniel Mtuka, dakika tano ndio wa mwisho.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuwa kitinda mimba katika mjadala huu wa leo. Nami napongeza Kamati hizi tatu kwa taarifa zao nzuri. Pia nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amesimama kidete sana katika kusimamia ukusanyaji wa mapato na ndiyo maana tunaona matokeo haya sasa, tunazungumza ujenzi wa mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye Kamati, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *TAMISEMI* na Utawala. Kamati hii imetoa taarifa nzuri, nijazie tu kidogo kwa upande wa ukurasa wa 57 kuhusu ujenzi na ukarabati wa Vituo vya Afya pamoja na zile hospitali 67 na vituo 350. Pale tumefanya ziara katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo dogo kwamba katika utoaji wa fedha hatukuangalia sana, tumetoa ile *flat rate*,

hatukuangalia utofauti wa maeneo. Maeneo yanatofautiana, kuna mengine yana udongo mbaya, *topography* nyingine ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, tulienda Kituo cha Afya Mlali, walipewa shilingi milioni 400. Kuna maeneo kweli zimetosha, lakini Mlali hazikutosha. Ukiona kile kituo, wanasema kimekamilika lakini ukiangali ubora wa majengo, kwa kweli hauko sawa sawa. Majengo yameanza kupasuka kabla hata hayajakabidhiwa. Kwa hiyo, utoaji wa fedha uangalie maeneo na maeneo.

Mheshimiwa Spika, kuna vituo vingine wamejenga, lakini fedha zimeisha na vituo havijakamilika, kwa maana kwamba walizingatia ubora. Sasa katika kuzingatia ubora, zile fedha zikawa hazitoshi. Serikali itoe zile fedha iongeze vituo vile vikamillike. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la elimu kidogo. Tunao Waraka wa Elimu Na. 2 wa mwaka 2016. Huu waraka unazungumzia ufaulu au kuruhusiwa Kidato cha Pili kurudia mwaka baada ya kufeli, kuvuka ile asilimia 30. Sasa hakuna waraka mwingine, ni huu katika *private* na shule za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuna taarifa ambazo tumeletewa katika Kamati, kuna shule zinarudisha wanafunzi au zinahamisha wanafunzi ambao wameshavuka hizi asilimia 30, wameweka viwango vya kwao 45 na 50, wakishindwa kuvuka hiyo wanarudishwa na wengine wanahamishwa kabisa wanaondolewa. Anaitwa mzazi kimya kimya, anaambiwa mzazi huyu mtoto hakufaulu, hapa siyo mahali pake, mpeleke shule nyingine.

Mheshimiwa Spika, natoa masikitiko yangu, huu ubaguzi unatoka wapi? Hawa watoto ni wetu. Vidole hivi ni vitano lakini havilingani pia. Hawa watoto ni wetu, tunalilia kujenga umoja, leo tunataka shule zetu watoto *cream*, yaani tunataka wawe na akili tu! Wote wanaofanana ili wapate *Division One* wote! Hii haikubaliki. Unaposema ahamishwe,

apelekwe wapi? Wewe humtaki, nani atampokea?  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba huu Waraka, atakaposimama kama atapata nafasi Waziri anayehusika, mwenye dhamana, Profesa wangu, hebu atoe msisitizo kwa hizi shule ambazo zinakataa hawa wanafunzi ambao wameshafafulu kwenye hii asilimia 30 lakini wanaondolewa ili tu kulinda hadhi ya shule waweze kuvutia biashara. Hii siyo biashara, hii ni huduma. Hudumieni hawa watoto, ni wa kwetu sote hawa watoto, ni wa Taifa hili. Sasa mnapoanza kuwabagua...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtuka. Nakushukuru sana kwa mchango wako, dakika tano zimeisha.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hizi Kamati zote tatu kwa taarifa zao nzuri. Nakushukuru kwa nafasi hii, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtuka, ile Mlali uliyokuwa unasema ni ya Kongwa au ya wapi?

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Ya Kongwa.

**SPIKA:** Nashukuru sana.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Ahsante.

**SPIKA:** Sasa tunaendelea na upande wa Waheshimiwa Mawaziri. Tunaanza na Naibu Waziri, Mheshimiwa Waitara dakika tano, Mheshimiwa Kandege dakika tano, halafu atafuata Mheshimiwa Waziri Jafo, dakika tano. Hapo hapo mlipo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA  
NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):**

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza naunga mkono hoja za Kamati zote tatu kama zilivyotolewa. Pia nitajairibu kupitia baadhi ya maeneo machache.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, nitoe tu taarifa kwamba kwa sababu mambo yamezungumzwa mengi upande wa elimu, niliarifu Bunge letu kwamba Serikali inapeleka fedha nyingi sana katika kuboresha elimu. Tunachoomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote na hasa Watumishi wa Umma ni kuhakikisha kila shilingi inapopelekwa, inasimamiwa vizuri ili tuangalie *value for money*. Hilo ni jambo la msingi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, ninapozungumza, hii elimu msingi bila malipo, mpaka ninapozungumza hapa, mpaka Desemba, 2018, Serikali ya Awamu ya Tano ya Chama cha Mapinduzi imeshapeleka shillingi billioni 634,189 ambazo zimeenda kwenye Elimu Msingi bila malipo. Hizo zinakwenda kwenye posho ya madaraka, Maafisa Elimu wale wa Kata, Wakuu wa Shule, motisha na vinginenvyo.

Mheshimiwa Spika, kwenye hoja mbalimbali, imejitokeza hapa hoja ya majengo ambayo yamesimamiwa kwenye ukarabati wa shule kongwe na *TBA*. Ni kweli, hoja hii ilijitokeza kwenye Kamati ya TAMISEMI ambayo nami nilikuwepo na Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya TAMISEMI imeshalipokea hili, inalfanya kazi, tutapitia mikataba ile na kuchukua hatua maeneo ambayo wameshindwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ziko shule nyingi kama Ihungo, Kigoma Sekondari, Songea Wasichana, Mirambo, Nangwa, Tosamaganga, Malangaze na nyingine ambazo mpaka leo hazijakamilika. Waheshimiwa Wabunge na Kamati ya TAMISEMI naomba niseme kwamba hili jambo linafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ni elimu ya msingi bila malipo, zimejitokeza hoja hapa na michango mbalimbali; Mheshimiwa Waziri wa Elimu yupo anaweza

akatoa ufanuzi zaidi, lakini tunao Waraka hapa Na.3 wa mwaka 2016 ambao unaonesha zoezi la kuimarisha elimu Tanzania ni zoezi shirkishi, ziko kazi ambazo zinafanywa na Serikali na fedha zinapelekwa kama zilivyotajwa, ziko kazi zinafanywa na wazazi, uko wajibu wa wanafunzi wenyewe na wadau mbalimbali wa elimu.

Mheshimiwa Spika, michango kwa elimu na miundombinu inaruhusiwa kwa utaratibu uliowekwa, Wakuu wa Wilaya wameelekezwa kwa kushirikiana na wazazi waunde Kamati mbalimbali wanachangisha wale wanaoweza, ambacho kimeelekezwa ni kwamba kusiwe na michango ambayo ni gandamizi, akinamama kunyang'anywa meza na mitaji yao midogo midogo, lakini michango ya kuchangia elimu na miundombinu yake inaruhusiwa kwa usimamizi wa Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi na kwa vibali maalum, Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge wasaidie hilo, liendelee kufanyika. Hili linaenda sambamba pamoja na zoezi la kumalizia maboma yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, juzi niliulizwa swali hapa juu ya maboma; nikawaambia tunahitaji takribani zaidi ya bilioni 417 kumaliza maboma yote nchi nzima, lakini, tutakuwa tunafanya kwa awamu kulingana na uwezo uliopo, mazungumzo yanafanyika na Wizara ya Fedha, kikao kilimeshafanyika chini ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kwa hiyo ina maana muda sio mrefu sana zoezi hili litapunguza idadi ya maboma ambayo yapo katika eneo hilo. Kwa hiyo, tuna uhakika kwamba ndani ya muda mfupi ujao, madarasa yatajengwa na watoto wetu hawataendelea kukaa chini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia niwatoe wasiwasi, wanafunzi wote ambao wamefaulu kwenda kidato cha kwanza mwaka 2019 wote wataingia darasani na watasoma. Mpaka kufikia mwezi wa Tatu kazi nzuri imefanyika na hili jambo linasimamiwa vizuri sana. Kwa hiyo wananchi na Watanzania wasiendelee kuwa na hofu, hili jambo linasimamiwa na Serikali ipo kazini, wasiwe na hofu.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja imejitokeza hapa ya kuimarisha usomaji, zile KKK (Kusoma, Kuhesabu na Kuandika). Tuna miradi miwili mikubwa, mradhi wa kwanza, unaitwa *EMIS* na tumeenda mbali zaidi na *EQUIP* ambao mradhi huu una fedha nyingi sana zinaenda. Tunafundisha Walimu wa darasa la kwanza na pili, mpaka la tatu na la nne. Tumejenga shule zinaitwa shikizi, ambazo unapunguza umbali kutoka nyumbani kwa mtoto na shule mama na Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi tumezikagua zinaendelea. Tumefundisha Kamati za Shule, tumefundisha Walimu, tumetoa *tablets*. Kwa hiyo mambo mengi makubwa sana yanafanyika katika eneo hilo. Naomba mtuunge mkono tuendelee kufanya kazi hiyo na kila mtu ambaye anaweza kuchangia elimu, achangie elimu lakini kuunga mkono juhudzi za Serikali kwa kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais anaifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli, baada ya elimu msingi bila malipo, changamoto ni kubwa ufaulu wa wanafunzi umeongezeka, watoto wengi wanaenda mashulenii waliokuwa wanashinda kwenye masoko, sasa hawaendi masokoni wanakwenda shuleni, wale ambao walikuwa wanapiga debe, sasa hawaendi, mtaani watoto hawapo, wote wameenda shuleni. Hili ni jambo kubwa, tumpongeze Mheshimiwa Rais na Serikali ya Awamu ya Tano ya Chama cha Mapinduzi kwa maamuzi thabiti kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la kuweka kumbukumbu hapa...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa...

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, dakika moja, tu...

**SPIKA:** Waitara. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, jambo la ufaulu ambapo matokeo yametolewa. Maafisa Elimu wameonesha kwamba shule za *private* zimefaulu zaidi kuliko shule za Serikali. Serikali inasimamia shule za msingi zaidi ya 16,000, shule za private ni shule 1,413 sawa na asilimia nane tu, lakini hawa wenzetu katika shule zao wanachuja watoto, kuna mitihani ya darasa la nne ya Serikali, ya kidato cha pili na cha nne.

Mheshimiwa Spika, kwa maelekezo ya Serikali kwa Waraka nilionao watoto wakifaalu wa darasa la nne, wakifaalu wa kidato cha pili, hawa wanamaliza mtihani darasa la saba, wamalize na kidato cha nne, wenzetu wanawachuja watoto, wanawarudisha nyumbani. Kwa hiyo wale wote ambao wameanza la kwanza mpaka la saba, la sita wamezuilliwa; wale ambao wameenda *form one* mpaka *three* wamerudishwa, sisi Serikali ni kokoro, wote tunawapokea, wanafanya mitihani, asilimia nane huwezi kulinganisha na asilimia 92.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa muda ulionipa. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri Kandege, dakika tano.

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kuchangia, kwanza kwa kuzipongeza Kamati zote tatu kwa taarifa ambazo wamezitoa, ni taarifa nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba nipongeze Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, ikiongozwa na Dkt. Jasson Rweikiza na Makamu wake na wajumbe wote kwa ujumla. Naomba nitoe takwimu chache, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, jumla tulipata bajeti tuliyopitishiwa na Bunge lako Tukufu Sh.1,803,400,959,500 na katika hizo, naomba

niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais, tumeweza kupata pesa kwa ajili ya shughuli za maendeleo jumla ya Sh.856,560,441,937. Hii ni sawasawa na asilimia 47.5, hiyo si haba na fedha zote hizo zimeenda kwa ajili ya shughuli za maendelo.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa fedha hizo, jumla ya Sh.141,605,849,192 zimepokelewa ofisi kuu kwa maana ya Wizarani na kati ya fedha ambazo ilikuwa jumla ya Sh.345,113,541,000, lakini bilioni 40 zimepokelewa kwenda kwenye Serikali za Tawala za Mikoa; kati ya bajeti ya Sh.93,184,414,000, jumla ya Sh.694,643,380,250 zimepokelewa kwenye Halmashauri za Serikali za Mitaa, kati ya jumla ya Sh. 1,365,107,004,500 zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, tunakushukuru sana, tunashukuru Wizara ya Fedha, hizi fedha zote zimeenda kufanya kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo, iko jumla ya bilioni mia moja nukta tano ambazo ni za kujenga hospitali 67 katika Halmashauri zetu. Tumepanga katika bajeti inayokuja tunaenda kuongeza hospitali 27 katika zile 67, kwa hiyo ukijumlisha utaona namna kazi nzuri ambayo inafanywa na Serikali ya CCM chini ya Uongozi wa Rais wetu, mpwendwa Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi zimeenda shilingi bilioni 23 kwa ajili ya kujenga Ofisi zetu za Halmashauri; lakini pia zimeenda shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kununua boti; zimeenda shilingi bilioni 11 kwa ajili ya kuchochaea maendeleo ya Jimbo, Waheshimiwa Wabunge ni wanufalka na naamini fedha hizo zitakuwa zimetumika kwenda kuchochaea kwenye shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ambazo zimeibuka ambazo ni vizuri tukatolea ufanuzi. Hoja ya kwanza inahusu suala zima la *TARURA*, tunaomba tupokee pongezi ambazo Waheshimiwa Wabunge wote waliopata fursa ya kuchangia wamepongeza kazi nzuri ambayo inafanywa na *TARURA*, lakini kuna upungufu ambao wanataka uboreshwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa fedha, asilimia 70 kwa 30 kwa mujibu wa Sheria iliyopo na *TARURA* tangu imeanzishwa ndio ina miaka miwili, kuna mapitio ambayo yanafanya ili tupate *formula* itakayokuwa nzuri, baada ya kujua mtandao mzima wa barabara na kiasi cha fedha ambacho kinatolewa, tujue namna gani ambayo tutawezesha chombo hiki kizuri ambacho kina upungufu mchache lakini Waheshimiwa Wabunge wengi wamesifia juu ya utendaji kazi wa *TARURA*. Kwa hiyo, tunaomba tuendelee kukiunga mkono.

Mheshimiwa Spika, hapa Waheshimiwa Wabunge wameongelea kuhusiana na suala la kuripoti; ni kweli, azma ya kuanzishwa kwa *TARURA* wengi tunajua, wakati ule, ilikuwa kila Mbunge ambaye sasa akirudi kule, Diwani anataka angalau wapate hata kilometra mbili, kwa hiyo, *value for money* kwa ujumla wake, ilikuwa haionekani, tunaamini kabisa, iko haja ya Waheshimiwa kushiriki katika kutoa mapendekezo, *TARURA* waende kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, yako mengi na dakika tano ni chache, hivyo, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa Josephat Kandege. *TARURA* ilipoanza Wahandisi wengi wa Halmashauri walihamishiwa *TARURA*; matokeo yake Halmashauri nydingi ni kama ama hazina Wahandisi, ama wamewabakizia mabaki mabaki, kwa nayo tulitazame huko mbele kuhusu mgawanyo wa Wahandisi angalau baadhi wabaki kwenye Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya shule na mengineyo. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa dakika tano.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nikupongeze wewe Spika wetu, kwa kutuongoza vizuri, lakini pia nizipongeze Kamati zote za Bunge zilizowasilisha taarifa zao nzuri sana. Vile vile niwapongeze

Manaibu wangu wawili ambao kwa kweli wametoa ufanuzi mpana, japo kwa muda mfupi sana.

Mheshimiwa Spika, yangu ni machache tu kwa ajili ya kuelezea kwa ujumla. Kwanza naomba nikuhakikishie wazi kwamba, Kamati ya TAMISEMI ambayo tunafanya nayo sisi Ofisini kwetu, imekuwa msaada mkubwa sana kutupa maelekezo muhimu kwa ajili ya Taifa letu. Nataka tuweke hizi rekodi vizuri kwa sababu leo hii unaona ni mashahidi karibuni wajumbe wote hapa wakisimama, wanazungumzia vituo vya afya, wanazungumzia hospitali za Wilaya, wanazungumzia barabara na wanazungumzia elimu. Hii yote japo inawezekana kuna upungufu wa hapa na pale, lakini ukifanya tathmini ya huko tulikotoka na tulipo hivi sasa ni vitu viwili tofauti. Kwa hiyo naishukuru sana Kamati kwa ushauri wake, mkubwa sana. Kamati hii kwa kweli imeweza kufanya mambo makubwa sana na ripoti yao tunaishukuru sana na naomba niseme wazi kwamba wametusaidia sana kuhakikisha Wizara hii inakwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mbalimbali ya kiujumla, ambayo sisi kwa upande wetu tunaomba tuyachukue kwa ajili ya kwenda kuyaboresha zaidi na hasa katika suala zima la bajeti, japokuwa tunafahamu mgao kama Naibu wangu alivyosema hapa, mgao ni kiduchu na napenda Wabunge wafahamu kwamba mtandao wa barabara ambao *TARURA* inahudumia ni wastani wa kilomita 127,000, kwa hiyo ni changamoto kubwa. Hata hivyo, sisi kama Serikali tutaendelea kuangalia jinsi gani tutafanya na hasa *team* yangu sasa hivi, kupitia Mtendaji Mkuu wa *TARURA*, niliwalekeza kwamba waone jinsi gani watafanya licha ya hizi fedha tunazopata katika Mfuko wa Barabara lakini wafanya *resource mobilization* kutoka maeneo mengine. Hivi sasa tuko katika *negotiation* na wenzetu wa *World Bank* kuangalia jinsi gani tutafanya kuiwezesha *TARURA* iweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ni kwa ujumla, tumesikia changamoto mbalimbali kwamba wakati mwingine fedha kutoka maeneo mengine zinakuwa na

upungufu hasa katika kuimarisha sekta ya afya na hasa katika miundombinu. Naomba niseme kwamba tumelichukua hili na ndio maana katika maelekezo yetu, tunaenda kuangalia jinsi gani tutafanya, lengo kubwa ni kwamba miundombinu iendelee kujengwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba niwashukuru sana Wabunge; katika haya mapinduzi makubwa, Wabunge wamefanya kazi kubwa sana katika maeneo mbalimbali. Katika ujenzi wa vituo nya afya, tunaona jinsi gani Wabunge wameamua kujipambanua wenyewe kushiriki nya kutosha, hili lazima *hansard* iweze kunukuu vizuri, kwamba Wabunge wa Bunge hili, wameweza kudiriki kufanya kazi kubwa sana. Nina imani katika ujenzi wa hospitali za wilaya ambao tumeuanza na tunaendelea nao hivi sasa, hospitali 67, lakini mwaka huu wa fedha tena tunaendelea na hospitali 27 kama Naibu wangu alivyosema, naamini tutafika vizuri.

Mheshimiwa Spika, na hata hivyo nafahamu kuna hospitali zipo, lakini hali yake ni mbaya, kwa sababu hata hapa nikisimama nikisema pale Kongwa kwa Spika wangu, hospitali yake ya Wilaya bado tia maji, tia maji. Kwa hiyo ni maeneo ambayo niseme kwamba, japokuwa wengine wanazo hospitali za wilaya, lazima twende tukaziangalie jinsi gani tutazifanya ziweze kutoa huduma vizuri zaidi. Hili ndiyo jambo ambalo tunaenda kufanya mwaka huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nikutoe mashaka kwamba, kuna maeneo mbalimbali tutayapa kipaumbele kwa lengo kubwa la kuona jinsi gani wananchi wetu, wanapata huduma vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na hoja ya Mbunge wangu, Mbunge wa Tanga nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo lile tumeshalifanyia kazi na barua imeshakwenda kwake kupitia kwa Mkurugenzi, lakini tumemkopi, kama hajaipata, basi tutawasiliana baadaye, lakini kila kitu kiko sawsawa kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni, aondoe hofu katika jambo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba niseme kwamba naunga mkono hoja za Kamati hizi zote ambazo zimewasilishwa vizuri sana na Wenyeviti wa Kamati. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Waziri Mheshimiwa Jafo, tunakushukuru sana. Sasa anafuata Mheshimiwa Naibu Waziri, Stella Ikupa, dakika kumi, Mheshimiwa Ikupa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WENYE**

**ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kila mmoja wetu aliyeko mahali hapa. Pia nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Wenyeviti wa Kamati zote waliowasilisha taarifa zao leo na kipekee kabisa nitumie nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti pamoja na wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Masuala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu mpPENDWA, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Naendelea kumpongeza kwa sababu ya haya mengi ambayo anaendelea kuyafanya katika nchi yetu ambayo yanatupelekea kuwa Tanzania ya kujitegemea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika maoni ya Kamati ya Masuala ya UKIMWI maeneo mengi imeshauriwa kwamba kama Serikali tuweze kujitegemea kwenye masuala ya UKIMWI. Kwa hiki anachokifanya Mheshimiwa Rais anatupeleka kwenye Tanzania ambayo baadaye tutaweza kuwa ni watu wa kujitegemea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nichangie katika eneo la mashirikiano kati Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika eneo la mapambano dhidi ya dawa za kulevyा.

Niseme tu kwamba ushauri wote amba o umetolewa na Kamati hii ya Masuala ya UKIMWI umepokelewa, lakini naomba nitoe ufanuzi kidogo. Naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba kuna mashirikiano mazuri kabisa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mapambano ya dawa za kulevyia kwa njia gani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, upande wa Zanzibar tuna Tume, lakini upande huu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano tuna Mamlaka. Kwa hiyo hii Mamlaka inashirikiana vizuri kabisa na Tume ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyia ya Zanzibar, kuna vikao mbalimbali ambavyo vimekuwa vikifanyika vya Baraza la Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyia, Tume imekuwa ikishiriki kikamilifu kabisa. Hata hivyo, pia kumekuwa na jumbe mbalimbali ambazo zinatoka Tanzania kwenda Klmatalfa katika eneo hilli la madawa ya kulevyia. Tume pia imekuwa ikishirikishwa vizuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyozungumza sasa hivi, Tume ya Zanzibar ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyia, iko katika mchakato wa kufanya mabadiliko na kuwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyia. Sambasamba na hilo, Tume pia iko katika mchakato na harakati za mwisho kabisa za kufanya marekebisho ya Sheria ya Kupambana na Dawa za Kulevyia ili sasa ile Sheria ya upande wa Zanzibar iweze kufanana na Sheria ya upande wa Tanzania Bara. Ni kwa nini tunafanya hivyo, kwa sababu ilionekana kwamba kuna *gape* kidogo kati ya upande wa Tanzania Bara na upande wa Tanzania Zanzibar. Kwa hiyo marekebisho hayo yakishafanyika ina maana kwamba sasa udhibiti wa dawa za kulevyia utaenda vizuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, vile vile kulikuwa na hoja ya kwamba hatuna Sera ya Udhibiti wa Dawa za Kulevyia. Ni kweli sera hii haipo, lakini, Tume iko katika hatua za mwisho kabisa za kuandaa huu mchakato wa Sera ya Taifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevyia. Katika hili pia kwa sababu Serikali yetu, Serikali ambayo inapenda ujumuishi, iliandaa

utaratibu mzuri kabisa wa kukusanya maoni na walijiwekea kwamba watakusanya maoni kutoka kwa Wadau wapatao 120, lakini pia kutoka kwenye Kanda zetu zote tano. Mpaka sasa hivi ninavyozungumza tayari tumekwishakusanya maoni kutoka kwenye kanda nne bado kanda moja. Tukishakamilisha kanda zote tano, watacaa chini na ku-compile maoni haya na hatimaye utaratibu wa kupatikana kwa sera utaendelea (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichangie katika eneo la kukinzana kwa Sera Mipango na Sheria mbalimbali za UKIMWI, lakini pia kuna mapendekezo ya Kamati ambayo yametolewa kwamba Sheria ifanyiwe mapitio. Niseme kwamba ushauri huu mzuri kabisa umepokelewa, lakini sambamba na hilo, naomba nitoe ufanuzi kidogo, Serikali kuititia Wizara husika, Wizara ya Afya tayari imekwishaandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria Na. 28 ya mwaka 2008. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mapendekezo haya ya mabadiliko ya Sheria, kuna baadhi ya vifungu ambavyo vitafanyiwa marekebisho. Vifungu hivi ni kifungu cha 13, 15, pamoja na 27. Katika kifungu cha 13 kinaongelea upimaji wa VVU, katika vituo ambavyo vimethibitishwa. Katika mapendekezo ya Sheria yanassema kwamba sasa hivi upimaji wa VVU uwe ni kwa hiyari lakini mtu aruhusiwe kujipima mwenyewe mahali popote alipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hili tunaamini kwamba tutapata matokeo mazuri ya ile 90 ya kwanza, kwa sababu inaonekana kwamba katika ile 90 ya kwanza tupo nyuma kidogo tofauti na ile 90 ya pili, ambayo tumefikia asilimia 91 na ile 90 ya tatu ambayo tumefikia asilimia 87.

Mheshimiwa Spika, sambasamba na hilo, pia kuna mapendekezo kwenye umri wa kuweza kupima virusi vya UKIMWI kwa hiari bila ridhaa ya mzazi. Katika sheria yetu, kifungu cha 15(2) kilikuwa kinalazimisha mtu anayepima UKIMWI awe ni yule mtu ambaye anakuwa na umri wa miaka 18 na kuendelea ambapo hapo sasa anakuwa anapima

mwenyewe kwa hiari yake bila ridhaa ya mzazi lakini chini ya hapo mtu alikuwa haruhusiwi kupima mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi sheria inapendekeza kwamba umri wa mtu kupima kwa hiari bila ridhaa ya mzazi/mlezi uwe ni miaka 15. Tumesikia Waheshimiwa Wabunge wengi wameliongelea hilo na Serikali yenu siku imelisikia na muda siyo mrefu mapendekezo haya yataletwa mbele ya Bunge lako Tukufu ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuyafanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia kuna kifungu kingine ambacho pia kinatarajiwa kufanyiwa marekebisho, kifungu cha 27 ambacho kinaelezea adhabu ya kosa la mtu ambaye anatangaza tiba ya UKIMWI kinyume cha sheria. Mwanzoni adhabu ilikuwa ni shilingi milioni moja ama kifungo cha miezi sita lakini sasa hivi inapendekezwa kwamba adhabu iwe shilingi milioni milioni tano au kifungo cha miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na suala la mahusiano kati ya shughuli za kiuchumi na ongezeko la maambukizi ya UKIMWI sanasana kwenye maeneo yale ambayo yanakuwa na msongamano mkubwa ama sehemu za miradi mbalimbali kama barabara, migodini na sehemu nyingine. Pamoja na elimu ambayo inatolewa, Serikali pia imeenda mbali zaidi kwa kutoa dawa kinga kwenye maeneo haya ili kuhakikisha makundi haya yanaendelea kuwa salama. Dawa kinga hii ni *Pre-exposure Prophylaxis* ambayo inasaidia kwa makundi haya ili yasiweze kuambukizwa na magonjwa ya VVU.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada hizo tumefika mbali kwa sababu tulianza kutoa dawa hizi mwezi Machi, 2018 kwa *pilot* ya mikoa tisa. Machi 2018 mpaka Septemba, tulikuwa tumeshafikia mikoa tisa lakini malengo yetu ilikuwa ni kufikia watu wapatao 16,000 na ndani ya mikoa tisa tulikuwa tumeshafikia watu 9,000. Kuanzia Oktoba tuliongeza mikoa mingine 12 na kufanya jumla ya mikoa kuwa 21. Tunategemea kabisa tutavuka lengo kwa sababu

katika mikoa tisa tulikuwa tumefikia watu 9,000 lakini katika mikoa hii mingine iliyoongezeka tunategemea kwamba tutaenda kuvuka lengo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kuna suala la Mfuko wa UKIMWI wa Taifa ambao huu unatupelekea kuondokana na ile dhana ya kutegemea wafadhili. Mfuko huu unafanya vizuri sana ambapo mwaka 2017 tuliweza kununua dawa za *Septrin* zenye gharama ya shilingi milioni 660. Pia kwa mwaka huu umeidhinishiwa kiasi cha shilingi milioni 455 ambayo inaenda kununua hizi dawa za *Septrin*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda na mimi naomba niunge mkono hoja za Kamati zote hizi tatu ambazo zimewasilisha taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Stella Ikupa. Tumepata maelezo ya kutosha kuhusiana na Kamati ya Masuala ya UKIMWI.

Sasa tunaendelea na Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, dakika 10 tafadhalii.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, nianze kuwashukuru Wajumbe na Wenyeviti wa Kamati kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameifanya ikiwemo kuleta mapendekezo mazuri katika kuboresha utendaji wa sekta ya afya na maendeleo ya jamiii. Kipekee niipongeze sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii pamoja na Kamati ya Masuala ya UKIMWI. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niseme katika hatua hii tumepokea maoni na ushauri wa Kamati. Nataka kukiri mimi na Mheshimiwa Naibu Waziri tumekuwa tukipata ushirikiano mzuri sana, maoni mazuri sana kutoka kwa Kamati na ndiyo maana sekta ya afya inafanya vizuri sana nchini Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nitoe ufanuzi katika maeneo makubwa manne. Eneo la kwanza ni kuhusu sekta ya maendeleo ya jamii, Kamati imeshauri kwamba katika kuimarisha uratibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali tuanzishe kanzi data ya *NGOs*. Tumeanzisha na tumeanza zoezi hili mwezi wa Juni, 2018 na tunataraji kwamba tutazindua katika Bunge lijalo la Aprili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala la kuanzisha Kitengo cha Udhibiti Ubora wa *NGO*, tayari tunacho Kitengo cha Uratibu na Ufuatilaji wa *NGO* lakini nataka kukiri tunahitaji kuongeza nguvu ili sasa kazi ya kufuatilia hela za *NGO*, kazi gani wamefanya na wanafanya tuweze kuzifahamu vizuri. Mwezi wa Oktoba, 2018 tumepitisha kanuni mpya kwa ajili ya kutaka uwazi na uwajibikaji wa mashirika ya *NGO* juu ya hela ambazo wanazipata. Kama tunavyofahamu *NGO* nydingi zinaomba fedha kwa kutumia majina ya Watanzania maskini. Kwa hiyo, tumepitisha kanuni tunataka watoe taarifa kila baada ya miezi sita hela hizo zimepatikana kiasi gani na zinatumika wapi na katika masuala mangapi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa upande wa sekta ya afya, tumepokea ushauri kuhusu kukamilisha mchakato wa kuanzisha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Mimi na Naibu Waziri tumeferajika sana kwamba suala hili linaungwa mkono na Wabunge wote. Nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba tupo katika hatua za mwisho za kukamilisha Muswada, tunategemea utatupa nafasi Bunge la Bajeti, najua hatujadili sheria lakini tulete sheria hii muhimu kwa sababu Serikali ya Magufuli imefanya kazi kubwa katika kuboresha upatikanaji wa dawa, kujenga hospitali, kuboresha vituo vya afya pamoja na vifaa tiba. Kwa hiyo, ni kweli wananchi hawatapata huduma bora za afya kama hawana uwezo wa kifedha. Bima ya Afya itakuwa ndiyo suluhisho la kuhakikisha kwamba wananchi wote wanapata huduma za afya bila kikwazo cha fedha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala la vifurushi tunalikamilisha, tumeanza na vifurushi mbalimbali, tunataka wananchi

wajipimie wenyewe huduma za afya ambazo wanataka kuzipata. Kama unataka ufile mpaka Muhimbili utajipimia kufika Muhimbili na kama unataka ufile *Dodoma Regional General Hospital* utafika. Kwa hiyo, tunakamilisha na tumeanza kwa mfano kifurushi kwa ajili ya wakulima (Ushirika Afya) kwa ajili ya wakulima wa korosho na kwa Sh. 76,800 mkulima wa korosho anapata uhakika wa matibabu mwaka mzima. Tumeanza pia bima ya afya kwa ajili ya watoto (*Toto Afya Card*) kwa Sh.50,400. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ester Mmasi suala la Bima ya Afya ya Wanafunzi ni Sh.50,400 tu. Kwa hiyo, vyuo binafsi wanafanya wizi kama wanachukua Sh.100,000 ya Bima ya Afya ya Wanafunzi. Tutaweka utaratibu wanafunzi walipe moja kwa moja *NHIF* badala ya kulipa kupitia vyuo kwa sababu bima ni Sh.50,400. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo tumelipokea ni kwamba tufanye tathmini ya ustahamilivu ya Mfuko wa Bima ya Afya. Tumefanya tathmini kwa takwimu za mwaka 2016, nataka niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge tunaweza kutoa huduma za afya hadi mwaka 2029. Ila pale ambapo tutaongeza idadi kubwa ya wananchi kujunga na bima ya afya, naamini mfuko utakuwa una ustahamilivu mzuri na hivyo kutoa huduma mbalimbali za afya.

Mheshimiwa Spika, suala la UKIMWI, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Ikupa amejibu baadhi ya hoja lakini nataka kukazia hoja moja ya Mheshimiwa Jacqueline Msongozi. Ile hoja ni muhimu sana kwa sababu tafiti zinaonyesha kwamba huduma za tohara kwa wanaume inakinga maambukizi ya VVU kwa hadi asilimia 60. Kwa hiyo, tusidharau wanaume kufanya tohara kwa wale ambao hawajafanyiwa tohara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa mikoa ya kipaumbele ya Iringa, Njombe, Tabora, Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Mwanza, Geita,

Kagera, Singida, Kigoma, Mara na Morogoro huduma za tohara kinga ni bure.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, nakuongezea dakika mbili itaje mikoa taratibu, umeenda haraka hatujaisikia hii mikoa. (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, huduma za tohara ni bure katika Mikoa ya kipaumbele ambayo ni 17 na Mikoa hii inajumuisha Iringa, Njombe, Tabora, Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Mwanza, Geita, Kagera, Singida, Kigoma, Mara na Morogoro; Dodoma haipo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka tu kusisitiza kwamba ni tafiti za kitaalam zimeonyesha kwamba tohara kwa wanaume inaweza kuzuia maambukizi ya VVU hadi kwa asilimia 60. Kwa hiyo, tulitilie maanani suala hili.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Msongozi ameongelea suala la kuambukiza saratani ya mlango wa kizazi. Saratani ya mlango wa kizazi inaambukizwa kutoka kwenye kirusi cha mwanaume kinaitwa *Human Papilloma*. Kwa hiyo, pale ambapo mtu ana mkono wa sweta inamuweka pia katika hali ya kuweza kuchochea mazingira ya kirusi kile cha *Human Papilloma* ambacho ndiyo kinasababisha saratani ya mlango wa kizazi. Kwa hiyo, nitoe rai kwa wanaume ambao hawajapata tohara waone suala hili kwamba ni la kipaumbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi tumeenda mbali, tumeanzisha Mpango wa Tohara kwa Watoto Wachanga kati ya siku 1 hadi siku 60. Lengo letu sasa ni kuhakikisha kwamba suala la tohara kinga linakuwa endelevu na tumeanza kutekeleza katika mikoa sita ya Njombe, Iringa, Tabora, Mbeya, Songwe na Rukwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la tiba, Kamati imetushauri kutoa ruzuku kwa hospitali ikiwemo Jakaya Kikwete, *MOI*,

MNH na Hospitali za Rufaa za Mikoa. Niseme sisi kama Serikali kwa mfano mwaka jana katika Hospitali ya Muhimbili tumepeleka shilingi bilioni 4.5 na mwaka huu tuna shilingi bilioni 5 lakini kwa *JCI* tumeshawapatia shilingi bilioni 1.2.

Mheshimiwa Spika, katika hili, nisema tu kwamba sisi kama sekta ya afya tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutuwezesha kufanya vizuri katika utoaji wa huduma za matibabu ya kibingwa. Nimemshangaa sana Mheshimiwa Sugu anaposema rufaa zimepungua kwa sababu watu wanaogopa kuandika rufaa.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe takwimu chache. Mwaka 2014, Hospitali ya Jakaya Kikwete ilikuwa inafanya upasuaji wa kifua wagonjwa 127. Kutokana na kazi nzuri ya Magufuli mwaka 2017 wamefanyia wagonjwa 275. Sasa tunataka tuwapeleke wapi kama huduma zinapatikana ndani ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini suala la upasuaji wa moyo bila kupasua kifua mwaka 2018 uwezo wa Jakaya Kikwete ulikuwa ni wagonjwa 100 tu, mwaka 2017 tumefanyia wagonjwa 770. Sasa tunapeleka nje kwa sababu gani? Huduma zimeboreka na Mheshimiwa Sugu anatakiwa *to appreciate* kwamba tunafanya *renal transplant* na tunafanya upandikizaji wa vifaa vya kusikia kwa watoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mfano wa mwisho, hospitali yetu ya *Ocean Road*, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais tumepata shilingi bilioni 9.4, tumenunua mitambo ya kisasa ya kutoa matibabu ya mionzi inaitwa *LINAC*. Kwa kipindi cha miezi mitatu, tumewafanyia wagonjwa 109 na kati ya hao wagonjwa 70 wote tungewapeleka India kwa kila mmoja shilingi milioni 50. Kwa hiyo, wenzetu mnatakiwa kukubali kwamba huduma za matibabu ya kibingwa chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli zimeboreka sana na ndiyo maana safari za India zimepungua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la fedha, Kamati inasema hatujapokea fedha za miradi ya maendeleo, nadhani tu ni takwimu lakini sisi hadi Desemba tumeshapokea shilingi bilioni 81 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikiwemo fedha za dawa na ndio maana hali ya upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutoa huduma za afya ngazi ya msingi na rufaa ni zaidi ya asilimia 90. Pia tumpokea fedha kwa ajili ya kujenga Hospitali za Rufaa za Mikoa katika Mikoa mipy ya Simiyu, Katavi, Njombe, Songwe na Geita. Kwa hiyo, tumpata hela za miradi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa suala la viwanda vya dawa au uzalishaji wa ndani wa dawa. Suala hili ni la Kipaumbele kwa Serikali na kwa Wizara ya Afya. Nafurahi kusema sasa hivi viwanda vinne vinajengwa na sekta binafsi. Tunacho Kiwanda cha Dawa Bahari, *Kairuki Pharmaceutical* naye anajenga kiwanda lakini pia Reginald Mengi naye anajenga kiwanda cha dawa na sasa hivi tumpata mwekezaji mwingine ambaye ataanza kujenga kiwanda cha dawa. Kwa hiyo, tunaamini kabla ya mwaka 2020 tutakuwa angalau tuna viwanda vinne vipya ambavyo vinazalisha dawa ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni la watumishi lakini naamini kaka yangu Mheshimiwa Mkuchika atalijibu lakini nakubaliana na maoni na ushauri wa Kamati kwamba sasa tuwekeze kuhakikisha vituo vya afya viliboreshwa vinafanya kazi na siyo kuwa na majengo ambayo yanaweza yakamalizwa kwa sababu ya popo. Kwa hiyo, kwenye hili, kipaumbele chetu sisi tunataka kutoka kwenye bora huduma twende kwenye ubora wa huduma. Kwa hiyo, suala la huduma bora za afya ndio kitakuwa kipaumbele chetu kikubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niseme tena naishukuru na kipongeza Kamati na kwa kweli Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ina watu vichwa sana na tunawashukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Asante sana Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, tunashukuru kuisifia Kamati ya Guantanamo. (*Makofî/Kicheko*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Prof. Ndalichako, Waziri wa Elimu, tafadhalii.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza kabisa, napenda kuanza kwa kusema kwamba ninaunga mkono hoja za Kamati tatu ambazo zimewasilishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, nami nichukue nafasi hii kuishukuru na kuipongeza kwa dhati kabisa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendelo ya Jamii kwa namna ambavyo wamekuwa wakitushauri kwa maoni na mchango mzuri. Hakika nikupongeze na wewe kwa namna ambavyo uliisuka hiyo Kamati, ina watu ambao wanajali kabisa na wana michango mizuri. Niseme mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba Kamati hii ni tofauti kabisa na namna ambavyo watu walikuwa wanai-perceive wakati unaiunda. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tunafanya nao kazi vizuri, wamekuwa wakitupa maoni mazuri na tumekuwa tukisonga mbele kwa sababu kuna ushirikiano mzuri na maoni mazuri kutoka kwa Kamati. Kwa hiyo, baada ya shukrani hizo niseme tu kwamba tumepokea maoni na ushauri wa Kamati na Serikali itayafanyia kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kutolea ufanuzi baadhi ya hoja ambazo zimejitokeza katika mjadala wa hoja iliyopo mezani leo hii. Kwanza kabisa, kuna suala ambalo limezungumzwa la upungufu wa Wahadhiri hasa wale wenye kiwango cha Shahada ya Uzamivu pamoja na Maprofesa na hasa katika Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mheshimiwa Spika, niseme kweli kuna upungufu wa Wahadhiri katika vyuo hivyo na ndiyo maana Chuo Kikuu cha Dodoma hakijaweza kudahili wanafunzi *capacity* yake ni 40,000 lakini tunafahamu kwamba chuo kikuu siyo majengo tu ni pamoja na kuwa na Wahadhiri wenyе sifa. Nilihakikishie Bunge lako kwamba Serikali inafanyia kazi suala hili kwa nguvu zote na katika bajeti ya mwaka 2018/2019, Serikali ilitenga shilingi bilioni 4 ambapo tayari kuna Wahadhiri 68 ambaao wanafadhiliwa na ufadhilli wa Serikali kwa ajili ya Shahada za Uzamivu na katи yao 14 wanatoka Chuo Kikuu Dodoma. (*Makofі*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na juhudи za Serikali kutoa fedha zake kusomesha Wahadhiri lakini pia Serikali imeendelea kutafuta *scholarship* mbalimbali. Tuna *scholarship* 77 ambapo wameenda kusoma China, 30 wameenda kusoma Hungary, 26 wameenda kwa utaratibu wa *Commonwealth* pamoja na *scholarship* nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nimshukuru Mheshimiwa Rais, pamoja hizi *scholarship* 77 za China lakini kwa juhudi yake aliongea na Serikali ya China akaomba tuongezewe kwenye fani ya udaktari ambako tuna upungufu mkubwa. Serikali ya China ikaongeza *scholarship* nyingine zaidi kufuatia ombi la Rais. Kwa hiyo, nilihakikishie Bunge lako kwamba Serikali inafanyia kazi uhaba wa watumishi wa vyuo vikuu. (*Makofі*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumziwa ni umuhimu wa kuimarisha mafunzo ya ufundi stadi na kuhakikisha kwamba tunakuwa na watu ambaao wamebobeaa na ambaao wanaweza hata kujiajiri. Naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inaona umuhimu wa kuimarisha mafunzo ya ufundi stadi na tumekuwa tukiendelea kuwekeza katika vyuo vya ufundi stadi. Kwa mfano, sasa hivi tunaendelea na ujenzi wa VETA za Mikoa katika Mikoa ya Rukwa na Geita lakini taratibu za kumpata mkandarasi Simiyu zinakamilika na kwa watani wangu Kagera nilikuwa huko juzi kuangalia maandalizi ya

kiwanja ambacho kimeshakamilika na mkandarasi anaweza akaanza kazi wakati wowote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumeendelea pia kuimarisha VETA za Wilaya na hata hivi karibuni mwezi Januari Serikali imetoa kiasi cha fedha shilingi bilioni 1 kwa ajili ya kuimarisha majengo ambayo Halmashauri imeipatia Serikali ili yaendelezwe kama vituo vya ufundistiadi. Tumepeleka fedha lleje, Palamawe kule Nkasi, Kamachumu, Urambo, Cherekeni pamoja na Kitangali kwa ndugu yangu Mheshimiwa Mkuchika. Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba tunaendelea kuimarisha vyuo vya mafunzo ya ufundistiadi. Sasa hivi pia tunaendelea na ukarabati wa vyuo 20 vya maendeleo ya jamii. Yote hii lengo lake ni kuongeza ujuzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kulitolea ufanuzi ni mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Waheshimiwa Wabunge wengi wamelizungumzia lakini pia hata katika taarifa ya Kamati wamezungumzia suala la vigezo vya mikopo na mambo mengine na kama nilivyosema ushauri wa Kamati tumeupokea. Hata hivyo, napenda kutoa ufanuzi wa mambo machache, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, vigezo vya mikopo vimeduwa vikiboreshwu kila mwaka ili kuangalia changamoto zilizojitokeza na kutoa fursa kwa mwaka ujao. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, kama wana maeneo mahsus ambayo wangefikiri ni muhimu Serikali iyazingatie katika utoaji wa mikopo, iko tayari kuyapokea na kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni la wanafunzi wanaohama kutoka chuo kimoja kwenda kingine. Utaratibu ni kwamba mwanafunzi anapohama anahama na masomo aliyokuwa anasoma na mkopo wake kama alivyokuwa anapata. Kama nilivyotoa taarifa wakati Mheshimiwa Ester Mmasi alivyokuwa anazungumza, iwapo kuna wanafunzi wanakwenda na kusoma kitu ambacho ni tofauti hilo ni tatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna wanafunzi 208 kati ya 1,699 ambao walihama na mpaka leo bado hawajapata mkopo. Hii inatokana na changamoto za taarifa zao kwa sababu kuna baadhi ya wanafunzi ambao unakuta taarifa zile za kozi aliyokuwa anasoma awali inatofautiana na kozi aliyokuwa anakwenda, ikitokea hivyo kwetu inakuwa ni tatizo mpaka hizo taarifa tuzihakiki lakini pia kuna ambao wana tatizo la masuala ya mitihani.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba huu ni uzembe wa baadhi ya vyuo na hatuwezi kuendelea kuwaumiza wanafunzi kwa masuala ambayo wao siyo wanaopeleka taarifa. Tayari Bodi ya Mikopo ilishaviandikia vyuo barua tangu tarehe 17 Januari wahakikishe huu utata wa taarifa unaondolewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa nasema hivi, ikifika tarehe 15 Februari, kusiwepo na mwanafunzi hata mmoja ambaye amehamishwa na bado hajapata mkopo wake kwa sababu kumekuwa na mvutano. Napendekeza Tume ya Vyuo Vikuu ingeangalia katika sheria yake namna ya kuviadhibu vyuo ambavyo vinashindwa kutoa taarifa za wanafunzi kwa wakati na matokeo yake wanafunzi wanaumia wakati hawana tatizo lolote. Hilo nadhani ni eneo ambalo tungeangalia kuvibana zaidi vyuo katika sheria zetu ili viache huo mfumo ambao wakati mwininge kutokana na taarifa hizo wanafunzi wanakuwa wanacheleweshwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala limezungumzwa la usajili wa shule kwamba kutokana kazi nzuri ya Mheshimiwa Rais wetu ya kutoa elimu bila malipo mwitikio wa wananchi umekuwa ni mkubwa, sasa ifike mahali Serikali iruhusu wanafunzi wakasome maturubai au madarasa ya nyasi. Mimi sioni kama tumefika hapo, kwanza Serikali inafanya kazi kubwa sana ya kukabiliana na ongezeko la wanafunzi ambao wanajiandikisha shulenii kutokana na elimu bila malipo na Serikali imekuwa ikijenga miundombinu lakini pia Halmashauri zetu tumeona kazi kubwa inafanyika. Niseme

hana elimu ni haki ya kila mtoto lakini pia ni jukumu la Serikali kuhakikisha ulinzi na usalama wa watoto.

Mheshimiwa Spika, leo hii tulivyokuwa tunatoka mvua ilikuwa inanyesha, Waheshimiwa Wabunge wote hakuna aliyeokuwa anakwenda, walikuwa wamekaa wanasubiri kwanza mvua iondoke. Hatuwezi tukaruhusu miundombinu ambayo ni hatarishi kwa maisha ya watoto wetu. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba kabla ya kuruhusu shule isajiliwe, itakaguliwa kuhakikisha kwamba miundombinu yote ambayo shule imeiandaa iko salama kwa ajili ya watoto wetu, waweze kupata elimu lakini tuna jukumu pia la kulinda usalama wa watoto wanapokuwa shulenii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumziwa ni kuhusu kuboresha mfumo wa elimu yetu lakini pia lugha ya kufundishia. Nashukuru hili suala kila linapojitokeza kunakuwa na mjadala ambao upande mmoja unaona tutumie Lugha ya Kiswahili lakini pia kuna hoja ya kwamba lugha peke yake siyo jawabu, suala ni kuangalia changamoto kwa nini wanafunzi hawafanyi vizuri. Nafurahi kwamba katika mjadala tumeonesha kwamba hesabu kwenye shule za msingi wanafundishwa kwa Kiswahili lakini hawafanyi vizuri. Kwa hiyo, ushauri nimeupokea, jambo la msingi ni kuangalia zile changamoto zinazosababisha wanafunzi wasifanye vizuri na Serikali izifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kwa ridhaa yako nizungumzie suala la uhaba wa walimu. Ni kweli kuna baadhi ya maeneo kuna uhaba wa walimu, kwa hiyo, tutaendelea kuomba Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuangalia pale ambapo kuna walimu ambao wamezidi kuwe na mgawanyo sawia. Mheshimiwa Kapteni Mkuchika ameshazungumzia suala la kuajiri kuziba zile nafasi za wastaafu ili zile shule ambazo kweli hazina walimu kabisa tuweze kuzipatia walimu kwa haraka. Pia Serikali itaendelea kuwasimamia walimu wafanye kazi yao vizuri na kuwapatia mafunzo kazini ili wawe na weledi wa kutosha na hivyo basi tuongeze ubora wa ufaulu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na kwa mara nydingine naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Ndalichako, Waziri wa Elimu. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Capt. Mstaafu Mheshimiwa Mkuchika, dakika kumi pia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipatia nafasi kufafanua baadhi ya mambo ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa Wabunge katika masuala yanayohusiana na Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, pill, nichukue nafasi hii kushukuru sana kwa uongozi madhubuti ambao Wizara yangu inapata kutoka katika Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa ambayo ndiyo Kamati inayohusika na Wizara yangu. Wanafanya kazi nzuri, Mheshimiwa Rweikiza, Makamu wake Mheshimiwa Mwanne Mcemba, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ile tunakwenda vizuri sana na mafanikio tunayoyapata katika Wizara yetu ni mafanikio pia yaliyochangiwa na Kamati hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikianza na suala la uhaba wa watumishi, nadhani juzi nililifanua na leo nitalisema kwa kifupi sana. Tunakubadili kwamba mwaka jana walimu wengi wamestaafu na wengine wameaga dunia, nikasema tayari tuliomba tupate takwimu hizo kutoka Wizara ya Elimu wamekwishatuletea tunangoja za TAMISEMI nao watuletee. Tunataka kwanza kujaza mapengo hayo, tukijaza mapengo hayo maana yake ni kwamba hakuna gharama ya mishahara mipya, tena kwa uhakika ni kwamba hata mishahara tutakayolipa ni pungufu kwa sababu hawa watakaowaaajiri ni wapya, wale waliostaafu walikuwa na mishahara mikubwa kuliko tunaotaka kuwaajiri. Kwa hiyo, haitupi mashaka na hatupati shida kutamka kwamba tutajaza mapengo kwanza baada ya hapo tutaangalia hali ya uchumi wetu tutakuwa na ajira mpya. Kwa hiyo, nilitaka niseme hivyo kwa upande wa watumishi hasa upande wa elimu na afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Iakini juzi pia nilipochangia nilisema kwa wimbi hili la kwamba tunajenga zahanati, vituo vya afya na hospitali kila mahali, msingoje mmalize kabisa, wale ambao wanajua kwamba zahanati au kituo chetu cha afya tutafungua tarehe fulani, tuleteeni maombi hayo ili jengo likikamilika, vifaatiba vikipatikana kazi ya tiba ianze mara moja. Naomba wote mfanye hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine amezungumza ndugu yangu, Mheshimiwa Selasini kuhusu masuala ya utawala bora. Kauliza swalii, je, hao tunaowateua tunawapekua? Kwa uhakika nataka nithibitishe tunaowateua kabla hatujakuteua tunajiridhisha, je, wewe raia, mwenendo wako, akili yako iko timamu, unaishi vizuri na watu, upekuzi tunafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo amelizungumza ambalo namuunga mkono na nataka niseme hii ni *practice* ya dunia nzima, utawala wa Rais mpya akiingia anafanya mabadiliko kwa jinsi anavyoona ye ye inafaa. Nilitoa mfano siku moja mule ndani, ukienda Marekani kule mpaka wapika chai wale wote *State House* mfagizi, dereva, wote wanaondoka kupisha timu mpya. Sasa hili liliofanyika ni kwamba uteuzi umefanyika lakini namuunga mkono mdogo wangu Mheshimiwa Selasini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la mafunzo kwa wale wanaoteuliwa, jambo hili nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tumelifanya. Tumefanya mafunzo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala na sasa tumeshaandaa tayari mafunzo kwa Makatibu Tawala wa Wilaya, yatafanyika muda wowote kuanzia leo. Kila kitu wameshapelekewa, nauli na jinsi watakavyofika, wanangoja tu tuwaambie lini na wapi, watapata mafunzo kwa sababu ni muhimu sana hawa Maafisa Tawala wa Wilaya wakapata mafunzo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo amelizungumzia ni *Regional Administration Act* ya mwaka

1997, nataka nirudie tena kufafanua, ambayo inampa Mkuu wa Wilaya madaraka ya kumweka mtu ndani muda wa saa 24. Nataka nirudie, muda wa saa 24, lugha iliyozungumzwa pale ni kwa usalama wake. Kwa usalama wake maana yake, ameua mtu, jamaa zake wamekasirika wanataka kumpiga yule aliyeua, unamweka ndani kwa usalama wake. Sheria inasema akishamaliza saa zile 24 asubuhi lazima umpeleke Mahakamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mahali popote, nilisikia siku moja, Mkuu wa Wilaya kumweka mtu ndani muda wa saa 48 ni makosa kwa sababu sheria inampa ye ye saa 24, Mkuu wa Mko a mepewa saa 48. Nataka niwahakikishie Watanzania kupitia Bunge hili, mimi ni Waziri wa Utawala Bora, kazi zangu sifanyi kwenye mkutano wa hadhara na kusema leo tumefanya haya na haya, watumishi wote wa umma wanahuksika na utawala bora. Kwa hiyo, inapokuja kwenye suala la utawala bora mimi ni Waziri wa Wizara zote, tunafuutilia tunachukua hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mkuu wa Mko a saa zake ni 48, anaweza akamweka saa 24 akipenda. Nachotaka kusema siyo lazima wewe umuweke mtu ndani kama ni *criminal offence OCD* yupo, kama ni suala la Uhamiaji, Afisa Uhamiaji yupo, kama amekwepwa kodi mtu wa *TRA* yupo, siyo lazima haya mambo utamke wewe!

**WABUNGE FULANI:** Sawa kabisa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Tuache. Yupo mzee wangu mmoja anasema kujimwambafai yaani uonekane wewe ni mwamba. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, nawaomba huko mlipo msiniharibie kazi yangu, mimi ndiye mwenye *title* ya utawala bora. Mimi ndio Waziri mwenye nafasi ya utawala bora, ukiendesha mambo kinyume na utawala bora unaniharibia kazi na sitaki Mheshimiwa Dkt. Magufuli anibadili. Mimi

nataka Mheshimiwa Dkt. Magufuli aseme mzee endelea hapohapo ulipo. (*Makofii/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, hili jambo humu ndani tumelizungumza na kwenye mafunzo tumelielekeza. Sasa nina hakika na upande mwininge pia mngepongeza maana ile vurumai siyo imepungua kidogo, imepungua sana, maji yametulia kwenye mtungi. Yametulia kwenye mtungi kwa sababu tumewapa elimu na wameelewa. Kwa hiyo, naunga mkono alichosema ndugu yangu Mheshimiwa Selasini kwamba tuwape elimu na tumewapa elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie, mkitaka kujuu kwamba masuala ya utawala bora nchi hii tunakwenda vizuri, mtupongeze tu. Jana, siyo juzi, Taasisi ya *Transparency International* inaonyesha kwamba mwaka 2017 duniani Tanzania tullkuwa wa 102 lakini jana tumekuwa wa 99. Kwa nchi zote duniani unazozijua wewe katika suala la utawala bora Tanzania ya 99. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nachosikitika tu ni kwamba bado hatujamshinda Rwanda katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, ye ye anaongoza sisi tunashika nafasi ya pili. Nasema kwa mwenendo huu tulipoacha kutianatiana ndani hovyo, nina uhakika tutakuwa wa kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limegusiwa na wachangiaji ni Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (*TASAF*) kutokufika baadhi ya maeneo. Nataka niwahakikishie *TASAF* tumefikia walengwa asilimia 70 nchi nzima, bado asilimia 30. Serikali imefanya maandalizi katikati ya mwaka huu malengo ni kufikia asilimia 30 iliyobaki. Kwa hiyo, wale ambao hamjafikiwa msiwe na wasiwasi, Serikali inafanya maandalizi ili tuweze kufikia maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, lakini katika hili la *TASAF* nataka kutoa onyo moja, mnisikilize ili huko mliko msije mkaniletea matatizo katika Wizara yangu. Baadhi ya viongozi wa Wilaya wanawalazimisha walengwa wa *TASAF* kutoa michango bila kuwashirikisha na hasa ile ya bima ya afya. Tunasema

zungumzeni nao wajunge bima ya afya lakini wilaya moja tumeshamfukuza yule wa *TASAF* na mkubwa wake pengine anasubiri ngazi za juu huko. Michango ya maendeleo vijijini, sijui wanajenga shule, zahanati, watu wakiwa wagumu kuchanga wanakwenda kukata hela za *TASAF*, hilo ni marufuku. Nasema wilaya moja imeshatoka, taarifa zimefika kwangu, yule wa *TASAF* tumemfukuza, wale wengine wanasubiri wakubwa waliowaweka wawachukulie hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani mtu anapata Sh.20,000 kwa mwezi baada ya miezi miwili halafu wewe unamkata Sh.15,000 unasema mchangno wa kujenga shule lakini wale ambao wana uwezo hawakuchanga, unakwenda kumchangisha maskini. Nasema ikitokea namna hiyo hatutavumilia. (*Makofi*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ilibaki pointi moja, walikuwa wanaomba wenzangu na mimi naomba hapohapo na kwa sababu unatupenda wote sawa utaniruhusu tu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu, humu ndani nilitoa ufanuzi nini maana ya barua kusema *UFS*, Kiswahili ni Kupitia Kwa, nikasema mtumishi yeyote wa Serikali ana haki ya kuwasiliana na mwajiri wake. Nikasema pia mtu akiandika barua ya kuomba uhamisho wewe Mkurugenzi, Mkuu wa Shirika, Katibu Mkuu anaandika barua inakwenda kwa mwajiri wake, anaomba barua ile ipite, wewe unachukua barua unaweka katika droo unasema mimi sипитиши. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilisema siku ile tukimpata kiongozi wa namna ile tutamuwajibisha. Anapopitisha barua kwako amekuheshimu, maana yake barua iende

Iakini *with comments*, anakupa fursa wewe kutoa maoni. Unaandika pale nakubali ahamishwe ili mradi nipate mbadala.

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Amekuja juzi hajamaliza miaka mitatu sipendekezi uhamisho huu. Barua lazima iende wenyewe kuamua kule kwamba uhamisho umekubaliwa au haukukubaliwa ni yule aliyemuandikia siyo wewe UFS. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Iakini na watumishi nao nataka niwape darasa, barua yako ikishapitishwa haina maana kwamba uhamisho wako tayari umeshakubaliwa, ni kwamba pale imepitia inasubiri uamuzi kule juu. Niliomba siku ile msitufanyie kazi ya kuamua sisi tulioandikiwa barua, tuachieni sisi wenyewe tuamue. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono taarifa za Kamati hizi, nakushukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kapteni Mkuchika. Jamani, wale wa kushoto kwangu hata maneno mazuri haya hata kushangilia kidogo, afadhali bwana. Mnagoma jumla? (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe tafadhalii, utufungie pazia.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Nazipongeza Kamati zote tatu kwa taarifa ambazo zimevasilishwa mapema leo asubuhi na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, pili, nina kila sababu kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

kwa uthubutu, upeo mpana alionao na ujasiri anaouonyesha hasa pale ambapo anaziona fursa za kusukuma mbele Taifa hili. Nasema hivyo kwa sababu mwaka jana tulitembelewa na Rais wa *FIFA* na alipofika Mheshimiwa Rais aliacha ujumbe mfupi sana na huo ujumbe aliwasilisha Waziri Mkuu wetu Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwamba Rais anachotaka ni viwanja kumi vizuri.

Mheshimiwa Spika, nafikiri Rais wa *FIFA* hajazoea vitu kama hivyo, kwa kweli aliupokea huo ujumbe kutoka nchi ambayo imedhamiria kazi. Alichoaahidi tu ni kwamba atashirikiana na nchi yetu na kuisaidia kuifungulia *TFF* haraka ile kesi iliyokuwa imefungwa na ana uhakika kwamba tutapata viwanja hivyo na tutawasiliana naye. Naomba tu nitoe taarifa kwamba sasa hivi tumefunguliwa na *FIFA*, msaada wa *FIFA* umeanza kuja. Kwa kweli ile rai ya Mheshimiwa Rais tutaanza kuitekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi napenda kusema kwamba tumekaa na wenzetu wa *TFF* na sehemu ya fedha fedha ambayo tumepata tutaitumia kuboresha viwanja kumi nchini kwa kuanzia kama ambavyo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alivyotaka. Kwa sababu Aprili, Rais wa *FIFA* Gianni Infantino atakuwa hapa si ajabu akaulizia kuhusu hilo, ndio maana kwa kweli tumeona hilo lazima tulitekeleze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mbali na viwanja hivyo kumi, tutakarabati upya kabisa Uwanja wa Karume, kujenga *hostel* mpya, ofisi na majukwaa ya uwanja huo. Mimi naahidi hatutarejea tulikotoka maana kulikuwa na udokozi mkubwa kweli *TFF*. Miaka kadhaa iliyopita nchi tano, sita kila nchi tulipewa dola 400,000, sisi tukaishia kujenga vile vibanda pale llala, lakini Rwanda na Sudan wana maghorofa, huwezi kuamini tulipewa pamoja. Vilevile tutajenga Hosteli ya *TFF* Tanga, madarasa na ukumbi mkubwa pamoja na kiwanja, kwa hiyo tunaendelea vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika fedha iliyoanza kuingia ilikuwa shilingi milioni kadhaa mara moja nimeona *TFF*

wakitenga pesa kwenda ZFA, zaidi ya shilingi milioni 100. Tutaendelea na ushirikiano namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja aliyoitoa leo asubuhi Mheshimiwa Khatib Haji kuhusu uhusiano kati ya *TFF* na *ZFA*. Kwa kifupi sana *TFF* na *ZFA* ni mashirikisho dada, nikutumia muktadha wa Kiingereza kama *sister federations*. Moja inasimamia soka upande wa Tanzania Bara na nyingine Tanzania Zanzibar. Mashirika haya mawili ni wanachama wa *CECAFA* wanaojitegemea, *CECAFA* ina nchi 11 lakini tukienda *CAF* vilevile tunajitegemea lakini ujumbe wa Zanzibar siyo kamili sana kwa sababu ni mwanachama ambaye ni *associate*, ni mshiriki. Ndiyo Zanzibar anapata kila kitu lakini hawezি kupiga kura. Tunapokwenda *FIFA* (Shirkisho la Mpira Duniani), hapa ndipo ambapo Zanzibar hawana nafasi kabisa inabidi kwa kweli wasimamiwe na wenzao wa *TFF*.

Mheshimiwa Spika, nachotaka kusisitiza hapa ni kwamba tutambue kwamba *TFF* na *ZFA* si idara za Serikali, hizi ni taasisi huru zenye vyombo vyake vya maamuzi, Wizara sisi tunao tu ule ushawishi wa kisera. Nataka niendelee kuamini kuwa *ZFA* itaendelea kupokea misaada mbalimbali kutoka *FIFA* kupitia *TFF*. Pale penye utata, vyombo hivi viwili viendelee kujadiliana na ukiwa mkubwa zaidi basi wasisite katuona sisi. Kwanza nisisitize tu kwamba wenzetu *ZFA* wasinyamaze wakiona kuna tatizo na pengine kutafuta mpaka Wabunge waje waliongee suala hilo ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Haji nikusitisizie tu kwamba tunaongelea Uwanja wa Gombani kama tulivyosema leo asubuhi tumeutolea mfano, ni kama vile ambavyo tunatoa mfano hapa wa viwanja viwili tu pamoja na ukubwa wa nchi hii; ni Uwanja wa Kaitaba na Uwanja wa Nyamagana. Ni kwa sababu tulikotoka kwa kweli matumizi ya pesa hayakuwa mazuri sana; pengine tungepata viwanja kumi kumi kama tungekuwa waangalifu lakini sasa tumefungua ukurasa mpya kama nilivyosema.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie suala la Mheshimiwa Nkamia na Mheshimiwa Kabati kuhusu Ligi ya Wanawake na ligi za Daraja la Kwanza na nyingine, pale ambapo ligi hizi hazina ufadhili (*sponsorship*) kwa kweli kuandaa *home and away matches* ni kuwatesa sana vijana wetu. Nawahakikishia kwamba tutakaa chini tuliangalie upya na nawaonea huruma Waheshimiwa Wabunge wengi sana wanabeba mizigo hiyo ya kusafirisha timu na kuzilaza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwamoto ameongelea kuhusu mashindano ya *AFCON*. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mwamoto kwamba limekaa vizuri kama ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu amelielezea vizuri leo asubuhi. Tuna *Local Organizing Committee* ambayo naiongoza mimi lakini ina wajumbe wengi kutoka taasisi mbalimbali za Serikali na tuna viongozi mbalimbali kama wajumbe akiwemo Waziri wa Maliasili na Utali, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji na viongozi wengine mbalimbali na kwa kweli tumejipanga ili mwezi Aprili kisiharibike kitu. Tarehe 12 naongea na Wahariri wa vyombo vyaya habari kuhusu ugeni mkubwa tutakaoupata na tutaanzisha hiyo kampeni nchi nzima. Vilevile tarehe 14 tunakutana tena kuweza kujadiliana kwa Kirefu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mara nyangi umeshakuwa mgeni rasmi kwenye mechii, Uwanja wa Taifa uko katika ukarabati mkubwa sana. Vilevile Uwanja wa Uhuru uko kwenye ukarabati mkubwa ambapo tunang'oa kabisa zile nyasi na nyasi zake za bandia ziko melini na tutaziweka baada ya muda si mrefu pale uwanjani. Uwanja mwingine wa Chamanzi ambaa utatumika ukarabati wake unamaliziwa, kwa hiyo umekaa vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi ameshangaa CCM kumiliki *Channel Ten* na *Magic FM*, sijui kama yupo...

**MBUNGE FULANI:** Hawezi kuwepo.

### **WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA**

**MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, atapata ujumbe tu kwamba asisahau kuwa CCM ina vyombo nya habari vyenye umri sawa na uhuru wa nchi hii. Vyombo vingine kimkakati ni kawaida duniani kushikiliwa na wapenzi wa chama na si kitu cha ajabu sana. Kwa mfano, gazeti la Tanzania Daima linamilikiwa na mpenzi wa CHADEMA, si la CHADEMA ni la mpenzi wa CHADEMA lakini siku litakapohamia CHADEMA utashangaa kweli? Huwezi kushangaa! Sasa unashanga kwa nini anashangaa mpenzi wa CCM aliyekuwa na chombo kwenda CCM, asishangae ndivyo mambo yanavyokwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabati ameongelea soka la kike. Naomba nimhakikishie kwamba soka la kike linakwenda vizuri, mimi mwenyewe nimefarijika sana. Naomba niwakumbushe tu wenzetu hapa kwamba tuna *Twiga Stars*, tunasahau tunashikilia tu timu za wanaume, *Twiga Stars* ni ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wamechukua kombe la *CecaFA* mara mbili mfululizo; mwaka 2016 na 2018. Hawa akina mama ni mashujaa kweli kweli na kwa kweli soka la kike tunalikazania sana. Kuna wenzao wengine *Kilimanjaro Queens* nayo imekuja juu; mmesikia hivi karibuni ikichukua ubingwa wa Afrika Mashariki kwa mara ya kwanza. Sifa ya timu hii ni kutokuwa na huruma inapocheza, inabamiza watu magoli mengi sana. Kwa mfano, mchezo wa kwanza na Burundi watu wengi walishangaa, ilikuwa ni taarifa Afrika nzima, baada ya kuipiga Burundi magoli nane kwa moja. Akina mama hawa hawana huruma kabisa, mchezo wa marudiano ikiwa tano bila. Ni timu nzuri sana na naomba nimirage mfungaji bora ambaye ni Mwanahamisi ambaye peke yake alifunga magoli saba. Tumezoea kuwataja wanaume tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie tu kwa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge ushiriki wao katika maandalizi ya *AFCON* ambayo yatafanyika Aprili na yatahusisha nchi nane bora katika Bara la Afrika. Tuiombee *Serengeti Boys*, timu ambayo kwa kweli imebeba matumaini ya Watanzania. Ikishinda mechi mbili tu Tanzania kwa mara

ya kwanza tangu uhuru tutashiriki katika Kombe la Dunia kupidia timu ya Serengeti.

Mheshimiwa Spika, sipendi uniambie nikae chini, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwakyembe kwa mchango wako. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Mwenyekiti mwenyewe Mheshimiwa Peter Serukamba anakuja kuhitimisha hoja yake, karibu sana, una dakika 15. (*Makofi*)

**MHE. PETER J. SERUKAMBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi hii uliyonipa na nawashukuru wachangiaji wote, ripoti yetu imechangiwa na watu 25. Yameongeleta mengi sana, nitajitahidi kuongea yale machache ambayo wameongea watu wengi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la kwanza ambalo Kamati yetu imelisisitiza na Waheshimiwa Wabunge wamelisema ni umuhimu wa Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote. Bado tunaiomba Serikali kama kuna zawadi Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli na Serikali yake tunaweza tukawapa Watanzania ni kuleta Bima ya Afya kwa Watu Wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni watumishi wa afya. Tumefanya kazi kubwa sana ya kujenga vituo vya afya na zahanati. Bahati nzuri kaka yangu Mheshimiwa George Mkuchika ametuahidi, ni muhimu sana kupata watumishi wa afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la tatu nataka kuipongeza Serikali kwa dhati kabisa. Serikai imefanya kazi kubwa katika uwekezaji mkubwa hasa Hospitali za Muhimbili, Jakaya Kikwete, Mloganzila, Benjaminsi Mkapa, *MO/na Ocean Road*. Pia tumejenga hospitali za mikoa, hospitali za wilaya na vituo vya afya. Kwa vyovvye vile haya ni mafanikio

makubwa. Naomba niipongeze Serikali kwa kazi hiyo kubwa wanayofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo kama Kamati tunaiomba sana Serikali, umefika wakati tuanze kuhangaika na kinga. Wanasema kinga ni bora kuliko tiba. Tukihangaika na kinga tutapunguza gharama kubwa za afya. Ili tuweze kuhangaika na kinga lazima tuhangaike na watu wanaoitwa *Community Health Workers*. Hawa ndiyo wako vijijiini, wanaishi na wananchi, watatoa elimu, watasaidia kwenye chanjo na wataeleza umuhimu wa usafi. Naomba nieleze tuliyoyaona Rwanda, wao hawa *Community Health Workers* wamesaidia kupunguza vifo ya akina mama kwa asilimia 80. Kwa hiyo, niiombe Serikali tuhakikishe tunaiangalia kwa makini kada hii na kuwasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la elimu. Tumeandika kwenye ripoti yetu na kila mwaka tumekuwa tunaandika na tutaendelea kuandika. La kwanza, Serikali inafanya vizuri sana kwenye kutoa mikopo ya watoto wanaokwenda vyuo vikuu. Ukiangalia nchi zote zinazotuzunguka wanazo tuzo kwa maana ya *scholarship award*. Naomba sana Serikali umefika wakati sasa tuanzishe *scholarship award*.

Mheshimiwa Spika, maana yake ni nini? *Scholarship award* ni watoto waliomaliza *form six* waliopata *point* tatu na *point* nne. Kama Serikali tuwaoneshe *appreciation* kwamba tumekubali wamefanya vizuri na watasomeshwa na Serikali. Tunapendekeza *scholarship award* hii ingeitwa *Magufull Scholarship Award*. Hii itaongeza *morale* shulenii na kwa vijana wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la *university classification*. Tuna *universities* nydingi sana, nadhani imefika wakati sasa tuanze ku-classify vyuo vikuu vyetu. Duniani huko *universities* ziko *classified*. Ukienda Marekani wanaitwa *Ivy League* maana yake ukisoma chuo hicho, hata mtu ukimwambia nimesoma Harvard kuna maswali haulizi. Kwa hiyo, nasi tutengeneze Harvard ya Tanzania kwamba labda

nimesoma *University* of Dar es Saalam, kama ndiyo *high classified* hata mwajiri anasema hapa ni pazuri. Kwa hiyo, naomba tuanze kuona umuhimu wa suala hili.

Mheshimiwa Spika, niipongeze sana Serikali ya Awamu ya Tano imefanya kazi kubwa sana kwenye elimu. Wazungu wanasema *access*, tumetoa *access*, watoto wote wa Tanzania wana *access* kwenye *education*, watoto wote wa Tanzania wanapata elimu bure. Baada ya hii ya *access* imekuja na changamoto ambayo itaenda kwenye ubora, vyumba nya madarasa na walimu.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nalisema hili? Tulilisema siku za nyuma, najua wengine inawezekana hawajalitafakari nya kutosha, amelisema Mheshimiwa James Mbatia na Waheshimiwa Wabunge wengi wamelisema. Nadhani umefika wakati, baada ya haya mafanikio makubwa tulionayo ya elimu hebu tuangalie upya mfumo wetu wa elimu, tujue kama tuna matatizo yako yapi, je, tatizo ni *financing*, walimu, vitabu, ni mitaala ama ni muda wa kufundisha? Tukifanya hivyo tutakuwa tume-solve tatizo la miaka 50 ijayo kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, huwa napenda kutoa mfano, mwaka 1981 Rais Reagan aliangalia hali ya Marekani ilikuwa inadorora kwenye *world stage* kwenye *education* wakaanzisha Tume ya Elimu ambayo ilifanya kazi kwa miezi 18 ikaja na ripoti na ripoti hiyo *famous*, inaitwa '*A Country at Risk*'. Taifa kubwa liliangalia likaona hapana tunakokwenda tutashindwa kuangalia.

Mheshimiwa Spika, sasa na sisi imefika wakati wa kuliangalia suala hili la elimu yetu. Watoto wetu wanamaliza chuo kikuu hebu tu-*taste output*. Maana wakati unafanya huo uchunguzi wata-*taste output*, je, lazima watoto wote waende *university* hakuna *tertiary education*? Maana tuna tatizo la ajira na tuna watoto wengi wana *degree* lakini pamoja na tatizo la ajira hatuna mafamasia, mafundi mchundo na wafanyakazi wa hoteli wazuri. Haya yote yatawezekana iwapo tutaunda Tume ya Elimu na kwa kweli

itatusaidia sana na tutakuwa tume-solve tatizo la miaka mingi ijayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la walimu wa hesabu na sayansi, tunarudi hapo hapo. Inawezekana tukasema tatizo letu ni walimu wa hesabu na sayansi lakini inawezekana hilo si tatizo peke yake. Pengine tunasema tatizo ni maslahi ya walimu inawewezeekana siyo tatizo peke yake. Tunaishawishi Serikali ione umuhimu wa kuleta Tume ya Elimu ili tuangalie mfumo wetu wote wa elimu kuanzia *kindergarten* mpaka *university* tuone kama liko tatizo liko wapi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumefanya vizuri sana wanasema kwenye *hard infrastructure*. Tunajenga reli, umeme na barabara; *these are the hard infrastructures*. Umefika wakati tuwekeze vya kutosha kwenye *soft infrastructure* ambazo ni pamoja na *education*. Nchi zote zilizoendelea miaka ya 60 siri yao namba moja ni elimu. Kwa hiyo, niombe sana tulifanyie kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la utafiti. Tulikubaliana tupeleke asilimia moja ya *GDP*. Hata hiyo tunayoipeleka inazidi kupungua. Suala la utafiti ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa mambo mawili. Moja, hapa Bunge wakati tumeanza 2016 tulitunga Sheria ya Vyombo vya Habari. Ni muombe sana Waziri wa Habari, Michezo, ile sheria ilipigiwa kelele sana lakini ilikuwa ni sheria nzuri sana kwa ajili ya kusimamia waandishi wa habari na vyombo vya habari. Tunajua Kanuni zimetungwa na sheria ile ilitaka tutunge vyombo fulani vya kusimamia wandishi wa habari, mpaka leo vyombo vile havijatungwa. Kwa hiyo, ni waombe Serikali wajitahidi watunge vyote vile ili tuanze kusimamia hii kada na tuendeleze weledi katika vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni michezo. Nimewasiliza Waheshimiwa Wabunge wengi sana waliozungumzia suala la michezo. Michezo ni ajira. Mwezi Aprili tunakwenda

kwenye mashindano ya AFCOIlakini tuulizane maswali, timu yetu iko kambini?

**WABUNGE FULANI:** Hapana.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Tunawezaje kushinda ikiwa mpaka leo hatujaenda kambini? Michezo iko Aprili leo ni Februari, mnataka tushindane tukiwa tumeanza kambi wiki moja kabla? Ni lazima kama nchi tuwekeze kwenye michezo na tuungeze bajeti ya Wizara ya Michezo. Tukifanikiwa hapo ninayo hakika vijana wengi watakwenda kucheza kimataifa wataleta dola nchini na kwa kweli itakuwa ni ajira ya uhakika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nami niwashukuru sana wote waliochangia na kwa vyovyote vile wamekubali tuliyoyapendekeza kama mapendekezo yetu ya Kamati. Pia niwashukuru sana Mawaziri, Mheshimiwa Waziri Ummy, Mheshimiwa Profesa Ndalichako na kaka yangu Mheshimiwa Harrison Mwakyembe. Nawashukuru sana kwa ushirikiano mnaotupa kwenye Kamati yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimemsikia Mheshimiwa Waziri Profesa Ndalichako anasema hukukosea kutuunda Guantanamo na naamini Mheshimiwa Spika hukukosea. Watu wanajituma sana na unajua ukishatengwa na ukapelekwa gerezani inabidi muungane ili mfanye vizuri zaidi. Hiyo ndiyo huwa sifa ya watu waliotengwa, wanaungana na wanafanya vizuri zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nitoe hoja kuomba Bunge lako Tukufu liweze kuitisha mapendekezo yetu yote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Hili la Guantanamo walijiita wenyewe jamani, hawajawahwi kuitwa na mtu, walijibatiza wenyewe. Niseme tu kwamba hamkutengwa na mtu yejote, hapana. (*Kicheko/Makofi*)

Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI. Karibu sana Mheshimiwa Oscar Mukasa, una dakika 15 pia. (*Makofi*)

**MHE. OSCAR R. MUKASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa mara nyingine na kwa uendelevu, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii tena, lakini nakushuru pia kwa kutuongoza vizuri hapa na kwenye kazi zetu zote za kila siku.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kuwashukuru wachangiaji wote waliochangia taarifa yetu. Wachangiaji kwa ujumla walikuwa 35 lakini waliogusia taarifa yetu ni wachangiaji 10 ambaao ni utashi mkubwa kabisa wa kisiasa kuonyesha kwamba Bunge letu wanatoa kipaumbele kabisa kwenye masuala ya UKIMWI ndiyo maana wametoa michango kuhakikisha mambo yanakwenda sawa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee pia nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri ambaao wamezungumza; wamezungumza vizuri sana, unaona kabisa utashi wa kupokea kwa kufanya kazi mapendekezo yetu mara pale ambapo yatakuwa yamepokelewa na Bunge lako Tukufu kwamba ni maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa namna nyingine tena naishukuru Serikali kwa kazi kubwa inayofanya. Tunaposema Serikali, tunamshukuru Mheshimiwa Rais na timu yake nzima, kwa sababu takwimu zinasema, *preverence* ya kwanza kabisa ya masuala ya UKIMWI nchi hii nafikiri ni mwaka 1992

au 1995, utanirekebisha, ilikuwa ni asilimia 7.2, lakini leo tunaongelea asilimia 4.7. Maana yake ni kwamba, pamoja na kwamba kazi bado ni kubwa mbele yetu, lakini kazi inafanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia, lakini kuna jambo moja ambalo ni vizuri tuliweke sawa ili tuwe na uelewa wa pamoja. Kuna Wabunge wamechangia vizuri sana kuhusu Mfuko wa Taifa wa UKIMWI, lakini unasikia kwenye maneno yao kuna mwelekeo wa uelewa kwamba kazi ya mfuko wa UKIMWI ni kwenda kuwalinda tu wale ambaو wameambukizwa, lakini kumbe kuna Majimbo mawili hapa kwenye habari ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni asilimia 4.7 ambaو wameshaambukizwa; hawa tunataka tuhakkishe maisha yao yanaendelea kuwa mazuri kiafya, kiuchumi na kijamii, lakini kuna asilimia 95 ambayo hajaambukizwa, hawa tuna kazi ya kuwalinda wasiambukizwe. Kwa hiyo, kuna hizi *constituency* zote mbili. Kwa hiyo, mtazamo wetu wa mapambano ya UKIMWI ni vizuri ukaenda kwenye Majimbo yote hayo mawili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la pili nilitaka nigusie Sheria ya UKIMWI kwa ufupi tu. Wamesema vizuri Mheshimiwa Waziri na unaona utashi wa kushughulika na hilo jambo la marekebisho, lakini niseme kwamba msingi wa kwa nini Kamati na sauti ya jamii inaomba marekebisho haya, misingi ni miwili mikubwa. Msingi wa kwanza ni takwimu kwamba maambukizi mapya ya UKIMWI kwa sasa kwa mujibu wa takwimu zetu wenyewe asilimia 40 iko kwa vijana wa miaka 15 mpaka 24 na miongoni mwa hao, asilimia 80 ni vijana wa kike. Kwa hiyo, huko ndiko maambukizi yapo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bila kujali kwamba kuna habari ya migongano ya sheria, wameolewa na nini, lakini ukweli ni kwamba asilimia kubwa ya maambukizi yako kwa vijana wa umri ule. Kwa hiyo, ni muhimu sana twende

kutazama kule kuna nini? Kwa hiyo, huo ni msukumo wa kwanza wa marekebisho ya sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, msukumo wa pili ni msukumo wa dunia kwa ujumla. Sasa hivi wanasema 90, 90, 90 na Tanzania pamoja na kazi nzuri ya kutoka *preference* ya asilimia 7.2 mpaka 4.7 sasa, lakini bado kwenye 90 ya kwanza hatufanyi vizuri, tuko asilimia 52. Kuna uwezekano ikafika 62 kwa sababu ya mambo ya kitakwimu yanafanyika, tutapara *report* hivi karibuni. Kwa hiyo, asilimia 52 bado haitoshi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, duniani huko watu wamechukua *measure* mbili kubwa; umri, kwamba watu wenye umri ambao maambukizi ni makubwa waingizwe kwenye kupima kwa hiari, lakini na *self testing*. Kwa hiyo, tuna misukumo miwili mikubwa ambayo ni muhimu tukaenda nayo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, misukumo hii inakuja na jambo lingine kwamba tuna kazi ya kuhakikisha kwamba Mfuko wa Taifa wa UKIMWI unaanza kusimama wenyewe. Ni kweli ni kazi ambayo haiwezi kukamilika ndani ya miaka michache lakini ni muhimu kazi hiyo ianze. Mfano, ni kwamba kuna taarifa zisizo rasmi lakini kwa bahati nzuri zitakuwa rasmi hivi karibuni; hivi tunavyozungumza wafadhilli wanakwenda kupunguza asilimia 23 ya pesa ya UKIMWI inayokuja nchi hii kwa sababu yoyote ile, lakini ni kwamba zinakwenda kupungua. Kwa hiyo, huu ni msukumo ambao unatufanya tunahitaji Mfuko wa *ATF* upate tozo maalum uweze kusimama wenyewe, vinginevyo tutapata shida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano hapa; duniani huko, kuna watu wanafanya *endowment fund*. Sasa hivi pesa yote ya UKIMWI inayokuja nchi hii, asilimia 60 inakwenda kununua *supplies*. Unavyosema *supplies* ni sindano, *gloves*, na kadhalika. Yaani vifaa vya kusaidia mapambano dhidi ya UKIMWI. Asilimia kubwa ya vifaa hivyo ni vile ambavyo tukiwekeza wenyewe vinaweza vikatengenezwa hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukitengeneza *endowment fund*, utashirikisha sekta binafsi, utatafuta hizo pesa za UKIMWI, zinattingia kwenye mfumo wa kiuchumi, kwa hiyo, zitajibu haja ya uchumi na haja ya masuala ya UKIMWI. Kwa hiyo, tunaomba tusisitize sana kwenye *ATFna endowment fund* ili tuweze kusimama wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Utumishi; Mzee Mkuchika namwomba kwa dhati kabisa, Wizara hii ndiyo ina dhamana ya kusimamia Sheria ya UKIMWI mahali pa kazi. Kuna baadhi ya Wizara tumezungumza nazo, unaona kabisa kwamba mtazamo wa kwamba ni jukumu lao, upo mbali sana, wanadhani ni jukumu la *TACAIDS*.

Kwa hiyo, hapa naoimba tuweke msukumo kwenye Wizara ya Utumishi kuzisimamia Wizara nydingine kwa kazi hiyo, lakini tuboreshe kitengo cha ndani ya *TACAIDS* ambacho kinapaswa kutazama hizo Wizar nydingine ili waweze kuwasimamia kwa nguvu zaidi.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Madawa ya Kulevyia ni muhimu sana. Sheria inafanya kazi vizuri, tumesikia mifano hapa, ni mfanu Tanzania kwa maana ya utekelezaji wa sheria, lakini sheria ambayo inafanya kazi nje ya sera ni wazi itakuwa na upungufu. Tunaomba ile kasi iongezwe ili jambo hilo lifanyike mara moja halafu tumalizane nalo na kasi iwe kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali maazimio yetu kwamba ni maazimio ya Bunge ili baada ya hapa sasa Serikali ipate maelekezo ya kufanya kazi kwa kasi na nguvu zaidi kwa ajili ya kupiga hatua.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Oscar Mukasa kwa hitimisho lako.

Nawashukuru sana Kamati ya Masuala ya UKIMWI kwa sababu tulipoanza mwaka wa kwanza, wale Wajumbe wa mwanzo waliwahi kuniita siku moja na kuniambia, yaani umeona sisi ndio tunafanana fanana na UKIMWI au kwa nini umetuteua kwenye Kamati hii? Nilipata shida sana ya kuwashawishi kwamba jambo hilo pia ni muhimu sana, linapaswa liangaliwe na Bunge letu. Baada ya kulazimishwa nao kwamba nivunje Kamati, tukaiunda upya na Mheshimiwa Oscar Mukasa akawa Mwenyekiti. Sasa nadiriki kusema Kamati hii kwa kufanya kazi na *ku-deliver* mambo ni namba moja katika Bunge hili. Hongereni sana, sana, sana. (*Makof/ Vigelegele*)

Sasa tumalizie na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Utawala na Serikali za Mitaa. Anakuja Mwenyekiti mwenyewe, Mheshimiwa Rweikiza, karibu sana. Una dakika 15, karibu Mheshimiwa.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuhitimisha hoja yangu niliyoitoa asubuhi.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja yangu ni Wabunge 18. Awali ya yote nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri; Mheshimiwa Jafo, Mheshimiwa Mkuchika na Waheshimiwa Manaibu Waziri; Mheshimiwa Kandege, Mheshimiwa Waitara na Mheshimiwa Mwanjelwa kwa michango yao ambayo imesaidia kutoa baadhi ya majibu.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Wabunge kadhaa wamechangia sana kuhusu elimu. Kamati yangu inakubaliana na Wabunge hawa kwamba elimu kwa kweli kuna kazi za kufanya kubwa sana mbele yetu. Tunahitaji

kuboresha Sekta ya Elimu na lazima Serikali iwe na mpango mkakati mzuri, mpango madhubuti wa kuboresha elimu. Walimu bado ni haba sana. Wanaostaafu nafasi zao hazijazwi, lakini wasomi wapo ambao wamesomea Ualimu na ingekuwa vizuri sana kuboresha sekta hii kwa kuajiri Walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, huwezi kuwa na shule ina wanafunzi 600, una Walimu watatu. Kwa keli hutoi elimu, isipokuwa tu wanapita pale, wanahitimu, wanaondoka, lakini hawaelimiki. Vifaa, madawati, majengo, madarasa, vyoo; ni vizuri mkakati ukaboreshwu kusudi elimu iweze kuwa bora zaidi. Ndiyo maana hapa Mheshimiwa mmoja ametoa takwimu, amelinganisha shule binafsi na shule za Umma. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri Waitara akijibu, akasema kwamba shule binafsi zinakaririsha. Nitangaze maslahi kwamba mimi nikko kwenye sekta hii ya shule binafsi.

Mheshimiwa Spika, kuna wakati ilikuwa ni fedheha kusoma shule binafsi huko nyuma miaka ya 1970, 1980; ilikuwa ni fedheha kwenda shule binafsi. Baadaye wazazi wakawa wanepeleka watoto wao Uganda, Kenya na nchi nyingine huko kupata elimu bora, lakini baadaye pia tena Watanzania wakajiongeza, wakajizatiti wakajenga shule humu ndani Tanzania nami ni mmojawapo. Sasa kwa kweli hawa wa binafsi wanazingatia sana ubora. Kwa hiyo, ndiyo tofauti iliyopo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikiboresha hivi vitu; Walimu, vifaa, madawati, vyoo na vifaa vingine, elimu itakuwa bora. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli kwa kusema elimu ni bure. Baadaye shule hizi zitakufa zenyewe tu, zitaondoka zenyewe kwa sababu zina gharama kubwa kuziendesha na ndiyo maana tunasema kama mpango wa elimu bure utafanikiwa, shule za binafsi zitakufa zenyewe. Hakuna haja ya kuzipiga vita, tunafanya kazi moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge wamechangia kuhusu suala la Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kunyanyasa

wananchi na kuwaweka ndani na mambo mengine. Nashukuru Serikali imechukua hatua, Mheshimiwa Mkuchika na Mheshimiwa Jafo wamepambana sana na hawa watu, walikuwa wanakiuka sheria. Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli na Mheshimiwa Waziri Mkuu wamekemea sana tabia hii, lakini haijaisha, bado ipo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna haja bado ya kuendelea kuwadhibiti Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya waache kunyanyasa watu. Kazi yao siyo kunyanyasa watu, ni kuwatendea kazi, kuwasaidia kwenye harakati za kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Nkamia amezungumzia jambo la uchaguzi kwamba maendeleo hayaji kwa uchaguzi. Ni kweli jambo hili linazungumzika na linafikirisha. Sisi tumeingia humu tuna miaka mitatu, leo homa imeshaanza ya uchaguzi wa mwaka kesho. Watu Majimboni wanapita huko, wanajipitisha huko, wanasumbua; tunakaa humu nusu nusu, uko nusu; mguu mmoja ndani, mmoja nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tungekuwa na miaka saba, labda mtu angekuwa ametulia hapa mpaka 2022. Sasa kwa sababu tunaelekea mwakani kwenye uchaguzi, homa imeshaanza humu, presha inapanda, inashuka. Sasa inakuwa taabu sana. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kuna nchi nyingine nyingi Afrika humu, Rais anagombea vipindi vingi tu miaka mitano, mitano, hata mara 10 kama ana uwezo huo na anaendelea na wanafanya vizuri; nimeziorodhesha hapa nchi kama 22 au 21; Chad, Cameroon, Comoro, Congo, Djibouti, Equatorial Guinea, Ethiopia, Gabon, Gambia, Liberia, Lesotho, Libya, Swaziland, Morocco, Mauritius, Sudan, Togo na Uganda hata Rwanda, nirudi nyuma tena sasa.

Mheshimiwa Spika, hawa hawana *limitya* kugombea, hata kwa nafasi ya Rais, anagombea hata vipindi vitatu,

vinne, vitano, kumi. Margaret Thatcher alikaa miaka 11, Waziri Mkuu wa Uingereza; Angela Markel ana miaka 16 na tuiseme kwamba sisi tumeendelea kuliko wao. Hata hao Waafrika, Ethiopia wanatuzidi maendeleo, Mauritius wanatuzidi maendeleo; Togo wako juu kuliko sisi, lakini wanagombea kwa muda mrefu na wanakaa. Wengine katika hawa wana vipindi vya miaka saba, saba kama Cameroon miaka saba, Gabon miaka saba na hakuna ukomo. Kwa hiyo, jambo hili ni la kuzingatia na inafaa kulijadili ili ikiwezekana Mheshimiwa Nkamia alete hoja yake hapa Bungeni tujadili halafu tuone inakwenda viperi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa wamechangia kuhusu *TARURA*. Kamati inasema kwamba *TARURA* ina kazi kubwa sana imeifanya. Tangu imeanzishwa muda mfupi uliopita, imesimamia kazi za barabara za vijijini na mijini. Barabara ndogo ndogo nyingi za Dar es Salaam ni za *TARURA*. Kwa hiyo, *TARURA* ina kazi kubwa sana lakini haina pesa. Kwa hiyo, tunasisitiza kwamba *TARURA* iongezewe fedha kutoka Mfuko wa Barabara (*Road Fund*) badala ya asilimia 30 iwe asilimia 50 ili barabara za *TARURA* ziweze kutengenezwa ziende vijijini kule kwenye mazao, zipeleke pembejeo mwaka mzima tuwe na huduma nzuri vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili la barabara za *TARURA* na *TANROADS*, barabara kuu zimekamilika bado kidogo tu; Katavi, Kigoma na sehemu nyingine. Kwa hiyo, ikienda asilimia 50 *TANROADS* itatosha kukarabati barabara ambazo zipo na kujenga zile mpya chache, lakini asilimia 50 iende *TARURA* ili nao waweze kupata uwezo wa kujenga barabara zao.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamechangia kuhusu *TASAF*. *TASAF*imefanya kazi nzuri sana ya kupigiwa mfano, lakini tunasisitiza kwamba Serikali itoe mchango wake kwenye *TASAF*, tusitegemee tu wafadhili pake yake. Serikali itoe mchango wake kusudi wale wa asilimia 30 ambao hawapati mchango wa *TASAF* wapate huduma hiyo na waweze kupata tija ya hela ya *TASAF*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge wamechangia kuhusu Sekta ya Afya. Naipongeza Serikali sana kwa kujenga hospitali 67 za Wilaya na Vituo vya Afya 650 kwa muda mfupi. Ni jambo kuba sana la kusifia, la kuishukuru Serikali. Kujenga hospitali moja inahitaji shilingi bilioni saba na nusu; fedha iliyotolea ambayo tunashukuru ni shilingi bilioni moja na nusu. Tunasisitiza kwamba hii iliyobaki shilingi bilioni sita itolewe kusudi hospitali hizi zijengwe ndani ya muda unaotakiwa na zikamilike kwa ukamilifu wake.

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa lingine, wataalam watafutwe, waanze kuajiriwa na kuandaliwa. Kwa sababu mwezi wa Sita siyo mbali sana, Madaktari, Wauguzi, Manesi na wengine wawepo kwa sababu hospitali 67 ni nyingi sana Vituo vya Afya 350 ni vingi kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamechangia kuhusu maji vijijini na hali ya maji vijijini haijawa nzuri, bado ni mbaya. Tumesema sana humu Bungeni kwa miaka mingi kwamba tuunde Wakala wa Maji Vijijini. Tunashukuru kwamba juzi juzi hapa sheria imepitishwa hapa ya RUWASA kuunda Wakala wa Maji Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Wakala huu tunataka uanze kazi mara moja, upewe fedha, uvezeshwe, kazi ianze. Kamati inaunga mkono kwamba ile shilingi 50 kwenye *petrol* na *diesel* ikatwe kusudi iende kwenye mfuko huu ambao unaanzishwa chini ya Wakala wa Maji kusudi huduma iweze kuwa nzuri kwa watu wa vijijini ambao wana shida kubwa sana ya maji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mwisho nimalizie kwa kusema kwamba, tumekuwa na dhana ya *D by D (Devolution by Decentralization)*; kazi nyingi zinafanyika kwente Halmashauri kule, kwenye Madiwani, kwenye vijiji, kwenye vitongoji, na mitaa. Kumekuwepo na mwelekeo sasa hivi wa kuondoa huduma hizi huko kuzirudisha Makao Makuu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, mambo ya maji, Hospitali za Mikoa zimesharudi Wizarani, kuna mambo ya ardhi yanarudishwa Wizarani. Sasa hii itakatisha tamaa, Halmashauri zitakosa kazi za kufanya; na iko kwenye Katiba kwamba *Decentralization* iendelee kuwepo ili wananchi waone kwamba wanamiliki miradi hii na wafanye kazi kwenye miradi hii kwa moyo na kwa kupenda.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa michango hii na mapendekezo haya ya Kamati yaweze kuazimiwa na Bunge hili ili Serikali iweze kuyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Utawala na Serikali za Mitaa.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tumefikia mahali ambapo nitawahoji endapo mnazipokea na mnaafiki taarifa za Kamati hizo tatu pamoja na maoni na mapendekezo yake yapitishwe kama maazimio ya Bunge.

*(Hoja illitolewa lamuliwe)  
(Hoja illiamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa za Kamati za Kudumu za Bunge za Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii; Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa na Kamati ya Masuala ya UKIMWI zilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Wote mmeafiki. Nawashukuruni sana Kamati zote tatu kwa jinsi ambavyo kwa mwaka mzima mmefanya kazi vizuri. Mmejitalidi sana. Najua tutakaporudi awamu inayokuja tutafanya ziara ya kwenda kuona baadhi ya mambo na utekelezaji uliofanyika kwa bajeti iliyopita, lakini

inapendeza kuona jinsi ambavyo Wajumbe wa Kamati wanavyofanya kazi katika Bunge letu. (*Makofi*)

Ukiwakuta Wajumbe wa Kamati yoyote ile, huwezi kujua huyu ni wa chama gani, huwezi kujua huyu nini; wanajadili vizuri, wanashirikiana vizuri sana. Tatizo, tukiingia humu, sasa sijui humu kuna shida gani! Tukishaingia humu, hata Wajumbe wa Kamati moja wanaanza kutoleana macho, wanataka kuparurana kabisa, lakini ni sehemu ya mambo ya Bunge. Niendelee kuwatia moyo, tuendelee kufanya kazi vizuri. (*Kicheko*)

Pia nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wote wahusika wa Kamati hizi kwa jinsi ambavyo mmetoa ushirikiano mkubwa sana pamoja na Makatibu Wakuu na Watumishi wote ambao wako chini yao. Mmefanya kazi nzuri sana illyotufikisha hapa. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ikayafanyie kazi maazimio haya, ni maazimio mazuri yenye nia njema ya kuisogezza mbele nchi yetu ya Tanzania. Tunawatakania kila la heri.

Katika kumalizia sasa hapa nina matangazo mawili; tangazo la kwanza, Waheshimiwa Wabunge tunafahamu kwamba kuna lile agizo la Mheshimiwa Rais kuwataka Mawaziri wa kwenye sekta zinazohusiana na Mifugo, Ardhi, Maliasili na kadhalika kuondoa ile migogoro na wananchi na masuala ya hifadhi mifugo, wakulima na kadhalika.

Sasa tunaombwa Waheshimiwa Wabunge kwamba kesho baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa 7.00 mchana, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na wataalam wa Wizara hiyo watakuwa katika Ukumbi wa Msekwa kwa ajili ya kupokea kero za ardhi katika Majimbo yenu au katika maeneo mnayotoka na hasa kama mna maeneo ambayo mnapendekeza kwamba ile Kamati Maalum iyatazame kipekee, maeneo yenye migogoro.

Kwa hiyo, tutawakumbusha tena na tangazo lingine kesho, lakini saa 7.00 watakuwa pale Ukumbi wa Msekwa kwa ajili ya kazi hiyo. Usikose kufika halafu baadaye tena

unakuja kulalamika, ooh, bado kuna mgogoro wa hapa na pale. Wakati ni huu, tutumie vizuri nafasi hiyo ya kesho.

Naona shughuli zilizopangwa leo zimekamilika. Basi, ule mpira unaoendelea, hivi sasa unakaribia *half time*; mpaka sasa Simba tatu, Mwadui bila. (*Kicheko/Makofii*)

**MBUNGE FULANI:** Unanunua mechii.

**SPIKA:** Kwa hatua hiyo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.40 Usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 8 Februari, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*